*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

### Kikao cha Sita – Tarehe 6 Februari, 2018

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:-**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 44 la tarehe 03 Novemba, 2017
(ii) Toleo Na. 45 la tarehe 10 Novemba, 2017
(iii) Toleo Na. 46 la tarehe 17 Novemba 2017
(iv) Toleo Na. 47 la tarehe 24 Novemba, 2017
(v) Toleo Na. 48 la tarehe 01 Desemba, 2017
(vi) Toleo Na. 49 la tarehe 08 Desemba, 2017
(vii) Toleo Maalum Na. 10 la tarehe 09 Desemba, 2017

(viii) Toleo Na. 50 la tarehe 15 Desemba, 2017
(ix) Toleo Ma. 51 la tarehe 22 Desemba, 2017
(x) Toleo Na. 52 la tarehe 29 Desemba 2017
(xi) Toleo na. 01 la tarehe 05 Januari, 2018
(xii) Toleo Maalum Na. 01 la tarehe 10 Januari, 2018
(xiii) Toleo Na. 02 la tarehe 12 Januari, 2018
(xiv) Toleo Na. 03 la tarehe 19 Januari, 2018
(xv) Toleo Na. 04 la tarehe 26 Januari, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imetayarisha pia nakala za magazeti hayo katika mfumo wa nakala tete ambazo zimesambazwa katika maeneo yetu ya kupokea taarifa za Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 *(Annual Report and Accounts of* Mzumbe *University for the year ended 30th June, 2016)*

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali yetu na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 69

### Huduma Hafifu ya Maji Maeneo Mengine Bukoba Vijijini

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Maeneo mengi ya Bukoba Vijijini kama vile Kata za Ruhunga, Kibirizi, Izimbya, Mugajwale, Rukoma, Kikomelo na nyingine yana tabu kubwa sana ya upatikanaji wa maji na kilio hiki kimekuwa cha muda mrefu sana:-

Je, ni kwa nini Serikali haichukui hatua ya kuwasaidia wananchi hao.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hali ya upatikanaji wa huduma za maji kwenye maeneo aliyoyataja bado ni changamoto. Hata hivyo, kwa uhalisia hali hiyo ni tofauti na maeneo mengi ya Halmashauri ya Bukoba Vijijini ambako Serikali imekamilisha hivi karibuni miradi 18 ya maji kwenye Kata za Nyakibimbili, miradi mitatu (3); Kyamulaile, miradi mitatu (3); Kemondo, miradi mitatu (3); Buteragunzi, miradi minne (4); Rubole, mradi mmoja (1); Karabagaine, mradi mmoja (1); Rubafu (mradi mmoja (1); na Mikoni, miradi miwili (2) iliyogharimu shilingi 3,552,117,690 inayohudumia wakazi

61,279; hali hiyo imeinua upatikanaji wa maji hadi kufikia asilimia 64 ya upatikanaji wa maji kwa wakazi wote wa Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji itapanda zaidi hadi kufikia asilimia 75 ifikapo mwezi Juni, 2018 kutokana na kukamilika kwa miradi ya Rukoma, Ubwera, Katoma na Kibirizi inayogharimu Sh.2,235,274,135 na itakayohudumia wakazi 18,449.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kuna visima 75 vinavyofanya kazi kwenye Kata ya Rukoma, Ruhunga, Butulage, Mgajwale, Izimbya, Katoro, Rubale, Kaibanja, Kishogo, Kasharu, Maruku na Kikomero; na vyanzo vingine 90 vya maji kwenye Kata za Nyakato, Buhendagabo, Katerero na Bujugo. Serikali itatekeleza miradi ya maji kwenye Kata za Ruhunga, Mugajwale, Izimbya na Kikombero ambako kwa sasa wakazi wake wanahudumiwa na visima 23 vyenye uwezo wa kuhudumia watu 7,500 kati ya wakazi 11,794 waliopo katika Kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa Mwaka 2018/2019 imetenga shilingi bilioni 2.5 endapo Bunge litaridhia ili kuboresha zaidi upatikanaji wa huduma za maji Bukoba Vijijini ikiwemo maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ingawa baadhi ya maeneo aliyosema yamekamilika, miradi yake haijakamilika. Nina maswali mawili ya nyongeza:

Swali la kwanza; maeneo niliyoyataja haya ya Kata ya Ruhunga, Kibirizi, Izimbya, Mugajwale, Rukoma, Kikomelo na mengine kama Kaitoke, Kyamuraire yana shida kubwa sana ya maji na swali hili nimeliuliza leo ni mara ya nne. Je,

niulize mara ngapi ili hawa wananchi nao wafikiriwe kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa vile tumeshapata ufumbuzi wa tatizo la maji nchi nzima maana yake siyo kwangu tu ni nchi nzima kuna tatizo la maji nao ufumbuzi huo ni kuunda wakala au Mfuko wa Maji nchi nzima kama ilivyo *REA* kwenye umeme. Tumelijadili humu mara nyingi na tumekubaliana. Je, kwa nini Mfuko huu hauanzi ili tatizo hili liweze kupata ufumbuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza huo mradi wa maji kwenye eneo lake tulishaujadili na tukaangalia uwezekano wa namna gani tunaweza tukapeleka maji pale kwa kutumia chanzo cha maji cha Ziwa Victoria kutoka kwenye mradi uliokamilika pale Bukoba na tayari tulishaagiza wataalam wanafanyia kazi ili tuweze kufikisha maji katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu uanzishaji wa Mamlaka ya Maji Nchini tunalifanyia kazi na tuko katika hatua nzuri kabisa wakati wowote tutaleta tangazo kwamba tayari Wakala wa Maji Nchini utaanzishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji pale tutakapopata ridhaa ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Matatizo ya maji yaliyoko Bukoba Vijijini yanafanana na matatizo tuliyonayo kule Karatu. Kata ya Rotia na Kata ya Mang'ola zina upungufu mkubwa wa maji kutokana na miundombinu iliyokuwepo kuwa ya muda mrefu na hivyo kushindwa kupeleka huduma ya maji stahiki. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha ili kuboresha huduma ya maji katika Kata hizo mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo yeye mwenyewe amekiri maeneo ya Karatu ni miongoni mwa maeneo ambayo tangu zamani kumekuwa na uwekezaji kwenye miradi ya maji na ndiyo maana miradi hiyo aliyoitaja amesema kwamba miradi ile ina uchakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa *program* ya maji tumeweka kipaumbele kikubwa kwanza kukarabati miradi iliyokuwepo ikiwemo hiyo ya Kata ya Rotya na Kata na Mang'ola ambayo kuna miundombinu ya maji ya muda mrefu. Kwa hiyo kipaumbele ni kukarabati kwanza hiyo kabla hatujaanza miradi mipya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali langu narudia pale pale kwamba kama alivyouliza Mheshimiwa Rweikiza ni kwamba ni lini Serikali itafikiria kuanzisha Mfuko huu wa Maji ili kuweza kuondoa kero kubwa kwa wananchi kuhusu matatizo ya maji kama ambavyo tumeweza kuondoa kero ya umeme sasa katika sehemu nyingi vijijini. Je, ni lini tutaanzisha huu Mfuko wa Maji? Nadhani ndiyo hoja ya msingi zaidi hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili; Mfuko ulishaanzishwa. Mfuko tayari tunao na Mwaka huu wa Fedha tulionao Mfuko una jumla ya shilingi bilioni 158. Suala la pili sasa tunataka kuanzisha Wakala kwa ajili ya kutumia huo Mfuko ili tuwe na wakala utakaohakikisha kwamba tunapata huduma ya maji vijijini kwa haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Augustino Manyanda Massele.

Na. 70

## Ujenzi wa Vituo vya Afya Nchini

**MHE. AUGUSTINO M. MASELLE** aliuliza:-

Ni Sera ya Taifa kuwa na Vituo vya Afya kwa kila Kata, na wananchi katika baadhi ya Kata wamejitahidi kujenga majengo kwa ajili ya vituo hadi kufikia usawa wa renta kwa nguvu zao:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo ya vituo vya afya vya Ikobe, Ilolangulu, Kagera na Bukandwe?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Watumishi wa Afya Wilayani Mbogwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutelekeza Sera ya Afya ya kuwa na kituo cha afya katika kila kata. Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ina vituo viwili vya afya ambavyo ni Kituo cha Afya Iboya na Masumbwe, vituo vingine viwili vya Nhomolwa na Kagera viko katika hatua ya ukamilishaji wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia uhisani wa Canada, Benki ya Dunia na Sweden imetoa kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuboresha na kujenga miundombinu ya vituo vya afya vya Masumbwe na Iboya sawa na shilingi milioni 400 kwa kila kituo ili kuboresha huduma za mama na mtoto. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Halmashauri ya

Wilaya ya Mbogwe imetenga kiasi cha shilingi milioni 35 kupitia ruzuku ya Maendeleo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo katika vituo vya afya Nhomolwa na Kagera pamoja na shilingi milioni 10 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wazazi katika zahanati ya Ilolangulu. Zahanati ya Bukandwe itatengewa fedha katika bajeti ya mwaka wa 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeajiri wataalam wa afya 2509 ambapo kati ya hao 16 walipangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe na watumishi 13 wameripoti na kupangiwa vituo vya kazi. Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa afya kadri wanavyohitimu na kupangwa moja kwa moja kwenye vituo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwanza naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuongeza pesa katika Sekta ya Afya na kuwezesha ujenzi huu na upanuzi wa vituo viwili hivi vya Iboya na Masumbwe. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuruhusu bajeti ya mwaka huu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe uanze baada ya mwaka huu kuiondoa hiyo bajeti kutokana na ukomo wa bajeti kwa maana ya *ceiling. Ceiling* ili-*burst* kwa hiyo, ile hela ambayo tulikuwa tumepanga kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya iliondolewa. Je, Mwaka huu wa Fedha itaruhusiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, yamekuwepo madai ya muda mrefu ya watumishi ya uhamisho kutoka katika Wilaya mama ya Bukombe kuja Wilaya ya Mbogwe wakiwemo Watumishi wa Idara ya Afya hawajalipwa. Je, malipo haya yatafanyika lini ili kuondoa usumbufu kwa watumishi hawa ambao wamekuwa wakidai kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Serikali tunazipokea pongezi zake za dhati maana yeye mwenyewe anakiri kwamba vituo viwili kwanza kujengwa kwa milioni 400, jumla milioni 800 siyo haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua je, Serikali itaruhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya baada ya kwamba haikuwezekana kutokana na ufinyu wa bajeti. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote Wilaya zote 64 na jana nilijibu, ambazo hatuna Hospitali za Wilaya, hospitali zinajengwa. Ninachoomba kwa kupitia Halmashauri yake ni vizuri wakatenga eneo na wao wakaanza ujenzi ili Serikali ije kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anauliza kuhusiana na suala la kuwalipa Watumishi ambao walihamishwa kutoka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wilayani kwake, lini watalipwa. Mara baada ya uhakiki kukamilika na Mheshimiwa Rais alilisema, kati ya madeni ambayo yanatakiwa kulipwa ni pamoja na madeni ya Walimu pamoja na Watumishi wa Afya. Zoezi hili litakamilika muda si mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndumbaro, halafu Mheshimiwa Maige.

**MHE. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote niwashukuru wananchi wa Songea Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge na kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Pili nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi, Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo lililopo katika Jimbo la Mbogwe ni sawa na tatizo ambalo lipo katika Jimbo la Songea Mjini katika ujenzi wa Vituo vya Afya hususan katika Kata tatu za Ndilimalitembo, Ruvuma na Likuyufusi ambazo wananchi wamejitolea kwa mguvu na wanahitaji msaada wa Serikali. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya katika Kata ya Ndilimalitembo, Kata ya Ruvuma na Kata ya Likuyufusi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kumpongeza kwa ushindi wake na karibu sana Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake anataka kujua lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kukamilisha vituo vya afya katika Kata zake hizo mbili. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinajengwa tena vinajengwa vingi ili kuondoa adha ya matibabu kwa wananchi kwa kutokwenda umbali mrefu kupata huduma ya matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza na vituo 205 baada ya hivi 205 kukamilika ni azma ya Serikali kuhakikisha na maeneo mengine na hasa ambayo kuna upungufu mkubwa na hasa kwa mijini kumekuwa na msongamano mkubwa sana wa wananchi kufuata huduma ya afya katika hospitali za Mikoa na Wilaya. Ni azma yetu kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinajengwa ili kupunguza mrundikano ikiwa ni pamoja na maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL G. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Msalala kama ambavyo umesikia maeneo mengine haya mawili ambayo yameuliziwa maswali Songea Mjini na Mbogwe, wao pia wana maboma ya zahanati na vituo vya afya na bahati nzuri wenyewe wamekwenda mbali zaidi, kuna maeneo ambapo kumetajwa kwamba maboma yako kwenye lenta. Wananchi wa Jimbo la Msalala wana vituo vya afya vinne ambavyo vimekwishakamilika maboma yake, zahanati 38 ambazo zimekwishakamilika maboma yake. Maboma haya yamejengwa zaidi ya miaka mitatu na sehemu vimeanza kubomoka. Imefika mahali sasa wananchi wanagomea michango mingine wakisema kamilisheni kwanza miradi tuliyokwishaianza.

Nataka tu kujua toka Serikalini ni lini sasa Serikali na yenyewe italeta nguvu yake ambayo wastani ni kama bilioni 1.6 ili kukamilisha maboma haya 42, manne ya vituo vya afya na 38 ya zahanati, Msalala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu swali refu na jibu kwa kifupi. Waheshimiwa jana Naibu Spika alitoa *ruling* maswali haya ya nyongeza yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa nianze kwa kumpongeza kwa jitihada kubwa ambazo anafanya kwa wananchi wa Jimbo la Msalala, kwa ujenzi mkubwa ambao umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiongea mara nyingi alichokuwa anaomba kwanza katika hizi pesa ambazo zimepatikana zikitumika zikakamilisha hayo majengo ambayo yanatakiwa kujengwa katika vituo vya afya, anataka hicho kiasi kinachobaki kipelekwe kwenye maeneo mengine. Jambo ambalo Serikalini wala hatuna ubishi nalo ni kuhakikisha kwamba jitihada za wananchi na tukibana vizuri pesa zikatumika maeneo mengine yaweze kujengwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa vituo vya kutolea afya 1,845 na hivi tutavikamilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakwenda, sasa tunaendelea na swali Namba 71, Mheshimiwa Magereli.

Na. 71

**Kugawa Ramani za Matumizi ya Ardhi Nchi Nzima**

**MHE. LUCY S. MAGERELI** aliuliza:-

Matatizo ya migogoro ya ardhi na Mipango Miji ni suala nyeti sana linalohitaji kutazamwa sana katika zama hizi; na hivi karibuni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi aligawa ramani za maeneo ya mitaa ya Jiji la Dar es Salaam lakini zoezi hilo halikufanikiwa kutokana na kukosa mkakati ulioambatana na matumizi ya ramani hizo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ramani hizo zinapatikana kwa nchi nzima ili kusaidia kuongoza matumizi ya ardhi katika miji mingi nchini?

(b) Waziri Mkuu aliyepita Mheshimiwa Mizengo Pinda alisema Serikali ingeuza *Government Bond* ili kupata fedha za kugharamia mradi huo; Je, agizo hili limefikia hatua gani katika utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 8 ya Mipango Miji ya Mwaka 2007 katika Kifungu cha 21(1) inazipa

Halmashauri mamlaka ya kupanga na kuhakikisha ramani za Mipango Miji ya jumla *(master plan)* na ile ya kina (michoro ya mipango miji) iliyoidhinishwa na Wizara yenye dhamana na ardhi zinahifadhiwa na kusambazwa kwa wadau. Halmashauri zinaendelea kutekeleza jukumu hili kwa kutoa elimu na tafsiri sahihi ya michoro ya Mipango Miji kwa wananchi ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi shirikishi kwa lengo la kudhibiti uendelezaji holela.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuuza *bond* ili kupata fedha za kugharamia mradi huu, suala hili halijatekelezwa badala yake kila Halmashauri imeelekezwa kutumia vyanzo vyake vya mapato ya ndani kwa kushirikiana na sekta binafsi. Utaratibu huu unatokana na Sheria ya Mipango Miji inayotoa fursa kwa wamiliki binafsi wa ardhi kuandaa mipango ya matumizi kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magereli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara ya Ardhi lakini bado uhitaji wa suala hili la uandaaji ramani ningeendelea kupendekeza kwamba lifanywe na Wizara ya Ardhi badala kurudishwa kwa Halmashauri kwa sababu bado Halmashauri zetu zina mbinyo mkubwa sana wa bajeti.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuandaa mipango maalum kupitia Wizara ya Ardhi kuhakikisha kwamba ramani za Mipango Miji ya jumla kwa maana ya *master plan* zinapatikana nchi nzima na kuacha zile *detailed plan* ndiyo zifanywe na Halmashauri?

Swali la pili, kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba ameacha Halmashauri zishirikiane na sekta binafsi kwa ajili ya kuandaa hizi ramani za Mipango Miji. Sitaki kukubaliana na ningependa nieleze tu bayana kwamba katika kuliachia Halmashauri zetu suala hili

linafungulia mianya ya rushwa na wananchi wengine kushindwa kumudu gharama, kwa sababu sasa hivi ukipeleka mchoro wako binafsi au kuomba mchoro binafsi unaambiwa wewe mwenyewe ndiyo uugharamie mpaka na kikao cha Halmashauri kikae kwa gharama ya mwombaji kupimiwa eneo la ardhi. Je, Serikali haioni kwamba inafungua mianya rushwa na kuwafanya wananchi washindwe kabisa kupata huduma hii kwa ufanisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba nakubaliana naye katika swali lake jinsi alivyouliza, kwa sababu taratibu zinazoendelea mpaka sasa suala zima la upangaji miji ni jukumu la Halmashauri zenyewe. Napingana naye kwenye suala la kusema kwamba Wizara ifanye kazi hii. Wizara kazi yetu ni kusimamia sera na tunaposimamia sera maana yake tunafanya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukumbuke mwaka 2016 Waziri alitoa ramani kama kuleta chachu kwenye Halmashauri zetu zote ili waweze kufanya jukumu hilo ambalo ni la kwao kama mamlaka za upangaji miji. Mara nyingi kama wananchi kule na hasa kwenye maeneo ya vijiji Wenyeviti wa Mitaa kama hawatambui maeneo yao migogoro inakuwa mingi. Kwa hiyo, nitoe rai tu kwa Halmashauri kuendelea kutekeleza jukumu lao la kuandaa zile ramani na baadaye kuzishusha mpaka kwenye maeneo ya vijiji na mitaa kule ili wale wenye dhamana kule waweze kuchukua jukumu lao la kuelimisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi linaloendelea la urasimishaji kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 37 (d)(4) ambapo urasimishaji unaendelea, bado zoezi la kugawa linatakiwa liendelee katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge akubaliane kwamba Wizara haiwezi

kupora mamlaka ya Halmashauri isipokuwa tutaendelea kuwakumbusha ili watimize wajibu wao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joyce, Mheshimiwa Nkamia umeitwa lakini wala hukuwepo nafasi yako imepita. Mheshimiwa Joyce.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 31Januari, 2018 Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dokta Kigwangala alitoa ilani kwenye kiwanja Namba 4091 kilichopo eneo la Njiro Mkoa wa Arusha kwamba wale watu ni wavamizi, wamejenga eneo la Serikali la kiwanja kinachoitwa kwa jina la Tanzania *Tourist Corporation*.

Swali langu, kwa nini Mheshimiwa Kigwangalla Waziri wa Maliasili na Utalii asikutane na watu hawa kwa sababu watu hawa pia ni wamiliki halali eneo lile kwa sababu wana hati pia na licha ya hivyo haoni kama huu ni uzembe wa Serikali yenyewe na je, kwa nini wasimtafute aliyehusika kufanya ili kabla hajawahukumu wananchi waliojenga katika eneo lile?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ametoa hilo tamko ametoa siku 30 kwa wale watu waliovamia wajisalimishe waje zile *documents* halali ili kusudi Serikali iweze kutathmini na kuangalia kama kweli hayo maeneo wameyapata kihalali. Kwa hiyo, siku 30 baada ya hapo ndipo tutafanya uamuzi unaostahili.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Najma Giga.

Na. 72

**Kero za Muungano**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Serikali zetu zote mbili zimekuwa kwenye jitihada za kukabiliana na kero za Muungano:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar kuhusu ushiriki wa Wizara zisizo za Muungano na Zanzibar kwenye Taasisi za Kimataifa zinazotambua utaifa wa wananchi katika uwakilishi wake?

(b) Je, Serikali inapata ugumu gani kuwafahamisha wananchi kwa uwazi kabisa kila kero za Muungano zinazopatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kwamba Wazanzibari kwa muda mrefu wamekuwa na kero ya kutoshirikishwa katika medani za Kimataifa. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mabadiliko yake, masuala ya mambo ya nje yapo chini ya mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo Zanzibar ni sehemu yake. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikishirikishwa kwa kiasi kikubwa katika taasisi za Kimataifa zinazotambua utaifa wa Tanzania kwenye Wizara zisizo za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

imeshirikishwa katika mikutano ya Kimataifa na taasisi za Kimataifa, kama vile Mikutano ya mabadiliko ya Tabianchi, Mikutano ya Shirika la Kazi Duniani, Mikutano ya Kamisheni ya Hali ya Wanawake, Mikutano ya Shirika la Kazi Duniani, Mkutano kuhusu utekelezaji wa lengo Namba 14 la Maendeleo Endelevu linalohusu Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Bahari na Rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Viongozi wa Mashirika ya Kimataifa waliofanya ziara hapa nchini kwa mwaka 2017, walitembelea pia Zanzibar na kufanya mazungumzo na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambao ni Wakurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Mkurugenzi wa *FAO*, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Mkurugenzi Mtendaji wa *UNAIDS*.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haijawahi kupata ugumu wala kugugumizi katika kuwafahamisha wananchi kwa uwazi kuhusu changamoto zilizopatiwa ufumbuzi na hata zile ambazo ziko katika hatua mbalimbali ya kutafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nikiwa Waziri mwenye dhamana ya Muungano, nimefanya jitihada kubwa za kuwafahamisha wananchi kwa uwazi kabisa kuhusu jitihada za Serikali katika kutatua changamoto za Muungano kupitia vyombo vya habari mfano *television*, redio na magazeti, makongamano, hotuba za viongozi wakati wa maadhimisho ya Muungano na hata kupitia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Najma Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri bado nina swali moja la nyongeza. Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutuletea taarifa zote pale ambapo changamoto za Muungano zinapopatiwa ufumbuzi ndani ya Bunge hili ili sisi Wawakilishi

wa Wananchi tuweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuzifikisha kwa wananchi kwa wepesi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais(Muungano na Mazingira) napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ambaye ni nyara ya CCM na tegemeo kubwa la CCM kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hilo ni zuri kwamba iko haja ya kuleta taarifa zote kwa namna ambavyo Ofisi ya Makamu wa Rais wanavyoweza kupitia Kamati yetu ya pamoja ya kero za Muungano hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu imekuwa ikitoa taarifa hizi kila wakati kama nilivyosema kwenye majibu yetu ya msingi. Zile taarifa ambazo zinatolewa kwenye maeneo hayo ya siku ya Muungano kwenye televisheni Mheshimiwa Waziri wetu tunatekeleza amekuwa akiongelea mambo haya, hata hapa Bungeni ambapo anasema ni vema tukazileta. Naomba nimhakikishie hizi *Hansard* hizi zimesheheni taarifa mbalimbali kuhusu namna ambavyo Serikali imekuwa ikitatua kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa, Mheshimiwa Najma nitakupatia hizi *Hansard* hizi na tayari nimeonesha maeneo yale ili usipate usumbufu ili uweze kuona namna ambavyo Serikali yeu inavyotoa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naendesha Bunge siendeshi mazungumzo, kama hamna mtu anayesimama, mnasimama kwa muda wenu swali limekwenda limekwisha.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Allan Joseph Kiula.

Na. 73

**Hitaji la Umeme wa REA-MKALAMA**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Wilaya ya Mkalama ina shida kubwa ya Nishati ya Umeme licha ya mpango wa *REA* II na *REA* III kuwepo nchi nzima:-

(a) Je, ni lini miradi iliyokuwa chini ya *REA* II itakamilika baada ya kutekelezwa katika Kata ya Ibega, Mwangeza na Mpambala?

(b) Je, ni lini *REA* III itaanza Mkalama hasa ikizingatiwa mikoa yote imepata wakandarasi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya *REA* II haikukamilika katika Mkoa wa Singida ikiwemo Wilaya ya Mkalama baada ya Mkandarasi aliyekuwa akitekeleza miradi hiyo kampuni ya *Spencon Services* kushindwa kukamilisha kazi hiyo kama ilivyopangwa. Utekelezaji wa miradi hiyo ulifikia asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Kampuni hiyo

kushindwa kukamilisha kazi kwa asilimia 35 iliyobaki, vifaa kwa ajili ya kazi hizo vimehifadhiwa katika Ofisi ya *TANESCO* Mkoani Singida. Vifaa hivyo vimekabidhiwa kwa Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo Mwezi Januari, 2018. Kazi za miradi zilizobaki zinatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Agosti, 2018

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi anayetekeleza miradi ya *REA* III Awamu ya kwanza katika Mkoa wa Singida ni Kampuni ya *CCCE-ETERN-HEI Consortium* ambapo mkataba wa kazi hiyo umesainiwa Mwezi Oktoba, 2017. Kazi za miradi zilianza Mwezi Oktoba, 2017 ambapo Mkandarasi amekamilisha kazi za upimaji na usanifu wa njia za kusambaza umeme pamoja na ununuzi wa vifaa. Mzunguko wa kwanza wa mradi huu Mkoani Singida unatarajwa kukamilika ifikapo Mwezi Juni, 2019, gharama ya mradi ni shilingi bilioni 41.5 wateja zaidi ya 2,997 wanatarajiwa kuunganishiwa umeme kupitia mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Kwanza kabisa namshukuru Waziri wa Wizara hiyo kwa sababu alifika na alifanya kazi mpaka saa mbili usiku na akanyeshewa na mvua alifika Ibaga. Pia Waziri aliacha maagizo ya kwamba umeme uende nyumba kwa nyumba usivuke na nguzo ziletwe zaidi ya 20. Nguzo zilizokuja ni 20 na umeme umekwishawaka lakini umetengeneza ubaguzi kwa sababu ziko taasisi za dini hazijapata, misikiti na baadhi ya wananchi. Kwa hiyo, umeme umewaka lakini bado umeleta matatizo. Je, ni lini agizo la Waziri litatekelezwa la kuongeza nguzo, umeme uwake katika maeneo hayo ili tatizo hilo liwe limekwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Mkalama wako tayari kutekeleza sera ya viwanda inayoasisiwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Je, yupo tayari baada ya Bunge kutembelea na kuwathibitishia wananchi

kuwaka kwa umeme kupitia *REA* III kwa Vijiji vya Mwanga, Kidarafa, Kikonda, Ipuli, Isanzu na maeneo mengine ya Mkalama ambayo yana uzalishaji mkubwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Allan Kiula kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia utekelezaji wa miradi hii, nimepokea shukrani za Mheshimiwa Waziri wangu kwa ziara yake. Napenda nisisitize agizo lake la Mheshimiwa Waziri la kuagiza kwamba, zifike nguzo za kutosha katika maeneo ambayo miradi Awamu ya Pili haikukamilika katika Mkoa wa Singida litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu kwamba, katika utaratibu huo mkandarasi mpya ambaye amepewa kazi ya kukamilisha miradi ambayo iliachwa na Mkandarasi wa awali *Spencon,* tumemwelekeza kwamba, maeneo yote nguzo zifike kwa wakati na ni nyingi na wananchi wote wa maeneo yale ambao wamekaa muda mrefu kusubiria umeme wa *REA* Awamu ya Pili wapatiwe huduma na pasiwepo kitongoji ambacho kimerukwa wala taasisi za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili; umekuwa utaratibu wa Wizara yetu kwa kuwa, tunatambua miradi hii inatekelezwa vijijini kufanya ziara, wilaya kwa wilaya, kata kwa kata na kijiji kwa kijiji ambako miradi inatekelezwa. Kwa hiyo, nimuahidi kwamba, ziara katika Mkoa wa Singida katika maeneo aliyoyataja ikiwemo Ipali, Mwanga na Isanzu itafanyika kama ambavyo ilivyokuwa kawaida ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel na baadaye Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REA* linahusu pia, Kata ya Soga, Kibaha Vijijini ambapo katika Kijiji cha Zogowale umeme ulifika kwa ajili ya ku-*pump* maji mpaka umefika Shule ya Waamuzi, Sekondari. Wananchi wa Kijiji cha Msufini walihamasishwa kutoa mazao na kutoa ardhi kwa ajili ya kupitisha umeme wa *REA,* huu ni mwaka wa tatu na hiyo kazi haijafanyika. Je, Wizara ina mpango gani kuhakikisha wale wananchi ambao wameshatoa mimea yao na wametoa ardhi zile nguzo za umeme zipite mpaka ufike Msufini pale Kata ya Soga na vijiji vya karibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ujiandae wapo wengi leo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani. Nimthibitishie maeneo aliyoyataja Zogowale na hapo Kijiji cha Msufini kwamba, maeneo haya yamezingatiwa katika Mradi wa *Peri Urban* ambapo kwa kweli Serikali baada ya kuona kuna maeneo ni vijiji ambavyo vimekuwa na ongezeko la makazi na vimekuwa vikubwa, Serikali ikaja na Mradi wa *Peri Urban* ambao ni nje ya *REA* Awamu ya Tatu. Kwa hiyo, nimtaarifu na nimthibitishie vijiji hivyo vipo katika mradi huu Mpya wa *Peri Urban* ambako kazi ilitangazwa na mchakato wa kumtafuta mkandarasi sasa unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la *REA* II katika vijiji vingi umeme umepita bila kugusa maeneo ya wananchi. Je, nini Kauli ya Serikali kwamba, vijiji vyote ambavyo vilipitiwa na *REA* II na haujafika kwa wananchi vinarekebishwa ili wananchi waendelee kupata umeme kuliko umeme umepita katika vijiji lakini haujawagusa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Dau, Mheshimiwa Aisharose na Mheshimiwa Oliver.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Julius kwa swali lake zuri na kwa kuwa, swali lake limejielekeza kwamba, utekelezaji wa miradi ya *REA II* kwamba kuna baadhi ya wananchi hawakufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali baada ya kuliona hilo kwamba, kuna maeneo yanatakiwa yafikiwe na miundombinu ya umeme ilikuja na mradi mpya *densification,* maana yake ujazilizi. Mradi huu unajielekeza kwenye maeneo ambako miundombinu ya umeme mkubwa imepita, lakini zipo kaya, vipo vitongoji, zipo taasisi za kijamii ambazo hazijafikiwa, kwa hiyo, huu mradi wa *densification* ambao umeanza kwa majaribio Mikoa Nane ikiwemo Mkoa wa Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Mara, Songwe, Iringa pamoja na Pwani umeonesha mafanikio na katika maeneo hayo kazi zinaendelea na wamefikia hatua sasa ya kufunga *transformer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu ambao umelenga vijiji 305 na kuunganisha wananchi elfu 53, kwa kuwa, Serikali imeona mradi huu una mafanikio mradi, nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hii *densification* sasa itaendelea na mikoa mingine. Hata sasa Mshauri Mwelekezi yuko katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutathmini na kuona namna ambavyo tutatekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtaarifu tu Bunge lako kwamba, kwa kweli, wananchi wasiwe na wasiwasi, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli itakamilisha miradi hiyo.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri sambamba na Waziri mwenye dhamana wamekuwa mara kadhaa wakijibu

maswali hapa na kuahidi kwamba, visiwa vidogo vyote nchi nzima vitapatiwa umeme wa *solar*. Sasa ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni lini umeme wa *solar* utakwenda katika Visiwa vya Jibondo, Chole, Juani na Bwejuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dau, Mbunge wa Mafia kwa swali lake zuri na tunatambua Mafia nako ni Wilaya ambayo ina visiwa vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize kwamba, hii miradi tunayosema, huu mradi kabambe wa *REA* awamu ya tatu tunaoutekeleza, vijiji ambavyo vimetamkwa 7,873 vinahusisha pia na vijiji ambavyo tunaviita *off grid.* Kwa hiyo, nimthibitishie mchakato wa kuwapata Wakandarasi wanaopeleka umeme katika maeneo ambayo si rahisi kufika miundombinu ya kawaida unaendelea. Kwa mfano, Mkuranga kuna visiwa ambavyo tulipeleka umeme kupitia *REA* hii na utaratibu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niseme siyo Mafia tu, lakini katika maeneo mbalimbali ambayo ni magumu kufikika kwa miundombinu ya kawaida, mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu ambapo vipindi vyake ni hii 2017/2018, 2018/2019 na 2019/2020 vijiji hivyo vitapatiwa. Hakuna kijiji ambacho kitaachwa kwa sababu tu ya mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Tatizo lililoko Iramba Mashariki halina tofauti na tatizo lililoko Singida Kaskazini, Manyoni Magharibi, pamoja na Jimbo la Ikungi. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwa vijiji vilivyobaki ambavyo vilikuwa katika mpango wa *REA II,* ukizingatia sasa tuko mpango wa *REA III,* ili wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika na Sera ya Viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nampongeza sana Mheshimiwa Aisharose kwa swali lake zuri. Naomba nimtaarifu tu katika maeneo ambayo ameyataja, Singida Kaskazini, Manyoni Magharibi, Ikungi, Mkandarasi ambaye anaenda kufanya kazi hizi zilizoachwa na Mkandarasi *Spencon* ameshateuliwa ambaye ni *Emek Engineering and Dynamic* na *System Company Limited.* Kwa hiyo, wako katika mchakato wa kumalizia tu masuala ya manunuzi ya kutoa *Performance Bond,* lakini kazi itaanza muda siyo mrefu na kwamba vijiji vyote ambavyo viliachwa awamu ya pili vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza. Matatizo yaliyopo Iramba Mashariki yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo Wilaya ya Ngara. Vijiji vingi vya Wilaya ya Ngara, hasa Tarafa ya Lulenge, havina umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika vijiji hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Wabunge Viti Maalum hongereni sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane nawe kuwapongeza Wabunge Viti Maalum na Wabunge wote ambao kwa kweli Bunge zima hili leo ni ushuhuda kwamba, limekuwa likifuatilia miradi ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Oliver kwa swali lake zuri ameuliza kwamba, Vijiji vya Wilaya ya Ngara ni lini vitapatiwa nishati ya umeme. Nataka nimjibu kwamba, kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa ndani ya Bunge lako na si taarifa tu kwamba labda ni porojo ni kweli, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya

Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli inatekeleza huu mradi kabambe wa kupeleka umeme katika vijiji vilivyosalia 7,873.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe pia ni shahidi. Jana wakati tunahitimisha taarifa ya Kamati yetu ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Waziri wangu wa Nishati alitoa taarifa kuwashwa kwa umeme katika vijiji 24 katika utaratibu huu wa *REA* awamu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Ngara Mkandarasi yupo anafanya kazi. Ameanza zile kazi za awali za upembuzi na kadhalika lakini kwa sasa Wakandarasi wote nchi nzima wana-*mobilise* vifaa na wengine wako *site* wanaendelea na kazi mbalimbali. Nataka nilitibitishie Bunge, ile awamu ya kwanza ambavyo ni vijiji 3,559 tumesema mpaka Juni, 2019 viwe vimekamilika halafu tunaanza safari nyingine ya kumalizia vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma ni Mikoa ambayo haijafaidika na miradi ya *REA* Awamu ya Tatu kwa sababu ya walioomba tenda kugombania tenda na kushtakiana Mahakamani. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua huo mgogoro ili wananchi wa Mikoa hiyo waweze kupata huduma ya *REA* awamu ya tatu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Kakoso kwa swali lake zuri. Nichukue fursa hii kuwapa pole na kuwaomba radhi wananchi wa Mikoa ya Kigoma na Katavi, lakini ameuliza Serikali ina mpango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimtaarifu suala hili lipo Mahakamani. Kwa kuwa, Mahakama ni chombo pekee ambacho kinatoa haki, sisi kama Serikali ya Awamu ya Tano tutasikiliza maamuzi ya Mahakama, kwa hiyo mgogoro huu utatatuliwa na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie kwa kuwa, Mamlaka ya Manunuzi *(PPRA)* hawakuwa na kipingamizi katika suala la mchakato, Wakala wetu wa Nishati Umeme Vijijini *(REA)* wameanza mchakato wa kumpata mkandarasi mpya, lakini kama yatatokea maamuzi mengine ya Mahakama tutaendelea kuyaheshimu, lakini kwa mpango ndani ya Wizara tunaamini kuanzia Machi 2018 Mkandarasi mpya atapatikana. Ahsante sana.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Mji wa Tunduma uko mpakani mwa Zambia na Tanzania na ni Mji ambao unahudumia Mataifa zaidi ya Nane yanaotumia Mpaka wa Tunduma, lakini kumekuwa na tatizo kubwa sana la umeme kukatika mara kwa mara na kusababisha usalama wa wageni pamoja na Wakazi wa Mji wa Tunduma kuwa hatarini. Je, ni lini Serikali itaweka umeme wa uhakika, kama ambavyo wenzetu wa Zambia pale ng'ambo walivyoweka umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na napenda nimshukuru Mheshimiwa Frank kwa swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme Wilaya ya Tunduma ipo katika Mkoa wa Songwe, Mkoa ambao awali ulikuwa Mkoa mmoja wa Mbeya, kwa hiyo *line* zote zinazopeleka umeme katika Mkoa mpya wa Songwe zinatokana na Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo ni wazi njia ndefu ya kupeleka umeme katika Mkoa wa Songwe inasababisha kukatikakatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kwa sasa pia ni kujenga *Sub Station* kubwa Tunduma ili kuwezesha upatikanaji wa umeme vizuri. Kwa sasa pia kuna mpango wa kujenga *line* ya *kV* 400 ambayo inaanzia maeneo ya Tunduma mpaka Mbeya inaenda mpaka Sumbawanga kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge Serikali ya Awamu ya Tano inatambua hilo tatizo, lakini mipango hii ipo na itatekelezeka na baada ya muda umeme utakuwa ume-*stabilize* katika Mkoa Mpya wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

Na. 74

**Mgongano Kati ya Katiba Mbili za Nchi**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD** aliuliza:-

Kumekuwa na mgongano mkubwa wa Katiba kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar unaosababisha ongezeko la Kero za Muungano na mgongano wa kimamlaka baina ya Serikali mbili:-

Je, ni lini Serikali ya Muungano italeta mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba ili kuondoa changamoto zilizomo ndani ya Katiba hizo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikatiba hakuna mgongano mkubwa wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar unaosababisha ongezeko kubwa la Kero za Muungano wala mgongano wa kimamlaka baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu mahsusi wa kushughulikia tafsiri ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano au utekelezaji wake inayobishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hadi sasa hakuna upande wowote baina ya Serikali hizi mbili ambao una tafsiri tofauti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano au utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa, hakuna mgongano wa Katiba kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar, Serikali haina sababu ya kuleta Mapendekezo ya Mabadiliko ya Katiba ili kuondoa changamoto hiyo ambayo haipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Hamad.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kwa ruhusa yako sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za karibuni kupitia Vyombo vya Habari tulimuona Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitoa maagizo kwa Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kikatiba, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana Mamlaka Kikatiba kutoa maagizo kwa Waziri kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika *level* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tunashuhudia Mawaziri wakizungumzia masuala mbalimbali ambayo hayahusu Muungano, yakiwemo masuala ya kilimo, masuala ya

biashara na shughuli nyingine. Je, Mheshimiwa Waziri anataka kudhihirisha sasa au anataka kutuambia kwamba, Tanzania Bara itaendelea kula kwa niaba ya Zanzibar hadi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema amesoma katika magazeti na magazeti siyo njia au sababu ya kueleza mambo hayo, ndio. Yeyote anayetumia magazeti hajui mamlaka na nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo ya Serikali yanatolewa kwa nyaraka, kwa barua. Sijawahi kupokea maagizo kwa gazeti au *sms,* napokea maagizo kwa barua au waraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo mamlaka yote ya mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi huru. Kwa hiyo, katika mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mkuu wa nchi ni mmoja tu, ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Yeye peke yake ndiye Amiri Jeshi, hakuna mtu mwingine yeyote wa kuyaamuru Majeshi ya Tanzania isipokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa sababu yeye peke yake ndiye Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar ni Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwenye heshima na hadhi ya Urais kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano yanayoihusu Zanzibar, lakini pia ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi yake hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia usawa wa wabia wa Muungano katika Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, ikiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatoka Tanzania Bara, Makamu atatoka Tanzania Zanzibar na ikiwa Rais atatoka Tanzania Zanzibar Makamu atatoka Tanzania Bara. Huo ndio usawa uliowekwa ndani ya Katiba na Ibara iko wazi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo basi, anayeiwakilisha nchi hii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mambo yote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ni wa aina yake ya kipekee na mara nyingi umewafanya watu wasielewe, ndiyo maana katika mambo yote duniani inayoonekana ni Jamhuri ya Muungano, lakini ndani ya Tanzania yenyewe kuna pande mbili, Tanzania Bara ambayo mambo yake yanasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tanzania Zanzibar ambayo mambo yake yanasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ndio maana nchi hii ina Katiba mbili, Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rukia Kassim, atafuata Mheshimiwa Khatib.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri katika Wizara ambayo ilikuwa ikishughulikia mambo ya Muungano, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye sasa hivi ni Makamu wa Rais, aliwahi kutuambia kwamba kuna kikao ambacho kilikaa kati ya pande hizi mbili, Wajumbe kutoka Zanzibar na Wajumbe kutoka Tanzania Bara waliokuwa wakizungumzia kuhusu kero ambazo zinahusu mambo ya Muungano. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia ni Wajumbe gani hao ambao walikuwa wakikutana kuzungumzia kero hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Muungano, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kumekuwa na taratibu mbalimbali za kushughulikia changamoto za Muungano hatuziiti kero ni changamoto za Muungano. Mwaka 2006 ukaanzishwa utaratibu mpya wa kikao cha Kamati ya Pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kikao kile cha Kamati ya pamoja kilikuwa kinaongozwa na Makamu wa Rais pamoja na Watendaji Wakuu wa Serikali za pande mbili. Maana ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar au Waziri Kiongozi kabla ya mabadiliko ya Katiba ya 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao kile kinajumuisha Mawaziri wote ni Mabaraza ya Mawaziri ya pande zote mbili za Muungano wetu. Kwa taarifa tu kikao cha mwisho kilikutana tarehe 13 Januari, 2017 kule Zanzibar ambapo kilijumuisha Mawaziri wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao hicho kinatanguliwa na kikao cha Makatibu Wakuu wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makatibu Wakuu wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kabla ya hapo kinatanguliwa na kikao cha wataalam wa masuala husika yatakayozungumzwa katika kikao hicho kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kikao hiki na utaratibu huu ni mkubwa, ni mzuri na umetusaidia sana kupunguza changamoto za Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Khatib, jiandae Mheshimiwa Nape.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sheria Namba 4 ya mwaka 1992 ya Jamhuri ya Muungano inampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kimikoa, Kiwilaya na kadhalika kwa kadri anavyoona. Pia Sheria Namba 2 (E) ya mwaka 1997 ya Katiba ya Zanzibar, pia inampa mamlaka Rais wa Zanzibar, kuvigawa visiwa vya Zanzibar Kimikoa, Kiwilaya kwa kadri anavyoona. Je, ni nani aliye na mamlaka zaidi juu ya Zanzibar. Je huu siyo mgongano wa Kikatiba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yeyote yenye Katiba zaidi ya moja, kama ilivyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tofauti na India ambayo ni Muungano una Katiba moja. Tanzania ni sawa sawa na Ethiopia yenye Katiba 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ujue ni jinsi gani unatafsiri na kuisoma Katiba ziko njia kuu tatu; unaangalia *Originalism, Textualism* na *Purposive.* Kwa maana hiyo haya ni mambo ambayo pia yamerejewa na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Kwa anayeangalia utaratibu wa kuziangalia Katiba mbili zinavyotekelezwa na zinapoonekana zina mgongano kazi ya kwanza ya Mahakama ni kufanya *harmonization of interpretation.* Hiyo nikusaidie nenda ukasome kesi ya *Attorney General versus* Butambala iliyoamuliwa na Mheshimiwa Jaji Samatta wa Mahakama ya Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ukitumia *purposive approach* hakuna mgongano kati ya Ibara hizo mbili. Maana yake Mamlaka ya Juu *Residuary Power* inabaki na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mamlaka ya Utekelezaji yanakuwa katika yule mtu aliyekasimiwa Madaraka yale. Kwa sababu wewe unasoma Quran nenda ujue panapokuwa na aya mbili za Quran ambazo*

*zinaonekana zina mgogoro unatumia rule of approbation. (Makofi)* **(Maneno hayo siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge*)***

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *Boss.*

**MWENYEKITI:** Mimi siyo *boss* wako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *Ok*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester kuwa na nidhamu. Waheshimiwa na hasa upande huu mnapenda kujaza maswali mkijazwa majibu hamtaki. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na mjomba wangu Profesa Kabudi na timu yake kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, itakumbukwa mwaka mmoja na zaidi uliopita niliuliza hapa na kuiomba Wizara itusaidie tufungue jengo la Mahakama ambalo tumeshalijenga, tumelikamilisha ni zuri na la kisasa, nikaahidiwa hapa kwamba Serikali itasaidia kukamilisha utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana, sasa ni mwaka na utaratibu haujakamilika. Sasa kama jambo hili limeshindikana Serikali ituambie ili tubadilishe matumizi tufanye shughuli nyingine kwenye lile jengo la Mahakama ambalo nia yetu ilikuwa ni kusogeza huduma za kimahakama kwa watu wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Nape swali hilo nilichukue nilifanyie kazi, kwa sababu amesema ni mwaka

mmoja na nusu na mimi leo ni mwezi wangu wa Kumi wa Uwaziri. Naomba anisaidie tuonane nilifuatilie ili tuone jengo hilo linatumika kwa Mahakama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mary Chatanda, kwa niaba yake Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

Na. 75

**Kupandishwa Cheo Mahakimu na Watumishi wa Mahakama**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n.y. MARY P. CHATANDA)** aliuliza:-

Mahakimu na Watumishi wa Mahakama hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu na hata wanaobahatika kupandishwa hawabadilishiwi mishahara:-

(a) Je, ni lini Serikali italifanyia kazi tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa Wanasheria wengine hupewa *house allowance:* Je, kwa nini hawa nao wasipewe kama sehemu ya motisha lakini pia wapewe *extra duty allowance?*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwapandisha vyeo Watumishi wenye sifa stahiki ni wajibu endelevu wa Serikali. Mahakama ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua kuwapandisha Mahakimu na Watumishi wa ngazi mbalimbali vyeo kuzingatia vigezo vilivyowekwa kisheria ikiwa ni pamoja na muda wa utumishi kazini, utendaji wa kazi, weledi na maadili pamoja na upatikanaji wa vibali kutoka Idara Kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, jumla ya Mahakimu na Wasaidizi wa Sheria wa Majaji 52 walipandishwa vyeo. Mwaka 2013/2014, jumla ya Watumishi 200 walipandishwa vyeo, mwaka 2014/2015, jumla ya Mahakimu na Wasaidizi wa Sheria wa Majaji 22 na Watumishi 686 walipandishwa vyeo na mwaka 2015/2016, jumla ya Mahakimu na Wasaidizi wa Sheria 59 na Watumishi 447 walipandishwa vyeo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa posho kwa watumishi wake kama sehemu ya motisha. Mahakama imeendelea kutoa motisha ya posho mbalimbali na stahili za watumishi kwa mujibu wa sheria, kulingana na uwepo au hali ya bajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Profesa mwenzangu kwa majibu mazuri na yenye msimamo. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mahakimu wengi wa Mahakama za Mwanzo wanafanya kazi katika mazingira magumu na wanapokwenda kwenye Mahakama za vijijini huwa wanatumia usafiri wa mabasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia usafiri kwa ajili ya usalama wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mahakimu wengi wanakaa katika nyumba za mtaani za kupangisha. Katika nyumba hizo huwa baadhi yao kuna watuhumiwa wanaowajua sehemu walipo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Mahakimu hao wanapata nyumba maalum kwa ajili ya usalama wao? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Jiandae Mheshimiwa Sabreena Sungura.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanafanya kazi katika maeneo magumu hasa maeneo ya vijijini yenye matatizo ya usafiri. Kutegemea hali

ya bajeti itakavyokuwa inaboreka Serikali ina mpango wa kuwapa vyombo vya usafiri, hasa Mahakimu ambao wanahudumia maeneo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba za Mahakimu Serikali pia inatambua umuhimu wa Mahakimu kuwa na nyumba na kwa kuwa sasa imeanza na mpango wa ujenzi wa Mahakama mara baada ya zoezi la ujenzi wa Mahakama litakapokuwa limefikia mahali pazuri basi Serikali ina mpango pia wa kufikiria kuanza kujenga nyumba za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hasa katika maeneo ambayo yana matatizo makubwa. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Mahakimu wengi wamekuwa wanaenda shuleni kwa kujiendeleza kwa maana ya shule ya sheria kwa vitendo *(Law School of* Tanzania*),* lakini wengi wao wameachwa wakifanya kazi kwenye Mahakama za Mwanzo, Mahakama ambazo haziendani na taaluma zao, huku katika Mahakama zetu za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi kuna upungufu wa Mahakimu. Nataka kujua ni lini Serikali sasa ita-*upgrade* wanafunzi hawa ambao wamepitia elimu ya sheria kwa vitendo ili waweze kufanya kazi kulingana na taaluma yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawapongeza sana Mahakimu wote ambao wamechukua hatua ya kujiendeleza kielimu na pia kwenda katika Shule ya Sheria kwa Vitendo au Taasisi ya Sheria kwa Vitendo. Kwa kuzingatia hilo kila mwaka Mahakama imekuwa na mpango wa kupitia wale waliopata sifa ili waweze kupandishwa madaraja kulingana na elimu walioyoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema ni sahihi kabisa kwamba lengo la Serikali sasa ni kuhakikisha pia kwamba Mahakimu wote wa Mahakama za mwanzo ambapo ndiko kwenye mashauri mengi wawe ni wale

ambao wana Shahada za Chuo Kikuu na kwa maana hiyo baada ya miaka michache ijayo Mahakama zote za Mwanzo zitakuwa na Mahakimu ambao wana Shahada ya Kwanza ya Sheria ukizingatia kuwa huko ndiko kwenye mashauri mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo kuendelea ku-*upgrade* hao ambao wamejiendeleza na tunawapongeza na tunawatia moyo waendelee kufanya hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Mbena.

Na. 76

**Huduma za Matibabu kwa Wagonjwa wa Akili**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Serikali haina utaratibu wa kuwachukua wagonjwa wa akili wanaoranda randa barabarani na mitaani na kuwapeleka kwenye hospitali za wagonjwa wa akili kupatiwa matibabu?

(b) Je, Serikali inafahamu idadi ya wagonjwa wa akili waliopo barabarani na mitaani kwenye wilaya za nchi yetu ambao wanahitaji huduma ya matibabu na inatoa maelekezo gani kwa Waganga Wakuu wa Wilaya kuhusu kuwahudumia wagonjwa hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kwanza la kulinda afya ya jamii kuanzia katika ngazi ya familia. Aidha, jamii zetu zimekuwa zikiwanyanyapaa, kuwabagua na kuwatenga wagonjwa wa akili kunakopelekea wagonjwa hawa kurandaranda mtaani. Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008 inawataka na ndugu na jamii wawaibue wagonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo vya kutolea huduma ili wapatiwe matibabu na wakishapata nafuu, huruhusiwa kwenda kukaa na familia zao na kwenye jamii wanazotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, Sehemu ya Tatu, kifungu cha sheria Namba 9 (1-3) kimeeleza wazi kuwa, Afisa Polisi, Afisa Usalama, Afisa Ustawi wa Jamii ngazi ya Wilaya pamoja na Viongozi wa Dini, Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji, wana jukumu la kubainisha mtu yeyote anayerandaranda na kutishia amani na usalama au vinginevyo kumkamata na kumfikisha katika sehemu ya magonjwa ya akili na ikithibitika taratibu za kumpatia matibabu huanza kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, Kifungu cha 11(7) na kifungu Namba 12 cha sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa idadi kamili ya wagonjwa wa akili haifahamiki nchini, inakadiriwa kwamba wagonjwa wa akili ni asilimia moja tu ya Watanzania wote. Kwa idadi ya Watanzania milioni 50 inafanya wastani wa wagonjwa laki tano. Kati ya hao asilimia 48 ndiyo wanafika katika vituo vya kutolea huduma za afya, asilimia 24 wanakwenda kwa waganga wa kienyeji na asilimia iliyobaki, wanapelekwa kwenye tiba za kiroho kwa maana Makanisani na Misikitini na wachache ndiyo wanarandaranda mitaani bila msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa maelekezo kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwahamasisha Jamii, Watendaji Kata na Serikali za Mitaa, wawaibue watu wanaoonekana kuwa na dalili za ungonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo vya afya ili wapatiwe matibabu, kwani huduma hii bila gharama yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe rai kwa jamii waache kuwanyanyapaa wagonjwa wa akili na badala yake wawafikishe kwenye vituo vya tiba mara wanapoona kuwa wana dalili za ugonjwa huo ili wapatiwe matibabu stahiki na waache kuhusisha na imani za kishirikina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbena.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na rai aliyoitoa kwa wahusika. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa tatizo hili linaonekana kuongezeka nchini; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Hospitali Maalum ya wagonjwa wa akili nchini yaani hospitali ya Mirembe inawezeshwa kiutaalam na vifaa ili kuweza kukabili tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwahakikisha kwamba hospitali zote za Wilaya pamoja na za Mikoa zinapatiwa angalau Daktari mmoja ambaye ni mtaalam wa mambo ya akili ili kuweza kutoa huduma ya karibu kwa wananchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuifanyia maboresho Hospitali ya Rufaa ya Mirembe. Hivi tunavyoongea tunakamilisha ukarabati ambao umetugharimu zaidi ya milioni 976 na itaongeza kupanua wigo sana kuiboresha hospitali yetu ili kutoa huduma nzuri na za ziada. Sambamba na hilo tumeendelea kuongeza Wataalam na kutoa mafunzo kwa wataalam walioko ili waweze kutoa huduma bora na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili alitaka kujua, je, tuna mkakati gani wa kupeleka wataalam katika ngazi za mikoa na wilaya. Katika utaratibu wetu wa

sasa ngazi ya rufaa katika masuala ya afya ya akili ni ngazi ya mikoa hili tunalifahamu na tuko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo Madaktari ili tuweze kupata Madaktari Bingwa wa Afya ya Akili kuweza kutoa huduma hizo katika ngazi ya rufaa ya Mikoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo wagonjwa wote wa akili wanaranda mitaani hata miongoni mwetu tunaweza kuwa wapo wagonjwa wa akili. Kwenye nchi za wenzetu wamefanya utafiti wa wagonjwa wa akili nchi kama Marekani, Uingereza na Australia, tafiti zao zinasema katika kila watu wanne kuna mgonjwa mmoja mwenye tatizo la akili. Je, ni lini sasa nchi yetu itamua kufanya utafiti kama huu ili kubaini tuna wagonjwa wangapi wa akili nchini? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order please.*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Tuanzie Bungeni.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Halima Bulembo kwamba, siyo wagonjwa wote wa akili wanarandaranda mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafsiri ya afya ya Shirika la Afya Duniani inasema kwamba *being health is not just merely absence of disease is mental, physical and social well-being.* Sasa siyo kwamba tu unapokuwa na mwili umeathirika ndiyo unaweza ukasema kwamba wewe umeathirika. Kwa hiyo, katika suala la afya ya akili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba si kila mtu anayerandaranda mitaani ndiyo mwenye ugonjwa wa akili, hata sisi inawezekana kama nilivyokuwa nimesema, katika

swali langu la msingi, tunakadiria kwamba asilimia moja ya Watanzania wana matatizo ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya akili naomba niendelee kutoa maelezo tuna matatizo mengi sana ya akili. Kuna sonona ambayo ni *depression, kuna schizophrenia,* kuna *mania*, *obsessive complusive disorder,* kuna mlolongo mkubwa sana ambao ni mpana sana na ambao kwa kweli hatuwezi tukafanya utafiti wa moja kwa moja kuweza kubaini katika jamii, ila tunaweza tukalifanya kwa wale ambao wanafika katika vituo vyetu vya afya na wale ambao tunaweza kuwabaini katika jamii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN J. A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba sasa hivi kuna magonjwa mengi ya akili na sasa hivi linaongezeka hili la vyuma kukaza watu wamekuwa na *stress* sana. Pamoja na kwamba Hospitali ya Mirembe ndiyo Hospitali ya Kuu na inafanyiwa maboresho na tunakubaliana kwamba magonjwa haya yamekuwa mengi na kwa maana hiyo jamii nzima ina haya magonjwa. Je, wana utaratibu gani kuhakikisha kwamba kwenye vituo huko mikoani, wilayani, wanaviboresha ili kuweza kuwasaidia hawa watu wenye matatizo ya magonjwa ya afya ya akili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Magonjwa ya akili yanasababishwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na kurithi kijenetiki lakini vilevile matumizi ya vilevi mbalimbali, changamoto na *stress* za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo Serikali inazifanya; moja ni kama tulivyosema tumeboresha huduma katika hospitali yetu ya Rufaa ya Mirembe. Sambamba na hilo tumeendelea kujenga uwezo katika hospitali zetu za Rufaa za Kanda na tumesema tutakwenda mbali zaidi na kwenda kuboresha katika hospitali zetu za Rufaa za Mikoa,

sambamba na hilo kuweka mifumo mizuri ya Rufaa kutokea ngazi ya dispensari hadi katika hospitali yetu ya Mirembe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara hiyo, Mheshimiwa Faida Bakar.

Na. 77

**Kuanzishwa Benki ya Wanawake Zanzibar**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Je, ni lini Benki ya Wanawake Tanzania itaanzisha tawi lake Zanzibar kwa madhumuni ya kuwapatia huduma za kibenki na mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuwainua kiuchumi wajasiriamali wanawake wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa mwaka 2009 kwa lengo la kuwawezesha wanawake kupata huduma za kibenki, ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu ili kujikwamua kiuchumi. Mpaka sasa, Benki imefungua matawi mawili yaliyopo jiji Da es Salaam na vituo vya kutolea mikopo na mafunzo 305 katika Mikoa Saba ya Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Mwanza, Ruvuma na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa benki ni kuhakikisha kwamba huduma zake zinawafikia wanawake waliopo katika mikoa yote ya Tanzania ikiwemo Zanzibar. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa mtaji wa benki hivyo, benki

imekuwa ikipanua huduma zake katika mikoa mbalimbali ya Tanzania kwa awamu kwa kufungua vituo vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali. Aidha, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha benki zinajiendesha kwa ufanisi na kukuza mtaji ikiwemo kufanya mabadiliko katika Benki kwa kuweka uongozi na watumishi waadilifu wenye uwezo pamoja kutafuta fedha kwa ajili ya mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Benki ya Wanawake Tanzania itaendelea kufungua vituo vya kutolea mikopo na mafunzo katika Mikoa yote ya Tanzania, ikiwemo Zanzibar kulingana na upatikanaji wa mitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika uanzishwaji wa Benki hii ya Wanawake wa Tanzania, Wabunge wengi hususan Wanawake wakati ule walichangia mtaji ama fedha katika benki hii. Hata hivyo, Wabunge hao na wengine sasa hivi siyo Wabunge tena, hawajapewa hata shukrani hata ya kutambulika tu, hata shukurani hawajapewa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wabunge hao wa wakati ule watapatiwa lini barua hiyo ya utambulisho na hata kupatiwa hisa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa uadilifu hapa hapana na kwamba wanataka kuteua tena Watendaji ama Maafisa mbalimbali ambao watakuwa waadilifu, ndiyo sasa imedhihirika kwamba, watendaji wa hii benki hawana uadilifu watendaji wake ndiyo maana ikafikia hapa ilipofikia. Je, uongozi na watumishi hao ambao si waadilifu wamechukuliwa hatua gani za kisheria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO,** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Dada yangu Mheshimiwa Faida Bakar kwa kazi nzuri sana ya kufuatilia masuala ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, sio tu Zanzibar lakini pia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la pili, hawa watumishi ambao wamekosa uadilifu wamechuliwa hatua gani. Kuanzia mwezi wa Agosti mwaka 2017 tumewapeleka katika vyombo vya usalama ikiwemo TAKUKURU na Polisi, Watumishi zaidi ya 20 akiwemo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji Magreth Chacha, kwa kukosa uaminifu na hivyo kusababisha benki kukosa hasara.

**MBUNGE FULANI:** Kupata hasara.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni benki kupata hasara, Kiswahili kidogo kimepiga chenga. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yamefanyika ya hovyo unakuta kuna *SACCOS* inakopeshwa shilingi bilioni moja, tunaifuatilia hiyo *SACCOS* haionekani hizo fedha zimeenda kwa nani. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Faida kwamba tunaamini *PCCB* na Polisi watakamilisha uchunguzi haraka na lengo letu watumishi hawa ambao hawakuwa waaminifu waweze kwenye mbele ya vyombo vya dola na kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa nataka kumthibitishia Mheshimiwa Faida kwamba, Serikali imedhamiria kuhakikisha tunapata fedha ya kukuza mtaji wa benki, tumepewa miezi sita na *BOT* na nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mkurugenzi mpya ambaye tumemwajiri amefanya kazi kubwa, niseme ingawa ni Benki ya Wanawake lakini tumeajiri Mkurugenzi mwanaume ambaye ndani ya

miezi mitano amefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba angalau hesabu za benki zinakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, lilikuwa ni suala la hisa, tunatambua mchango mkuwa sana wa Wabunge wa Bunge la Tisa ambao waliweza kununua hisa kwa ajili ya kuhakikisha mtaji wa benki unakua na moja ya jambo ambalo limekwama ni lile la *BOT* kwamba lazima tuweke vizuri suala la *shareholders,* halafu ndiyo tutawapa *certificate* zao za hisa. Kwa hiyo, suala hili pia tutalikamilisha ndani ya siku chache. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hongera pia tumeona namna ulivyokuwa unahangaika na timu ya mpira ya *Coastal Union*. Nimekuona wewe, January Makamba hongera sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Nassir na Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Benki hii imekuwa ikikiuka taratibu za kibenki kwa muda mrefu sana jambo ambalo limepelekea *BOT* kuwapa karipio kali. Je, Serikali imejiridhisha vipi kwamba ubadilishwaji wa Menejimenti ndiyo dawa au suluhisho pekee la uendeleaji mzuri wa benki hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama alivyosema katika maelezo yake ya awali Mheshimiwa Waziri, ni kwamba baada ya kufanya mapitio ndani ya Benki yetu tukaona kwamba kulikuwa kuna upungufu, hatua ambazo tulizichukua moja ni kufanya mabadiliko ya Menejimenti na kuanzia mwezi Mei, tumeweka Mkurugenzi mpya, tumepitia mfumo wa utendaji na uongozi katika benki ile na kuajiri watumishi wapya ambao ni waadilifu, sasa hivi hatua ambazo zimechukuliwa kwa haraka na imetusaidia kuhakikisha kwamba hata ule mtaji wetu umezidi kukua na hasara kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa ndani ya muda mfupi, ndani ya mwaka huu tutakuwa tumepiga hatua nzuri na benki itarudi kwenye mstari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dkt. Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwa kuwa benki hii ukiitazama na kwa namna ambavyo anaongea kwamba inaelekea kupata hasara ni kwamba benki hii inaweza ikafa na Serikali ilikwishaahidi kuinusuru kwa kuipatia mtaji. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya kuipatia mtaji ili benki hiyo iweze kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sharti ambalo tulipewa na Serikali, nikiimanisha Waziri wa Fedha ni kwamba tufanye *forensic audit* ambayo tuliifanya mwaka jana na hiyo *actually* ndiyo imetusaidia tukabaini upungufu ambao ulionekana, kwa hiyo na Waziri wa Fedha anatusikiliza. Naamini kwa sababu tumeshafanya *forensic audit,* tumeteua Bodi mpya ya Benki lakini pia tumeweka Menejimenti mpya, kwa hiyo naamini Waziri wa Fedha atatimiza ahadi ya Serikali ya kuipatia mtaji benki kama walivyoahidi mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Dkt. Kikwembe kwamba licha ya kuwa tunategemea kupata fedha kutoka Serikalini, lakini tayari tumeanza mazungumzo na Benki nyingine ambazo sitaki kuzitaja ziko tayari kufanya *partnership* na Benki ya Wanawake ili tuhakikishe kwamba huduma za Tanzania *Women Bank* zinatolewa pia katika Benki hiyo, kwa hiyo, tunakwenda vizuri na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pia iko tayari kuhakikisha inawezekeza katika Benki ya Wanawake, kwa sababu hii ni Benki ya wote na wanufaika wakubwa wa benki hii ni wanawake. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu unakwenda, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Susan Lyimo.

Na. 78

**Kuboresha Makazi ya Wazee**

**MHE. SUZAN A. LYIMO** aliuliza:-

Makazi ya Wazee yapo katika hali mbaya sana pamoja na kuhojiwa Bungeni muda mrefu sana:-

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wazee hao walioshiriki katika ukombozi wa nchi hii?

(b) Je, ni lini makazi haya pamoja na miundombinu itaboreshwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa waliotoa Wazee katika ukombozi wa nchi hii. Aidha, Wazee ni rasilimali muhimu katika ustawi na maendeleo ya nchi. Serikali inawahakikishia wazee wote nchini wakiwemo wale walioko kwenye makazi kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo huu wa Serikali umejidhihirisha kwa kuweka sehemu kwa maana ya *subsection* ya wazee katika Idara Kuu ya Ustawi wa Jamii na katika jina la Wizara, ambalo linasomeka, Wizara ya Afya,

Maendeleo ya Jamii na Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeweka mkakati kuboresha maisha ya wazee.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuboresha hali ya miundombinu ya Makazi ya Wazee kwa kufanya ukarabati kwa awamu. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa mabweni ya Wazee katika makazi ya Kolandoto – Shinyanga, imekarabati Makazi ya Wazee ya Kilima- Kagera na kujenga uzio katika makazi ya Njoro- Kilimanjaro kwa jumla ya Sh.285,120,383.25. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga fedha jumla ya Sh.568,000,000 ili kukarabati Makazi ya Wazee Ipuli – Tabora, Nunge – Dar es Salaam na Kibirizi – Kigoma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUZAN J. A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tutambue kwamba sisi sote ni Wazee watarajiwa na kwa maana hiyo tunapaswa kuweka miundombinu imara ya kuweza kusaidia wazee hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa umesema kwamba Awamu ya Tano imedhamiria kuboresha na ukaelezea Ilani ya CCM, ninavyoelewa hii ni Ilani ya Kumi na Mbili ya CCM toka tumepata Uhuru au Ilani ya Nane kuanzia mwaka 1977 lakini bado tuna tatizo kubwa sana la masuala ya wazee; Ni miujiza gani Awamu hii ya Tano ya Hapa Kazi Tu mtafanya kuhakikisha kwamba hawa wazee wanaboreshewa maslahi yao na mahitaji yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa toka mwaka 1999 Serikali iliamua kwa dhati kuwa na Sera ya Wazee, Sera ambayo ilitengenezwa mwaka 2003. Mpaka leo hakuna sheria iliyoletwa, hawajaleta Muswada hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wakati huo akiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Ummy, aliahidi na ameendelea kuahidi akaja Kigwangalla akaahidi na leo sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Ndungulile, wanaiambia nini nchi

hii. Je, ni kwa nini hawaleti Muswada ambao utatatua matatizo yote ya wazee katika nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO;** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano sasa hivi takribani inaingia mwaka wa tatu na nimeainisha katika jibu langu la msingi hatua ambazo tayari tumeanza kuzichukua katika kuboresha makazi ya wazee, sambamba na hilo kuhakikisha kwamba Wazee wale wanapata huduma ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tutenga bilioni mia nne tisini na tisa. Mpaka sasa hivi tumeshaweza kutoa milioni mia tatu hamsini na tatu elfu kwa ajili ya vyakula katika kambi hizi 17 za Wazee. Changamoto ambayo ipo na niendelee kusisitiza ni kwamba jukumu la kwanza la kutunza wazee ni la familia, baada ya hapo inafika ndugu na baada hapo ni jamii. Serikali inakuja mwishoni. Kwa hiyo, nataka niliwekee msisitizo hili ili nasi kama wanajamii tuweze kulitambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameulizia ni lini Serikali italeta sheria, Sera ambayo ameiongelea Mheshimiwa Mbunge ni ya mwaka 2003 imepitwa na wakati. Sasa hivi tuko katika mapitio mapya ya sera ili sasa tuhuishe mahitaji ya wazee kwa sasa na baada ya hapo tutaelekea kutunga sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Devotha Minja na Mheshimiwa Kiteto jiandae.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kwa Wazee kupata matibabu bure, Kambi ya Funga Funga ya Mjini Morogoro, ambayo inahudumia wazee wengi hivi sasa wanakosa huduma ya matibabu kutokana na hospitali ya Mkoa wa Morogoro kukosa madawa ya kutosha, hivi sasa wazee wale wakifika hospitali wanapewa panado na madawa mengine wanaambiwa wakanunue kwenye

*pharmacy* za nje ya hospitali. Nataka kujua, je, Sera hii ya matibabu bure kwa Wazee inatekelezeka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 imetamka wazi kwamba matibabu kwa Wazee wasiojiweza itakuwa bure na hili tunalitekeleza kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hatuna uhaba wa dawa sasa hivi, bajeti ya dawa imeongezeka sana kutoka bilioni 30 kufikia takribani bilioni 270, dawa zote za muhimu zinapatikana. Kama kuna suala mahsusi kuhusiana na Kambi hii Mheshimiwa Devotha Minja ningependa kupata maelezo ya ziada ili tuweze kuchukua hatua stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kituo cha Kulelea Wazee Bukumbi Mkoani Mwanza kinakabiliwa na changamoto ya kukosa uzio na hivyo kuhatarisha usalama wa Wazee hawa ambao tunawapenda sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka mkakati kwa ajili ya kuweka uzio katika vituo vyote hapa nchini Tanzania ambapo pia ni vichache vya hawa Wazee ili kuhakikisha usalama wa wazee hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua changamoto ya Makazi ya Wazee ya Bukumbi na makazi mengine kama ya Mwanzagi ambayo nayo yamekuwa na changamoto kama hiyo. Tunaendelea kutenga fedha kwa awamu na nimuahidi Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, katika mwaka huu wa fedha tutatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha Bukumbi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda, hivyo tunaendelea na Wizara ya Maliasili, swali linaulizwa na Mheshimiwa James Francis Mbatia, kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Selasini.

Na. 79

**Mapato Yaliyotokana na Mlima Kilimanjaro kwa Kipindi cha Miaka Kumi Iliyopita**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. JAMES F. MBATIA)** aliuliza:-

(a) Je, kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita Mlima Kilimanjaro umeliingizia Taifa mapato ya fedha kiasi gani kwa njia ya utalii?

(b) Je, ni asilimia ngapi ya mapato hayo yametumika kuweka miundombinu endelevu ya kuuhifadhi Mlima huo?

(c) Je, ni asilimia ngapi ya mapato hayo yametumika katika dhana nzima ya ujirani mwema katika kutoa huduma zinazokuza utu wa wananchi wanaozungukwa na Mlima huo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi Taifa Tanzania *(TANAPA)* ni Shirika la Umma ambalo limeanzishwa kwa Sheria Na. 482 ya mwaka 1959 na kufanyiwa marejeo na kuwa Sheria Na. 282 ya mwaka 2002. Shirika linatekeleza majukumu yake ya uhifadhi na kuendeleza utalii katika Hifadhi za Taifa 16.

Kati ya Hifadhi hizo ni hifadhi tano tu ndizo zinazokusanya mapato ya ziada yanayotumika kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11. Hifadhi hizo ni Serengeti, Mlima Kilimanjaro, Tarangire, Ziwa Manyara na Arusha. Mapato yaliyotokana na Mlima Kilimanjaro na fedha zilizotumika kuweka maendeleo endelevu ya kuhifadhi mlima na kiasi kilichotumika katika dhana ya ujirani mwema kwa wananchi wanaozunguka mlima huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mapato ya Hifadhi ya Kilimanjaro katika kipindi cha miaka kumi, yaani kuanzia mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2016/2017 ilikuwa ni shilingi bilioni 471.5.

(b) Fedha zilizotumika kutekeleza majukumu ya uhifadhi ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu ya kuendeleza mlima ni shillingi bilioni 67.5 ambazo kati ya hizo shilingi bilioni 20.89 zilitumika kwa maendeleo na shilingi bilioni 46.6 zilitumika katika uendeshaji wa hifadhi.

(c) Fedha zilizotumika katika kuendeleza miradi ya kijamii katika vijiji vilivyo jirani na Hifadhi ya Kilimanjaro ni shilingi bilioni 2.28.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu ya swali hili na niombe kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyakati ambazo mlima Kilimanjaro unapata ajali ya moto na kwa sababu hiyo wananchi wanaotokana na halmashauri zinazozunguka mlima wanafanya kazi ya kuzima moto huo, hususan wananchi wa Wilaya ya Rombo na kikubwa wanachoambulia ni nusu mkate. Sasa kwa kuwa kuna utaratibu wa kutoa mrabaha kwa halmashauri ambazo zina madini; je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa mapato yanayotokana na mlima Kilimanjaro kiasi fulani kitolewa kama mrabaha kwa halmashauri zinazozunguka

mlima ili iwe kama *incentive* na kuwafanya wananchi hao waweze kuulinda mlima wakati majanga ya moto yanapotokea? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna vijana wapagazi *(porters)* ambao wanabeba chakula, maji, gesi na kadhalika kwa ajili ya kuwasaidia watalii kupanda mlima. Vijana hawa wana malalamiko makubwa sana kwamba malipo yao ni ya kinyonyaji. Je, Serikali iko tayari kuchunguza malalamiko haya na kuwasaidia hawa vijana ili waweze kupata stahiki zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakishiriki katika kuzima moto pale unapojitokeza katika hifadhi ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mrabaha hasa kwenye Halmashauri zile ambazo zinazozunguka mlima Kilimanjaro, naomba niseme kwamba hilo tutalifanyia kazi, tutangalia kama hilo linaweza likafanyiwa kazi. Kwa utaratibu uliopo hivi sasa ni kwamba katika bajeti nzima ya hifadhi za Taifa *(TANAPA)* asilimia tano mpaka saba huwa zinatengwa kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali inayoibuliwa na wananchi walioko katika maeneo yaliyo jirani na hifadhi mbalimbali. Kwa hiyo, katika hili ambalo amelisema basi tutalifanyia kazi tuone kama nalo linaweza likafanyiwa kama tulivyofanya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la kuhusu wapagazi, kama atakumbuka hapo tulipokuwa tunajibu swali lililokuwa linahusu maslahi wapagazi na waongoza utalii tulisema; katika kikao kilichofanyika Arusha kati Serikali wapagazi na vyama vyao pamoja; katika utatu huo tulikubaliana kabisa viwango ambavyo vimependekezwa na ambavyo tulifikia muafaka. Tukaagiza kwamba sasa wale

wote, mashirika yote, taasisi zote, kampuni zote za kitalii lazima ziingie mikataba na hao wapagazi ili angalau kuhakikisha kwamba kwa siku kila mmoja anapata fedha zisizopungua dola elfu kumi kwa siku. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa na kinachoingiza pesa za kigeni kwa kiwango kikubwa kama kilivyotajwa. Je, ni lini sasa Serikali itaboresha miundombinu ya upandwaji wa milima huo kama inavyofanyika katika nchi zingine za *Brazil*, kule *Rio De Janeiro* na *Cape Town, South Africa* kwa kutumia *cable* ili kuongeza mapato zaidi kupitia mlima huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana, lile swali lililohusu *REA* limetuchukulia muda mwingi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Mahawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini tutaboresha miundombinu, tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali za kuboresha miundombinu katika hifadhi zetu. Hili alilolipendekeza kuangalia uwezekano wa kuweka labda vitu kama *cable car* na vitu vinginevyo basi tutaliangalia kwa kadri bajeti itakavyoruhusu pale ambapo tunaweza kutekeleza ili liweze kuwavutia watalii wengi zaisi na kuweza kufanikisha hili jambo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, Wizara hiyo hiyo, Swali linaulizwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

Na. 80

**Mgogoro wa Ardhi ya TANAPA na Wananchi**

**MHE. ORAN M. NJENZA** aliuliza:-

Kuna mgogoro wa muda mrefu wa ardhi kati ya *TANAPA* na Wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Uleuje na wananchi walikuwa tayari kuachia ardhi yao ili upanuzi wa Hifadhi ya *TANAPA* lakini Serikali imeshindwa kuwalipa wananchi hao fidia:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya tathmini mpya ya fidia kwa wananchi wa Ilungu, Igoma na Uleuje?

(b) Kama Serikali imeshindwa kulipa fidia; je, ni lini itarudisha eneo hilo kwa wananchi wa Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Oran Manase Njenza, Bunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa Kitulo ilianzishwa mwaka 2005 ili kuhifadhi vyanzo vya maji kwa ajili ya Bonde la Ziwa Nyasa, Bonde la Usangu na Mto Ruaha Mkuu ili kuhifadhi *baioanuai* ya aina za mimea adimu zikiwemo Chitanda. Hifadhi ya Taifa Kitulo imejumuisha maeneo yaliyokuwa yakimilikiwa na taasisi za Serikali. Maeneo hayo yanajumuisha Msitu wa *Livingstone*, Msitu wa Numbe na eneo lililokuwa shamba la mifugo *(Diary Farming Company-DAFCO).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini iliyofanywa na Mkoa wa Mbeya kufuatia malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Kikondo, Kata ya Ilungu ilibaini kuwa kuna baadhi ya wananchi ambao taarifa ziinaonesha kuwa hawakulipwa fidia mwaka 1965 wakati shamba la *DAFCO* lilikuwa linaanzishwa. Serikali inakusudia kufanya uthamini kwa

wananchi mwezi Februari mwaka 2018 ambao hawakulipwa fidia mwaka 1965. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mbeya itahakikisha kuwa fidia inalipwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJENZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, napenda vile vile kushukuru majibu ya Serikali na pia nipende kutambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya mkoa na *TANAPA* vile vile kwa kushiriki katika ujenzi wa kituo cha afya pale Ilungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwa vile hii fidia ni ya muda mrefu 1965; je, Serikali inathibitisha kuwa hii fidia itakayolipwa mwaka huu itazingatia thamani na sheria zilizopo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile Mji wa Mdogo wa Igoma unakua kwa haraka sana na pale kuna eneo la hifadhi ambalo limezungukwa na mji; je, Serikali itakuwa tayari kuliachia lile ili liweze kutumiwa na shule pamoja na huduma zingine za kijamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu hilo swali, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya katika kufuatilia fidia hii ya wananchi wake na amefuatilia kwa muda mrefu na taarifa ziko nyingi sana na wananchi wajue kwamba Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi nzuri sana hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia, kama nilivyosema kwenye swali la msingi tunafanya tathimini upya mwezi Februari mwaka huu. Kwa hiyo, baada ya tathimini hiyo ni wazi kabisa kwamba tutabaini kwamba mahitaji au

fidia inayotakiwa italingana na hali halisi ya leo na si ya mwaka 1965. Kwa hiyo wananchi watapata nafasi nzuri kabisa ya kupata fidia inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi yanayohusu hapa kujenga makao makuu kutokana na ongezeko la watu. Naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maeneo mengi yameleta maombi ya namna hiyo yanayofanana, lakini hili ombi ambalo amelileta Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie tu nitachukua jukumu la kwenda kwanza kukutana na wananchi wenyewe ili niangalie hilo eneo kama kweli linafaa kutolewa kwa ajili ya huduma za jamii. Hata hivyo, mkazo zaidi utaendelea kusisitizwa kwamba hifadhi ni muhimu kuliko vitu vingine vyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Janet Mbene.

Na. 81

**Kuendeleza Maeneo ya Uwekezaji**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Serikali imetenga maeneo kadhaa kwa ajili ya uwekezaji nchi nzima:-

Je, ni lini Serikali itatafuta fedha za kutosha kuweka miundombinu muhimu katika maeneo haya ili kuvutia uwekezaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Mbene, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *EPZA* na halmashauri za wilaya na mikoa imetenga maeneo ya uwekezaji sehemu mbalimbali nchini. Kama alivyosema Mheshimiwa Janet Mbene maeneo ya namna hii ni muhimu katika kuvutia uwekezaji katika sekta ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendelezaji wa maeneo hayo kwa kuweka miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi, Serikali imebuni mpango wa kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza maeneo hayo kama ilivyofanyika kwa Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo. Kwa maeneo yatakayokuwa na uhitaji wa haraka wa kuendelezwa kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina tutayatengea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa viwanda vidogo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya kujenga miundombinu ya *SIDO* kwenye mikoa mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kweli nasikitika hili jibu ni la juu juu mno. Hii Wizara imeshafanya mambo mengi tunayoyajua, ningetegemea hapa ingekuwa ndio wakati Serikali ingetueleza ambayo wameshafanya na yale ambayo bado. Hata hivyo, tumeletewa taarifa ambayo mwananchi wa kawaida anayesikiliza sasa hivi wala haelewi kama Serikali imefanya chochote katika masuala ya viwanda katika maeneo maalum wakati nafahamu kuwa yameshafanyika mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi baada ya kusema hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Sasa katika hayo maeneo ambayo yametengwa ambayo nayafahamu kuna *industrial parks*, *stand alones* na kuna maeneo mengine ambayo ni ya Wilayani; ni mangapi ambayo mpaka sasa hivi yameshawekewa hiyo miundombinu saidizi na miundombinu

wezeshi na kiasi gani ambacho tayari kinazalishwa na mapato kiasi gani nchi inapata na ajira kiasi gani kimeshazalishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuzingatia kuwa katika changamoto ambazo zinakwamisha na ambazo zimekuwa zikikwamisha kuendelezwa maeneo haya nyingi ziko katika uwezo wetu kuzitekeleza. Hiyo miundombinu inayozungumzwa ni kitu ambacho kiko kwenye uwezo wetu tukiamua. Haya masuala ya utata kati ya *special economic zones* na *economic processing zones* yanaweza kutatuliwa. Sasa ni kwa nini basi hatujakamilisha japo tuwe tuna maeneo mawili kila mwaka yanayofanyiwa kazi? Maana yameshatengwa na wananchi wamezuiwa kuyaendeleza lakini sisi hatujayafanyia chochote zaidi ya miaka 10 sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru pia kwa majibu na maelezo ya Mheshimiwa Mbene. Kimsingi majibu yaliyoletwa ni majibu sahihi isipokuwa kwa maswali yake ya nyongeza naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; katika suala la uendelezaji wa maeneo hayo, ninavyofahamu ni kwamba katika uendelezaji wa miundombinu kuna miundombinu ambayo ni *direct* inayotokana na uwekezaji wa moja kwa moja katika eneo la *economic processing zone* au (*SEZ);* lakini pia kuna maeneo wezeshi yanayofanywa na sekta nyingine kama nishati pamoja na maji na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, kwa mfano, ukisikiliza katika michango ya jana kuna uwezeshaji mkubwa uliofanyika na Serikali kwa ajili ya bomba la gesi ambalo mpaka sasa limezunguzwa kwamba itatumika takribani asilimia sita; lakini bomba hilo itakuwa tayari kuwekeza viwanda 190 vinavyotarajiwa katika *Bagamoyo*

*Economic Zone* na maeneo mengine. Kwa hiyo, ni tayari Serikali imeshawekeza fedha nyingi katika miundombinu ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukirudi pia Benjamini Mkapa pale kuna miundombinu ambayo imewekezwa na Serikali lakini pia na wadau binafsi jumla yake ni takribani bilioni thelathini na saba na ina uwezo kuajiri watu moja kwa moja 5,000 ambao wanazalisha ajira zisizo rasmi zaidi ya 12,500. Hiyo yote ni uwekezaji ambao umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa upande wa *Kigoma economic processing zone,* pale tumepata mwekezaji binafsi ambaye yeye amewekeza umeme wa sola wa takribani *mega watt* 5 ambao uko tayari inangojewa tu kuunganishwa kwa upande wa TANESCO. Kwa hiyo kimsingi Serikali imekuwa ikiwekeza na inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande maeneo ambayo yalitengwa katika mikoa Serikali imelipa fidia maeneo mbalimbali ikiwemo Kurasini ambayo tumelipa takribani shilingi bilioni mia moja na tatu na maeneo mengine kama Songea na Mara na mengine. Kimsingi tunachozungumza sasa hivi ni kwamba badala ya kuchukua fedha yoyote ya Serikali kuifungia katika kuilipia maeneo na wakati mwingine hao wawekezaji wanakuwa hawajajitokeza. Kwa hiyo tunachofanya sasa ni kuwashirikisha wawekezaji wenyewe ili yule anayehitaji eneo maalum basi aweze kusaidia katika kulipa fidia na kulitumia kwa malengo ambayo yanakuwa yamekusudiwa kwa *win win stuation* kwa upande wa Tanzania na huyo mwekezaji wetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha; tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani umeruka swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani swali namba 82 halijasomwa.

**MWENYEKITI:** Sawa, swali namba 82 la Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 82

**Kukamilisha Ujenzi wa Masoko ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kukamilisha ujenzi wa masoko ya kimataifa ya Nkwenda na Murongo ambayo yamekaa miaka mingi bila kukamilishwa wakati yangekamilishwa yangewapatia soko la uhakika wananchi wa Kyerwa na Mkoa mzima wa Kagera?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masoko ya Kimkakati ya Kimataifa ya Nkwenda na Murongo ni miongoni mwa masoko matano yaliyokuwa yanajengwa kama sehemu ya utekelezaji wa *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* kupitia mradi wa uwekezaji katika sekta ya kilimo ngazi ya Wilaya *(District Agriculture Sector Investment Project – DASIP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa masoko hayo mpaka sasa umekamilika kwa hatua za awali. Katika soko la Nkwenda ujenzi umekamilika kwa asilimia 25 hadi 30 na soko la Murongo ujenzi umekamilika kwa asilimia 40 hadi 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa masoko haya ulisimama baada ya mradi wa *DASIP* kufikia ukomo wake mwaka 2013 na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* iliyokuwa ikifadhili ujenzi huo kusitisha utoaji wa fedha kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha mradi wa ujenzi wa masoko hayo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inayoratibu *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo katika bajeti ya mwaka wa 2017/2018, imetenga Sh. 385,914,778 kwa soko la Nkwenda na Sh.561,232,364 kwa soko la Murongo. Ujenzi wa masoko hayo utaendelea pindi fedha hizo zitakapotolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu miradi hii ni ya muda mrefu na miundombinu yake inazidi kuharibika kama vile vifaa ambayo viko pale kuna kama nondo na vifaa vingine vinazidi kuharibika, kwa sababu Serikali imeshatenga pesa kwenye bajeti ya 2017/2018, kwa nini Serikali isichukue hatua za dharura kupeleka pesa hii ili iweze kukamilisha miradi hii kwa sababu ya umuhimu wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale kwenye miradi ile kuna walinzi ambao walikuwa wamewekwa pale, walinzi hao wametelekezwa muda mrefu na imefikia wakati hao walinzi wameondoka, pale hakuna walinzi. Serikali haioni pasipokuwa na walinzi inaweza ikasababisha vifaa vingine kuibiwa na kuharibu miundombinu ya mahali pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amezungumza kwamba miradi hii ni ya muda mrefu, lakini ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, nimuahidi tu kwamba nitafuatilia kuona kwamba kama tunaweza tukapata fedha hizo zilizotengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na walinzi, niiombe Halmashauri ya Kyerwa kuhakikisha kwamba hata kwa kutumia wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ni vema kuendelea kulinda miundombinu hii ambayo tayari ipo wakati tukiendelea kupata fedha kwa ajli ya kukamilisha miradi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekwenda; sasa tutakwenda Wizara ya Maji, Mheshimwa Shabani Shekilindi

Na. 83

**Tatizo la Maji Safi na Salama – Jimbo la Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Jimbo la Lushoto linakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji hususan katika maeneo ya Ubiri, Makanya, Kwemashai, Gare, Mlola, Mbwei, Malibwi na Kilole:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi hao majisafi na salama ili waondokane na adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omar Shekilindi, maarufu kama Bosnia, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Vijij vya Ubiri, Makanya, Kwemashai, Gare, Mlola, Mbwei, Malibwi na Kilole. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi katika vijiji hivyo ambapo kwa mradi wa Mlola ujenzi wake umefika 85%; miradi ya maji katika maeneo ya Kwemashai na Ngulu imefikia 75%; wakati mradi wa maji Malibwi umekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Ubiri ulijengwa Mwaka 1972 ili kuwahudumia wakazi 2,013. Hata hivyo kutokana na ongezeko la wakazi huduma ya maji inayotolewa kwa sasa haitoshelezi mahitaji. Hivyo Halmashauri ina mpango wa kutoa maji kutoka Kijiji cha Ngulu pindi mradi wa kijiji hicho utakapokuwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Gare ambao ulijengwa na Wamisionari Mwaka 1978 haukidhi mahitaji ya sasa, hivyo Halmashauri imeuweka kwenye mpango wa kuufanyia upanuzi na usanifu wa kina ili kuuongezea uwezo na idadi ya vituo vya kuchotea maji. Aidha, miradi katika Vijiji vya Makanya, Kilole na Mbwei imewekwa katika mpango wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuwaondolea adha ya upatikanaji wa maji wananchi wa Halmashauri ya Lushoto, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.66 kwa ajili ya Halmashauri hiyo kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa pamoja na kuanzisha miradi mipya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi iliniweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pia nishukuru kwa kutupatia bilioni 1.66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji katika Mji Mdogo wa Lushoto ilipatiwa fedha kwa ajili ya kujenga tenki la lita za ujazo 650,000 na banio katika eneo la Kindoi, lakini mpaka sasa mradi ule bado haujaanza. Nilifuatilia kwa Mkurugenzi wa Tanga *UWASA* alisema taratibu tushazikamilisha hivyo tunasubiri kibali kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wamesubiri mradi ule haujaanza kwa muda mrefu sasa,

naamini wananchi wananisikia na kuniona. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri kibali hicho kitapatikana ili Mkandarasi aanze kazi mara moja, kwani mradi ule ukikamilika utaendelea kuhudumia Kata za jirani ambayo ni Ngulu na Ubiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina vyanzo vingi vya maji pamoja na mito inayotitririka maji kutoka milimani. Je, Serikali ipo tayari kwa sasa kuhakikisha inatumia vyanzo hivyo pamoja na maji yanayotiririka kutoka milimani kujenga mabwawa na kutumia vyanzo hivyo ili kuwapatia wananchi wa Lushoto maji safi na salama na hasa kutimiza dhana nzima ya kumtua mama ndoo kichwani; hasa kina mama wa Kwekanga, Kwemakame, Mkuzi, Mazashai, Mazumbai, Ngwelo, Miegeo, Handei, Masange, Kwemashai, Gare pamoja na Magamba Coast? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Shekilindi kwa jinsi anavyofuatilia huduma ya maji katika Jimbo lake; na kwamba nishakwenda Lushoto, mazingira ya Lushoto ni mazuri, ni milima milima upo uwezekano mkubwa kabisa kuwapatia wananchi wa Lushoto maji safi na salama kwa zaidi ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la Mbunge linahusu kibali, nitahakikisha kabla ya Bunge hili kukamilika kibali kitatolewa; kwa hiyo naomba sana tuwasiliane ili kibali kitolewe na utekelezaji wa mradi uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ni kweli kuna vyanzo vingi vya maji Lushoto na tutahakikisha kwamba tunaweka mabanio ya kutosha kule milimani na kuweka mabomba kwa sababu maji ni ya mserereko hayana gharama kubwa na pale itakapobidi tutajenga hadi mabwawa ili maji yawe ya kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, kawaida ya maswali mwisho ni saa 4.30. Kiti kinatumia tu madaraka kuongeza kwa sababu ya *burning issues* ambazo Wabunge mnazo, lakini kwenda zaidi ya hapo inakuwa ni kinyume cha taratibu za Kibunge, kwa hiyo tuvumiliane tu.

Sasa ni kipindi cha kutambulisha wageni. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni wawili wa Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; ni Dokta Wellington Chibebe, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki, *thank you very much, welcome to the Parliament*. Ndg. Anthony Rutabanzibwa Afisa Mratibu Mwandamizi wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO).* Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe Mbunge, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambao ni Viongozi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Profesa Kitila Mkumbo. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 16 wa Mheshimiwa Felister A. Bura Mbunge ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni Dodoma na kwenye Bunge. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba Mbunge, ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mwalimu Emmanuel Shemdoe. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Allan Joseph Kiula Mbunge, ambao ni Diwani Kata ya Kihonda, Mheshimiwa

Hamis Nkungu kutoka Jimbo la Iramba Mashariki, Wilayani Mkalama, Mkoa wa Singida, amefuatana na msaidizi wake. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King amboa ni Walimu wa *St. John's University* ya Mkoani Dodoma wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo Profesa Timothy Simalonga, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni Viongozi kutoka RK Redio iliyopo Ngara Mkoa wa Kagera, karibuni Bungeni.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hamoud Jumaa ambao ni Viongozi wa Chama cha Wafugaji Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama hicho Ndg. Esther Lamani Moreto. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 100 wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Dodoma ambao wamekuja kutembelea Bunge kwa mafunzo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia kwenye *Pigeonhole* zenu umewekwa Waraka wa Elimu Na. 3 ya Mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa Elimu Msingi bila malipo. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuchukua Nyaraka hizo muhimu.

Nina tangazo lingine, naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake *TWPG* kuwa leo tarehe 6 Februari, 2018 kutakuwa na Semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa mara tu baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge kuanzia saa 7.00 mchana. Naomba Wabunge ambao si wanawake msiende. *(Kicheko)*

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wenye Imani ya Kikristo; Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuhudhuria Ibada katika Ukumbi wa Pius

Msekwa *Chapel* ghorofa ya pili leo tarehe 6 Februari, 2018 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, Mtumishi wa Mungu Mwalimu Emmanuel Shemdoe atahudumu katika Ibada hiyo pamoja na kwaya ya Safina kutoka Kanisa la *Anglican* Dodoma. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka tu niseme kitu kingine Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya Wabunge wanapenda kuleta barua kwenye kiti na katika barua hizi hawaandiki majina yao, lakini wanaandika lugha zisizo za Kibunge. Kitu ambacho mnashindwa kuelewa huwa mnaleta barua mnaandika lugha si za Kibunge, lakini huwa mnaleta barua kuomba maombi yenu na hapa akikaa Spika, akikaa Naibu Spika na sisi Wenyeviti tuna mafunzo ya *photographic memory*. Kwa hiyo tunajua nani anaandika hizi barua. *(Makofi)*

Nataka niwaase tu, tuvumiliane, tuwe na ustaarabu, hili ni Bunge na sisi wote ni Wabunge humu ndani. Mkileta mambo ambayo hayana maana, matokeo yake ni kuumizana na si jambo jema, wala si jambo zuri. Sisi tunakuwa na *high tolerance* hapa, sababu tunavumilia na nyinyi mvumilie.

Tukitumia hizi Kanuni kila saa, matokeo yake ni watu kuumizana na si jambo jema. Kwa hiyo naomba mjaribu ku-*refine* muwe Wabunge na mfuate maadili ya Kibunge. Hivi vibarua vipo vingi vinaletwa na tunawajua, sababu tumefundishwa kuwajua. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Dkt. Suleiman, Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Khatib. Haya, twende kazini. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni

ya 68(7) juu ya kukiukwa kwa Kanuni ya 64(1) ambapo anatakiwa Mbunge au Waziri, hatasema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Waziri wa Katiba na Sheria, alilipotosha Bunge na amesema uongo Bungeni, pale ambapo Mheshimiwa Waziri akieleza kwamba katika maelezo yake, pale ambapo kuna mgongano wa aya mbili za *Qur-an.* Mheshimiwa Waziri ni Waziri wa Katiba na Sheria, naomba Mwongozo wako, kwa sababu *Qur-an* haijui vizuri na haielewi kabisa. Ukienda kwenye Sura ya Pili, *Suratul-baqarah* inasema *Bismillah-rrahmani-rrahim "Dhalikal-kitab laraibafihi huddanlil-muttaqiin"* Kitabu hicho hakina shaka, kimekamilika hicho hakina masahihisho ya aina yoyote.

Ukienda kwenye Sura ya Nne *Annisaa,* Aya ya 82 inaeleza waziwazi Mwenyezi Mungu amesema kama *Qur-an* inatoa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi mngaliona ni tofauti yaani migongano. Kwa hiyo inaonesha kuwa hakuna mgongano katika *Qur-an,* hakuna tofauti ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako juu ya Waziri wa Katiba na Sheria, aliyelipotosha Bunge na kudhalilisha watu wengine. Naomba Mwongozo wako, aombe radhi na kauli hii aifute kwa sababu amesema uongo Bungeni leo mchana kweupe. Nashukuru sana na naomba Mwongozo wako

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba Mwongozo kwa Ibara hiyo ya 68(7) kuhusiana na suala lililojitokeza wakati swali langu namba 81 lilivyokuwa likijibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lile swali halikujibiwa vizuri, bahati nzuri niliuliza maswali ya nyongeza ambayo yalimwezesha Waziri sasa kutoa zile taarifa tunazohitaji. Vile

vile, hata maswali ya nyongeza hayakuruhusiwa. Hili ni suala lilikuwa ni muhimu sana, nchi hii tunaenda kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangependa sana kujua Serikali inafanya nini katika maeneo haya. Mimi Mbunge wa Jimbo nasimama kuuliza swali, limejibiwa hovyo hovyo lakini bado hata ya nyongeza yamezuiwa. Hata hivyo, wakati huo huo maswali mengine yanaulizwa hapa yanarudiwa, yanarudiwa na bado yanakuwa *entertained* naomba kiti chako kiwe kinatoa muda wa kutosha kwa kila swali kujibiwa sawa bin sawa ili kila mtu apate kujibiwa vizuri na wananchi wapate taarifa wanazohitaji. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dokta Suleiman.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah-rrahmani-rrahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nasimama kwa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7), lakini kabla sijaendelea nasikitika kwamba mwenye kupewa habari hii baada ya kulikoroga kakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Kabudi anajibu swali la Mheshimiwa Khatib, katuchanganya sana aliposema kwamba iwapo aya mbili za *Qur-an* zitagongana. Je, anao ushahidi kwamba ziko aya mbili katika *Qur-an* ambazo zimegongana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waislamu wenyewe tunakatazwa kata kata kusema uongo, kusema jambo lolote ambalo hatulijui. Ukienda katika *Suratul-Israa* ambayo ni Sura ya 17 aya ya 36 Mwenyezi Mungu anasema: *"Walataqfu malaysalaka bihi-ilmu, inna-ssamaa, walbaswara, walfuada, qullu ulaika kana anhumasu-ula"* na usiseme chochote ambacho hukijui, huna elimu nacho, kwa sababu masikio, macho na nyoyo basi yote hayo yataulizwa siku ya kiama, kwa nini ukasema uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, naomba Mwongozo wako ili nijue je, anaruhusiwa Waziri, Mbunge au Mtu yeyote kupotosha dini za wengine? Ikiwa Mheshimiwa, hairuhusiwi naomba kumuuliza, je, yuko tayari kuomba radhi Waislamu wote kwa ujumla dunia nzima kwa sababu kawapotosha, halafu kufuta maneno yake na kauli yake ile ya upotovu aliyoitoa hapa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) nikiomba Mwongozo wako juu ya swali namba 77, Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu alipokuwa akijibu swali lile, aliloulizwa ni lini wanahisa wa benki ya Wanawake watapewa *Share Certificates* zao. Swali lile lilijibiwa kisiasa akasema kuna mambo anarekebisha rekebisha watawa *Share Certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni karibu miaka nane wanahisa wa benki ya wanawake hawajapewa vyeti vyao vya kununua hisa kinyume na sheria ya makampuni, kwenye *table A* ambayo *regulation eight* inalazimisha mwana hisa baada ya kununua hisa ndani ya miezi miwili anapaswa kupewa *share certificate*. Sasa ni miaka nane hawajapewa *share certificate,* Mheshimiwa Waziri anajua ni kinyume na sheria tuliyotunga humu humu Bungeni, lakini kama hiyo haitoshi benki inaweza kutozwa faini na afisa yoyote ambaye anahusika kama inavyoelezwa katika kifungu namba 82 cha sheria hiyo hiyo ya makampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu naamini swali hili halikujibiwa vizuri na wana hisa hawa wananyimwa haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI**: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti nami nasimama kwa kanuni ya 68(7), na kwa kuokoa muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingelazimika tena kuomba mwongozo huu kwa sababu unafanana na uliiombwa na wenzangu. Hata hivyo ninalazimika kwa sababu moja tu, nahofia kuja kutumika ile *technical knockout* ya kuwatoa kama wao si wauliza swali husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, narudia pale kwamba Mheshimiwa Kabudi, alipojibu swali langu alini-*point* kwamba hata mimi najua pale aya mbili za *Qur -an* zinapogongana. Jambo ambalo nikiwa kama Muislamu kukiri hilo nimeukosea uislamu na nimemkosea Mungu Mtakatifu na nimeritadi na nitajitoa katika uislamu wangu. Hivyo kwanza nakana kwamba hata mimi sijui na siwezi kujua kwa sababu nakubaliana na kauli ya Mwenyezi Mungu katika *suratul-baqarah* aya ya pili aliyosema, hakika *Qur - an* ni kitabu kitakatifu na kisicho shaka ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo toka baada ya suala lile limekuwa nikipata *message* nyingi za Waislamu; na kwa kuwa najua ulimi hauna mfupa na heri kujikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi. Ninachoomba kwa kuweka sawa jambo hili ambalo Waislamu wengi wanasikitika sana, juu ya masuala yale ambayo ameyasema Mheshimiwa Kabudi, naomba mwongozo wako kwa sababu *hansard* imeandika, Je, yuko tayari sasa kusimama hapa akaeleza wazi kwamba hana ujuzi juu ya *Qu-ran* na hakupaswa kuingilia masuala ya kuongelea *Qu-ran (makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa nia njema ili Watanzania na Waislamu wote waondokane na mkanganyiko uliotolewa na Profesa huyu wa sheria na si Profesa wa *Qur - an.* Ahsante sana *(makofi).*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru, miongozo tulikuwa nayo mitano, mitatu ilikuwa na hoja moja; Mheshimiwa Makamba alikuwa na hoja ya hisa na Mheshimiwa Janet Mbene alisema swali lake halikujibiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mbene mwongozo wangu, tumia kanuni tu ya kuomba tu swali lako lirudiwe tena na mimi natoa taarifa kwako utaratibu wa kutokuridhika na swali lako basi kwenye kanuni ya nafikiri 43 na 46 kwa hiyo baadaye nitakuongoza vizuri.

Mheshimiwa Makamba nitamwomba Waziri mhusika aliyejibu kuhusu hisa za hii benki atolee majibu.

Pia nitamwomba Mheshimiwa Kabudi na yeye atoe majibu kuhusu hayo yaliyosemwa. Aliyejibu kuhusu hisa kwa bahati mbaya hayupo basi Mheshimiwa Kabudi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nimerudi hima ndani ya Bunge ili niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, naheshimu kwa dhati dini zote ikiwa pia ni dini ya Kiislamu ambayo mimi ninaye mjomba Muislamu, Shehe Mustapha Mwendi, Imamu kabisa, na namshukuru. Pia ninayo heshima kubwa sana kwa dini ya kiislamu, mwaka 1961 na 1962 nimesoma Madrasa ya Mzee Idd Mulewa pale Kilimatinde kwa Waibadhi *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima sana kwa Waislamu kwa sababu mke wangu ninayempenda sana Amina, chimbuko lake ni imani hiyo. Nauheshimu ukristo nauheshimu uhindu na nawaheshimu pia wale ambao Mungu amewanyima daraja la kujua yupo mpaka wanapoyakaribia mauti. Kwa hiyo, mimi ni mtu wa mwisho kwa namna yoyote ile kuibeza, kuitweza, kuikejeli, kuidhihaki imani yoyote ya mtu yule ikiwa ni pamoja na mjomba wangu na ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najibu lile swali ambalo kwa bahati mbaya sana halikutoa nafasi ya kupata majibu kwa sababu ya yowe na zogo, yowe na zogo ndiyo maana neno halikusikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokusudia kusema kwamba wako watu mwenye upungufu wa elimu ya dini na nilikuwa hapa nina mifano siyo tu kwenye *Qur-an,* lakini hata kwenye Biblia. Wako watu ambao wamefunzwa kutafsiri *Qur-an* na ziko njia ya kuitafsiri *Qur-an* na kitabu hicho hakina migongano na wako watu waliofundishwa ndio maana nilitumia neno iwapo, wapo watu wanaodhani sikusema ina migongano, na kama nilisema hivyo, ngoja...*(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Na kama nilisema hivyo, nasema hivi naomba mnisikilize; na kama nilisema hivyo....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Na kama nilisema hivyo naomba aya hiyo ifutwe kwenye *Hansard (makofi).*

Kama nilisema hivyo naomba sentensi hiyo ifutwe katika *Hansard* kwa sababu gani? Si kwa sababu ninyi mmelisema, lakini kwa sababu dhamira yangu inaheshimu dini zote. Kwa hiyo naomba kabisa kwa Waislamu wote, wajue kwamba nawaomba radhi kama hivi nilivyofahamika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hili limekwisha. Mheshimiwa Ummy.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikujibu kisiasa, tatizo lililo kuwepo ile benki ilikuwa tubadilishe Sheria iwe ni *public company*. Kwa hiyo wakati imeanzishwa

ilikuwa kama a *kind of private company*. Kwa hiyo ilibidi tubadilishe usajili wa benki ili sasa tuweze kuuza hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato huu tuliukamilisha mwaka 2016 na sasa vyeti vya wanahisa viko tayari na kabla ya mwisho wa mwezi nitaweza kuwapa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamenunua hisa kutoka benki ya wanawake; naomba niahidi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pia kuliitishwa mkutano wa wanahisa, mwezi ulipita, hakuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamekwenda. Kwa hiyo pia nitoe wito, tunaposema wanahisa wote kuna mkutano, *Annually General Meeting* ya wanahisa inabidi mjitokeze ili muweze kufuatilia maendeleo ya benki yenu. Hata hivyo, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa chachu katika kuanzisha Benki ya Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, katibu!

## HOJA ZA KAMATI

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017**

**Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunakwenda kwenye hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii *(Makofi).*

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi na afya na uzima na hata kuweza kusoma taarifa hii ya Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge ukiwemo wewe mwenyewe, Mawaziri wa Wizara ambazo Kamati yetu inasimamia pamoja na watendaji wote wa Wizara hizi na Ofisi ya Bunge. Kwa umuhimu wa kipekee nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wa kuchambua, kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo sasa naomba nianze kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwa sababu ya muda naomba taarifa yote iingie kwenye *hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Januari 2018, ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi; sehemu ya pili inaelezea utekelezaji na majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 na matokeo yaliyobainishwa; sehemu ya tatu inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati; na sehemu ya nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 Septemba, 2017 Kamati ilifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa lengo la kujionea hali halisi ya maendeleo ya hifadhi. Aidha, Kamati ilielezwa mgogoro wa ardhi unaoendelea kati ya

Hifadhi ya Taifa ya Saadani na wananchi wa Kitongoji cha Uvinje waliokataa kupewa fidia kwa maslahi yao binafsi. Kamati ilipata maelezo kutoka kwa uongozi wa Hifadhi, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo pamoja na wananchi wa Kitongoji cha Uvinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yao Kamati ilibaini kuwa mwekezaji huyo mwenye maslahi binafsi amewashawishi na kuwaahidi kuwapa wakazi wa Kitongoji cha Uvinje misaada mbalimbali ikiwemo fedha za kuanzisha *SACCOS* iwapo watampa ardhi ya eneo la Uvinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mazingira ya mgogoro huu, Kamati imejiridhisha kuwa mgogoro huo unachangiwa na watu kwa maslahi yao binafsi. Aidha, upimaji wa eneo kinyume cha taratibu kwa namna moja au nyingine umechangia kukua kwa mgogoro huo ambao umechukua muda mrefu bila majibu, hivyo kuufanya kuwa sugu na mgumu. Serikali ijenge utaratibu na utamaduni wa kushughulikia migogoro hii kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inashauri Mwekezaji asiruhusiwe kufika katika eneo alilopewa na wananchi wa Uvinje, mpaka vyombo vya usalama vijiridhishe na shughuli anazofanya katika eneo hilo na endapo ana vibali vyote vya Serikali. Kamati inashauri uchunguzi ufanyike ili kuweza kubaini uwepo wa boti zinazotia nanga usiku katika eneo la Saadan alilopewa mwekezaji kuweza kujua kuwa boti hizo zinakuja usiku kufanya nini na zinabeba vitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe moja Septemba, 2017, Kamati ilitembelea Mapango ya Amboni yaliyoko katika Halmashauri ya Jiji la Tanga na kujionea uzuri wa mapango hayo ambayo ni miongoni mwa vivutio vikubwa vya utalii katika Jiji la Tanga. Pamoja na umuhimu wa mapango hayo katika kuchangia Pato la Taifa bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali kutowekeza vya kutosha ili kivutio hiki kiweze kutoa mchango mkubwa unaotarajiwa. Miundombinu ya barabara

kuelekea katika mapango hayo ni mibovu, mto unaopita pembezoni mwa Mapango hayo umeanza kumegua kingo za mapango, shughuli za kibinadamu hasa uchimbaji wa kokoto kwa kutumia vilipuzi na mchanga karibu ya mapango zinatishia usalama wa mapango hayo, uhaba wa watumishi, pamoja na kukosekana kwa kituo cha kupumzikia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuyapa Mapango ya Amboni thamani inayostahili ili kuinua utalii nchini:-

Kuyatangaza pamoja na vivutio vingine vilivyoko katika Jiji la Tanga; kuzuia shughuli zote za uchimbaji madini ya kokoto na mchanga karibu na mapango; kujenga kituo cha kupumzikia watalii katika Mapango ya Amboni; kuboresha mazingira hasa kingo za mto ili zisiendelee kumomonyoka na kuhatarisha kutoweka kwa mapango; kuweka miundombinu ya barabara kuelekea Mapango ya Amboni pamoja na vitendea kazi vya kutosha kama tochi zenye mwanga mkali za kuangazia ndani ya mapango ili iwe rahisi kwa watalii kutembea ndani ya mapango; na kuweka watumishi wa kutosha kuhudumia watalii katika vivutio hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika jamii ya wanyamapori ya Wami Mbiki. Katika ziara hii Kamati imejionea jinsi hifadhi ulivyoathiriwa na shughuli za binadamu zikiwepo ufugaji, kilimo makazi ya binadamu, ukataji miti, uchimbaji wa madini na uchomaji wa mkaa, shughuli zinazofanywa kinyume cha sheria kanuni na taratibu ambazo zinapelekea wanyamapori kuhama, kuhangaika kutafuta njia zao kupita wanapohama kwenda hifadhi jirani za Mikumi, Saadan na Pori la Akiba la Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine binadamu waliojenga katika mapito ya wanyama (Shoroba) wamekuwa wakishambuliwa na wanyamapori wakali, pia kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa Misitu ya asili ya Pagale na Gwami pamoja na kuharibu kingo za Mto Wami. Kamati inashauri eneo hili la Wami Mbiki lipandishwe hadhi

na kuwa Hifadhi ya Taifa ili lisimamiwe kwa ufanisi zaidi na Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika hifadhi ya misitu asilia ya milima ya Uluguru. Kamati inapongeza kwa kazi nzuri inayofanywa na Wakala katika kuhifadhi misitu hiyo. Hata hivyo zipo changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kuzuia uharibifu wa misitu. Baadhi ya changamoto hizo ni kama uvamizi unaofanywa kupitia shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo yaliyohifadhiwa. Shughuli hizo ni kilimo, ujenzi wa makazi, uvunaji wa asali na uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi hizo waelimishwe umuhimu wa hifadhi hizo na pale ambapo tatizo ni kubwa basi Serikali iangalie uwezekano wa kuwahamisha wananchi katika maeneo hayo ili kunusuru uharibifu wa misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tarehe 9 Machi, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji ya hifadhi hiyo. Katika ziara hii Kamati ilibaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mseto ya ardhi ambapo uhifadhi wa wanyamapori na maliasili unaenda sambamba na makazi ya wananchi wenyeji kwa mujibu wa Sheria ya Eneo la Ngorongoro. Ongezeko la binadamu, shughuli zao na mifugo; inakadiriwa kuwa wakati Hifadhi ya Ngorongoro ilipoanzishwa mwaka 1959 ilikuwa na wakazi wenyeji takribani 8,000 lakini kufikia Desemba 2017, idadi ya wenyeji ilifikia 93,851.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi kufahamu kuwa eneo hilo linabaki kuwa pale pale lakini watu ndio wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba, pamoja na changamoto nyingine zote, hatua ya kwanza ya kuinusuru Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ni kuhuisha

sheria ya kuanzishwa kwake ili iandane na hali halisi ya sasa. Aidha, Serikali ifanye utafiti wa kina na tathmini ya mfumo wa matumizi mseto ya ardhi katika hifadhi na kutoa mapendekezo yatakayoleta tija. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia wafugaji mashamba nje ya hifadhi ili kupunguza mzigo mkubwa wa mamlaka kuwapa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 23 Januari, 2018 Kamati ilifanya ziara ya kutembelea makumbusho, kituo cha Bonde la Olduvai kilichopo ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa utafiti umethibitisha kwa kutumia vinasaba kwamba binadamu wote wanaoishi duniani chimbuko lao ni Bonde la Olduvai. Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga kituo kizuri na cha kisasa cha kuvutia utalii wa nchi yetu na kwa kuweza kufua umeme kwa kutumia upepo kwa ajili ya kutumika katika Makumbusho hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya zipo changamoto zinazokikabili kituo hiki zikiwemo hali mbaya ya barabara inayoelekea katika kituo hiki na uhakika wa upatikanaji wa maji badala ya kutegemea kuvuna maji ya mvua. Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukitangaza kwa nguvu zote kivutio hiki ili kuweza kuongeza watalii wengi hapa nchini na kuongeza Pato la Taifa; Kuzitaka shule kuanzisha programu maalum ya kupeleka wanafunzi katika kituo hiki kwa lengo la kujifunza historia ya mwanadamu na historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 24 Januari, 2018 Kamati imetembelea Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara iliyoanzishwa mwaka 1960. Katika ziara hii Kamati ilishuhudia vivutio mbali mbali vilivyopo katika hifadhi hii ikiwa ni pamoja na idadi kubwa ya tembo, ndege maji aina ya heroe, batamaji, bata jahazi, korongo na wengineo, ukuta wa

bonde la ufa, msitu wa maji ya ardhini, makundi ya viboko pamoja na chemichemi za majimoto zinazobubujika toka ardhini zenye maji ya moto yanayokadiriwa kuwa na nyuzi joto kati ya 65 na 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za hifadhi kuingia ubia na mwekezaji ambaye amejenga daraja la kupita juu ya miti lenye kina cha mita kumi na nane kutoka ardhini na mzunguko wa mita mia nne. Daraja hili limeongeza thamani ya uhifadhi na kuvutia watalii wengi zaidi kuitembelea hifadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hifadhi inakabiliwa na changamoto za kupungua kwa kina cha maji ziwa Manyara kunakosababishwa na shughuli za binadamu hususan kilimo na uchimbaji madini. Imeelezwa kuwa kina cha ziwa kimepungua kutoka mita kumi hadi kufikia mita moja na nusu hali inayotishia kukauka na kutoweka kwa Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kulinusuru ziwa hili. Hatua hizo ni pamoja na kupiga marufuku shughuli za uchimbaji madini katika eneo hilo pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu kilimo cha kutumia makinga maji ili kupunguza mmomonyoko wa udongo unaopeleka udongo katika ziwa na kusababisha kina cha ziwa kupungua. Aidha, Hifadhi ya ziwa Manyara inakabiliwa na changamoto ya kuzibwa kwa shoroba zinazounganisha ikolojia ya Ziwa Manyara-Tarangire na Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Katika ziara hiyo Kamati ilijionea wanyamapori wengi yakiwemo makundi makubwa ya tembo. Kamati inaipongeza hifadhi kwa juhudi kubwa inazofanya kuzuia ujangili wa wanyamapori hasa tembo. Hifadhi inakabiliwa na tishio la kukauka kwa Mto Tarangire ambao ni tegemeo pekee la wanyamapori ndani ya hifadhi. Kupungua kwa maji katika Mto Tarangire kunakosababishwa na uharibifu wa vyanzo vya maji katika Milima ya Kondoa

kutokana na shughuli za binadamu katika maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuunusuru Mto Tarangire na kuzuia shughuli za binadamu katika Milima ya Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na mwenendo wa Serikali pale inapobaini tatizo lakini inachukua muda mrefu kuchukua hatua na hivyo kusababisha kukua kwa tatizo na gharama kubwa kulipatia ufumbuzi kama ilivyotokea katika bonde la Ihefu ambapo Mto Ruaha Mkuu ulianza kukauka kutokana na kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

Kamati ilifanya ziara katika mradi wa Mji wa Viungani *Satelite Town* – Iyumbu, Dodoma. Katika mradi huu unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa, Kamati ilijionea nyumba za aina zilizojengwa na shirika katika eneo la Iyumbu. Kamati inapongeza kwa kazi nzuri ya upangaji wa mji na kasi ya kutekeleza ujenzi wa nyumba hizo. Hata hivyo Kamati inashauri uwekwe utaratibu wa wateja kushirikishwa kuchagua aina ya nyumba kabla ya ujenzi, hii itawawezesha wateja kuwa na mchanganuo wa aina mbalimbali za nyumba itakayosaidia kuvutia wateja wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Kamati inashauri wateja waelimishwe kuhusu hati pacha *(Unit Title)* itakayowawezesha kuelewa aina hiyo ya umiliki na matumizi yake kama ilivyo kwa hati nyingine za kawaida. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa bei za nyumba zinaendana na kipato cha wananchi walio wengi.

Mheshimiwa mwenyekiti, ziara katika mpango kabambe wa kuendeleza Jiji la Arusha. Kamati ilifanya ziara katika Mpango kabambe wa kuendeleza Jiji la Arusha. Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa kuhusu mpango kabambe wa kuendeleza Jiji la Arusha, pamoja na kutembelea eneo la mpango litakalojulikana kama Mji wa

Bondeni. Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta mpango miji utakaoboresha mwonekano wa Jiji la Arusha na kusaidia kupatikana kwa huduma mbalimbali kwa uharaka. Aidha Kamati inashauri kuwa mipango ya aina hii ifanyike katika majiji mengi kama Mbeya, Tanga na mengineyo ili kupata Tanzania yenye muonekano nadhifu na iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imeshtushwa na gharama zilizotumika kuandaa mradi huu kwa kutumia wataalam elekezi kutoka nje ya nchi, ikiwa ni Dola za Kimarekani 6,081,590 ambapo hadi sasa Serikali imeshalipa Dola za Kimarekani 3,332,621, sawa na asilimia 54.8 ya gharama ya mpango. Deni lililobaki ni Dola za Kimarekani 2,748,968 sawa na asilimia 45.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi Kamati inashauri kuwa katika mipango ya kuendeleza majiji mengine Serikali ijielekeze kutumia wataalam wa ndani ili kupunguza gharama. Aidha, Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha kwamba inalipa deni lililobaki kiasi cha Dola za Kimarekani 2,748,968 ili kuwezesha mpango uweze kukamilishwa, kuidhinishwa na kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji wa Tume za Matumizi ya Ardhi nchini. Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Matumizi ya Ardhi. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti na upungufu wa wataalam uliopelekea utendaji wa Tume kuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Tume ya Matumizi ya Ardhi ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuhusisha makampuni binafsi ya upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi ili kuongeza kasi ya upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi kwa halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya Ardhi nchini; kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu

kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha mgongano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha, mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ili kuhakikisha kuwa ardhi yote inapimwa na kupangiwa matumizi, hali ambayo itachangia kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kuyawezesha majiji, manispaa na halmashauri zetu kwa kuzipatia vifaa vya upimaji na wataalam wa kutosha ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa yaliyotelekezwa; Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu mashamba makubwa yaliyotelekezwa hapa nchini. Katika taarifa hiyo Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na zoezi la uhakiki wa umiliki wa mashamba makubwa yaliyotelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hilo mpaka kufikia Oktoba 2016 jumla ya mashamba 1,912 yalihakikiwa na mashamba 271 kati ya hayo, yalibainika kuwa yametelekezwa. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi sambamba na upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa ardhi nchini *(Land Tenure Support Programme*). Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha programu hii kwa kuwa imelenga kuongeza faida kwenye mikataba ya uwekezaji katika mashamba makubwa kwa kuweka utaratibu bora wa umiliki ardhi pamoja na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria ya ardhi vijijini ili kuwapa uelewa wananchi kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji ardhi ili iweze kuwawezesha wananchi kupata hakimiliki watakazotumia kama dhamana ya kupata mikopo ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati inaishauri Serikali iandae mipango bora wa matumizi ya ardhi vijijini kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya utendaji wa Shirika la Hifadhi la *TANAPA*. Katika taarifa ya utendaji ya Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* Kamati ilibaini kuwa kati ya hifadhi 16 zinazosimamiwa na Shirika ni hifadhi nne tu ndizo zinazojitegemea na ambazo mapato yake hutumika kusaidia hifadhi zingine 12 ni tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zikiwemo za ujangili na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi, na wanyama waharibifu kuvamia mashamba ya wananchi au kujeruhi na kuua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya sheria ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyama waharibifu kwani utaratibu uliopo sasa hauwaridhishi wananchi, hali ambayo inawafanya wawachukie wanyamapori na hivyo kutotoa ushirikiano wa kutosha kulinda maliasili hii adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili hali ya ujangili nchini. Kamati ilitaarifiwa kuwepo na mbinu mpya ya ujangili ambapo majangili wanatumia sumu kuua wanyamapori. Mbinu hii mpya ni hatari sana kwa uhifadhi. Siyo tu inaua wanyamapori wengi kwa wakati mmoja bali pia inaua wanyama wasiokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, majangili wamekuwa wakibadili mbinu za usafirishaji wa nyara za Taifa mara kwa mara na kufanya zoezi la kuwadhibiti kuwa gumu. Kamati inaishauri Serikali kubadili mbinu za kupambana na majangili kwa kuongeza vifaa vya mawasiliano, silaha za kisasa na kuunda kikosi maalum kwa ajili ya kupambana na ujangili na kutumia kikosi chake cha Kiintelijensia kubaini mtandao wa ujangili wa tembo nchini ili kuokoa rasilimali hii muhimu iliyo hatarini kutoweka. Kamati inapongeza Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwa na Jeshi Usu *(Paramilitary)* katika kulinda rasilimali za wanyamapori.

Meshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Maendeleo ya Misitu na Nyuki Nchini. Kamati ilipokea taarifa kuhusu maendeleo ya rasilimali ya Misitu na Nyuki nchini. Katika taarifa hiyo kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto inayotokana na mfumo wa usimamizi na ugawanyiko wa rasilimali za misitu ambao kwa kiasi kikubwa unaleta mgongano na mwingiliano katika kusimamia rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Serikali Kuu kupitia Wakala wa Misitu inamiliki na kusimamia misitu yenye hekta milioni 15.84 sawa na asilimia 35, Serikali za vijiji hekta 21.6 milioni sawa na asilimia 45, Serikali za Mitaa hekta 3.36 milioni sawa na asilimia 7.o, Sekta binafsi hekta 3.36 sawa na asilimia 7.0, Ardhi ya nyumba hekta 2.4 milioni sawa na asilimia 5.0 na Ardhi za miliki nyingine hekta 480,000 sawa na asilimia 1.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa Serikali za vijiji na Serikali za Mitaa kwa pamoja zinamiliki asilimia 52 wakati Serikali kuu inamiliki na kusimamia asilimia 35 tu. Aidha, uharibifu mkubwa wa misitu unatokea katika misitu ya Serikali za Vijiji na ile ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa ili kukabiliana na changamoto hii ni vyema usimamizi wa rasilimali za misitu zisimamiwe na mamlaka moja yenye nguvu lakini umiliki wa misitu hiyo ubaki na wahusika. Ili kufanikisha hilo ni muhimu Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

akafanywa kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia rasilimali za misitu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kujadili changamoto za kuzibwa kwa shoroba katika hifadhi za Taifa. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yenye wanyamapori, yakiwemo mapori Tengefu, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Jamii na Hifadhi za Taifa. Aidha, yapo maeneo mengi yasiyohifadhiwa yaliyotumika kama mapitio ya wanyama toka enzi kutoka hifadhi moja kwenda hifadhi nyingine yaani shoroba. Kwa muda mrefu hapakuwa na sheria ya katazo la shughuli za kibinadamu katika maeneo haya, wala hapakuwa na alama zilizokuwa zinaonesha kuwa maeneo hayo ni mapitio ya wanyama hali iliyosababisha shoroba nyingi kuvamiwa na sasa ni makazi na mashamba ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, upanuzi wa miundombinu ya barabara, umeme, simu na maji pamoja na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi kumesababisha shoroba nyingi kuzibwa hali inayosabisha mgogoro wa wanyama kuvamia maeneo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo hayo, kuzibaini shoroba zote zilizopo na zilizofungwa ili zifunguliwe na kutungiwa sheria ili ziweze kuheshimiwa na kutumiwa na wanyamapori, hali ambayo itapunguza migogoro inayotokana na wananchi kushambuliwa na wanyamapori wanapopita katika njia zao za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili Maendeleo ya Utalii Nchini. Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu maendeleo ya utalii nchini. Mbali na mafanikio katika sekta ya utalii bado Serikali haijawekeza vya kutosha katika utalii wa aina nyingine kama vile utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine. Serikali imeelekeza nguvu nyingi katika utalii wa wanyamapori hasa ukanda wa kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati itakayohakikisha kuwa vivutio vyote vya Utalii vilivyopo nchini vinaendelea na kutangazwa ipasavyo ili kuvutia watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza Pato la Taifa litokanalo na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wadau wa uwindaji wa Kitalii nchini na kupokea malalamiko yao kuhusu hatua ya Waziri wa Maliasili na Utalii kufuta leseni zote za umilikaji katika vitalu kwa kipindi cha mwaka 2018 - 2022 zilizotolewa kihalali na Wizara. Serikali inapaswa kufahamu kwamba biashara ya utalii inahitaji umakini mkubwa *(very delicate)* hivyo mabadiliko kidogo yanaweza kuathiri mpango mzima. Aidha, ni biashara inayohitaji muda kujipanga, kujitangaza na kuwapa imani watalii na wawekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii umeonesha kuwa mapato yameshuka kutoka Dola za Kimarekani milioni 23.5 mwaka 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 11.2 mwaka 2015 kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya mfumo mzima wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji nchini kwani ni eneo ambalo limelalamikiwa sana na wadau na kwamba kutokuwepo na mfumo thabiti na mabadiliko ya mara kwa mara yamelikosesha Taifa mapato, kwa vile watalii wa uwindaji wamezisitisha safari zao mara nyingi kutokana na kukosekana kwa uhakika wa biashara hii. Aidha, Kamati inalishauri Bunge Kupitia Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuunda Kamati Maalum itakayochunguza changamoto zilizoko katika Tasnia hii na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Ufinyu wa bajeti na fedha kutotolewa kwa wakati kumesababisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kufanya ukaguzi wa maeneo na uandaaji

wa mipango bora ya matumizi ya ardhi kusababisha ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuandaa miundombinu ya mifugo nje ya hifadhi kunasababisha wafugaji kuvamia hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, mapori tengefu na misitu ya hifadhi na kuzidisha uhasama baina ya wafugaji na wahifadhi na kusababisha kuharibika kwa mazingira katika maeneo hayo na kuchangia kukauka na kuharibika kwa vyanzo vya maji, ukame na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa utulivu katika sekta ya uwindaji wa kitalii kunakotokana na matamko ya mara kwa mara ya Serikali, pamoja na kubadilika kwa taratibu mbalimbali za ugawaji wa vitalu bila kushirikisha wadau kunasababisha wawekezaji kusita kuwekeza, watalii wawindaji kusitisha safari zao na kulikosesha Taifa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokubainishwa kwa mipaka kati ya hifadhi na wananchi wanaopakana na hifadhi kunachangia kuongezeka kwa migogoro ya mipaka katika hifadhi hali inayojenga mahusiano mabaya baina ya hifadhi na wananchi na kusababisha kuongezeka kwa uhasama kati ya askari wa wanyamapori na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokurekebisha kanuni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakupa sekunde 30.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA- MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa Mapendekezo na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi.

KWA KUWA kulikuwa na zoezi la kuainisha na kuhakiki maeneo ya mipaka;

NA KWA KUWA zoezi hilo lilionekana kukwama kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kuendeleza zoezi hilo;

HIVYO BASI Serikali ifikirie upya na kutenga fedha za kutosha kwa lengo la kuendelea kuainisha mipaka ya maeneo katika hifadhi ili kumaliza migogoro ya ardhi katika hifadhi na mapori tengefu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro kati ya Hifadhi na Wafugaji.

KWA KUWA kumekuwa na malalamiko mengi...

**MWENYEKITI:** Ahsante, taarifa yako imeshaingia kwenye *Hansard*. Hata hivyo, nikupongeze kwa kusoma vizuri, umeitendea haki Kamati yako. Toa hoja. (*Makofi)*

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA- MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2017, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEZO YA JUMLA

### 1.0 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Januari 2018, ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Taarifa hii ina Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya **Kwanza** inaelezea **Utangulizi**, Sehemu ya **Pili** inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha Mwaka 2017/2018 na matokeo yaliyobainishwa. Sehemu ya **Tatu** inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati, na Sehemu ya **Nne** ni hitimisho.

### 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kamati yameainishwa katika Nyongeza ya Nane chini ya kanuni ya 118, kifungu cha 6 (6) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016, kuwa:-

*"…Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za Wizara mbili nazo ni*
*(a)Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na*
*(b) Wizara ya Maliasili na Utalii".*

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Wizara zinazosimamiwa na Kamati ni pamoja na Miswada ya Sheria

na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara tajwa, Taarifa za utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo pamoja na utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba. Aidha, mbali na majukumu tajwa, Kamati ina jukumu la kushughulikia jukumu lolote litakaloletwa katika Kamati na Mheshimiwa Spika kwa kuzingatia Kanuni 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

## 1.2 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA MWAKA 2017

### 1.2.1 ZIARA

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017 Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

- Hifadhi ya Taifa ya Saadan,
- Miradi ya upandaji miti mashamba ya watu binafsi-Ifakara,(Private Forest plantation)
- Malikale – Mapango ya Amboni
- Hifadhi ya Jamii ya Wamimbiki
- Hifadhi ya Misitu asilia ya milima ya Uluguru
- Pori Tengefu la Loliondo
- Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro
- Malikale-Makumbusho, kituo cha Bonde la Olduvai
- Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara
- Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

Kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo;-

- Mradi wa upimaji na Umilikishaji Ardhi wilaya ya Kilombero

- Mradi wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Jiji la Arusha

- miradi ya ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa-Iyumbu Dodoma.

### 1.2.2 MIKUTANO

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Januari 2017 mpaka Januari 2018 Kamati ilifanya mikutano na Wizara na baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara kwa kupokea na kuchambua taarifa mbali mbali zilizoletwa mbele ya Kamati. Kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa zifuatazo:-

- Utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi,
- Hali ya migogoro ya Ardhi Nchini,
- Uaandaaji na Utekelezaji wa Mpango kabambe wa kuendeleza jiji la Mwanza
- Utendaji wa Bodi ya Uthamini
- Utekelezaji wa Shirika la Nyumba la Taifa
- Utendaji wa Chuo cha Ardhi Tabora
- Urasimishaji makazi katika Jiji la Dare Es Salaam
- Uandaaji Mpango Kabambe wa Jiji la Arusha
- Mradi wa Safari City-Mateves, Arusha na
- Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2016/2017 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa zifuatazo:-

- Utendaji wa Shirika la Hifadhi la Taifa ( TANAPA )
- Utendaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ( NCAA )
- Utendaji Malikale Mapango ya Amboni
- Utekelezaji wa agizo la Serikali la Kuondoa Mifugo katika mapori ya akiba na mapori Tengefu nchini
- Utendaji wa Hifadhi ya msitu wa maporomoko ya Kalambo
- Utendaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa- kuhusu Hifadhi tegemezi
- Utendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania-Hifadhi za Misitu Asilia

· Utendaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania-Hali ya Uvamizi wa mifugo katika Mapori ya Akiba.
· Mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan na Wakazi wa Kitongoji cha Uvinje
· Mapango ya Amboni

· Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2016/2017 pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
· Utendaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania.

### 1.2.3 SEMINA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya semina na mikutano mbalimbali katika nyakati tofauti kwa lengo la kuongeza uelewa wa wajumbe katika maeneo yanayohusu Sekta wanazozisimamia. Semina hizo ni kama zifuatazo;-

· Nishati itokanayo na Tungamo taka ilitolewa na Tanzania Forest Conservation group (TFCG)
· Uharibifu wa mazingira katika maeneo ya hifadhi za Taifa unaotokana na uvamizi wa mifugo iliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii

· Changamoto za migogoro ya Ardhi katika ardhi ya vijiji iliyotolewa na Oxfam Tanzania

· Changamoto za mgongano wa sheria za ardhi za vijiji, sheria ya wanyamapori na sheria ya mazingira zilizotolewa na lawyers Environmental Action Team na Mradi wa Legislative Support Programme ( LSP II )

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu matokeo yaliyopatikana kutokana na kazi zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2017. Kazi hizo zilitekelezwa kupitia Wizara na

taasisi inazozisimamia kwa njia ya ziara zilizofanywa na Kamati, taarifa zilizowasilishwa na Wizara na taasisi zake mbele ya Kamati kwa nyakati tofauti tofauti, semina, pamoja na miswada kama ifuatavyo;-

## 2.1 ZIARA

### 2.1.1 Ziara Katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan

Mheshimiwa Spika, Tarehe 2 Septemba, 2017 Kamati ilifanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa lengo la kujionea hali halisi ya maendeleo ya hifadhi.Aidha Kamati ilielezwa mgogoro wa ardhi unaoendelea kati ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani na wananchi wa kitongoji cha Uvinje waliokataa kupewa fidia kwa maslahi binafsi. Kamati ilipata maelezo kutoka kwa uongozi wa Hifadhi, Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo pamoja na wananchi wa kitongoji cha Uvinje. Katika maelezo yao Kamati ilibaini kuwa eneo lote la kitongoji cha Uvinje liko ndani ya mipaka ya iliyokuwa Pori la akiba Saadani na kwa kuzingatia Tangazo la Serikali la 1974 eneo hilo liko ndani ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa Saadani kwa kuzingatia Tangazo la Serikali Na. 282 la 2005.

Kamati ilibaini kuwa mgogoro wa Saadani kwa namna moja au nyingine unachochewa na mwekezaji ambaye amenunua ardhi ya wananchi kinyume cha sheria kwa lengo la kuwekeza katika mradi wa hoteli ya kitalii kwa ubia na wananchi katika eneo hilo ambalo liko ndani ya hifadhi bila kushirikisha uongozi wa hifadhi, ramani ya upimaji Na. E 4/7 kiwanja Na.2 Uvinje, upimaji uliofanywa na Mtumishi wa Halmashauri ndugu **Volstan Tesha** aliyepima eneo hilo kinyume na sheria. Mtumishi huyu alihamishwa baada ya kuonekana kusababisha migogoro mingi ya ardhi wilayani Bagamoyo lakini kwa mshangao mkubwa baada ya awamu ya tano kuingia madarakani amerudishwa kinyemela.Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa mwekezaji huyu mwenye maslahi binafsi amewashawishi na kuwaahidi kuwapa wakazi wa Kitongoji cha Uvinje misaada mbalimbali ikiwemo fedha za kuanzisha SACCOS iwapo watampa ardhi ya eneo la Uvinje.

**Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia mazingira ya mgogoro huu Kamati imejiridhisha kuwa mgogoro huo unachangiwa na watu kwa maslahi yao binafsi, Aidha upimaji wa eneo kinyume cha taratibu kwa namna moja au nyingine umechangia kukua kwa mgogoro huo. Kamati inashauri mwekezaji asiruhusiwe kufika katika eneo alilopewa na wananchi wa Uvinje mpaka vyombo vya usalama vijiridhishe na shughuli anazofanya katika eneo hilo na endapo ana vibali vyote vya serikali.**

**Aidha kamati inashauri kuwa ni vyema taratibu za uhakiki na upimaji wa maeneo zikazingatiwa wakati wa uuzaji wa maeneo.Pamoja na hayo Kamati inashauri kuwa taratibu za kinidhamu zichukuliwe kwa yeyote atakayebainika anapima maeneo kinyume cha taratibu na sheria za nchi. Kamati inashauri uchunguzi ufanyike ili kuweza kubaini uwepo wa Boti zinazotia Nanga usiku katika eneo la Saadani alilopimiwa mwekezaji kuweza kujua kuwa boti hizo zinakuja usiku kufanya nini na zinabeba vitu gani.**

**Mheshimiwa Spika,mgogoro huu umechukua muda mrefu bila majibu, hivyo kuufanya kuwa sugu na mgumu. Serikali ijenge utamaduni wa kushughulikia migogoro hii kwa haraka.**

### 2.1.2 **Ziara Katika Miradi ya upandaji miti mashamba ya watu binafsi-Ifakara, (Private Forest plantation)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa upandaji miti mashamba ya watu binafsi unaotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa fedha za wafadhili. Wajumbe walipata fursa ya kuona baaadhi ya mashamba ya mfano na kubaini yafuatayo:-

- Kutokuwepo kwa uwazi kuhusu kiasi halisi cha fedha wanazopewa na Makampuni yanayowasimamia wakulima hao wala mikataba kati ya wakulima hao na makampuni yanayowasimamia
- Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na Mji wa Ifakara kutokushirikishwa katika uanzishwaji vikundi hali inayotia

mashaka katika utaratibu mzima wa uendeshwaji wa mradi huo

· Wakulima wadogo kutoelimishwa kuhusu haki zao katika mikataba ya kulima miti na hivyo kusababisha kutokuwa na uwazi katika utekelezaji wa mradi,na

· Wizara kutokushirikishwa kikamilifu

**Kamati inashauri, katika utekelezaji wa mradi huu Halmashauri ihusishwe moja kwa moja katika zoezi zima la kuunda vikundi ili kulinda haki zao. Aidha Wizara ishiriki kikamilifu kwa kupatiwa takwimu sahihi za kiasi cha fedha zinazoletwa na wafadhili kwa makampuni ili kuongeza uwazi na uwajibikaji zaidi.**

### 2.1.3 Ziara katika Mapango ya Amboni

**Mheshimiwa Spika, Tarehe 1 Septemba, 2017** Kamati ilitembelea mapango ya Amboni yaliyoko katika Halmashauri ya Jiji la Tanga na kujionea uzuri wa Mapango hayo ambayo ni miongoni mwa vivutio vikubwa vya utalii katika jiji la Tanga. Pamoja na umuhimu wa mapango katika kuchangia pato la Taifa bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na serikali kutowekeza vya kutosha ili kivutio hiki kiweze kutoa mchango mkubwa unaotarajiwa, Miundombinu ya barabara kuelekea katika mapango hayo ni mibovu, mto unaopita pembezoni mwa Mapango hayo umeanza kumegua kingo za Mapango, Shughuli za kibinadamu hasa uchimbaji wa kokoto kwa kutumia vilipuzi na mchanga karibu ya mapango unatishia usalama wa Mapango hayo, uhaba wa watumishi,pamoja na kukosekana kwa kituo cha kupumzikia watalii.Kamati inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuyapa Mapango ya Amboni thamani inayostahili ili kuinua utalii nchini:-

· **Kuatangaza pamoja na vivutio vingine vilivyoko katika jiji la Tanga mfano Hifadhi Asilia ya Amani, Fukwe za Bahari zilizoko Pangani, Hifadhi ya Taifa ya Saadan, Chemchemi ya maji moto ya *Sulphur* Amboni pamoja na magofu ya Tongoni hii itasaidia watu kufahamu uwepo wa**

**vivutio hivyo na itavutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio hivyo na kuongeza pato la Taifa katika utalii.**

- **Kuzuia shughuli zote za uchimbaji madini ya kokoto na mchanga karibu na Mapango**

- **Kujenga kituo cha kupumzikia watalii katika Mapango ya Amboni**
- **Kuboresha mazingira hasa kingo za mto ili zisiendelee kumomonyoka na kuhatarisha kutoweka kwa Mapango**

- **Kuweka miundombinu ya barabara kuelekea mapango ya Amboni pamoja na vitendea kazi vya kutosha kama Tochi zenye mwanga mkali za kuangazia ndani ya Mapango ili iwe rahisi kwa watalii kutembea ndani ya Mapango, na**

- **Kuweka watumishi wa kutosha kuhudumia watalii katika vivutio hivi.**

- **Kuweka vijitabu vinavyoelezea historia ya mapango pamoja na ramani inayoonyesha jinsi ya kuingia na kutoka katika mapango haya**

- **Kuboresha muonekano wa alama za kuingia na kutoka katika mapango**

2.1.4 **Ziara katika Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Wamimbiki**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Hifadhi ya Jamii ya Wamimbiki yenye ukubwa wa km za mraba 2400 ambayo ni makazi ya wanyamapori yenye misitu ya asili, mapito ya wanyamapori inayounganisha ikolojia ya Selous-Mikumi- Simanjiro – Hifadhi ya mto Wami hadi katika Hifadhi ya Saadan. Katika ziara hii Kamati imejionea jinsi hifadhi ilivyoathiriwa na shughuli za binadamu zikiwemo **ufugaji, kilimo, makazi ya binadamu, ukataji miti, uchimbaji wa madini na uchomaji wa mkaa**, shughuli zinazofanywa kinyume cha sheria kanuni na taratibu ambazo zinapelekea

wanyamapori kuhama, kuhangaika kutafuta njia ya kupita wanapohama kwenda hifadhi jirani za Mikumi, Saadan na Pori la Akiba Selous. Kwa upande mwingine binadamu waliojenga katika mapito ya wanyama (**Shoroba**) wamekuwa wakishambuliwa na wanyamapori wakali, pia kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa Misitu ya asili ya Pagale na Gwami pamoja na kuharibu kingo za mto Wami.

Kutokana na uwezo mdogo wa kifedha na kitaaalam wa jumuiya ya Wamimbiki na hivyo kulazimu taasisi zingine kama TAWA, TANAPA na TFS kuisaidia kufanya doria kutokana na umuhimu wake kiikolojia, **Kamati inashauri eneo hili la Wamimbiki lipandishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ili lisimamiwe kwa ufanisi zaidi na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

### 2.1.5 Ziara katika Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea wakala wa Mbegu za Miti iliyoko mjini Morogoro na kupokea Taarifa kuhusu utendaji wa Wakala huyo.Katika taarifa iliyotolewa Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zikiwemo:-

- Kutokuwepo kwa Sheria inayohusu mbegu za miti inayoweza kudhibiti biashara na upandaji wa mbegu za miti. Sheria inayotumika kwa sasa ni sheria ya mbegu za kilimo ambayo haizungumzii mbegu za miti pamoja na vipandikizi hali iliyosababisha biashara ya mbegu za miti kufanyika bila ya kuwa na udhibiti
- Gharama kubwa za kuzalisha mbegu za miti ikilinganishwa na bei za mbegu
- Uchakavu wa vifaa vya maabara hali inayosababisha Wakala kutofanya baadhi ya vipimo kwa usahihi vya mbegu pamoja na
- Uhaba wa Wataalam katika nyanja muhimu za uzalishaji mbegu kama vile Botany,Tree Breeding na Seed Pathology

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri serikali kutekeleza yafuatayo ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa wakala:-

· **Serikali ianze mchakato wa kuandaa sheria ya mbegu za miti**

· **Kuongeza bajeti ya wakala ili kuiwezesha kukarabati maabara na kusomesha wataalam wa kutosha katika fani muhimu kwa wakala**

· **Kuiwezesha wakala kuanzisha mashamba ya mbegu za miti ili kupunguza gharama za uzalishaji mbegu na hivyo kufanya bei ya mbegu za miti kuwa nafuu**

2.1.6 **Ziara katika Hifadhi ya Misitu asilia ya milima ya Uluguru**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea hifadhi ya misitu Asilia ya milima ya Uluguru katika Mkoa wa Morogoro na kujionea jitihada zinazofanywa na wakala wa Misitu Tanzania ikiwa ni pamoja na kuhifadhi milima hiyo ili iweze kutoa huduma za kutunza vyanzo vya maji na kuzuia mmomonyoko wa udongo unaotokana na uharibifu wa misitu. Kamati inapongeza kazi nzuri inayofanywa na wakala katika kuhifadhi misitu hiyo. Hata hivyo zipo changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi ili kuzuia uharibifu wa misitu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na **uvamizi unaofanywa kupitia shughuli za kibinadamu katika maeneo yaliyohifadhiwa. Shughuli hizo ni kilimo, ujenzi wa makazi, uvunaji wa asali na uchomaji wa mkaa**.

**Kamati inashauri wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi hizo waelimishwe umuhimu wa hifadhi hizo na pale ambapo tatizo ni kubwa basi Serikali iangalie uwezekano wa kuwahamisha wananchi katika maeneo hayo ili kunusuru uharibifu wa misitu yetu.**

2.1.7 **Ziara katika Pori Tengefu la Loliondo**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 7 Machi 2017 Kamati ilitembelea Pori Tengefu la Loliondo na kujionea changamoto mbali mbali zinazolikabili pori hilo. Yapo maoni na ushauri uliotolewa na kamati wakati wa ziara hii ambayo Serikali imeanza kuyafanyia kazi baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ikiwa ni pamoja na kuanza zoezi la kuainisha na kuhakiki maeneo ya mipaka ya Pori Tengefu la

Loliondo na kusajili upya NGOS zote zinazofanya kazi katika eneo hilo. Lengo ni kumaliza migogoro na kuendeleza hifadhi kwa maslahi ya Taifa letu.

2.1.8 **Ziara katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tarehe 9 Machi, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji ya hifadhi hiyo. Katika taarifa hiyo Kamati ilielezwa kuwa licha ya upekee iliyonayo Mamlalaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ya kuwa na matumizi mseto ya ardhi na eneo la urithi wa dunia, hifadhi inakabiliwa na changamoto nyingi ambapo zisipofanyiwa kazi zinatishia siyo tu kupoteza hadhi yake ya kuwa eneo la urithi wa dunia bali kutoweka kabisa kwa hifadhi hiyo. Changamoto hizo ni pamoja na;-

- Matumizi mseto ya ardhi ambapo uhifadhi wa wanyamapori na maliasili unaenda sambamba na makazi ya wananchi wenyeji kwa mujibu wa Sheria ya Eneo la Ngorongoro.

- ongezeko la binadamu, shughuli zao na mifugo, inakadiriwa kuwa Wakati Hifadhi ya Ngorongoro ilipoanzishwa mwaka 1959 ilikuwa na wakazi wenyeji takribani **8,000** lakini kufikia Desemba 2017, idadi ya wananchi wenyeji ilifikia **93,851**. Ongezeko hili ni kubwa na wafugaji hawa wamekuwa wakiingiza mifugo katika hifadhi hususan kreta na kupelekea uharibifu wa vyanzo vya maji, uoto wa asili, uvamizi wa mapito ya wanyama, kutoweka kwa baadhi ya wanyama katika hifadhi ambavyo vyote hupelekea kupungua kwa idadi ya watalii.
- Sheria Na. 413 ya mwaka 1959 R.E cap Na. 284 ya mwaka 2002 iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngororngoro kupitwa na wakati ambapo utekelezaji wa matakwa ya kisheria katika eneo la hifadhi hii yanapelekea kukuza ukinzani kati ya Mamlaka kwa upande mmoja na wenyeji Wamasai wakazi wa eneo la Hifadhi kwa upande mwingine. Ukinzani huu unatokana na Sheria kuweka masharti yanayoonekana kuwa magumu kiutekelezaji kuhusu matumizi ya ardhi ndani ya eneo la Hifadhi hususan kuzuia kabisa shughuli za kilimo, matumizi ya vyombo vya moto, masharti ya namna ya kufanya kazi na maeneo ya kufanya shughuli za ufugaji.

· Mabadiliko ya tabia ya nchi inayopelekea uhaba wa maji na malisho. Hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa maji na malisho katika eneo la Hifadhi hali inayopelekea mvutano baina ya Mamlaka ya Hifadhi na wananchi wenyeji wa Ngorongoro

· Gawio la fedha zinazotolewa na Mamlaka kwenda kwa wenyeji nalo ni sehemu ya tatizo kwani sasa viongozi wa Baraza la wafugaji wamefanya kama mradi wao

· Huduma zinazotolewa na Mamlaka kwa wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi zinawafanya wananchi hao kujiona ni wa pekee kwani wanapata fedha, elimu, Afya n.k bure

· Ufugaji ndani ya Hifadhi hasa katika maeneo yenye mahoteli ni kero kwa watalii kwani mifugo hulishwa na kupitishwa jirani na maeneo hayo.

**Kamati inashauri kwamba pamoja na changamoto nyingine zote, hatua ya kwanza ya kuinusuru Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ni kuhuisha sheria ya kuanzishwa kwake ili iandane na hali halisi ya sasa. Aidha Serikali ifanye utafiti wa kina na tathimini ya mfumo wa matumizi mseto ya ardhi katika hifadhi na kutoa mapendekezo yatakayoleta tija. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia wafugaji mashamba nje ya hifadhi ili kupunguza mzigo mkubwa wa mamlaka kuwapa chakula.**

Vilevile, Katika lango la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, kamati ilionyeshwa Mfumo mpya wa malipo wa kielektroniki na jinsi mfumo huo unavyofanya kazi. Ilielezwa kuwa mfumo huu huyawezesha makampuni ya utalii kulipia na kukata vibali vya kufanya shughuli za utalii bila ya kulazimika kufanya malipo kwa kupanga foleni kwenye malango ya hifadhi. Utaratibu huu umesaidia sana kuondoa usumbufu na msongamano kwa kuokoa muda wa watalii wanapofika kwenye lango la kuingilia hifadhini. Aidha utaratibu huu umeweza kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

### 2.1.9 Ziara katika Makumbusho, Kituo cha Olduvai

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 Januari, 2018 Kamati ilifanya ziara ya kutembelea makumbusho, kituo cha Bonde la Olduvai kilichopo ndani ya eneo la Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. Katika kituo hiki pamoja na mambo mengine Kamati ilifahamishwa historia ya mwanadamu wa kwanza na chimbuko lake, zama za mawe za kwanza, kati na zama za mwisho zilizohifadhiwa katika bonde la Olduvai.

Kamati ilionyeshwa mabaki ya binadamu hao kuanzia kwa *Zinjanthropus*, *Homohabilius* na *Homoerectus* aliyeishi zama za tatu. Aidha Kamati iliweza kuona nyayo za *zamadamu* wa *laetoli* na kijifunza historia mbalimbali za mwanadamu wa kale na maendeleo yake (evolution) mpaka kufika mwanadamu aliyepo sasa. Aidha Kamati ilifahamishwa kuwa utafiti umethibitisha kwa kutumia vinasaba kwamba binadamu wote wanaoishi duniani chimbuko lao ni Bonde la Olduvai. Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga kituo kizuri na cha kisasa cha kuvutia utalii wa nchi yetu na kwa kuweza kufua umeme kwa kutumia upepo kwa ajili ya kutumika katika Makumbusho hii.

Pamoja na mafanikio haya zipo changamoto zinazokikabili kituo hiki zikiwemo hali mbaya ya barabara inayoelekea katika kituo hiki na uhakika wa upatikanaji wa maji badala ya kutegemea kuvuna maji ya mvua. Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo:-

- **kukitangaza kwa nguvu zote kivutio hiki ili kuweza kuongeza watalii wengi hapa nchini na kuongeza pato la Taifa.**
- **Kuzitaka shule kuanzisha programu maalumu ya kupeleka wanafunzi katika kituo hiki kwa lengo la kijifunza historia ya mwanadamu na historia ya nchi yetu kwa ujumla**
- **Kurejesha masalia halisi ya *Zamadamu* aliyegunduliwa katika Bonde hili kwa vile sasa kuna jengo bora na la kisasa**
- **Katika eneo lililofanyiwa uvumbuzi wa mwanadamu linaloonyesha uhalisia wa asili wa eneo husika, lihifadhiwe**

**badala ya kuliacha linapotea kwa hoja kwamba asili ichukue mkondo wake**

· **Kuwekwe Maabara na Maktaba za kisasa zilizosheheni vifaa vya kutosha ili kuwavutia watafiti wengi zaidi kuja kufanya utafiti katika eneo hilo**

2.1.10 **Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 24 Januari, 2018 Kamati imetembelea Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara iliyoanzishwa mwaka 1960 ikiwa ni sehemu ya ikolojia ya Tarangire-Manyara yenye eneo la kilomita za mraba 687. Kuanzishwa kwa hifadhi hii kumelenga kuwezesha kukamilika mzunguko na mahitaji ya wanyama waishio katika hifadhi ya Tarangire na eneo la Ngorongoro, pamoja na kuhifadhi bioanuwai kubwa ya eneo la Ziwa Manyara na kuongeza vivutio kwa watalii wanaotembelea Hifadhi ya Serengeti na eneo la Ngorongoro.Kamati ilishuhudia vivutio mbali mbali vilivyopo katika hifadhi hii ikiwa ni pamoja na;-idadi kubwa ya tembo, ndege maji aina ya heroe, batamaji, bata jahazi, korongo na wengineo, aina nyingi za ndege, ukuta wa bonde la ufa msitu wa maji ya ardhini, makundi ya viboko pamoja na chemichemi za majimoto zinazobubujika toka ardhini zenye maji ya moto yanayokadiriwa kuwa na nyuzi joto kati ya 65 na 80 C.

Kamati inapongeza jitihada za Hifadhi kuingia ubia na mwekezaji ambaye amejenga daraja la kupita juu ya miti lenye kina cha mita kumi na nane kutoka ardhini na mzunguko wa mita mianne. Daraja hili limeongeza thamani ya hifadhi na kuvutia watalii wengi zaidi kuitembelea hifadhi hii. Hatahivyo, hifadhi inakabiliwa na changamoto ya **kupungua kwa kina cha ziwa Manyara kunakosababishwa na shughuli za binadamu hususan kilimo na uchimbaji madini**. Imeelezwa kuwa kina cha ziwa kimepungua kutoka mita kumi hadi kufikia mita moja na nusu hali inayotishia kukauka na kutoweka kwa Ziwa Manyara.

**Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kulinusuru ziwa hili. Hatua hizo ni pamoja na kupiga**

**marufuku shughuli za uchimbaji madini katika eneo hilo pamoja na kuwaeleimisha wananchi kuhusu kilimo cha kutumia makinga maji ili kupunguza mmomonyoko wa udongo unaopeleka udongo katika ziwa na kusababisha kina cha ziwa kupungua. Aidha Hifadhi ya ziwa Manyara inakabiliwa na changamoto ya kuzibwa kwa shoroba zinazounganisha ikolojia ya Ziwa Manyara-Tarangire na Ngorongoro.**

### 2.1.11 Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire tarehe 25 Januari, 2018 na kupokea taarifa ya utendaji ya Hifadhi hiyo. Katika ziara hiyo Kamati ilijionea wanyamapori wengi yakiwemo makundi makubwa ya Tembo. Kamati inaipongeza hifadhi kwa juhudi kubwa inazofanya kuzuia ujangili wa wanyamapori hasa Tembo.

Pamoja na kazi nzuri zinazofanyika hifadhi inakabiliwa na changamoto ya kuzibwa kwa shoroba zinazounganisha hifadhi ya Tarangire za ikolojia za Ziwa Manyara na Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha hifadhi inakabiliwa na tishio la kukauka kwa mto Tarangire ambao ni tegemeo pekee la wanyamapori ndani ya hifadhi, kupungua kwa maji katika mto Tarangire kunakosababishwa na uharibifu wa vyanzo vya maji katika milima ya Kondoa kunakotokana na shughuli za binadamu katika maeneo hayo. **Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuunusuru mto Tarangire kwa kuzuia shughuli za binadamu katika milima ya Kondoa. Aidha serikali ichukue hatua ya kuzibainisha shoroba zote za wanyamapori zilizopo katika eneo hili na kuziwekea mipaka na alama ili wananchi wazijue. Vilevile serikali iharakishe mchakato wa kutunga kanuni za kulinda shoroba zetu haraka iwezekanavyo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na mwenendo wa serikali pale inapobaini tatizo lakini inachukua muda mrefu kuchukua hatua na hivyo kusababisha kukua kwa tatizo na gharama kubwa kulipatia ufumbuzi kama

ilivyotokea katika bonde la Ihefu ambapo mto Ruaha mkuu ulianza kukauka kutokana na kilimo cha mpunga.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo;-

2.1.12 **Ziara katika Mradi wa mji wa viungani (Satelite Town)-Iyumbu, Dodoma**

Katika mradi huu unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa, Kamati ilijionea nyumba za aina mbalimbali zilizojengwa na shirika katika eneo la Iyumbu.Kamati inapongeza kazi nzuri ya upangaji wa mji na kasi ya kutekeleza ujenzi wa nyumba hizo.

Hata hivyo Kamati **inashauri uwekwe utaratibu wa wateja kushirikishwa kuchagua aina ya nyumba kabla ya ujenzi, hii itawawezesha wateja kuwa na machaguo ya aina mbalimbali za nyumba itakayosaidia kuvutia wateja wengi zaidi, aidha Kamati inashauri wateja waelimishwe kuhusu hati pacha *(Unit Title)* itakayowawezesha kuelewa aina hio ya umiliki na matumizi yake kama ilivyo kwa hati nyingine za kawaida. Aidha Kamati inashauri Serikali ihakikishe kuwa bei za nyumba zinaendana na kipato cha wananchi walio wengi.**

2.1.13 **Ziara katika Mpango kabambe wa kuendeleza jiji la Arusha**

Katika Mpango kabambe wa kuendeleza jiji la Arusha, Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa kuhusu Mpango kabambe wa kuendeleza Jiji la Arusha pamoja na kutembelea eneo la mpango litakalojulikana kama mji wa Bondeni.Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta mpago miji utaoboresha muonekano wa jiji la Arusha na kusaidi kupatikana kwa huduma mbalimbali kwa uharaka. Aidha Kamati inashauri kuwa mipango ya aina hii ifanyike katika majiji mengine kama Mbeya, Tanga, na mengineyo ili kupata Tanzania yenye muonekano nadhifu iliyopangwa.

Hata hivyo Kamati imeshitushwa na gharama zilizotumika kuandaa mradi huu kwa kutumia wataalamu elekezi kutoka nje ya nchi ikiwa ni **USD 6,081,590.00** ambapo hadi sasa Serikali imeshalipa **USD 3,332,621.51** sawa na asilimia **54.8** ya gharama ya mpango. Deni lililobakia ni USD **2,748,968.49** sawa na asilimia **45.2, hivyo basi kamati inashauri kuwa katika mipango ya kuendeleza majiji mengine Serikali ijielekeze kutumia wataalamu wa ndani ili kupunguza gharama.Aidha Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha kwamba inalipa deni lililobakia kiasi cha USD 2,748,968.49 ili kuwezesha mpango uweze kukamilishwa, kuidhinishwa na kuanza kutekelezwa**.

### 2.1.14 MIKUTANO

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilikutana, kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizo chini ya wizara hizi. Aidha, Kamati ilikutana na wawekezaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii nchini kwa lengo la kujadili maendeleo ya uwindaji na changamoto mbalimbali zinazondelea kuwakabili kwa lengo la kuboresha sekta ya uwindaji wa kitalii hapa nchini.

### 2.1.15 Mikutano na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa nyakati tofauti, kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilioletwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo;-

### 2.1.16 Taarifa kuhusu utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti na upungufu wa wataalam uliopelekea utendaji wa tume kuwa hafifu. **Kamati**

**inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Tume ya Matumizi ya Ardhi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuhusisha Kampuni binafsi za upimaji na upangaji matumizi ya ardhi ili kuongeza kasi ya upimaji na upangaji matumizi ya ardhi kwa Halmashauri zetu.**

### 2.1.17 **Taarifa kuhusu Migogoro ya Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha mgongano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

**Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ili kuhakikisha kuwa ardhi yote inapimwa na kupangiwa matumizi hali ambayo itachangia kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuyawezesha Majiji, Manispaa, na Halmashauri zetu kwa kuzipatia vifaa vya upimaji na wataalam wa kutosha ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi nchini**.

### 2.1.18 **Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2016/2017 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2016/17, pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2017/18 na kuiwasilisha Bungeni.

### 2.1.19 **Taarifa kuhusu Mashamba Makubwa Yaliyotelekezwa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu mashamba makubwa yaliyotelekezwa hapa nchini. Katika taarifa hiyo kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaendelea na zoezi la uhakiki wa umiliki wa mashamba makubwa yaliyotelekezwa. Katika Zoezi hili mpaka kufikia Oktoba 2016 jumla ya mashamba **1,912** yalihakikiwa na mashamba **271** kati ya hayo, yalibainika kuwa yametelekezwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuchukua hatua ya kuanza kubatilisha umiliki wa baadhi ya mashamba yaliyotelekezwa na kuyapangia matumizi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya hazina ya ardhi (*land bank*), lakini zipo changamoto zinazoikabili Wizara katika kutekeleza jukumu hili. Changamoto hizo ni pamoja na upungufu mkubwa wa fedha za kuendesha zoezi la uhakiki ardhi, kukosekana kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi vijijini, na gharama kubwa za kuandaa mpango bora wa matumizi ya Ardhi nchini. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi sambamba na upangaji wa matumizi ya ardhi.**

### 2.1.20 Taarifa Kuhusu Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi Nchini

**Mheshimwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa ardhi nchini, *(Land Tenure Support Programme*). Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha programu hii kwa kuwa imelenga kuongeza faida kwenye mikataba ya uwekezaji katika mashamba makubwa, kwa kuweka utaratibu bora wa umiliki ardhi pamoja na matumizi yake. Aidha, programu imeendelea kuratibu zoezi la upimaji na urasimishaji wa ardhi za kimila katika wilaya mbalimbali hapa nchini kwa kuanza na wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi, ambapo takribani **hakimiliki 300,000** na **hati miliki za ardhi 25,000** zimetolewa

kwa muda wa miaka 3, ambazo zitatumika kama dhamana ya kuwawezesha wakulima na wafugaji kupata mikopo.

**Kamati inaishauri Serikali kutoa Elimu kwa umma kuhusu sheria ya ardhi vijijini ili kuwapa uelewa wananchi kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza Kasi ya upimaji na urasimishaji ardhi ili kuwawezesha wananchi kupata hakimiliki watakazotumia kama dhamana ya kupata mikopo ili waweze kujikwamua kiuchumi. Vilevile Kamati inaishauri Serikali iandae mipango bora ya matumizi ya ardhi vijijini kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.**

2.1.21 **Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mikutano mbalimbali na** Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika mikutano hiyo, taarifa zifuatazo zilijadiliwa:-

2.1.22 **Taarifa kuhusu Utendaji wa Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA)**

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa ya utendaji ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kamati ilibaini kuwa kati ya hifadhi 16 zinazosimamiwa na Shirika ni hifadhi 4 tu zinazojitegemea na ambazo mapato yake hutumika kusaidia hifadhi zingine 12 ambazo hazijaweza kujitegemea kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo kutotangazwa vya kutosha na kukosa miundombinu ya kuleta watalii..

Vile vile Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazozikabili hifadhi zetu ikiwa ni pamoja na ujangili na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Kamati imefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa jinsi linavyowashirikisha wananchi hususan wanaoishi kuzunguka Hifadhi za Taifa katika kuzilinda Maliasili zetu kupitia mpango wa ujirani mwema**.** Hata hivyo ipo changamoto ya

wanyama waharibifu kuvamia mashamba ya wananchi kujeruhi au kuua wananchi.

**Kamati inaishauri Serikali kupitia upya sheria ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyama waharibifu kwani utaratibu uliopo sasa hauwaridhishi wananchi hali ambayo inawafanya wawachukie wanyamapori na hivyo kutotoa ushirikiano wa kutosha kulinda maliasili hiyo adimu.**

### 2.1.23 Taarifa kuhusu hali ya Ujangili nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kuwepo kwa mbinu mpya ya ujangili ambapo majangili wanatumia sumu kuua wanyamapori. Mbinu hii mpya na ni hatari sana kwa uhifadhi kwani siyo tu inaua wanyama wengi kwa wakati mmoja bali pia inaua wanyama wasiokusudiwa. Aidha majangili wamekuwa wakibadili mbinu za usafirishaji wa nyara za Taifa mara kwa mara na kufanya zoezi la kuwadhibiti kuwa gumu.

**Kamati inaishauri Serikali kubadili mbinu za kupambana na majangili kwa kuongeza vifaa vya mawasiliano, silaha za kisasa na kuunda kikosi maalumu kwa ajili ya kupambana na ujangili na kutumia kikosi chake cha Intelijensia kubaini mtandao wa ujangili wa Tembo nchini ili kuokoa rasilimali hii muhimu iliyo hatarini kutoweka. Kamati inapongeza Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwa na jeshi Usu (Para military) katika kulinda raslimali za wanyamapori.**

**Aidha, Serikali iongeze kasi ya ushirikishwaji wa wananchi wanaishi kuzunguka hifadhi zetu kwa kuwapa elimu na kuhakikisha wanafaidika na Raslimali hiyo, hii itakuwa njia bora zaidi na yenye gharama nafuu ya kupambana na ujangili.**

### 2.1.24 Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2016/2017 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na kuiwasilisha Bungeni.**

2.1.25 **Taarifa kuhusu Maendeleo ya Misitu na Nyuki Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa kuhusu maendeleo ya rasilimali ya Misitu na Nyuki inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Katika taarifa hiyo faida mbali mbali za misitu ziliainishwa ikiwa ni pamoja na kuhifadhi mazingira, kutoa ajira, kupunguza umaskini, kuhifadhi bioanuai, kuhifadhi udongo, chanzo cha nishati na maji. Aidha, misitu ni muhimu katika kurekebisha mfumo wa hali ya hewa na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inatambua mchango mkubwa wa sekta ya misitu katika kukuza uchumi wa nchi kwani huchangia wastani wa **asilimia 3.2** ya Pato la Taifa, na **aslimia 5.9** ya mapato yatokanayo na biashara ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja mchango mkubwa unaofanywa na na sekta hii, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji makubwa ya mazao ya misitu ikilinganishwa na ongezeko la ujazo wa miti, upanuzi wa makazi usio na mipango endelevu ya ardhi na kuwa kichocheo kikubwa cha uvamizi wa misitu ya hifadhi, migogoro ya mipaka baina ya hifadhi za misitu na jamii inayoizunguka hifadhi, matukio ya moto katika misitu, kukosekana kwa nishati mbadala, pamoja na upungufu wa watumishi walioajiriwa kulingana na ukubwa wa eneo la misitu wanalolisimamia.

**Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika usimamizi wa rasilimali misitu kwa kuajiri askari wa kutosha pamoja na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa misitu katika maisha ya kila siku. Aidha, serikali iongeze wataalam wa misitu ili waweze kufanya shughuli za ugani. Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwa nishati**

**mbadala kama vile umeme, gesi na mafuta ya taa hali ambayo itatoa bei nafuu kwa nishati hizi na kuwavutia watumiaji wengi kupunguza utegemezi katika matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kuokoa misitu yetu.**

**Mheshimiwa Spika,** ipo changamoto inayotokana na mfumo wa usimamizi na mgawanyo wa raslimali za misitu ambao kwa kiasi kikubwa unaleta mgongano na mwingiliano katika kusimamia raslimali hizo. Mfano:-

- Serikali kuu kupitia Wakala wa Misitu inamiliki na kusimamia misitu yenye hekta 15.84 millioni sawa na asilimia 35
- Serikali za vijiji hekta 21.6 millioni sawa na asilimia 45
- Serikali za Mitaa hekta 3.36 millioni sawa na asilimia 7
- Sekta binafsi hekta 3.36 sawa na asilimia 7
- Ardhi ya jumla hekta 2.4 millioni sawa na asilimia 5 na,
- Ardhi za miliki nyingine hekta 480.000 sawa na asilimia 1

Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali za vijiji na Serikali za mitaa kwa pamoja zinamiliki asilimia 52 wakati Serikali kuu inamiliki na kusimamia asilimia 35 tu. Aidha uharibifu mkubwa wa misitu unatokea katika misitu ya Serikali za vijiji na ile ya Serikali za mitaaa.

Kamati inashauri kuwa ili kukabiliana na changamoto hii ni **vema usimamizi wa raslimali za misitu zisimamiwe na Mamlaka moja yenye nguvu lakini umiliki wa misitu hiyo ubaki kwa wahusika. Ili kufanikisha hilo ni muhimu Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ikafanywa kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia raslimali za misitu nchini. Aidha Serikali ihakikishe inakiimarisha Chuo cha Misitu cha Olmotonyi ili kitoe wahitimu wa kutosha watakaohudumia misitu yetu kuanzia ngazi ya vijiji.**

### 2.1.26 Taarifa Kuhusu Changamoto ya Kuzibwa kwa Shoroba Katika Hifadhi za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yenye wanyamapori, yakiwemo mapori tengefu,

Mapori ya Akiba, Hifadhi za Jamii (WMA) na Hifadhi za Taifa. Aidha, yapo maeneo mengine yasiyohifadhiwa yalitumika kama mapito ya wanyamapori toka enzi kutoka hifadhi moja kwenda nyingine yaani shoroba. Kwa muda mrefu hapakuwa na sheria ya katazo la shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo,wala hapakuwa na alama zilizokuwa zinaonesha kuwa maeneo hayo ni mapito ya wanyama hali iliyosababisha shoroba nyingi kuvamiwa na sasa ni makazi na mashamba ya watu.

Vile vile, upanuzi wa miundo mbinu ya barabara, umeme, simu na maji pamoja na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi kumesababisha shoroba nyingi kuzibwa hali inayosabisha migogoro ya wanyama kuvamia maeneo ya watu. Kamati ilipata bahati ya kutembelea Jumuiya ya Hifadhi ya wami Mbiki na kujionea jinsi shughuli za kibinadamu zinavyotishia kuziba shoroba hii muhimu inayounganisha ikolojia ya saadan, Mikumi, na Pori la Akiba la Selous inavyotishiwa kutoweka. Aidha Kamati ilijionea jinsi shoroba inayounganisha ikolojia ya Tarangire, Ziwa Manyara na

Ngorongoro inavyotishia kutoweka kutokana na shughuli za binadamu zinazoendelea katika maeneo hayo**. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo hayo, kuzibaini shoroba zote zilizopo na zilizofungwa ili zifunguliwe na kutungiwa sheria ili ziweze kuheshimiwa na kutumiwa na wanyamapori hali ambayo itapunguza migogoro inayotokana na wananchi kushambuliwa na wanyamapori wanapopita katika njia zao za asili.**

### 2.1.27 Taarifa kuhusu Maendeleo ya Utalii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu maendeleo ya utalii nchini. Mbali na mafanikio katika sekta ya utalii bado Serikali haijawekeza vya kutosha katika utalii wa aina nyingine kama vile utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine. Serikali imeelekeza nguvu nyingi katika utalii wa wanyamapori hasa ukanda wa

kaskazini. **Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati itakayohakikisha kuwa vivutio vyote vya Utalii vilivyopo nchini vinaendelezwa na kutangazwa ipasavyo ili kuvutia watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato la Taifa litokanalo na utalii.**


**Aidha, TANAPA iangalie uwezekano wa kupata maeneo ambayo wanaweza kutumia kama Vivutio vya Utalii kwa kuweka Wanyama Pori mbalimbali pamoja na shughuli za Kitalii zinazopatikana kwenye Hifadhi ili kuvutia Watalii wengi zaidi ambao hawana muda wa kufika kwenye Hifadhi. Hii itachangia kukuza Utalii wa ndani na kuongeza ajira kwa Watanzania hasa wanaozunguka maeneo husika.**

### 2.1.28 Mkutano na Wadau wa Uwindaji wa Kitalii nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wadau wa uwindaji wa Kitalii nchini na kupokea malalamiko yao kuhusu hatua ya Waziri wa Maliasili na Utalii kufuta leseni zote za umilikaji vitalu kwa kipindi cha 2018-2022 zilizotolewa kihalali na wizara. Serikali inapaswa kufahamu kwamba biashara ya utalii inahitaji umakini mkubwa *"very delicate"* hivyo mabadiliko kidogo yanaweza kuathiri mpango mzima. Aidha ni biashara inayohitaji muda kujipanga, kuitangaza na kuwapa imani watalii na wawekezaji katika sekta hii.

**Kamati inaishauri serikali kuangalia upya mfumo mzima wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji nchini kwani ni eneo ambalo limelalamikiwa sana na wadau na kwamba kutokuwa na mfumo thabiti na mabadiliko ya mara kwa mara yamelikosesha Taifa mapato kwa vile watalii wa uwindaji wamesitisha safari zao mara nyingi kutokana na kukosekana kwa uhakika wa biashara hii.Mwenendo wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii unaonesha kuwa mapato yameshuka kutoka Dola za kimarekani million 23.5 mwaka 2010 hadi kufikia Dola za Kimarekani million 11.2 mwaka 2015 kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja hapo chini.**

**Kamati inalishauri Bunge Kupitia Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuunda Kamati maalum itakayochunguza changamoto zilizoko katika Tasnia hii na kuishauri Serikali ipasavyo.**




KIELELEZO: Mwenendo wa Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii katika kipindi cha Miaka Sita (2009 - 2015) katika Milioni za Dola za Kimarekani (US$ Milion)

## 2.1.29 **SEMINA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipewa Semina tatu kutoka Mashirika yasiyo ya kiserikali kama ifuatavyo:-

1. *Tanzania Forest Conservation Group* - Semina ilihusu urasmishaji wa sekta ya Mkaa nchini.

2. Oxfam - Semina ilihusu changamoto mbali mbali katika sekta ya ardhi.

3. *Lawyers Environment Action Team na LSP II*- Semina ilihusu mgongano wa kisheria katika usimamizi wa maliasili na ardhi.

Katika semina hizo Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- Wananchi wengi hawazijui sheria za ardhi na hivyo kujikuta wakiingia katika migogoro ya ardhi bila kujua.Vilevile

imebainika kuwa wananchi wengi wanamilikishwa ardhi kwa kutumia majina yasiyo rasmi, hali hii inasababisha mtu mmoja kumiliki viwanja vingi bila kuwa na uwezo wa kuviendeleza na kuwanyima fursa wananchi wengine wenye uwezo wa kuendeleza viwanja hivyo

· Hakuna Sera wala sheria inayoelekeza upandaji,utunzaji na uvunaji wa miti kwa ajili ya matumizi ya mkaa na kuni ambavyo ni vyanzo vikubwa vya nishati majumbani na kwa hali hiyo basi vimekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa Misitu kutokana na ukataji holela wa miti na uchomaji wa mkaa na hivyo kutishia nchi yetu kugeuka jangwa.

· Gharama kubwa za nishati mbadala kama umeme, gesi, na mafuta ya taa zinazosababishwa na tozo mbalimbali zinazotozwa katika nishati hizo na hivyo kuwafanya watu wengi washindwe kumudu gharama zake na kulazimika kutegemea mkaa na kuni pekee kumeongeza shinikizo katika kutumia misitu.

· Kuna mgongano wa baadhi ya sheria ya Ardhi ya vijiji, Sheria ya wanyamapori, Sheria ya Misitu na nyinginezo nyingi zinavyoathiri utekelezaji wa sera mbalimbali.

**Kamati inaishauri serikali kurasimisha sekta ya mkaa kwa kuitungia sera na sheria ili kuinusuru misitu yetu. Aidha Kamati inaishauri serikali kuongeza jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu sheria za ardhi na wajibu wao katika kuzitekeleza ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kwa kukosa elimu. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kuziangalia upya baadhi ya sheria zenye mgongano na kuzirekebisha ili kuondoa mgongano uliopo na kuongeza ufanisi.**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 MAONI

i) Ufinyu wa bajeti na fedha kutotolewa kwa wakati kumesababisha wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kufanya

ukaguzi wa maeneo na uandaaji wa mipango bora ya matumizi ardhi na kusababisha ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi

ii) Kutokuandaa miundombinu ya mifugo nje ya hifadhi kunasababisha wafugaji kuvamia Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Misitu ya Hifadhi na kuzidisha uhasama baina ya Wafugaji na Wahifadhi na kusababisha kuharibika kwa mazingira katika maeneo hayo na kuchangia kukauka na kuharibika kwa vyanzo vya maji, ukame na mabadiliko ya Tabianchi.

iii) Kukosekana kwa utulivu katika sekta ya uwindaji wa kitalii kunakotokana na matamko ya mara kwa mara ya Serikali, pamoja na kubadilika kwa taratibu mbalimbali za ugawaji wa vitalu bila kushirikisha wadau kunasababisha wawekezaji kusita kuwekeza, watalii wawindaji kusitisha safari zao na kulikosesha Taifa mapato

iv) Kutobainishwa kwa mipaka kati ya hifadhi na wananchi wanaopakana na hifadhi kunachangia kuongezeka kwa migogoro ya mipaka katika hifadhi hali inayojenga mahusiano mabaya baina ya hifadhi na wananchi na kusababisha kuongezeka kwa uhasama kati ya askari wa wanyamapori na wananchi

v) Kutorekebisha kanuni zinazohusu maswala ya fidia kama kifuta jasho, na kifuta machozi zilizopitwa na wakati kunapelekea wananchi kutolipwa fidia wanavyostahili na kusababisha hasara na hasira kwa wananchi pale mazao yao yanapoliwa na wanyama waharibifu, au pale wanapojeruhiwa au wanapouawa na wanyama wakali. Aidha inaleta mtazamo hasi kwa wananchi kuwa nchini Tanzania wanyamapori ni bora kuliko binadamu

vi) Serikali kutoweka mikakati, sheria na kanuni madhubuti za kulinda maeneo ya hifadhi hasa njia na mapitio ya wanyama (*Widlife corridors)* kumesababisha baadhi ya shoroba kuzibwa na nyingine zimo hatarini kutoweka.

vii) Kukosekana kwa mikakati thabiti ya kuhamasisha na kutangaza utalii wa ndani kumesababisha mapato yatokanayo na utalii wa ndani kuwa madogo

viii) Uvamizi wa misitu kwa shughuli za binadamu ikiwemo kilimo, ufugaji, makazi na uchimbaji wa madini kumesababisha uharibifu mkubwa wa misitu na hivyo kutishia kuenea kwa jangwa nchini

ix) Kutokuwepo kwa mamlaka moja inayosimamia matumizi ya rasilimali za misitu kunapelekea kukosa udhibiti wa matumizi na kusababisha uharibifu mkubwa wa misitu inayomilikiwa na vijiji na serikali za mitaa

x) Kutotenga fedha za kutosha kwa ajili ya upimaji wa ardhi kunapelekea zoezi la upimaji wa maeneo na uainishaji wa mipaka kukwama na kusababisha ongezeko la migogoro ya Ardhi baina ya watumiaji mbalimbali.

xi) Kutozingatia matumizi ya sheria za ardhi kumesababisha wananchi kuvamia mashamba hasa yale yaliyotelekezwa na ambayo yapo kwenye hatua za ubatilisho na kupelekea ongezeko la migogoro ya ardhi;

xii) Kumiliki ardhi kwa kutumia majina yasiyo rasmi kumesababisha watu wachache kuhodhi ardhi kubwa bila kuiendeleza na kuwanyima fursa watu wengine wenye uwezo wa kuiendeleza

## 3.2 MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

## 3.3 Migogoro ya Ardhi katika maeneo ya hifadhi

Kwakuwa kulikuwa na zoezi la kuainisha na kuhakiki maeneo ya mipaka, na kwa kuwa zoezi hilo lilionekana kukwama kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kuendeleza zoezi hilo, hivyo basi **Serikali ifikirie upya na**

**kutenga fedha za kutosha kwa lengo la kuendelea kuainisha mipaka ya maeneo katika hifadhi ili kumaliza migogoro ya ardhi katika hifadhi na mapori tengefu hapa nchini.**

### 3.4 Migogoro kati ya Hifadhi na Wafugaji

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi ya Wafugaji kukamatiwa mifugo yao kwa madai kuwa wameingiza katika hifadhi, na kwa kuwa hali hiyo imesababisha migogoro mingi kati ya wafugaji na Wahifadhi ikiwa ni pamoja na uhasama, rushwa na mifugo kupigwa mnada au kutaifishwa kinyume cha sheria, Hivyo basi **Kamati inashauri Bunge liunde kamati Teule ya kuchunguza malalamiko na migogoro kati ya Wahifadhi na wafugaji ili iweze kuibaini na kuishauri Serikali hatua za kuchukua kumaliza malalamiko na migogoro hiyo**.

### 3.5 Uvamizi wa Mifugo katika Hifadhi

Kwa kuwa kumekua na ongezeko kubwa la mifugo kuvamia hifadhi kutokana na kukosa miundombinu ya mifugo nje ya hifadhi na kwa kuwa ongezeko hili limesababisha uharibifu kwa uoto wa asili na vyanzo vya maji na kusababisha baadhi ya mito kukauka, hivyo basi kamati inashauri Serikali kujenga mabwawa, visima na malambo katika vijiji vyote vinavyozunguka mapori na hifadhi kwa ujumla.

### 3.6 Uwindaji wa Kitalii

kwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii ametangaza kufuta leseni zote za vitalu vya uwindaji kinyume cha sheria na kusababisha taharuki katika Tasnia ya uwindaji,na kwakuwa hatua hiyo imeondoa utulivu hali inayofanya wawekezaji kusita kuendelea kuwekeza katika vitalu kwa kukosa uhakika wa kumiliki vitalu na baadhi ya wawindaji wa kitalii kusitisha safari zao,hali ambayo imepelekea kushuka kwa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii, Hivyo basi **Kamati inaliomba Bunge kuunda kamati ndogo ya uchunguzi ili ijiridhishe kama mikakati inayochukuliwa na**

**Serikali ya kugawa vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada pamoja na maboresho mengine yatachangia kuongeza pato la taifa litokananlo na sekta ya uwindaji wa kitalii.**

### 3.7 Mabadiliko ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

Kwa kuwa sheria na 413 ya Mwaka 1959 iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imepitwa na wakati, na kwa kuwa sheria hio inaonekana kusababisha mazingira magumu kwa Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kuweza kuwahudumia wananchi wenyeji wa eneo la Ngorongoro, na kwa kuwa ukosefu wa huduma hizo unapelekea migogoro kati ya wananchi wenyeji na wahifadhi, hivyo basi Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuhuisha Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili iendane na hali halisi iliyopo sasa.

### 3.8 Kufanya tathimini ya mfumo wa matumizi mseto ya ardhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitumia mfumo wa matumizi mseto ya ardhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, na kwa kuwa mfumo huo umeleta changamoto nyingi ikiwemo ongezeko la watu na mifugo katika hifadhi linalopelekea kuongezeka kwa gharama za Mamlaka kuwahudumia wananchi wao, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi mseto ya ardhi ili kubaini kama una tija.

### 3.9 Kuzibwa kwa shoroba katika hifadhi za Taifa

Kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali imeshindwa kuorodhesha shoroba na kuziwekea mipaka na sheria, na kwa kuwa hali hio imesababisha wananchi wengi kuvamia shoroba hizo kwa shughuli za binadamu na kupelekea shoroba nyingi kuzibwa na kusababisha baadhi ya vinasaba vya wanyama pori kupotea na kuongezeka kwa matukio ya

wananchi kushambuliwa na wanyama pindi wanyama hao wanapopita katika njia zao za asili (Shoroba), hivyo basi, **Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali ibainishe maeneo yote ya shoroba na kuyawekea mipaka pamoja na kanuni za kuyatambua maeneo hayo ili wanyamapori waendelee kupita bila kusababisha madhara kwa binadamu na mali zao.**

## 3.10 Maendeleo ya Utalii

Kwa kuwa Serikali imewekeza zaidi katika utalii wa Wanyamapori, Na kwa kuwa Serikali haijaonyesha kabisa nia ya kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vingine vya Utalii na hivyo kusababisha kushuka mapato yatokanayo na Utalii, hivyo basi **Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya Utalii vilivyopo nchini ili kuvutia Watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato litokanalo na Utalii. Aidha, serikali inashauriwa kuboresha miundombinu katika maeneo yenye vivutio vya utalii ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo ya utalii**

## 3.11 Kuanzisha mamlaka moja ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu

Kwakuwa kumekuwepo na utaratibu wa wamiliki mbalimbali wa misitu kusimamia matumizi ya misitu wanayomiliki na kwa kuwa hali hiyo imesababisha uharibifu mkubwa wa misitu inayomilikiwa na vijiji na Serikali za Mitaa kwa kukosa udhibiti wa matumizi, hivyo basi Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kuibadilisha Wakala wa huduma za Misitu kuwa Mamlaka itakayosimamia matumizi ya rasilimali za misitu huku misitu ikiendelea kumilikiwa na mamlaka husika.

## 3.12 Mpango kabambe wa kuendeleza miji nchini

Kwakuwa kumekua na ujenzi holela wa makazi ya watu katika miji mingi na maeneo mbalimbali hapa nchini, na kwakuwa ujenzi huo usiofaa unapelekea watu kujenga

bila kuwa na vibali vinavyostahili na kupelekea kuwa na miji isio na mpangilio na hadhi inayostahili mijini, hivyo basi Wizara ya Ardhi kushirikiana na Tamisemi wahakikishe wanaanda mipango kabambe ya kuendeleza miji mikubwa hapa nchini kama ilivyofanya kwa Mwanza na Arusha kwa lengo la kutokomeza ujenzi holela, kuleta hadhi na kuendeleza miji iliyopo nchini Tanzania

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka 2017, yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na wadau wetu wote, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kukushukuru kwa ushirikiano tulioupata kwa mwaka mzima wakati Kamati inatekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai pamoja na sekretarieti ya Kamati hii Ndugu Athuman Hussein, Dickson Bisile,Gerald Magili, Haika Mtui na Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee niwashukuru waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wao kwenye Kamati, hali iliyowezesha kufanikisha kazi zote za Kamati yetu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe.Kemilembe J. Lwota, Mb, - M/Mwenyekiti
2. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb, - Mjumbe

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Mhe. Devotha Mathew. Minja, Mb, | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb, | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb, | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Khalifa Salim Sulemain, Mb, | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Lucy Fidels Owenya, Mb, | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Omari Abdallah Kigoda, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Risala Kabongo, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe.Shabani Omari Shekilindi, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - | Mjumbe |
| 23. | Mh. Nappe Moses Nnauye, Mb | - | Mjumbe |

## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2017, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe.Kemilembe J. Lwota, Mb
**M/MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,**
**MALIASILI NA UTALII**
9 Februari, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa Viti Maalum wameshawasha taa wanakuja hao. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 ili iweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ina sehemu kuu nne. Utangulizi, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu, Maoni na Mapendekezo na mwisho Shukrani na Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza mpaka ya tatu nitaisema kwa ufupi sana, nitajielekeza zaidi kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge Nyongeza ya Nane, kifungu cha (7) Toleo la Januari, 2016 kuwa ni Kusimamia shughuli za Wizara za Maji na Umwagiliaji. Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yatakuwa yameelezwa kwa kirefu katika taarifa yetu na naomba taarifa yote iingizwe katika *hansard* kwa sababu nitasema kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya taarifa yetu ni uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Sehemu ya Pili ya taarifa ninayoiwasilisha inahusu kazi zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika, Kamati ilitekeleza majukumu ya msingi yaliyoainishwa Kikanuni ambapo iliweza kukutana na Wizara na Taasisi inazozisimamia kisha kuchambua na kujadili taarifa za utendaji na uendeshaji na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijielekeze kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji. Baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa kwa kirefu katika taarifa yetu kwa kipindi cha mwaka mmoja, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inasikitishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji uliotolewa mwezi Februari, 2017 Kamati ilipowasilisha taarifa yake ya mwaka 2016/2017 na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu. Hivyo, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wake kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naomba kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati katika maeneo yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza bajeti ya sekta na fedha kutolewa kwa wakati. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji mdogo wa sekta za kilimo, mifugo na maji unachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mdogo katika sekta. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga asilimia 4.9 tu ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatahadharisha kuwa, endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa katika

kuinua sekta hizi, ni dhahiri kuwa mdororo wa uchumi na mnyororo wa umaskini utaendelea kuwa kilio cha wananchi mahali pengi nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanza sasa kutekeleza kwa vitendo Azimio la Maputo, ambalo linazitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sekta ya maji, pamoja na kuwa maji ni hitaji muhimu na la msingi katika kila sekta ya binadamu, bado kumekuwepo na mtiririko usioridhisha wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji nchini. Kwa mfano, Wizara ya Maji - Fungu 49, iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 408.6, hadi kufikia Desemba 2017, kiasi kilichotolewa ni asilimia 25% tu ya fedha za ndani. Aidha, fedha za nje iliidhinishiwa shilingi bilioni 214.9 ambapo hadi Desemba, 2017 fedha iliyopokelewa ni asilimia 1.86% tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 5, iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 5.6, hadi kufikia Desemba, 2017, hakuna fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Tume iliidhinishiwa fedha za nje kiasi cha shilingi bilioni 14.5, hadi Desemba 2017, Tume imepokea fedha za nje asilimia 1.6 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa utoaji fedha haukidhi kiu ya wananchi kupata huduma ya maji. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuwa na uhakika wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa maslahi mapana ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza mipango ya uzalishaji wa mbolea nchini. Pamoja na mafanikio yaliyokwishaonekana katika utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, bado ipo haja ya kuondokana na uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuzalisha mbolea hapa nchini kwa kujenga viwanda vya

kuzalisha mbolea au kuweka mazingira rafiki kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika kuwekeza katika tasnia ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, Kamati inashauri Serikali kuanza ujenzi wa viwanda vya mbolea vya Kilwa na Mtwara. Pendekezo hili linazingatia ukweli kuwa, asilimia 90% ya mbolea inayotumika nchini kwa sasa inaagizwa kutoka nje na kwamba, hadi kufikia Februari 2018, kiasi cha mbolea iliyoingizwa nchini ni tani 233,001.49 ambayo ni asilimia 48 ya mahitaji na hivyo kuwepo kwa upungufu wa asilimia 52%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na hatua ya Serikali kufanya ununuzi wa mbolea kwa pamoja, bado upatikanaji wa mbolea nchini katika maeneo ya uzalishaji mkubwa haukidhi mahitaji. Bei ya mbolea haijashuka kama ilivyokusudiwa na upatikanaji wa mbolea umekuwa siyo wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya mafanikio ya malengo ya mpango huu, kisha kuchukua hatua stahili. Vilevile Kamati inashauri kuwa, ili kuifanya Kampuni ya Mbolea ya Taifa *(Tanzania Fertilizer Company)* kuwa na ufanisi wa kutosha katika tasnia ya mbolea, Serikali ihamishe kampuni hii chini ya usimamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na kuiweka chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili likitekelezwa litasaidia kuondokana na vikwazo na hujuma zinazoweza kutokana na siasa ya dunia inayofungamana na biashara ya mbolea inayofanywa na makampuni ya kimataifa ya mbolea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji, masoko na usalama wa chakula nchini. Utoshelevu wa chakula ni nguzo muhimu katika kupanga kiwango cha uzalishaji, kujenga mazingira mazuri ya kilimo cha biashara na uratibu wa masoko. Kamati imebaini kuwa, katika nyakati tofauti Serikali imekuwa ikitoa maagizo na amri au zuio kuhusu biashara ya

uuzaji mahindi nje ya nchi ambayo kwa kiasi fulani yamekuwa yakiathiri biashara ya mahindi na uzalishaji, hususan wanaofanya kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uratibu wa usimamizi kwa kutekeleza mikakati madhubuti ya kupata takwimu sahihi na kwa muda unaostahili kuhusu kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali zitakazosaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi kwa mwenendo wa biashara ya ndani na nje ya mipaka hususan kwa mazao ya nafaka bila ya kusababisha athari mbaya katika uzalishaji, biashara na bei ya mazao. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kujenga na kukarabati maghala ili kuwa na uhakika na usalama wa hifadhi ya nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuimaririsha masoko ya mazao ya mahindi na mbaazi kwa wakulima nchini. Kamati inaitahadharisha Serikali juu ya uwezekano wa uzalishaji kwa msimu kwa 2017/2018, kuwa pungufu kutokana na wakulima kutouza mahindi hivyo kukosa fedha za kununulia pembejeo kwa msimu huu. Aidha, baadhi ya wakulima wa mahindi na mbaazi kutolima kabisa baada ya kukata tamaa ya kukosa soko la mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalishauri Bunge, liitake Serikali kuharakisha kutafuta masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi ili wakulima waweze kuuza mazao yao na kufanya kilimo cha biashara. Kamati inaitahadharisha Serikali kutotegemea nchi moja ya India kwa ajili ya soko la mbaazi na kunde kwa ujumla. Aidha, Serikali itoe fedha za ziada kwa *NFRA* na *CPB* kama hatua ya dharura ya kuziwezesha kununua mahindi na mbaazi ambazo bado hazijanunuliwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nilizoeleza, kulikuwa na upungufu wa chakula katika maeneo mengine ya nchi na kupelekea bei kuwa juu. Kamati inaishauri Serikali kuratibu na kusimamia masuala ya uzalishaji masoko, bei ya nafaka na mazao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji na masoko ya mazao ya biashara. Kamati imebaini kuwa katika miaka ya hivi karibuni mazao ya biashara yakiwepo pamba, tumbaku na kahawa yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, matumizi duni ya teknolojia na pembejeo, masoko machache ya ndani na utegemezi wa soko la nje, kuendelea kupungua na kukosekana kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kukosekana kwa mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kuchukua hatua madhubuti kusimamia na kuimarisha vyama vya ushirika, kuongeza matumizi ya teknolojia ya kisasa na pembejeo katika uzalishaji, kutafuta masoko ya uhakika ya mazao na muhimu zaidi kuchukua hatua za makusudi katika kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji na masoko ya mazao ya bustani. Sekta ndogo ya mazao ya bustani ikihusisha mbogamboga na matunda imekuwa ikitoa ajira kwa wananchi na hasa vijana na kinamama. Kuongezeka kwa mahitaji ya matunda na mboga kunatoa fursa ya ajira, kipato na uchumi wa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uzalishaji wenye tija, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira rafiki kwa kutunga sera, sheria, kanuni za kilimo hiki. Pia kuongeza kasi, kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ya uzalishaji, kuchakata na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa ili kuwa na uhakika wa kufikisha mazao hayo katika masoko bila ya kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Ukosefu wa mikopo ya uhakika na yenye riba nafuu kwa wakulima walio wengi ni kikwazo kwa wakulima kutoweza kukopa na kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Benki ya Kilimo hadi mwezi Desemba, 2017 ilikuwa na mtaji wa

kiasi cha Sh.66,785,790,739. Aidha, kiasi cha mtaji kilichoombwa ni shilingi bilioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili ibebe jukumu hili la kutoa mikopo kwa wakulima wengi zaidi katika maeneo mbalimbali ya nchi. Aidha, ili kufikia azma hii, Kamati inasisitiza kuwepo uwiano wa mtawanyiko wa huduma zitakazotolewa na benki hii katika maeneo ya uzalishaji vijijini ili kutoa elimu na kuhamasisha utoaji mikopo ya kilimo cha biashara badala ya ilivyo sasa ambapo inaendesha shughuli zake katika maeneo machache ya mjini, ambayo si wakulima wote wanaweza kuzifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la migogoro ya matumizi ya ardhi. Migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na kuathiri uzalishaji katika sekta mbalimbali za kilimo na ufugaji kutokana na hofu, uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mali na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kamati inasisitiza kuwa, migogoro ya matumizi ya ardhi ni mtambuka na hivyo suluhu yake inaweza kupatikana kupitia jitihada za pamoja miongoni mwa sekta husika. Kamati imeelezwa kuwa katika kulifanyia kazi suala hili, katika nyakati tofauti Serikali imeunda Tume na kuhusisha Wizara tano zinazohusika na migogoro hii ya ardhi. Kamati inahoji juu ya lini mapendekezo ya Tume hii yatatoka na yatatekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa taarifa za mamlaka mbalimbali za Serikali zinaeleza kuwa suluhisho la migogoro iliyopo ni kutekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi nchini. Kamati inalishauri Bunge liazimie kuitaka Serikali kutekeleza kwa vitendo maoni na mapendekezo yaliyokwishatolewa na Tume iliyoundwa. Aidha, Serikali iongeze kasi ya kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na. 5 ya mwaka 1999, pamoja

na kuhuisha sheria zingine zinazosimamia matumizi, umiliki, uhifadhi ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna malalamiko mengi ya ardhi kutoka kwa wananchi na hasa wafugaji ili kutenda haki, Kamati iliomba tuunde Kamati Ndogo ndani ya Kamati ili kuangalia na kufuatilia malalamiko kati ya wafugaji na hifadhi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali za uvuvi na udhibiti uvuvi haramu nchini. Sekta ya uvuvi haijalinufaisha Taifa kwa kiwango kinachostahili. Makisio ya rasilimali za uvuvi nchini ni tani 2,143,211. Makadirio ya kiasi cha samaki wanaoweza kuvuliwa ni tani za 730,000 kwa mwaka. Aidha, kiasi kinachovuliwa kwa sasa ni tani za mita 350,000 tu kwa mwaka. Mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa ni asilimia 2% tu na uwezo wa mchango wa sekta ya uvuvi endapo kungekuwa na uwekezaji wa kutosha unaozingatia uwezo wa rasilimali za uvuvi zilizopo ni tani za mita 730,000 na ingeweza kuchangia asilimia 4.2 katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya kuongeza tija katika sekta ya uvuvi imeshindwa kutekelezeka kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa, kuidhinishwa na kutolewa. Kwa mfano, katika bajeti ya 2017/2018 miradi ya maendeleo katika sekta ilitengewa kiasi cha Sh.6,000,000,000, hadi kufikia Desemba 2017, hakuna fedha yoyote iliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na mwenendo huu wa kutotolewa fedha zinazoidhinishwa katika sekta ya uvuvi. Aidha, inaomba Bunge kupitisha Azimio la kuitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha na kuitoa kwa wakati stahiki ili kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya uvuvi hususan kutekeleza Mpango wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kule Dar es Salaam au Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika utendaji wake imebaini kuwepo malalamiko mengi yanayohusu namna kampeni ya kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Viktoria inavyoendeshwa na kwamba imesababisha hasara kubwa

kwa wavuvi kwa kuchomewa kambi za wavuvi, mitumbwi, nyavu na nyenzo zingine. Kufuatia malalamiko yaliyopo, Kamati inatilia shaka njia zinazotumika katika udhibiti vitendo vya uvuvi haramu kama inaweza kuleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na ukweli kuwa, jitihada kubwa zilipaswa kuelekezwa katika kudhibiti utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi, badala ya kuharibu nyenzo za uvuvi kama mitumbwi ambayo si nyenzo haramu na kuacha wananchi wavuvi wakiwa maskini na bila ya msaada wowote wa zana bora na mafunzo ya mbinu bora za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ikizingatiwa kuwa Ziwa Viktoria linatumiwa pia na nchi ya Uganda na Kenya jitihada hizi zilipaswa kushirikisha nchi zote, ili kuwa na namna moja ya kudhibiti uvuvi haramu, kwani baadhi ya nyezo zinazokatazwa kutumika Tanzania, zinatumika katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hatari ya Watanzania kuhifadhi rasilimali katika Ziwa Viktoria na wanufaikaji kuwa wavuvi wa nchi jirani. Kamati inashauri Serikali kutathmini hatua na njia zinazotumika kudhibiti uvuvi haramu ili ziwe shirikishi zaidi pamoja na msisitizo kuwa ni kuzuia utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika Ranchi ya Taifa. Ranchi ya Taifa ni rasilimali muhimu na fursa kubwa katika kuchangia pato la Taifa na uchumi wa wafugaji. Tanzania ina jumla ya ranchi 13 zenye ukubwa wa jumla ya hekta 627,856, katika mikoa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi, Kamati imeelezwa hali ya uwekezaji uliopo katika Ranchi za Taifa, changamoto na mafanikio na kujiridhisha kuwa fursa na rasilimali ya Ranchi za Taifa haijatumika ipasavyo. Ili kuwa na uwekezaji wenye tija kwenye Ranchi za Taifa, Kamati

inaishauri Serikali kufanya uwekezaji wa kisasa katika Ranchi za Taifa ambao utasaidia wafugaji wengi kujifunza mbinu za ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza ushauri uliokwishautoa mwaka jana wa kuitaka Serikali kufanya tathmini ya matumizi yaliyopo, kisha kuweka mikakati ya kuona namna ya kuruhusu wananchi waishio karibu na ranchi hizi, ili kupata huduma za malisho na maji kwa ajili ya mifugo kwa utaratibu utakaoonekana unafaa. Aidha, ni vyema Serikali ikaandaa na kutekeleza mkakati wa makusudi wa kuongeza thamani ya mazao ya mifugo kwa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo ili kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa kutambua kuwa nchi yetu ina fursa na maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo takwimu zinaonesha Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo, eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hadi sasa ni hekta 461,326 sawa na asilimia 1.6 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho wa uzalishaji wa zao la mahindi kwa hekta kwa kufanya umwagiliaji ni tani 3.75 kwa hekta, wakati kulima kwa kutegemea mvua ni tani 2.7 kwa hekta. Kwa zao la mpunga ni tani nne mpaka tano kwa hekta, wakati uzalishaji kwa kutegemea mvua ni tani mbili hadi tatu kwa hekta. Hii ni katika maeneo yanayofanana na matumizi ya pembejeo na teknolojia sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tofauti hii ya uzalishaji, Kamati inashauri kuwa, katika kipindi hiki ambapo mabadiliko ya tabianchi yamepelekea mvua kutokuwa za uhakika na kuathiri uzalishaji, umwagiliaji ni moja ya njia muhimu ya kuongeza na kuimarisha uzalishaji wenye tija, hivyo Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kuitengea Tume ya Taifa ya Umwagiliaji bajeti ya kutosha itakayowezesha

Tume kuandaa miundombinu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na hivyo kupunguza utegemezi wa kilimo cha mvua ambacho kinazidi kutotabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuainisha maeneo machache ya kipaumbele yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha hizo katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza kazi ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya kimkakati. Kamati ilibaini kuwepo miradi ya mabwawa nchini ambayo inachukua muda mrefu kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha. Kutokamilika kwa ujenzi wa mabwawa kwa muda uliopangwa kunaisababishia Serikali hasara kutokana na miundombinu ya miradi hiyo kuchakaa kabla ya kuanza kutumika, lakini pia kuongezeka kwa gharama za ujenzi tofauti na ilivyokadiriwa na hivyo kuwakosesha wananchi huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kujenga na kukarabati miradi inayoendelea ili kuepusha hasara inayoweza kutokea kutokana na miradi kuchukua muda mrefu lakini pia kuweza kufikia malengo na makusudio ya miradi hiyo kwa wananchi kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa hadi Desemba, 2017, hali ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa wastani wa asilimia 56 kwa vijiji na asilimia 69 kwa mijini. Aidha, malengo ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni asilimia 85 kwa vijijini na 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina wasiwasi juu ya kufikiwa kwa malengo hayo kwani kumekuwa na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maji. Kwa mfano, katika

bajeti ya mwaka 2017/2018, fedha za maendeleo zilizotengwa kwa Fungu 49 ni asilimia 17 tu na zilizotolewa hadi kufikia Desemba, 2017, kiasi kikubwa asilimia 77 zikiwa ni fedha za Mfuko wa Maj. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na kwamba fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maji vijijini kutokana na Mfuko wa Maji, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri uliotolewa katika Taarifa ya Kamati ya mwaka 2016 kuwa Bunge liazimie kuitaka Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 kwa kuweka tozo ya Sh.100 kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli. Mapendekezo haya yakizingatiwa yataiwezesha miradi ya maji kutekelezwa kwa ufanisi nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya uratibu wa Mfuko wa Maji Mjini kwa ajili ya kupata fedha za uhakika kwa ajili ya miradi ya maji mjini ambapo takwimu zinaonesha kuwa bado upatikanaji wa maji katika maeneo mengi mjini siyo wa hakika. Vilevile kutokana na dosari iliyobainika ya kuwepo na usimamizi usiokidhi wa uendeshaji wa miradi ya maji katika maeneo mengi vijijini, Kamati inalishauri Bunge liazimie kuitaka Serikali kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini ambao pamoja na mambo mengine utakuwa na jukumu la kuratibu na usimamizi wa miradi ya maji vijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali kuongeza kasi ya utoaji fedha za bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya maji kadri zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekwa kwa mazingira bora ili kuchochea sekta binafsi kushiriki kuwekeza katika tasnia za kilimo, mifugo, uvuvi na maji. Utendaji wa Kamati katika nyakati tofauti na maeneo mbalimbali umebaini kuwepo malalamiko kutoka kwa wadau wa Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji ya kutokuwepo mazingira wezeshi ya

kuwekeza katika sekta tajwa kwa tija. Kwa ujumla, malalamiko yao yanajikita katika kuwepo changamoto ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuwepo mamlaka nyingi za Serikali za Udhibiti unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji;

(ii) Ushindani usio wa haki unaosababishwa na bidhaa kutoka nje;

(iii) Tozo nyingi kwa baadhi ya bidhaa, mfano ladha ya maziwa, vifungashio na mengine;

(iv) Ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini unaosababisha ugumu wa kulima kufikisha bidhaa katika masoko au viwanda kwa muda unaostahili; na

(v) Ukosefu wa umeme wa uhakika kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto hizi kwa kuongeza kasi ya kuwekeza na kuweka mazingira bora yasiyo na urasimu yatakayowezesha na kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwa faida katika sekta hizi ili vijana wapate ajira, mazao yawe mengi na masoko vilevile yawe mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mktaba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi. Baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, na kwa kuwa mkataba huu unahusisha Nchi za Tanzania na Malawi ambazo zimekuwa na mgogoro wa mara kwa mara kuhusu mpaka wa Ziwa Nyasa, Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari na kuhakikisha utekelezaji wa mkataba

huu hauathiri faida ambazo nchi imekuwa ikipata kutoka Ziwa Nyasa na Mto Songwe;

(ii) Kwa kuwa nchi ya Tanzania na Malawi zimekuwa na mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa kwa muda mrefu na kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa, kama nilivyosema, ni Mto Songwe, pamoja na kwamba mkataba huu unahusu Mto Songwe, Kamati inaishauri Serikali kupitia fursa ya mkataba huu kufanya utambuzi wa mipaka ya Ziwa Nyasa, hatua ambayo inaweza kumaliza kabisa mgogoro huo;

(iii) Kwa kuwa mkataba huu unahusisha nchi mbili, ni vyema baada ya kuridhiwa na Bunge Serikali ihakikishe inatunga sheria na kanuni zake ili wananchi wa Tanzania waanze kunufaika.

(iv) Baada ya nchi wanachama kuridhia utekelezaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la...

**MWENYEKITI:** Nakupa dakika moja utoe maazimio, muda wako umekwisha, si imeshaingia kwenye *Hansard*.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO, NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* lakini kulikuwa na suala la wadudu katika kilimo cha pamba, naomba Serikali ione kwamba wadudu hawa hawamalizi zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la korosho ambayo imewekewa mchanga na mawe, naomba Serikali ione kila inachowezekana ili ichukue hatua kwa wale wanaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ni hitimisho na shukrani. Napenda kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mifugo na Maji na Kilimo. Nawashukuru sana Wajumbe na Bunge

zima kwa ushirikiano ambao wametoa. Nawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote kwa ushirikiano waliotupa na tutaendelea kushirikiana nao. Hii ni sekta iliyo muhimu sana, hili ni eneo ambalo Watanzania wote wanategemea tujadili na tuisaidie Serikali iweze kufanya yale inayotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na nakushukuru wewe binafsi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA MWAKA 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**[***Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016***]**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MAELEZO YA JUMLA**

**1.0 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, ili iweze kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

1.1 **Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane kifungu cha 7, Toleo

la Januari, 2016 kuwa ni kusimamia shughuli za Wizara za Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, kifungu cha 7(1) kinafafanua majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambayo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ni moja kati ya Kamati hizo na ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kushughulikia bajeti za Wizara ya Maji na Umwagiliaji,Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara; na

(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### 1.2 Njia/Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, kwa mujibu wa kanuni, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali zilizosaidia kazi za Kamati kufanyika kwa ufanisi. Mbinu hizo ni pamoja na:-

(a) Kufanya vikao vya kupitia, kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali kuhusu utendaji katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji;

(b) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha juu ya thamani ya fedha (*value for money*) zilizogharamia miradi hiyo;

(c) Kufanya ziara za mafunzo katika miradi iliyotekelezwa na sekta binafsi ikiwemo Muungano wa Vikundi vya wakulima Tanzania- MVIWATA mkoani Morogoro pamoja na shughuli zilizotekelezwa au kuwezeshwa na Ushoroba wa

Kilimo Kusini mwa Tanzania- SAGCOT katika mikoa ya Iringa na Njombe;

(d) Kukutana na wadau na kupokea maoni yaliyotumika kuboresha Azimio la Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe; na

(e) Kupata mafunzo na semina mbalimbali zilizoandaliwa na wadau wanaojihusisha kwa namna moja ama nyingine na shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na maji.

### 1.3 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuundwa kwake, Kamati imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo:-

(a) Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017;

(b) Kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018;

(c) Kushughulikia taarifa za utendaji kuhusu masuala mbalimbali ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2017/ 2018;

(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara za Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017;

(e) Kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017; na

(f) Kufanya ziara za mafunzo katika miradi iliyotekelezwa na MVIWATA katika mkoa wa Morogoro na shughuli zinazotekelezwa au kuwezeshwa na Ushoroba wa Kilimo Kusini mwa Tanzania- SAGCOT katika mikoa ya Iringa

na Njombe kwa lengo la kupata ufahamu kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi na uratibu wa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuweza kuishauri Serikali hatua madhubuti za kuchukua kuongeza tija katika uzalishaji na pato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla; na

(g) Kuhudhuria Semina zilizotolewa na wadau mbalimbali wa sekta kwa lengo la kutoa elimu juu ya masuala ya sekta, kama ifuatavyo:-

i) Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Kilimo mnamo tarehe 28 April na 03 Mei 2017, lengo la semina hizi lilikuwa ni kuwapa uelewa mpana Wajumbe wa Kamati kuhusu shughuli na programu za SAGCOT na NFRA ambazo zinatekelezwa na Wizara, ili waweze kuishauri Serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

ii) Semina iliyoandaliwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), tarehe 30 Mei,2017 lengo la semina hii ilikuwa ni:-

- Kuwezesha uzalishaji endelevu na kuongeza uzalishaji na ushindani katika kilimo;

- Kuimarisha soko la bidhaa za kilimo kikanda na kimataifa;

- Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na ya Umma kwenye uwekezaji wa mnyororo wa thamani kwenye sekta ya kilimo; na

- Kupunguza vihatarishi vya kijamii na kiuchumi kwenye ukanda wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC) kutokana na usalama wa chakula na lishe.

iii) Semina iliyoandaliwa na Tanzania Civil Society Forum on Climate Change (FORUM CC), iliyofanyika tarehe 16 Septemba 2017. Dhumuni la Semina hii ilikuwa ni kuwasilisha Utafiti ambao ulihusu uchambuzi wa jinsia juu ya Sera ya Bajeti kuhusu Kilimo.

iv) Semina iliyoandaliwa na OXFAM, iliyofanyika tarehe 14 Novemba, 2017. Lengo lilikuwa ni kuwapa uelewa Wajumbe wa Kamati kuhusu masuala ya haki ya ardhi na mambo mengine kuhusiana na hayo.

v) Semina iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Uvuvi katika Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority*) iliyofanyika 17 Oktoba 2017, lengo lilikuwa ni kuwapa Wajumbe uelewa wa pamoja kuhusu fursa zitokanazo na uvuvi wa Bahari Kuu, changamoto zilizopo, hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua ili kunufaika na mazao yatokanayo na bahari.

vi) Mafunzo kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa miswada na uchambuzi wa bajeti.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Taarifa ninayoiwasilisha inahusu kazi zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018. Katika kipindi husika, Kamati ilitekeleza majukumu ya msingi yaliyoainishwa Kikanuni ambapo iliweza kukutana na Wizara na Taasisi inazozisimamia kisha kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji na Uendeshaji na hatimae kutoa maoni, ushauri na mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika,** ufuatao ni uchambuzi wa shughuli /maeneo yaliyoshughulikiwa na Kamati tangu Januari 2017 hadi Januari 2018

## 2.2 Mpango wa bajeti na umuhimu wa sekta za kilimo, mifugo, na uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Mpango unabainisha kuwa, Tanzania imeendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Wananchi wake, kwa kuwa kilimo kinatoa ajira kwa **asilimia 75%** ya Watanzania na inachangia **asilimia 100%** ya chakula kinachopatikana nchini. Aidha, kutokana na asilimia kubwa ya wananchi kushiriki katika shughuli za kilimo, kilimo kinachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini na kuongeza kipato; Mfano Sekta ya Kilimo imechangia **asilimia 28.0** ya pato la Taifa kwa mwaka 2014 na kupanda kufikia **asilimia 29** mwaka 2015.[1] Vile vile Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa vinatambua Kilimo kama sekta muhimu katika Uchumi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, Kamati ina wasiwasi kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa malengo hayo kutokana na mwenendo unaojidhihirisha wa kiasi kidogo cha bajeti inayotengwa na kutolewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa sekta ya kilimo kama unavyoelezewa kupitia Mipango, Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali, bado sekta hii imekuwa haipewi msukumo wa kutosha kama kipaumbele cha uhai na ustawi wa sekta zingine za uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake, imebaini kuendelea kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo kila mwaka. Kwa mfano: kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 bajeti ya kilimo ilikua asilimia **7.8%,** ya bajeti yote ya Serikali, Mwaka wa Fedha 2011/2012

---

[1] Taarifa ya Baraza la Kilimo Tanzania kuhusu mchango wa sekta ya Kilimo katika pato la Taifa

ilikua asilimia **6.9%** ya bajeti yote ya Serikali na Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali ilitenga **asilimia 4.9%** tu ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya Sekta za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** kuendelea kushuka kwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya Kilimo, kumepelekea uwekezaji mdogo na hivyo kusababisha ukuaji mdogo wa sekta hii, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ukuaji wa sekta ya kilimo ni asilimia **1.7%** ikilinganishwa na sekta zingine kama madini ambayo ukuaji wake ni asilimia **16.6 %,** uchukuzi asilimia **15.6,** habari na mawasiliano asilimia **13.5%.**[2] Aidha, katika kipindi cha nusu mwaka, disemba 2017, kilimo kinakadiriwa kukua kwa asilimia **3.1%.** Ukuaji huu bado hauridhishi ukilinganishwa na ukubwa wa sekta yenyewe.

### 2.3 Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement*)

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Kilimo ya Taifa ya mwaka 2013 inaelezea umuhimu wa kuongeza matumizi ya pembejeo za kisasa (mbolea, madawa ya kilimo, mbegu bora na zana za kilimo) kama mhimili imara wa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao; kupunguza umaskini; na kuwa na usalama wa chakula na lishe. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa pembejeo hapa nchini. Hata hivyo, suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo, bei kubwa, usambazaji na matumizi yaliyo sahihi ya Mbolea, Mbegu Bora, pamoja na Madawa ya Viuatilifu kutokidhi mahitaji.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yanajihidhihirisha kwenye taarifa ya Benki ya Dunia ambayo inaeleza kuwa, ili kuwa na kilimo chenye tija, wastani wa matumizi ya mbolea ni kilo **119.9** kwa hekta. Hapa nchini matumizi ya mbolea ni wastani wa kilo **10** za mbolea kwa hekta moja, kiwango ambacho ni chini sana ya viwango stahiki.

---

2 Taarifa ya Baraza la Kilimo Tanzania kuhusu ukuaji mdogo wa sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** matumizi hayo kidogo ya mbolea hapa nchini hayajaleta tija inayokusudiwa katika kilimo. Katika kukabiliana na changamoto na kuongeza matumizi ya mbolea na kuongeza tija katika uzalishaji, Serikali imeanzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement*), mfumo ambao unalengo la kuwawezesha wakulima wadogo kupata mbolea yenye ubora na kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi, Kamati ilielezwa na kuridhika na faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, ambazo ni pamoja na:-

(i) Kudhibiti bei ya mbolea kwenye soko holela;

(ii) Nchi itafaidika kwa ununuzi wa pamoja kwa lengo la kupata punguzo kutokana na kiasi kingi kinachonunuliwa (*economies of scale*) na kupunguza gharama za uendeshaji (*overhead cost*);

(iii) Kupunguza monopoly na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kukua na kushiriki katika biashara ya mbolea na hivyo kuimarisha mtandao wa usambazaji hadi ngazi ya mkulima;

(iv) Kuongeza upatikanaji wa mbolea;

(v) Kupunguza bei ya mbolea;

(vi) Mfumo utasaidia kuimarisha utaratibu wa usambazaji wa mbolea ambapo wadau wote watapata uhakika wa upatikanaji wa mbolea kwa bei ya ushindani katika soko;

(vii) Itaongeza ufanisi kwa kudhibiti mbolea kutoka nje kwa kuagiza mara chache kwa kiwango kikubwa, tofauti na hali ilivyo sasa ambapo mbolea imekuwa ikiingizwa mara nyingi kwa kiwango kidogo kidogo;na

(viii) Kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mbolea nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida hizo zinazotarajiwa kupatikana kutokana na kuanza kutekelezwa kwa mfumo huu katika msimu wa kilimo wa 2017/2018; Kamati imebaini ipo vita kubwa inayofanywa na kampuni kubwa na za kimataifa za mbolea ambazo zimekuwa zikifanya biashara ya mbolea hapa nchini kwa kuwauzia mbolea kwa bei kubwa wakulima wetu wadogo na maskini hali iliyosababisha wakulima wadogo kuendelea kunyonywa, kuwa maskini na kutopata faida ya kazi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hali hiyo, Kamati ilijiridhisha na faida za utaratibu mpya wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, kisha kutoa maoni na ushauri kwa Serikali wa tahadhari za kuzingatia na namna bora ya kuhakikisha kuwa utaratibu mpya unamaliza changamoto ya matumizi yasiyokidhi ya mbolea nchini. Hivyo, kamati iliitaka Wizara kuchukua tahadhari muhimu na kuhakikisha kuwa hakuna uwezekano wa kampuni kubwa za ndani na nje ya nchi za utengenezaji na usambazaji mbolea kutoweza kuhujumu mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja na kuhakikisha kuwa katika msimu wa kilimo 2017/2018 upatikanaji wa mbolea, kwa bei nafuu na kwa wakati unaostahili unakuwa wa uhakika.

### 2.4 Usalama wa Chakula Nchini

Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Hali ya Chakula nchini. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa hali ya chakula kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ni nzuri na imeendelea kuimarika kulingana na mavuno mazuri na ya ziada yaliyopatikana msimu wa kilimo wa 2015/2016. Tathimini iliyofanyika mwezi Julai 2016 imeonesha nchi ilikuwa na hali ya chakula ya kiwango cha utoshelevu wa ziada kwa **asilimia 123** ambapo mazao ya nafaka ni **asilimia 113** na mazao yasiyo ya nafaka ni **asilimia 140**.

Katika uchambuzi, Kamati ilibaini kuwa yamekuwepo malalamiko mengi ya namna ambavyo Serikali imekuwa

ikiweka na kuondoa makatazo/zuio la kuuza baadhi ya mazao ya chakula nje ya nchi. Makatazo haya yamekuwa yakikatisha tamaa wazalishaji kwani hawana uhakika wa kurudisha gharama za uzalishaji.

Kufuatia hoja hiyo, Kamati ilipata ufafanuzi kuwa, agizo la serikali la kufunga mipaka ya masoko ya mazao ilikua ni hatua ya dharura katika kukabiliana na kasi kubwa ya uondoaji wa mazao nje ya nchi, kutokana na vibali mbalimbali vilivyotolewa na mamlaka mbalimbali, hali iliyoashiria wizara kushindwa kudhibiti uratibu wake wa kuhakikisha kuwa kunakua na usalama wa chakula nchini. Na kwamba lengo la Serikali halikua kuzuia biashara ya mazao yote kama ambavyo ilieleweka kwa baadhi ya wananchi na wadau, bali ililenga mazao ya nafaka hususan mahindi, mchele na mpunga ambayo kwa takwimu za wizara, vibali vilivyokuwa vimetolewa vilikua vinaruhusu utoaji wa mazao hayo zaidi ya kiasi

kilichokuwepo nchini. Hali hii iliashiria kutishia usalama wa chakula nchini. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa, pamoja na nchi kuwa na utoshelezi wa chakula, yalikuwepo maeneo yaliyokuwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na uzalishaji katika maeneo hayo kuwa mdogo pamoja na kukosekana kwa uratibu mzuri wa uondoaji nafaka kutoka katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa kwenda maeneo yaliyokuwa na upungufu.

### 2.5 Mikakati ya kuimarisha masoko ya mazao ya mahindi na mbaazi kwa wakulima nchini

Kumekuwapo na ukosefu wa masoko ya uhakika ya mahindi na mbaazi yaliyozalishwa kwa wingi msimu uliopita 2016/17. Wakulima wengi bado wana mazao hayo majumbani mwao na wamekosa pa kuuza na hivyo kupata wakati mgumu wa kumudu gharama za pembejeo kwa kilimo cha msimu 2017/18. Kamati ilitaka kupata taarifa ya Wizara kuhusu hatua ilizochukua kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mazao hayo.

Kwa zao la mbaazi Wizara ilieleza kwa kina changamoto iliyotokea ya ahadi ya Serikali ya India kununua mbaazi kwa wingi katika msimu uliopita, ahadi ambayo ilisababisha Serikali kuhamasisha uzalishaji zaidi wa zao hilo. Baada ya wakulima kuzalisha kwa wingi wakati wa mauzo ahadi ya kupata fursa ya soko nchini India ilifutwa. Hatua hii ilipelekea wakulima kubaki na mazao yao. Kamati imeelezwa kuwa Serikali inaendelea na jitihada za kupata soko la mbaazi ndani na nje ya nchi. Jitihada ambazo, mpaka sasa hazijafanikisha kupata soko la kutosheleza.

Kwa upande wa mahindi, Kamati ilielezwa kuwa Taasisi za umma za NFRA NA CPD zimepewa maelekezo ya kununua mahindi kutoka kwa wakulima kama njia ya kupunguza uhaba wa soko la mahindi. Pamoja na jitihada hizo, bado wakulima wengi wanayo mahindi waliyozalisha msimu uliopita na hawajui pa kuyauza. Kamati inaitahadharisha Serikali juu ya uwezekano wa uzalishaji kwa msimu wa 2017/2018 kuwa pungufu kutokana na wakulima kukosa pembejeo na baadhi kutolima kabisa baada ya kukata tamaa ya kukosa soko la mazao yao.

### 2.6 Mikakati ya kuinua baadhi ya mazao ya biashara ya Korosho, Pamba, Tumbaku na Kahawa

Mazao ya Korosho, Pamba, Tumbaku na Kahawa ni mazao ya biashara ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakichangia fedha nyingi za kigeni kwenye pato la Taifa. Katika miaka ya hivi karibuni mazao haya yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, matumizi duni ya teknolojia na pembejeo, masoko machache ya ndani na utegemezi wa soko la nje, kuendelea kupungua na kukosekana kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kwa mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo.

Kwa msingi huu Kamati iliibua hoja za kuitaka Serikali kuainisha Mipango na utekelezaji wake ili kuinua uzalishaji wa mazao tajwa kwa lengo la kuongeza mchango wa

mazao hayo katika pato la Taifa na uchumi wa mtu mmoja mmoja. Pamoja na hoja za jumla zilizoibuliwa, Kamati pia ilitaka kupata maelezo ya Serikali juu ya hatua zinazochukuliwa, ambapo ilitaka kupata maelezo juu ya:-

a) Hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na kuendelea kushuka kwa mahitaji ya tumbaku duniani na vita dhidi ya matumizi ya bidhaa ya Tumbaku.

b) Hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kudhibiti kampuni kubwa zinazojihusisha na ununuzi wa tumbaku nchini, ambazo zimekuwa zikifanya njama ya kuzuia wadau wengine pamoja na kutengeneza mazingira magumu kwa wazalishaji kusudi kampuni hizo ziendelee kuwanyonya Wakulima.

c) Sababu zinazopelekea asilimia 80% ya korosho ghafi kuuzwa nje ya nchi, badala ya kubanguliwa nchini ili kunufaika na mnyororo wa thamani ya korosha na kukuza uchumi wa viwanda kupitia Kilimo.

d) Agizo la Serikali la kutaka kahawa yote iuzwe kupitia minada na kuzuia wanunuzi binafsi wa kahawa kutoka kwa wakulima na kusafirisha nje ya nchi. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kudhibiti utoroshaji wa kahawa nje ya mipaka, Kamati ilitaka kujua namna ambavyo Serikali imejipanga kuhakikisha bei nzuri kwa wakulima kupitia minada kwani Ushirika utasababisha kukosekana ushindani wa soko pamoja na kuondoa mnyororo wa baadhi ya wanunuzi ambao walikua wakinunua, kuchakata na kusafirisha kahawa nje ya nchi.

### 2.7 Mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya Bustani

Takwimu zinaoniesha tangu mwaka 2013/2014 kumekuwepo na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni mboga na matunda, ongezeko lililochangiwa na juhudi za Serikali katika kuhamasisha kilimo cha mazao ya bustani kwa kutumia skimu za umwagiliaji. Vilevile kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika sekta

ndogo ya mazao ya bustani kumesaidia kuongezeka kwa mazao ya bustani na hivyo kutoa ajira kwa wananchi na hasa vijana na kinamama. Kuongezeka kwa mahitaji ya matunda na mboga kunatoa fursa ya ajira, kipato na uchumi kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, pamoja na maendeleo yanayoonekana kufikiwa katika uzalishaji na biashara ya mazao ya bustani, zipo taarifa za malalamiko ya wananchi kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili, changamoto tajwa ni pamoja na:-

(a) Upotevu wa mazao tangu shambani, yanapovunwa hadi kumfikia mlaji;

(b) Ubora duni wa mazao yanayozalishwa;

(c) Ukosefu wa mikopo kwa wakulima wa mazao ya bustani, mikopo ambayo ingewezesha wakulima hao kuwekeza katika teknolojia zinazotumika baada ya kuvuna;

(d) Upatikanaji wa nishati ya umeme isiyoaminika;na

(e) Hali mbaya ya barabara za vijijini na ukosefu wa usafiri mbadala,

(f) Upatikanaji wa vifaa vya kuhifadhi na vifungashio usiotosheleza.

## 2.8 **Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

Serikali ilianzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji wa utoshelezi na usalama wa chakula pamoja na kuchagiza mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kuwa kilimo cha biashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali ili kuchagiza sekta ya kilimo, kilimo cha Tanzania bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiwango kidogo cha uzalishaji kutokana na ukosefu wa mbinu na teknolojia za kisasa, ukosefu wa mitaji na upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao, pamoja na kutokuwepo ongezeko la thamani ya mazao ya kilimo na ukosefu wa mnyororo wa thamani ya mazao kwa ujumla.

Uchambuzi wa kamati umebaini kwamba, pamoja na sababu nyingine, changamoto za sekta ya kilimo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kukosa mtaji wa kutosha kuwezesha benki hiyo kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Serikali itekeleze kusudio lake la kutoa mtaji kwa Benki na kuimarisha uendeshaji wake.

### 2.9 Kilimo cha Umwagiliaji ili kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi na uhusiano wake na utoshelezi wa chakula

**Mheshimiwa Spika,** uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi umepelekea maeneo mengi ya nchi kuwa kame na hivyo kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kukidhi mahitaji ya chakula cha kutosheleza nchi, hivyo kilimo cha umwagiliaji kina nafasi kubwa ya kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kupatikana ziada itakayouzwa nje ya nchi na kuliongezea Taifa fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** kilimo cha umwagiliaji kinafaa zaidi kutokana na nchi yetu kuwa na maji mengi katika mito, maziwa, mabonde, malambo na maji yanayopatikana chini ya ardhi sambamba na maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo. Kwa muktadha huu Kamati inaishauri Serikali kuitengea Tume ya Taifa ya Umwagiliaji bajeti ya kutosha itakayowezesha Tume kuandaa miundombinu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na hivyo kupunguza utegemezi wa kilimo cha mvua ambacho kinazidi kutotabirika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuainisha maeneo machache ya kipaumbele yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na

kuelekeza fedha hizo katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

### 2.10 Migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya Wakulima, Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi

Kamati ilielezwa juu ya hatua mbalimbali ambazo Serikali imekuwa ikichukua ili kukabiliana na migogoro ya ardhi. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji imeendelea kuongezeka na kusababisha uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mazingira na utwezaji. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, Serikali imekua ikichukua hatua zisizoridhisha kukabiliana na migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Kutokana na hatua hizi zisizokidhi ukubwa wa migogoro iliyopo bado vipo viashiria vya kuendelea kuwepo migogoro katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati inatahadharisha kuwa, migogoro ya ardhi itaendelea kuathiri uwekezaji katika kilimo na sekta nyingine za kiuchumi endapo hatua za makusudi hazitafanywa kupata suluhu ya kudumu.

### 2.11 Mipango Mikakati ya Serikali kuinua Sekta ya Uvuvi

Kamati ilikutana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kupokea taarifa kuhusu uratibu wa shughuli za uvuvi nchini. Kamati ilitaka kupata taarifa ili kuweza kufahamu mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa na mipango mikakati iliyopo ya kuwezesha sekta ya uvuvi kuchangia Pato la Taifa kwa kiwango kinachostaili pamoja na kuinua kipato cha wavuvi.

Uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa Sekta ya Uvuvi haijalinufaisha Taifa kwa kiwango kinachostahili. Aidha, mipango iliyopo imeshindwa kutekelezeka kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa, kuidhinishwa na kutolewa. Aidha, Kamati katika nyakati tofauti imekuwa ikishauri juu ya Serikali kuwekeza katika bandari ya uvuvi kama njia ya

kuliwezesha Taifa kunufaika ipasavyo na rasilimali za uvuvi hususan katika bahari kuu, hata hivyo utekelezaji wa ushauri huu umekuwa ni wa kusuasua kwa maelezo kwamba fedha zikipatikana Bandari ya Uvuvi itajengwa.

Aidha ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, Kamati ilitaka kufahamu hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kukabiliana na uvuvi haramu nchini. Kamati ilielezwa kwamba zana za kukabiliana na uvuvi haramu zinagharimu fedha nyingi, na kwamba bajeti ndogo inayotengwa katika sekta ya uvuvi inakwamisha utekelezaji wa mipango inayolenga kudhibiti uvuvi haramu. Hata hivyo Kamati ina hoja kuwa, kwa kutambua kuwa ulinzi wa rasilimali za uvuvi ni jukumu ambalo halinabudi kulitekeleza kwa vitendo, udhibiti wa uvuvi haramu hauna mbadala.

### 2.12 Uwekezaji katika Ranchi za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kupokea na kujadili taarifa kuhusu uendeshaji wa Ranchi za Taifa. Kamati ilibaini kuwa, Ranchi za Taifa ni rasilimali muhimu na fursa kubwa katika kuchangia pato la Taifa na uchumi wa wafugaji. Tanzania ina jumla ya Ranchi **13** zenye ukubwa wa jumla ya hekta **627,856;** katika mikoa **10** nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi, Kamati imeelezwa hali ya uwekezaji uliopo katika Ranchi za Taifa, changamoto na mafanikio na kujiridhisha kuwa fursa na rasilimali ya ranchi za Taifa haijatumika ipasavyo.

Kamati ilibaini kuna uwekezaji mdogo usiowezesha Ranchi za Taifa kujiendesha kibiashara na hivyo kuzifanya kutokuwa na tija. Ranchi nyingi hazina uangalizi stahiki, zingine zinahodhi maeneo makubwa ambayo hayatumiki ipasavyo na hivyo kupelekea wananchi kuvamia maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa Ranchi za Taifa zinapaswa kuwa shamba darasa kwa wafugaji nchini,

pamoja na kutoa huduma za kitaalamu na, malisho na maji kwa mifugo ya wafugaji waishio pembezoni mwa ranchi. Hivyo Serikali hainabudi kutambua fursa ya biashara iliyopo katika ranchi na kuwekeza ipasavyo ili kuzifanya zizalishe kwa tija.

### 2.13 Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti Wizara ya Maji na Umwagiliaji ya Mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, tathimini ya Kamati katika kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umebaini kwamba fedha zinazoombwa hazikidhi mahitaji makubwa ya Maji kama yalivyoelezwa katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Awamu ya I&II) ambayo imebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji, viwanda, usafirishaji na uchukuzi na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kwamba, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo na kushindwa kuzitoa kama zilivyoidhinishwa. Kwa mfano; katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha shilingi **915,193,813,609** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi **181,209,813,609** sawa na asilimia **19.8** tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Maji **Fungu 49,** iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shiling **billioni 408.6,** hadi kufikia disemba 2017, kiasi kilichotolewa ni asilimia **25%** ya fedha za ndani. Aidha fedha za nje iliidhinishiwa **billioni 214.9** ambapo hadi disemba 2017 fedha iliyopokelewa ni asilimia **1.86%** tu.

Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji **Fungu 5**, iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shilingi billioni **5.6,** hadi kufikia disemba 2017, hakuna fedha za ndani zilizotolewa

kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha Tume iliidhinishiwa fedha za nje kiasi cha **shilingi billioni 14.5**, hadi disemba 2017, Tume imepokea asilimia **1.6** tu ya fedha za nje. Mwenendo huu wa utoaji fedha haukidhi kiu ya wananchi kupata huduma ya maji. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuwa na uhakika wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa maslahi mapana ya wananchi.

### 2.14 **Programu ya maendeleo ya maji vijijini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kupokea Taarifa kuhusu Programu ya Maendeleo ya Maji vijijini ili kufahamu utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa katika Sera ya Maji ya mwaka 2002. Aidha, Kamati ilitaka kufahamu Mpango Mkakati uliopo na hatua zinazochukuliwa ili kuongeza kasi ya utoaji huduma ya maji safi na salama vijijini.

Uchambuzi wa Kamati umebani kuwa, upatikanaji wa maji si wa uhakika mahali pengi nchini.Takwimu zinaonesha kuwa, kitaifa upatikanaji maji vijijini hadi disemba 2017 ni wastani wa asilimia **56%** tu. Hali hii inachangiwa na kutokamilika kwa miradi ya maji kwa wakati, miradi ya visima na mabwawa kuwa na dosari za kiufundi hivyo kupelekea visima kutotoa maji, mabwawa kukauka, gharama kubwa za uendeshaji miradi, pamoja na usimamizi mbovu wa miradi yenyewe kutokana na uelewa mdogo wa watumiaji maji vijijini. Kamati inalishauri Bunge liazimie kuitaka Serikali kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, ambao pamoja na mambo mengine utakuwa na jukumu la uratibu na usimamizi wa miradi ya maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufanikisha adhima ya upatikanaji wa maji ya uhakika na salama vijijini, Serikali imeanzisha Mfuko wa Maji vijijini kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, hata hivyo Kamati inasisitiza kuwa, fedha zitokanazo na Mfuko wa Maji hazitoshelezi mahitaji ya ujenzi wa miradi kwa sasa kutokana na mahitaji kuwa makubwa. Lakini pia kutokana

na ukweli kuwa, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutotoa fedha za Miradi ya maendeleo kadiri zinavyoidhinishwa na Bunge, hivyo fedha pekee za uhakika zinazopatikana na kutolewa ni Fedha za Mfuko wa maji.

### 2.15 Upatikanaji wa maji ya uhakika, safi na salama mijini

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa, hadi disemba 2017 hali ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa ni wastani wa asilimia **69%** kwa mijini. Aidha malengo ya upatikanaji maji safi na salama Kitaifa kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ( 2016/ 2017 hadi 2020/2021) ni asilimia **95%** kwa mijini ifikapo Mwaka 2021. Kwa jiji la Dar es salaam ni asilimia **95%** 2020/21. Kamati ina wasiwasi juu ya kufikiwa kwa malengo haya kwani, kumekuwa na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maji. Kwa mfano katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018, fedha za maendeleo zilizotengwa kwa fungu **49** ni asilimia **17.16%** tu zimetolewa hadi kufikia disemba, 2017, kati ya hizi kiasi kikubwa asilimia **77%** zikiwa ni fedha za Mfuko wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Mamlaka za Maji za Jiji la Dar es salaam (DAWASCO) na Mamlaka ya Maji safi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ili kufahamu mikakati ya Serikali katika kuhakikisha maeneo ya mijini nayo yanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji ya uhakika na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilianza na maeneo ya Dar es salaam na Dodoma kwa kuzingatia kuwa Dar es salaam ni jiji kuu la biashara Tanzania ambalo lina changamoto kubwa ya ongezeko la idadi ya watu. Aidha, Dodoma ilichaguliwa kutokana na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kuhamia Dodoma uamuzi ambao utapelekea mji wa Dodoma kuwa na ongezeko la watu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako kuwa kwa upande wa Jiji la Dar es salaam Kamati iliridhishwa na kupongeza mafanikio yaliyopatikana kwa Serikali

kukamilisha mradi wa maji kutoka Bagamoyo mpaka Dar es saaam (Ruvu chini) - Dar es salaam *Water Supply and Sanitation Project.* Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa, katika bajeti ya Mwaka 2017/2018, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuimarisha na kukarabati mitandao ya kusambazia maji, ambayo miundombinu yake imechakaa na haikidhi mahitaji makubwa yaliyoko hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mji wa Dodoma Kamati iliridhishwa na mkakati ulioandaliwa na ambao umeanza kutekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA), ambapo wakazi wa mji huu watapata huduma ya maji kutoka chanzo cha maji cha Bwawa la Farkwa lililopo Chemba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua mahitaji makubwa ya maji yatakayotokana na Serikali kuhamia Dodoma, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mkakati wa makusudi kuiwezesha kifedha na kitaalamu Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA)ili iweze kutekeleza jukumu hilo kwa wakati.

### 2.16 Mikakati ya Serikali katika kujenga na kukamilisha skimu za umwagiliaji nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kupokea taarifa kuhusu Mikakati ya Serikali katika kuinua Sekta ya Kilimo kupitia kilimo cha Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kufahamu mikakati iliyopo ili iweze kuishauri Serikali hatua muafaka za kuchukua na hasa ikizingatiwa kwamba kilimo cha Tanzania kwa kiasi kikubwa hutegemea mvua ambayo inaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na kuathiri uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kwa muktadha huu kilimo cha umwagiliaji ni moja ya njia muhimu za kuongeza tija katika uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonyesha Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa **hekta 29.4 milioni** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hadi sasa ni **hekta 461,326** sawa na **asilimia1.6** ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa asilimia ndogo ya eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji imetokana na sababu mbalimbali zinazojumuisha ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha, ushiriki mdogo wa sekta binafsi kwenye kilimo cha umwagiliaji na kutotumika ipasavyo kwa maji ya maziwa kutokana na sura ya nchi inayozunguka maziwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeskitishwa na taarifa ya Serikali kuwa kati ya hekta **29.4** milioni za eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ni asilimia **1.6** tu ya eneo hilo ndilo linalotumika kwa sasa. Kamati inaitahadharisha Serikali kuwa sekta ya kilimo haiwezi kuwa na tija kwa kuendelea kutegemea misimu ya mvua katika kilimo kutokana na hali halisi ya mabadiliko ya tabia nchi ambapo mvua zimekuwa si za uhakika.

### 2.17 Uchimbaji na Ukarabati wa Mabwawa ya kimkakati na Visima kwenye maeneo kame nchini na uvunaji wa maji ya mvua

**Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyochimbwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwani ujenzi wa mabwawa ukikamilika kasi ya uvunaji maji ya mvua utasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, majumbani, mifugo, viwandani na uzalishaji wa umeme.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa ujenzi wa mabwawa nchini bado kasi ya ujenzi wa mabwawa hauendani na mahitaji kwa wakati huu. Aidha, kutokana

na mabadiliko ya tabianchi visima vingi vya asili na vilivyojengwa na Serikali katika maeneo mbalimbali nchini vimekauka na hakuna hatua za haraka zilizochukuliwa kwa maelezo kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa miradi ya visima na mabwawa kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na maelezo haya kwani wapo wawekezaji wenye teknolojia rahisi na ya kisasa na wana fedha za kuwekeza katika sekta ya Maji kwa mikopo nafuu na misaada. Kwa mfano:- Kamati ilikutana na kampuni ya ***Investglobal and Associate*** ambao wako tayari kuingia ubia na Serikali katika ujenzi wa miradi ya visima kwa kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa kipindi cha malipo ya kati ya miaka 10 hadi 20, mkopo utakaoanza kulipwa kuanzia miaka 2-3 baada ya mradi kukamilika na asilimia 35 ya mkopo huo ni msaada. Vilevile kampuni hii itabeba dhamana ya visima hivyo kuendelea kutoa maji kwa kipindi cha miaka kumi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na uhaba wa maji katika maeneo kame nchini ikiwa ni pamoja na kuepukana na changamoto zilizopo za miradi mingi ya visima kutotoa maji na mabwawa kukauka muda mfupi baada ya uchimbaji na hivyo kupoteza fedha za Serikali, Kamati inaishauri Serikali kuondokana na urasimu usiokuwa wa lazima na kutumia fursa za kushirikiana na sekta binafsi (*Public Private Partnership*) kwa kuchukua hatua kujiridhisha na masharti ya mikopo, misaada na faida zinazoonesha kuambatana na wadau wa sekta binafsi waliotayari kushirikiana na Serikali.

### 2.18 Mradi wa kimkakati wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni wazo lililoasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere miaka ya 1980. Bwawa la Kidunda lina umuhimu mkubwa katika uhai wa Mto Ruvu kwani kukamilika kwa ujenzi wa bwawa hili kutawezesha mikoa ya Dar es salaam na Pwani kuwa na uhakika wa maji kwa kipindi

chote cha mwaka mzima pamoja na kuzalisha umeme wa megawati 20 ambao utachochea pamoja na mambo mengine uzalishaji wa mazao ya kilimo na uvuvi kwa ajili ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** usanifu wa bwawa hili ulioanza mwaka 2010 ulikamilika mwaka 2012 ambapo gharama ya ujenzi wa mradi inatarajiwa kuwa Dola za Marekani milioni 215 sawa na shilingi bilioni 430.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa bwawa hili hatua mbalimbali za kutafuta vyanzo vya fedha za kutekeleza mradi huo zimekuwa zikichukuliwa, hata hivyo upatikanaji wa fedha za uhakika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili umekuwa wa kusuasua.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa, tarehe 2 Machi, 2015, Tume ya Mipango iliiandikia barua Wizara ya Fedha na kuishauri Serikali kuwa ujenzi wa bwawa la Kidunda ni moja ya vipaumbele vya Serikali. Kamati inasisitiza kuwa, ni muda muafaka kwa Serikali kutekeleza adhma hii kwa vitendo.

### 2.19 **Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi)***

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilichambua na kuwasilisha Maoni na Ushauri kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua,kutathmini na kujiridhisha na sababu na dhumuni la msingi la kuanzishwa

kwa Mkataba wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe kuwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi, uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Mto Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzishwa kwa Mkataba huu ni muhimu kufuatia faida zitakazopatikana kwa nchi wanachama, kwani unalenga kuwezesha:-

a) Kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo huharibu kingo za mto na kusababisha mkondo wa mto kuhama na kuathiri mpaka wa nchi hizi mbili;

b) Kuanza ujenzi wa mradi wa Bwawa la Songwe Chini litakalotumika kuzalisha umeme (Megawati 180.2), kutoa huduma ya maji kwa ajili ya

c) matumizi ya majumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, hifadhi ya mazingira na utalii na hivyo kuongeza fursa za kiuchumi na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa eneo la Bonde; na

d) Kuwa na chombo madhubuti kitakachoweza, pamoja na kazi zingine, kutafuta rasilimali fedha kwa niaba ya nchi wanachama kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa katika Bonde la Mto Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na faida hizo za kiujumla, Kamati iliridhika kuwa, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na faida mbalimbali kwenye sekta nyingine kisiasa, kiulinzi, kiusalama, kiuchumi na kijamii.

## 2.20 Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti

Kamati ilifanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inahusu uchambuzi wa Mapato na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha husika pamoja na kuchambua utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika.

### a) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa bajeti, Kamati ilichambua fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo na makisio ya fedha zitokanazo na ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu. Kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganishwa na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, baadhi ya miradi ya maendeleo haikupata fedha kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu wa kushuka kwa Bajeti ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi una athari kubwa katika ustawi wa pato la wakulima na uchumi wa nchi kwa ujumla kwani **asilimia 75%** ya Watanzania wanajihusisha na shughuli za kilimo. Kamati inatahadharisha juu ya mdororo huu wa sekta za kilimo kuwa utapelekea kuongezeka kwa hali ya umaskini nchini pamoja na usalama mdogo wa chakula endapo hatua muafaka na za haraka hazitachukuliwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili, 2016/2017 na 2017/2018 katika mafungu ya sekta za kilimo kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

| Fungu | Bajeti ya Mwaka 2016/2017 | Bajeti ya Mwaka 2017/2018 | % ongezeko |
|---|---|---|---|
| 43 | 101,525,497,000 | 150,253,000,000 | 48 % |
| 24 | 00 | 4,165,000,000 | 100 % |
| 99&64 | 15,873,215,000 | 12,000,000,000 | -24 % |
| | | | |

**Chanzo cha Taarifa: Randama ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili mfululizo kwa mafungu yote ya Wizara. Kamati imebaini kuwa, jumla ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mafungu yote kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi, **182,318,893,059** ikilinganishwa na shilingi **117,400,712,000** zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 36 %.** Kati ya fedha hizi, fedha za ndani zikiwa ni **asilimia 36%** tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kiasi kidogo cha fedha za ndani zinazotengwa, kwani fedha za nje zimekuwa hazitoki kwa muda na wakati uliokusudiwa. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizo kadiri zilivyotengwa ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka miwili mfululizo Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 imekuwa haitengewi fedha yoyote kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka huu wa fedha (2017/2018) Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetengewa kiasi cha shilingi **4,165,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha za maendeleo kwa Fungu 24 ili kuiwezesha Tume ya maendeleo ya ushirika kujiimarisha na kuinua ushirika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Kamati imesikitishwa na kushuka fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 fedha za maendeleo zilizotengwa ni pungufu kwa **asilimia 24%** ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017 kama inavyoonesha kwennye jedwali juu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Kamati ilibaini kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha za ndani ukilinganisha na fedha za nje, lakini fedha hizo zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa. Hili siyo jambo dogo katika utekelezaji wa Mipango ya Serikali, linahitaji ufumbuzi wa haraka kuwezesha utekelezaji wa miradi.

**b) Wizara ya Maji na Umwagiliaji,**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa upande wa miradi ya maji, Serikali imetoa fedha za miradi ya maendeleo kwa kiasi kidogo ukilinganisha na mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo iliyotolewa kwa Mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa fedha unaomalizika fedha za miradi ya maendeleo iliyotolewa ni shillingi 181,209,813,609 sawa na asilimia **19.8.** Hatua hii ni ya kusikitisha na hasa ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilioidhinishwa na Bunge umeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliidhinishwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 550,005,000 Hadi kufikia Machi 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 467,633,790 ambayo ni sawa na

asilimia 85 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo.

### 2.21 Ufuatiliaji wa tekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2016/2017

#### 2.21.1 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuweza kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni ya 98(1) ambayo inaitaka Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka uliomalizika 2016/2017 kutokana na baadhi ya miradi ya sekta ya kilimo kutopelekewa fedha yoyote na kushindwa kutekelezwa. Aidha, kwa baadhi ya miradi iliyopata kiasi kidogo cha fedha zilitumika katika hatua za awali za uratibu wa kutekeleza miradi iliyopangwa, hivyo hakukuwa na miradi iliyotekelezwa kwa namna ya kuweza kukaguliwa katika kipindi kilichopangwa Kikanuni kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, imekuwa ni kawaida kwa fedha za nje kutolewa zikiwa pungufu au kwa kuchelewa wakati fedha za ndani zinazotengwa kwa miradi ya maendeleo mara nyingi hazitolewi kabisa. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kutoa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani, kwani kutumia fedha za ndani kunadhihirisha utayari wa Serikali katika kujitegemea na kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kweli.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kutotolewa fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa sekta ya Kilimo, ililazimu Kamati ifanye kazi zingine nje ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kufuatia hali hiyo, Kamati ilikagua miradi na shughuli zinazotekelezwa na Wizara ambazo zilitengewa na kupelekewa fedha katika bajeti za miaka ya nyuma katika

Sekta ya kilimo, lakini pia Kamati ilikagua shughuli za sekta binafsi katika maeneo ya mifugo na uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** mantiki ya Kamati kukagua shughuli zinazotekelezwa na sekta binafsi kwenye masuala ya uvuvi na mifugo ilikuwa ni kujifunza namna sekta binafsi inavyoshiriki katika shughuli za kukuza uchumi kupitia kilimo, mifugo na uvuvi na changamoto wanazokutana nazo hatimae Kamati iweze kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuiwezesha setka binafsi kushiriki kikamilifu katika kuongeza pato la taifa na kukuza ajira. Katika ziara hiyo, miradi iliyokaguliwa ni pamoja na:-

**a) Ghala la Hifadhi ya Taifa ya Chakula mkoani Shinyanga**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Ghala la Hifadhi ya Taifa ya chakula mkoani Shinyanga ili kujiridhisha na akiba ya chakula iliyohifadhiwa katika kukabiliana na kuwepo kwa upungufu wa chakula mahali pengi nchini.

**Mheshimiwa Spika, katika** ukaguzi huo, Kamati ilibaini kuwa, ghala la Hifadhi ya Taifa ya chakula mkoani Shinyanga lilikua na mahindi yaliyohifadhiwa kiasi cha tani **8,622.619,** na kwamba kiasi hicho kinatosheleza mahitaji ya mkoa wa Shinyanga na mikoa jirani. Aidha, Kamati ilibaini pia kuwa, mahindi yaliyohifadhiwa ni ya muda mrefu kwani mahindi hayo yalinunuliwa wakati wa msimu wa mwaka 2014/2015 na endapo mavuno ya msimu wa 2016/2017 yangekuwa ya kutosheleza, huenda shehena iliyopo isingeweza kutolewa kwa wakati na kusababisha hasara ya mahindi kuharibika na kutupwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kunusuru mahindi hayo kuharibika, Kamati iliishauri Serikali kutoa mahindi hayo na kuyauza kwa bei nafuu kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa chakula hatua ambayo ingepelekea kupunguza uhaba wa mahindi na kudhibiti bei ya mahindi ambayo imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na kwa kuanzia Serikali imekwishatoa **tani 500** za mahindi yaliyohifadhiwa katika ghala la Hifadhi ya Taifa ya chakula mkoa wa Shinyanga na kuipatia Wilaya ya Serengeti ambayo ilikuwa na uhaba mkubwa wa chakula kutokana na tembo kuvamia mashamba ya wananchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanya hivyo katika maeneo mengine pindi kukiwa na uhaba wa chakula.

**b) Kiwanda cha uchakataji samaki cha Tanzania *Fish Processors Limited* – Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua uwekezaji unaofanywa na sekta binafsi kwenye shughuli za uvuvi ambapo Kamati ilikagua Kiwanda cha Uchakataji Samaki cha Tanzania *Fish Processors Limited* kilichoko Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa kiwanda cha Tanzania *Fish Processors Limited* kinaajiri zaidi ya Watanzania 400 pamoja na kulipa kodi mbalimbali za Serikali (*direct and indirect tax*) kiasi cha **shilingi bilioni 3.2** kwa mwaka ambayo ni **asilimia 5%** ya pato lake ambalo ni shilingi **bilioni 64**[3].

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hii, Kamati ilibaini pia kuwa tangu mwaka 2006 uzalishaji wa kiwanda hiki umekuwa ukishuka kila mwaka kutokana na kuendelea kupungua kwa samaki katika ziwa Victoria kunakosababishwa na uvuvi haramu pamoja na biashara ya samaki inayofanywa nje ya mipaka ( *cross border fish trading*).

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara ya Kamati kiwandani hapo, Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali:-

---

[3] Taarifa ya *Tanzania Fish Processors Limited* iliyowasilisha kwenye Kamati tarehe 24 Machi, 2017

i) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti shughuli za uchakataji haramu wa samaki;

ii) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti na kukomesha vitendo vya uvuvi haramu; na

iii) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti biashara ya kuvuka mipaka (*cross border trade*)

**c) Kiwanda cha kusindika nyama cha Kampuni ya Chobo - Mwanza**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea kiwanda cha kusindika nyama cha kampuni ya Chobo na kuona uwekezaji mkubwa uliofanywa katika mazao yatokanayo na mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya kiwanda ilieleza kwamba kiwanda kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 600, mbuzi na kondoo 920 kwa siku na kuhakikisha upatikanaji wa soko la uhakika katika mkoa wa Mwanza na mikoa ya jirani. Taarifa ya kiwanda ilibainisha uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na muingiliano na mgongano wa kimamlaka na utendaji kutoka katika Taasisi na Wakala wa Serikali. Kwa mfano Mamlaka ya udhibiti ubora wa chakula na dawa (TFDA), Shirika la viwango nchini (TBS) na Idara ya Afya, Taasisi hizi zinahusika na usalama na ubora wa bidhaa nchini, zimekuwa na muingiliano wa majukumu unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa kiwanda.[4]

Kufuatia taarifa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kutathimini majukumu ya Mamlaka zake ili kubaini muingiliano wa kiutendaji uliopo na kurekebisha maeneo yanayolalamikiwa na sekta binafsi ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji.

---

[4] Taarifa ya *Chobo Investment Company Limited*, iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 24 Machi, 2017

### 2.21.2 Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ambayo inaitaka Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka uliomalizika 2016/2017. Katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kamati ilitembelea miradi miwili ifuatayo;

**a) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Shinyanga, Mwadui, Kishapu na Maganzo,**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa wizara ya Maji na Umwagiliaji, Kamati ilfanya ziara katika mkoa wa Shinyanga kukagua mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Shinyanga, Mwadui, Kishapu na Maganzo, mradi ambao ulitengewa shilingi **1,000,000,000.00** na fedha zote kutolewa kwa wakati.

Katika ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa, mradi huu umetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na thamani ya fedha iliyotengwa na kutolewa imetumika ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua ujenzi wa tanki kubwa la maji katika mji wa Kishapu ilibaini kwamba hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa tanki hilo ni ya kuridhisha. Aidha, kutokana na mji wa Kishapu kutokuwa na miundombimu ya usambazaji maji, Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti itakayowezesha Halmashauri kujenga kwa wakati miundombinu itakayokidhi kusambaza maji hayo pindi mradi huu utakapokamilika.

**b) Mradi wa maji na usafi wa mazingira wa ziwa Victoria awamu ya pili (LV WATSAN II)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mkoa wa Mwanza, Kamati ilikagua mradi wa maji na usafi wa mazingira wa ziwa Victoria awamu ya pili (LV WATSAN II)-Mwanza. Mradi unatekelezwa katika Wilaya ya Sengerema. Mradi ambao unagharimu dola za kimarekeni milioni 30.4 na umekuwa

ukitekelezwa kwa awamu tangu mwaka 2011 na unategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi wa maji na usafi wa mazingira wa ziwa Victoria awamu ya pili (LV WATSAN II) ulitengewa shilingi **1,804,358,000.00,** hadi Kamati ilipokagua mradi huu mwezi Machi, 2017, mradi ulikuwa umepokea shilingi **614,966,347.00** ambazo ni sawa na **asilimia 34** ya fedha iliyotengwa. Kamati iliishauri Serikali kutoa fedha zilizosalia kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kuwezesha mradi huu kukamilika kwa muda uliopangwa ambao ni Desemba 2017, ushauri ambao Serikali iliutekeleza na Mradi kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na hatua ya utekelezaji miradi iliyofikiwa ikiwa ni pamoja na thamani ya fedha zilizotumika. Kamati ilipongeza Serikali kwa kutekeleza kwa vitendo matumizi ya rasilimali maji ya ziwa Victoria na hivyo kuwezesha wananchi wanaozunguka ziwa hilo kuondokana na tatizo la muda mrefu la kukosekana kwa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji kwenye vijiji vilivyolengwa kufikiwa na mradi huu. Lakini pia kubuni na kutekeleza miradi ya aina hiyo katika maeneo mengine ambayo kuna maziwa, mabonde na mito ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kuondokana na uhaba mkubwa wa maji safi na salama ambayo imekuwa ni kero ya muda mrefu.

### 2.21.3 **Ziara za mafunzo kuhusu shughuli za MVIWATA -Morogoro**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya mafunzo Mkoani Morogoro tarehe 10 juni, 2017, kufuatia mwaliko wa Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania-MVIWATA, ili kuwa na uelewa wa pamoja wa changamoto zinazokabili wakulima ili kuweza kushauri namna bora ya kuzipatia ufumbuzi. Ziara ilifanyika katika maeneo yafuatayo:-

### a) Soko la mazao la Kinole

Kamati ilitembelea Soko la mazao la Kinole. Soko hili lililopo Wilayani Mvomero ni mojawapo ya masoko manne ambayo yamejengwa na MVIWATA kupitia mradi wa maendeleo ya masoko vijijini (RMDP) ambao ulitekelezwa katika Wilaya za Morogoro, Mvomero na Kongwa. Masoko mengine ni Tawa, Nyandira na Kibaigwa). Kamati ilifahamishwa kuwa, chimbuko la ujenzi wa masoko haya ni kuwepo kero zilizokuwa zinakabili wakulima katika kuuza mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na umbali wa masoko, mazao kuharibika na kukosa soko la uhakika kwa bei nzuri za mazao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wajumbe wa Bodi ya soko la Kinole, Kampuni ya wakulima ya KINOTA (ambayo inajihusisha na kukusanya na kuuza mazao ya viungo), Watendaji wa SACCOS ya Kinole (ambayo inatoa mikopo kwa wakulima, Vikundi vya wakulima na Wafanyabiashara wa mazao ya kilimo za shughuli nyinginezo) na kutembelea kituo cha mafunzo ya kilimo cha Chief Kingalu Mwana Banzi wa XIV.

Kamati ilielezwa kuwa, Soko la Kinole linaendeshwa kwa ushirikiano kati ya MVIWATA na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, ambapo bodi ya soko ina makubaliano na Halmashauri ya Wilaya kukusanya ushuru wa mazao na tozo mbalimbali kwa niaba ya Halmashauri. Na kwamba, asilimia 65 ya mapato huenda Halmashauri na asilimia 35 hutakiwa kubaki katika kampuni ya soko kwa ajili ya gharama za uendeshaji na mfuko wa uchakavu.

Kwa ujumla, tangu kukamilika na kuanza kutumika kwa soko la Kinole oktoba 2004 limekua likitoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i) Kuwezesha eneo maalaum na salama la kuuzia na kununulia mazao hususan ndizi, mananasi, machungwa, magimbi na viungo vya pilipili manga, karafuu na mdalasini.

ii) Kuhifadhi mazao yakisubiri kuuzwa au kusafirishwa

iii) Kutoa taarifa ya bei za mazao na kuweka uwazi katika uuzaji

iv) Kuhakikisha ubora wa mazao yanayotoka sokoni kwa afya za walaji

v) Kupima mazao kwa kutumia mizani ili kuwa na udhibiti wa vipimo.

Kwa upande wa SACCOS ya Kinole, Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia mwezi Mei 2017, ilikua na mtaji wa jumla ya shilingi 1,540,988,086. Na kwamba inatoa mikopo ya aina nne ikiwa ni mikopo ya kilimo, mikopo ya kijamii, Mikopo ya biashara na mikopo ya karadha. Na kuwa, mikopo ya kilimo inatozwa riba ya asilimia **17%** kwa mwaka na ya biashara ni asilimia 19% kwa mwaka. Aidha takwimu zinaonesha kuwa mikopo hii imekuwa ikichangia katika kukuza kilimo, kuongeza ajira kwa njia za biashara, maduka na usafirishaji.

Kwa upande wa kituo cha mafunzo cha Chief Kingalu Mwana Banzi wa XIV, ni moja kati ya vituo vitatu vinavyomilikiwa na MVIWATA. Kamati ilielezwa kuwa kituo hiki kimejengwa na MVIWATA kwa ufadhili wa Serikali ya Ufaransa kwa lengo la kuwezesha mafunzo ya wakulima vijijini sambamba na shughuli za masoko. Kituo kimefanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima 120 kwa mwaka kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania. Kwa ujumla vituo vina uwezo wa kutoa mafunzo na mbinu za kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima 360 kwa mwaka.

Pamoja na faida nyingi zinazotokana na uwepo wa soko, SACCOS na vituo vya mafunzo, ikiwa ni pamoja na kukua kwa biashara ya mazao, kukua uchumi, kutoa ajira, ongezeko la makusanyo ya ushuru na kuchochea uzalishaji zaidi, Kamati ilifahamishwa kuwepo changamoto kadhaa, ambazo ni kikwazo katika ustawi wa wakulima, uzalishaji na soko. Changamoto zilizopo ni pamoja na:-

i) Kutorejeshwa gawio la ushuru wa asilimia 35 ambao unapaswa kubaki katika kampuni ya soko kwa sababu ya gharama za uendeshaji na kwa ajili ya mfuko wa uchakavu.

ii) Ubovu wa barabara ya Madam-Kinole, ambayo baadhi ya maeneo wakati wa mvua haipitiki na hivyo kukwamisha wafanyabiashara kufika sokoni.

iii) Kukosekana kwa mnyororo wa thamani kwa baadhi ya mazao hususan viwanda vya kuchakata na kufungasha viungo ili kuwa na soko la uhakika kwa wakulima.

iv) Kwa upande wa SACCOS ya Kinole, ipo changamoto ya kodi kubwa ya mapato inayotozwa kwa vyombo vya kifedha (30%) ya mapato.

**b) Soko la mazao la Nyandira – Mgeta**

Kamati ilitembelea Soko la mazao la Nyandira lilipo Mgeta, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Soko hili pia ni mojawapo ya masoko manne ambayo yamejengwa na MVIWATA kupitia mradi wa maendeleo ya masoko vijijini (RMDP) Mvomero.

Katika ziara, Kamati ilikutana na Bodi ya soko la Nyandira pamoja na mtandao wa vikundi vya wakulima kata ya Nyandira. Kwa ujumla Mtandao wa wakulima Nyandira umewezesha kuwa na sauti ya pamoja katika kukabiliana na changamoto zinazokabili wakulima wadogo. Aidha imefanikisha kuwa na bodi ya soko na usimamizi thabiti wa wakulima kupata elimu ya kilimo, miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa barabara na huduma ya maji safi kwa wakazi wa kata ya Nyandira.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa mtandao unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uhaba wa mitaji kwa wanavikundi na Halmashauri kukusanya tozo kutoka katika vyanzo vyote vya

mapato ya soko na kufanya soko kukosa fedha za uendeshaji, usimamizi na ukarabati wa miundombinu ya soko.

Kwa ujumla, Kamati iliweza kutambua jitihada zinazofanywa na MVIWATA katika kuhamasisha kilimo cha biashara kisha kushauri namna bora ya kukabiliana na changamoto zilizobainishwa na wanakikundi wa MVIWATA. Aidha, Kamati ilikubali kuendelea kufanya mashauriano na Serikali ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hizi. Hoja ambazo Kamati iliahidi kuzifuatilia na kushauriana na Serikali ni pamoja na:-

i) Kujadiliana na Serikali ili kufanya maboresho ya sheria inayonyang'anya masoko vyanzo vya mapato vya wakulima ili kurejesha gawio la ushuru wa asilimia 35% kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya soko pamoja na usimamizi na uendeshaji masoko

ii) Kuhimiza Halmashauri na Serikali kutambua umuhimu wa barabara ya Madam-Kinole katika ustawi wa sekta za kilimo, uchumi na jamii na kuona namna ya kuweza kuongeza kasi ya kufanya matengenezo na kuijenga ili ipitike kwa majira yote ya mwaka.

iii) Ili kuwa na uhakika wa soko la mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na kuongeza uzalishaji, Kamati iendeleze hoja na kuisimamia Serikali kuongeza mnyororo wa thamani kwa kujenga viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao ya kilimo na mifugo kwa ujumla.

iv) Kamati kuwa na ajenda ya kuendelea kuishauri serikali kupunguza riba ya asilimia **30%** inayotozwa kwenye mapato ya vyombo vya fedha.

### 2.21.4 Ziara ya mafunzo kuhusu shughuli za Ushoroba wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)-Iringa na Njombe

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya kikazi katika Mikoa ya Iringa na Njombe kuanzia tarehe 18-22,

Septemba, 2017 ikiwa ni mwitikio wa mwaliko uliotolewa na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Ushoroba wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT). Lengo la mwaliko huo lilikuwa ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kufahamu shughuli zinazotekelezwa na SAGCOT, mafanikio ambayo yamepatikana na changamoto zilizopo, ili hatimaye waweze kushauri namna bora ya kukabili changamoto zinazokabili sekta za kilimo na mifugo ili ziweze kuwa na tija na hatimaye kuongeza uchangiaji katika pato la Taifa. Kamati ilifahamishwa kuwa, Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ulioanzishwa kwa lengo la kuendeleza kilimo cha kibiashara na kuchochea mapinduzi katika kilimo kwenye Nyanda za Juu kusini mwa Tanzania. Programu hasa inalenga kuendeleza wakulima wadogo (kupata mitaji, ujuzi, huduma stahiki, masoko na miundombinu muhimu) kusudi shughuli za uzalishaji kwenye mlolongo/mnyororo wa thamani zilete faida inayotarajiwa. Ziara ilifanyika katika maeneo yafuatayo:-

**a) Kiwanda cha maziwa cha Asas Dairies Co.-Ltd**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Kiwanda cha Maziwa cha ASAS DAIRIES CO.LTD, Iringa. Kamati ilielezwa kuwa kiwanda hiki kimeanza uzalishaji rasmi mwaka 2000. Kwa sasa kiwanda kinanunua maziwa kutoka kwa wakulima wapatao 2500 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Iringa na Mbeya ili kuyasindika kupata bidhaa mbalimbali za maziwa. Kiwanda kina uwezo wa kusindika lita 50,000 kwa siku, lakini kwa sasa kinasindika lita 17,000 tu kwa siku kutokana na uhaba wa maziwa. Ilielezwa kuwa, ASAS DAIRIES CO. LTD, inamiliki na kuendesha kiwanda cha kutengeneza chupa za plastiki kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na kiwanda cha maziwa. Kwa ujumla, taarifa ya kiwanda ilisisitiza kuwa, pamoja na mafanikio yanayotokana na kuwepo kiwanda cha maziwa na kuhakikisha soko la maziwa kwa wakulima, zipo changamoto ambazo zimekua sababu ya kasi ndogo ya kuweza kufikia matarajio ya kukidhi uwezo wa uzalishaji na kuongeza tija. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Ushindani usio wa haki unaosababishwa na bidhaa za maziwa zisizo na viwango za bei nafuu zinazoingizwa nchini hivyo kupelekea kukosekana kwa soko la uhakika la bidhaa za maziwa ya kiwanda.

ii) Tozo nyingi za aina za bidhaa za maziwa na vifungashio, ambazo zinapelekea gharama za uzalishaji kuwa za juu; na

iii) Ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini unaopelekea ugumu wa wakulima kufikisha maziwa kiwandani kwa wakati au gharama za kukusanya maziwa kutoka maeneo ya vijijini kuwa kubwa.

**b) Kiwanda cha Kusindika Nyanya cha Darsh**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kiwanda cha kusindika nyanya cha DARSH, katika eneo la Ihemi Iringa. Kiwanda cha DARSH kilianza rasmi uzalishaji katika kipindi cha Disemba 2015. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 200 za nyanya kwa siku. Kiwanda kina vituo vya kukusanya nyanya kutoka kwa wakulima wadogo, kwa sasa kiwanda kinatoa soko la nyanya kwa wakulima wapatao 10,000 ambao wanauza nyanya kiwandani. Kiwanda kinasindika nyanya na kuwekwa kwenye vifungashio, makopo kwenye hali ya bidhaa za kutumiwa na mlaji wa mwisho kama *tomato paste*, *tomato sause na ketch up.*

Taarifa ya kiwanda iliainisha changamoto zinazokabili uzalishaji wa nyanya na usindikaji wa nyanya kiwandani, kuwa ni:-

i) Uzalishaji mdogo wa nyanya katika kanda kutokana na bei kubwa ya vifaa vya pembejeo na magonjwa ya nyanya ikiwepo mdudu wa "kantangaze"

ii) Upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kiwango kisichokidhi mahitaji ya kiwanda

iii) Mtandao mbovu wa barabara za vijijini unaopelekea kuharibika kwa nyanya baada ya kuvuna kwa kutofika kiwandani kwa muda stahiki

**c) Kampuni ya Mtanga Foods Ltd-Ugwachanya-Iringa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kampuni ya Mtanga Foods Ltd- Iringa. Kampuni inajihusisha na ufugaji wa ng'ombe na kondoo, uchinjaji, uchakataji wa nyama na usambazaji wa nyama. Vilevile kampuni inajihusisha na uzalishaji wa mbegu za kisasa za viazi mviringo na uzalishaji wa viazi, lakini pia kuwasambazia wakulima wadogo hususan katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mbegu za viazi.

Kwa sasa, Kampuni pia inanunua ng'ombe kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kuwanenepesha na kuchinja kutoka kwa wafugaji wadogo, hivyo kutoa soko la ng'ombe kwa wafugaji wadogo. Kampuni ina uwezo wa kuzalisha nyama tani 90 kwa mwezi. Aidha, Kampuni imeweza kusambaza mbegu kwa wakulima wapatao 5000, na inakadiriwa kuwa hadi mwisho wa mwaka 2017 wakulima wapatao 15,000 watakuwa wamenufaika na Mbegu za kisasa za viazi.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Kampuni inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni:-

i) Udogo wa soko la ndani la nyama kulinganisha na uwezo wa uzalishaji. Kwa mfano pamoja na kampuni kuwa na uwezo wa kuzalisha tani **90** za nyama kwa mwezi, inalazimika kuzalisha tani 25 tu, kutokana na ufinyu wa soko

ii) Ushindani mkubwa wa soko la viazi kutoka nje ya Tanzania katika masoko makubwa kama Dar es salaam, ambapo viazi kutoka Kenya vinaingizwa bila ya kulipiwa ushuru, hivyo kuuzwa kwa bei nafuu ukilinganisha na viazi vinavyozalishwa nchini

iii) Kukosekana kwa umeme wa uhakika, Kampuni ililazimika kugharamia kununua transfoma, ambayo ni mali ya Tanesco lakini Tanesco walikataa kurejesha gharama hizo

**d) Kampuni ya Silverlands Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kampuni ya Silverlands Tanzania ambayo inajihusisha na uzalishaji vifaranga vya kuku pamoja na kutengeneza vyakula vya kuku. Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa Kampuni ina uwezo wa kuzalisha vifaranga 180,000 kwa wiki moja. Aidha ina uwezo wa kukuza kuku 50,000 na imepanga kuongeza uwezo kukuza kuku **160,000**.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni inatoa ajira kwa wakazi wa vijiji vya karibu wapatao 1,000. Aidha inatoa soko kwa mazao ya mahindi, soya na alizeti kutoka kwa wakulima 14,000 wa vijiji vya karibu kwa ajili ya kutengeneza chakula cha kuku. Kampuni pia inachangia katika kutoa huduma za kijamii katika mashule, vituo vya afya, ambapo thamani ya jumla ya misaada kwa 2017 ni jumla ya shilingi **74,000,000.**

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Kampuni inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni :-

i) Magonjwa ya kuku na ukosefu wa chanjo za uhakika

ii) Bei kubwa ya gharama za kuzalisha vyakula vya kuku na kufanya bei ya vifaranga kuwa juu

iii) Uingizaji vifaranga na bidhaa za kuku kutoka nje visivyo na ubora au bila ya udhibiti kibiashara

iv) Kutopata ushirikiano wa kutosha kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania wakati wa kukagua vifaranga na mayai yanavyosafirishwa nje ya nchi ambapo, umekuwa ukisababisha hasara kutokana na Mamlaka kufungua makontena yenye viwango maalum vya ubaridi kwa ajili ya uhifadhi, badala ya kufanya ukaguzi huo kabla ya kuyafunga shambani.

### e) Kampuni ya Chai ya Unilever Tanzania Ltd

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kampuni ya Chai ya Unilever Tanzania Ltd, Mkoani Njombe. Kampuni hii ina mashamba sita ambayo ni Kilima, Lupembe, Lugoda, Ngwazi na Kivere yote katika Wilaya ya Mufindi yenye jumla ya hekta 3,586 ya mashamba ya chai, hekta 1,252 ya miti ya mikaratusi na milingoti na hekta 7,000 ya misitu ya asili. Kampuni ina viwanda vitatu vyenye uwezo wa kusindika tani 300 ya majani ya chai kwa siku.

Kwa kipindi cha miaka 3 iliyopita Kampuni imezalisha wastani wa tani 46,356 kwa kila mwaka. Aidha, Kampuni ina wafanyakazi zaidi ya 4500 ambao huongezeka kwa takriban 2000 wakati wa msimu wa chai.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa, Tanzania huzalisha **5%** ya chai katika Bara la Afrika na asilimia **0.6%** ya chai yote Duniani. Chai ya Tanzania inajulikana kwa kuwa na ladha bora lakini huambulia ubora wa kati sokoni kutokana na changamoto za hali ya hewa na mbinu za kilimo. Na kwamba biashara ya chai katika miaka mitatu iliyopita imepata changamoto kadhaa na kukosa faida kutokana na kodi na tozo kubwa zinazopelekea gharama kubwa za uzalishaji,uwezeshaji mdogo wa Serikali kupitia ukosefu wa barabara nzuri zinazopitika muda wote, sekta ya viwanda kutoshirikishwa ipasavyo katika maamuzi ya biashara na haki za ardhi na maji kutopatikana kwa wepesi.

Kufuatia changamoto zilizoainishwa, Kamati ilitaka kujua hatua zinazochukuliwa ili kuifanya sekta ndogo ya chai kuwa na faida, lakini pia hatua za kuimarisha mahusiano kati ya mamlaka za Serikali na wawekezaji katika sekta ili kuongeza ushiriki katika maamuzi muhimu na kujenga mazingira bora ya uwekezaji.

Kwa ujumla, Kamati iliridhishwa na jitihada zinazofanywa na SAGCOT katika kuhamasisha kilimo cha biashara, chenye tija na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kushirikiana na sekta za umma katika kuinua sekta za

kilimo kwa ujumla. Lakini pia Kamati iliahidi na inaendelea kufanya mashauriano na Serikali ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto zilizoainishwa kwa faida ya wadau wote wa kilimo. Hoja ambazo Kamati iliahidi kuzifuatilia na kushauriana na Serikali pamoja na kuendelea kushauri serikali kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora yasiyo na urasimu yatakayowezesha na kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwa faida nchini. Hoja za kushughulikia, ambazo ni:-

i) Kupunguza mamlaka nyingi za Serikali za udhibiti unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji,

ii) Kulinda viwanda vya ndani kwa kudhibiti bidhaa kutoka nje na zisizo na ubora kusababisha kukosa masoko ya uhakika ya bidhaa za ndani,

iii) Kupunguza tozo nyingi kwa baadhi ya bidhaa, mfano ladha za maziwa na vifungashio,

iv) Kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini ili kuwezesha wakulima kufikisha bidhaa katika masoko au viwanda kwa muda unaostahili, na

v) Kuwa na umeme wa uhakika kwa ajili ya viwanda.

**2.19.5. Ziara ya kukagua hatua ya utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es salaam**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kikazi katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dres salaam tarehe 20-21 Januari, 2018 ikiwa ni mwitikio wa mwaliko uliotolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Lengo la mwaliko huo lilikuwa ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji na umwagiliaji, mafanikio ambayo yamepatikana na changamoto zilizopo, ili hatimaye waweze kushauri Serikali ipasavyo.

**a) Mkoa wa Arusha**

Katika ziara hii, Kamati ilipokea taarifa ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka ya Mkoa wa Arusha (AUWASA) kuhusu hali ya upatikanaji maji katika Mkoa na miradi inayotekelezwa na Mamlaka. Na kwamba Mamlaka inasimamia na kuendesha huduma ya usambazaji majisafi na salama kwa ajili ya Jiji la Arusha lenye jumla ya wakazi **416,442** (sensa 2012), yenye ongezeko la watu asilimia 2.7 kwa mwaka.Eneo la kutoa huduma ni km za mraba 272. Mamlaka pia ina jukumu la kusimamia uendeshaji na matengenezo ya huduma ya uondoaji maji taka. Aidha mahitaji ya maji kwa Jiji la Arusha kwa siku ni meta za ujazo **93,270**. Mtandao wa bomba za usambazaji maji umeenea kwa asilimia **44% tu** ya eneo la Jiji. Kwa sasa wastani wa uzalishaji maji kwa siku ni meta za ujazo **30,000** (kipindi cha kiangazi) ambazo ni asilimia **37%** ya mahitaji hadi meta za ujazo **60,000** (kipindi cha mvua ambazo ni asilimia **64%** ya mahitaji. Miundombinu ya uondoaji maji taka katika Jiji una mtandao ulioenea kwa asililima **7.66%** wa eneo la Jiji.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliainisha changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na;

- Wezi wa maji wanaotumia maji bila kulipia

- Gharama kubwa za fidia kwa maeneo yenye maji ardhini, ambayo AUWASA inayahitaji kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa

- Vyanzo vya maji kuvamiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii,

- Ukosefu wa mfumo wa awali wa kusafisha majitaka kwenye viwanda

- Utoaji wa huduma ya maji katika maeneo ambayo hayajapimwa

- Madeni ya Taasisi za serikali, kutolipa Ankara za maji.

Baada ya wajumbe kupokea taarifa waliibua hoja kadhaa ambazo zilihitaji ufafanuzi, hoja zilizohitaji ufafanuzi ni pamoja:-

- Hatua zinazochukuliwa kuwataka wenye viwanda kuwa na mfumo wa awali wa usafishaji majitaka na kuunganishwa na mfumo wa maji taka wa Jiji,

- Kiasi ambacho taasisi za serikali zinadaiwa na hatua zinazochukuliwa ili kuzitaka zilipe madeni ya Ankara za maji,

- Ufanisi wa mbinu zinazotumika kukabiliana na vishoka na kama wanashirikiana na watumishi kuiba maji na hatua walizochukuliwa,

- Mpango mkakati wa kutambua mapema na kuhifadhi vyanzo vya maji, kwa ajili ya uhakika wa usalama wa maji na matumizi endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa Kamati ilifanya ziara kwa kutembelea miradi kadhaa ikiwa ni pamoja na;

i) Mradi wa AUWASA unaotoa huduma kwa H/W-Arusha

ii) Mradi wa maji Jiji la Arusha

iii) Mradi wa vijiji 10 H/W –Longido

Kwa ujumla, Kamati iliridhishwa na hatua za utekelezaji wa miradi hii kuwa itasaidia kuinua wastani wa upatikanaji wa maji kwa Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Arumeru. Hata hivyo Wajumbe walibaini kasoro kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa uchimbaji visima 3 virefu (m 300) katika Shamba la Mbegu la Magereza (Awamu ya 1&2) ambazo endapo hazitafanyiwa kazi zinaweza kuwa kikwazo kwa miradi hii kuwa na tija iliyokusudiwa.

Kasoro zilizobainika na kutakiwa kutolewa maelezo ni pamoja na:-

i. Kuchelewa kumalizika kwa mradi huu Awamu ya kwanza baada ya mkandarasi wa awali kushindwa kukamilisha kutokana na uchimbaji ulipofika mita 140 kukutana na aina ya mwamba wa volcano unaomegekea ndani na kushindwa kuendelea na uchimbaji.

ii. Mkandarasi wa pili, kushindwa kukamilisha awamu ya kwanza ya uchimbaji visima viwili, kadiri ya makubaliano ambapo alipaswa akamilishe januari 9, 2018.

iii. Mkandarasi aliepo kutaka kufanya mabadiliko ili atumie bomba za plastiki tofauti na ilivyokubaliwa kwenye mkataba ambao unaonesha kutumia bomba za chuma.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia dosari hizi, Kamati ilitaka maelezo kuhusu:-

- Sababu za wakandarasi wa kwanza na wa pili kushindwa kutekeleza mradi kwa muda uliopangwa, na hatua zinazochukuliwa

- Sababu za mkandarasi wa pili kutaka kutumia mabomba ya plastiki badala ya chuma kama ilivyo katika mkataba na hatua zinazochukuliwa.

- Kujua kama changamoto zilizomkumba mkandarasi wa awali alieshindwa kukamilisha mradi zilifahamika na kuelezwa mkandarasi anaeendelea na kazi kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Kamati kuridhika na hatua ya utekelezaji miradi, ilishauri Mamlaka ya AUWASA na Wizara ya Maji kutambua maeneo ya kimkakati kwa ajili ya hifadhi ya mazingira ili kulinda vyanzo vya maji na kwa ajili ya matumizi endelevu. Vilevile itasaidia kupunguza gharama kubwa za kupata maeneo ya kujenga miundombinu ya maji pindi ikihitajika.

Kwa upande wa Mradi wa vijiji 10 H/W –Longido, Kamati ilishauri Halmashauri kuongeza eneo la uhifadhi wa msitu wenye chemchem ya maji ambayo ni chanzo cha maji ya mradi. Na kwamba ili kufanikisha hili Halmashauri iratibu na kutekeleza uwekaji wa sehemu ya kunyweshea mifugo maji mbali na eneo la chemchem, ili mifugo isiende katika chanzo.

**b) Mkoa wa Kilimanjaro**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi) – MUWSA kuhusu hali ya upatikanaji maji katika Mkoa na miradi inayotekelezwa na Mamlaka.

Taarifa ya MUWSA ilieleza kuwa, Mamlaka inahudumia eneo la Manispaa lenye wakazi wapatao 197,840 (sensa 2012) Na kwamba wakazi wanaopata huduma ya maji safi katika manispaa ya moshi ni asilimia 100 ya wakazi wote. Na kwamba kuanzia mwezi machi 2016, Mamlaka imeongezewa kuhudumia eneo la Mji mdogo wa Himo unaokadiriwa kuwa na wakazi **45,153.** Lakini pia Mamlaka inatoa huduma kwa wakazi wapatao 33,000 walioko pembezoni mwa eneo la huduma kisheria kutoka maeneo ya Wilaya ya Hai na Moshi Vijijini. Kwa ujumla Mamlaka inatoa huduma ya majitaka katika manispaa kwa asilimia 18% ya eneo na asilimia 32 ya wakazi wa Moshi. Aidha mji mdogo wa Himo hauna huduma ya maji taka.

**Mheshimiwa Spika,**Taarifa iliainisha changamoto kadhaa ambazo zinaikabili mamlaka ambazo ufumbuzi wake umekuwa mgumu kupatikana,ikiwa ni pamoja na:-

i) Taasisi za Serikali kutolipia huduma kwa wakati, ambapo hadi kufikia disemba 2017 Mamlaka inazidai Taasisi za Serikali kiasi cha **1,875,337,124.60**

ii) Madai ya kodi ya TRA ya shilingi **2,680,289,748.20,** ambayo inaelezwa kuwa ni corporate tax

wakati mamlaka kisheria haipo kibiashara bali ni kutoa huduma.

Pamoja na mafanikio ya mamlaka, Wajumbe waliibua hoja na kutaka maelezo kuhusu:-

i) Hatua zinazochukuliwa kuzibana mamlaka ya serikali kulipa ankara za maji kwa wakati

ii) Hatua zinazochukuliwa na Mamlaka kupata tafsiri sahihi ya sheria ya kodi, kuhusu kulipa *corporate tax* kwa taasisi za umma zinazotoa huduma kama MUWSA.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa, kujadili na kushauri namna bora ya kutatua changamoto zilizopo, Kamati iliendelea na ziara yake kutembelea miradi katika H/W-Mwanga ambapo ilitembelea:-

i) Mradi wa skimu ndogo ya Umwagiliaji ya Kileo

ii) Mradi wa Maji wa Same –Mwanga-Korogwe

Kwa ujumla, Kamati iliridhika na utekelezaji na ufanisi wa miradi hii. Hata hivyo kamati ilibaini kuwepo kasoro chache na kushauri hatua za kuchukua ili kuzirekebisha ili wananchi waweze kupata faida za miradi zilizokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kasoro kadhaa na kushauri hatua za kuchukua kama ifuatavyo:-

i) Malalamiko ya wananchi kuhusu uwezo wa mashine ya kukoboa mpunga katika ushirika wa mradi wa Kileo. Wananchi walionesha wasiwasi kuwa mashine hiyo haina

ii) ufanisi na uwezo wake ni mdogo, kutokana na baadhi ya sehemu ya mashine kuwa haijaletwa, wakati viongozi wa ushirika na Halmashauri wakisisitiza kuwa mashine ina uwezo wa kutosha na inatoa huduma nzuri. Kamati ilielekeza watendaji wa Halmashauri na viongozi wa ushirika

kuweka wazi taarifa zinazohusu uwezo wa mashine .Vilevile kuendelea kuishauri wizara ifuatilie kujua ukweli wa jambo hilo.

iii) Malalamiko ya wananchi kuwa maji yanayotumika katika mradi ambayo yanahudumia pia Nchi jirani ya Kenya, huenda yanawanufaisha wakenya zaidi, hivyo kutaka ukubwa wa mradi uongezwe. Kamati iliishauri Halmashauri kufanya tathmini kuona kama mradi unaweza kupanuliwa zaidi na kunufaisha wananchi wengi zaidi.

iv) Malalamiko ya wananchi kuhusu mradi kujengwa chini ya kiwango, wakati watendaji wa Halmashauri wakisisitiza kuwa mradi una viwango, tatizo ni wananchi kutokuwa makini katika kuutunza na ukarabati pindi uharibifu unapotokea. Kamati ilishauri Halmashauri, Wizara na Wanaushirika kutathmini hali ya miundombinu ya mradi toka kwenye chanzo hadi mashambani kuona umadhubuti wa miundombinu. Lakini pia kuhakikisha kuwa mradi unafanyiwa matengenezo kadiri inavyohitajika ili udumu kwa muda mrefu.

v) Katika Mradi mkubwa wa Maji wa Same-Mwanga –Korogwe, Kamati iliridhika na hatua na maendeleo ya ujenzi. Hata hivyo inaisisitiza Wizara kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji ili umalizike kadiri ya makubaliano.Vilevile kuiomba Serikali kutoa fedha kadiri ya makubaliano ili ujenzi wake ukamilike kwa wakati.

**c) Mkoa wa Dar es salaam**

Kamati ilipokea taarifa ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Dar res salaam (DAWASA) ambayo ilieleza kuwa mahitaji ya maji kwa jiji la Dar es salaam ni mita za ujazo 544,000. Aidha maji yanayozalishwa sasa mara baada ya mtambo wa Ruvu Juu kuanza kazi ni mita za ujazo 502,000 kwa siku. Hata hivyo, pamoja na kuwepo ongezeko la maji kutoka mita za ujazo (300,000 hadi 502,000) bado baadhi ya maeneo hayajafikiwa, na Mamlaka inaendelea na jitihada za kupanua miundombinu ya mitandao ya usambazaji maji safi. Aidha huduma ya uondoaji maji taka kwa jiji la Dare es salaam ni asilimia **10%** pekee. Taarifa pia imeeleza

changamoto kuwa, kwa robo mwaka inayoishia disemba asilimia **55%** ya maji yanayozalishwa hayalipiwi (non revenue water) kutokana na uvujaji unaosababishwa na uchakavu wa mambomba, kumwagilia mashamba na uunganishaji haramu wa mabomba.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia taarifa hii wajumbe walitaka maelezo kuhusu hatua zinazochukuliwa:-

i) Kukabiliana na changamoto ya maji mengi yanayopotea kwa kuvuja au kuibiwa

ii) Kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya utoaji maji taka.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa Kamati iliendelea na ratiba ya kutembelea miradi ambapo ilikagua miradi kadhaa ifuatayo:-

i) Ujenzi wa vituo vinne vya kusukuma maji (Makongo,Wazo,Salasala na Bunju)

ii) Ujenzi wa Matenki ya maji (Wazo, Salasala, Bunju na Changanyikeni

iii) Mradi wa ulazaji mabomba ya kusambaza maji (Mbezi temboni na Msakuzi)

iv) Mradi wa uzalishaji maji -Mtoni Ruvu Darajani *(intake*)

v) Mradi wa kusafisha maji –Ruvu juu *(treatment process)*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Kamati iliridhika na utekelezaji wa miradi hii ambayo inalenga kuongeza usambazaji maji kwa wakazi wa maeneo ya Jiji la Dar es salaam, Kamati ilibaini kuwepo kasoro chache ambazo hazina budi kufanyiwa kazi ili kuwezesha wananchi kupata faida za miradi zilizokusudiwa. Kasoro hizo ni pamoja na:-

i) Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa usambazaji maji awamu ya kwanza ambao ulipaswa kukamilika tarehe 16 Novemba, 2017 na kuongezwa muda hadi tarehe 24 Februari, 2018. Wakati Kamati ilivyotembelea utekelezaji wa mradi ulikua ni asilimia **72%.** Kamati ina wasiwasi kama katika kipindi cha mwezi mmoja kilichosalia kufikia tar 24 februari,2018 mradi utakamilika

ii) Mradi umepangwa kugharimu kiasi cha USD $ 32.9 millioni. Ikiwa ni mkopo nafuu kutoka Benk ya Exim ya China. Kamati ilionesha wasiwasi kuhusu unafuu wa mkopo huu kutokana na aina ya mkopo ambayo masharti yake yameelekeza mkandarasi wa mradi, wataalamu, vifaa vya mradi, mshauri mwelekezi wa mradi watoke India. Aina hii ya mkopo hauweki ushindani ulio sawa, unanyima Kampuni za ndani zabuni, unanyima watanzania fursa za ajira na utaalamu, unanyima viwanda vya ndani soko la vifaa na vipuri, lakini pia unaweka mazingira magumu ya Serikali kuweza kusimamia ubora na ufanisi wa utekelezaji mradi kutaja kwa uchache. Kamati inatahadharisha Serikali juu ya kutathmini unafuu unaoelezwa katika mikopo ya aina hii ambayo haioneshi kuwa na tija kubwa kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia kasoro zilizobainika, Kamati inaishauri Serikali iendelee kusimamia ipasavyo matakwa ya mkataba ili mkandarasi aweze kukamilisha ujenzi wa miradi kama ilivyokubaliwa. Aidha Serikali itathmini na ikiwezekana iachane na aina ya mikopo ambayo inakuwa na masharti yanayoonekana kutokuwa na manufaa kwa Taifa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati inasikitishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mapendekezo

na ushauri wa Kamati katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji uliotolewa mwezi februari, 2017, Kamati ilipowasilisha taarifa yake ya mwaka 2016 na kuridhiwa na Bunge lako tukufu. Hivyo Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza kazi ya utekelezaji wake kwa manufaa ya Taifa. Aidha naomba kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati katika maeneo yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

### 3.1 Kuongeza bajeti ya sekta na fedha kutolewa kwa wakati

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji mdogo wa sekta za kilimo, Mifugo na Maji unachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mdogo katika sekta.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano: kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilitenga **asilimia 4.9** tu ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kamati inatahadharisha kuwa, endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa katika kuinua Sekta hizi, ni dhahiri kuwa mdororo wa uchumi na mnyororo wa umaskini utaendelea kuwa kilio cha wananchi mahala pengi nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanza sasa kutekeleza kwa vitendo Azimio la Maputo, ambalo linazitaka nchi wananchama kutenga **asilimia 10** ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya kilimo**.**

Kwa sekta ya maji, pamoja na kuwa maji ni hitaji muhimu na la msingi katika kila sekta ya binadamu, bado kumekuwepo na mtiririko usioridhisha wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji nchini. Kwa mfano, Wizara ya Maji **Fungu 49,** iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shilling **bilioni 408.6,** hadi kufikia disemba 2017, kiasi kilichotolewa ni asilimia **25%** ya fedha za ndani. Aidha fedha za nje iliidhinishiwa **billioni 214.9** ambapo hadi disemba 2017 fedha iliyopokelewa ni asilimia **1.86%** tu. Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji **Fungu 5**, iliidhinishiwa fedha za ndani kiasi cha shilingi billion **5.6,** hadi kufikia disemba 2017, hakuna fedha za ndani zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha

Tume iliidhinishiwa fedha za nje kiasi cha **shilingi billioni 14.5**, hadi disemba 2017, Tume imepokea fedha za nje asilimia **1.6** tu. Mwenendo huu wa utoaji fedha haukidhi kiu ya wananchi kupata huduma ya maji. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuwa na uhakika wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa maslahi mapana ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** endapo pendekezo hili litatekelezwa katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi litasaidia kuongeza ajira, maligafi kwa ajili ya viwanda, kuongeza pato na ustawi wa wakulima, udhibiti wa uvuvi haramu lakini pia kuongeza pato la Taifa kwa ujumla na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika sekta ya maji litasaidia kuondokana na kero za muda mrefu za ukosefu wa huduma ya maji ambayo ni huduma muhimu katika ustawi wa binadamu, wanyama, mazingira na uzalishaji mali, kupungua kwa migogoro ya wakulima na wafugaji.

### 3.2 Kutekeleza mipango ya uzalishaji mbolea nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyokwisha onekana katika utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, bado ipo haja ya kuondokana na uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo adhma yake ya kuzalisha mbolea hapa nchini kwa kujenga viwanda vya kuzalisha mbolea au kuweka mazingira rafiki kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika kuwekeza katika tasnia ya mbolea. Kwa kuanzia

Kamati inashauri Serikali kuanza ujenzi wa viwanda vya mbolea vya Kilwa na Mtwara. Pendekezo hili linazingatia ukweli kuwa, asilimia **90%** ya mbolea inayotumika nchini kwa sasa inaagizwa kutoka nje. Na kwamba, hadi kufikia februari 2018, kiasi cha mbolea iliyoingizwa nchini ni tani **233,001.49** ambayo ni asilimia 48 ya mahitaji na hivyo kuwepo kwa upungufu wa asilimia **52%.** Aidha pamoja na hatua ya serikali kufanya ununuzi wa mbolea kwa pamoja, bado upatikanaji

wa mbolea nchini katika maeneo ya uzalishaji mkubwa haukidhi mahitaji. Bei ya mbolea haijashuka kama ilivyokusudiwa na upatikanaji wa mbolea umekuwa sio wa uhakika. Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya mafanikio ya malengo ya Mpango huu, kisha kuchukua hatua stahili. Vile vile Kamati inashauri kuwa, ili kuifanya Kampuni ya Mbolea ya Taifa (Tanzania Fertilizer Company) kuwa na ufanisi wa kutosha katika tasnia ya mbolea, Serikali ihamishe kampuni hii chini ya usimamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na kuiweka chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Pendekezo hili likitekelezwa litasaidia kuondokana na vikwazo na hujuma zinazoweza kutokana na siasa ya dunia inayofungamana na biashara ya mbolea inayofanywa na makampuni ya kimataifa ya mbolea duniani.

### 3.3 Uzalishaji, masoko na usalama wa chakula Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Utoshelevu wa chakula ni nguzo muhimu katika kupanga kiwango cha uzalishaji, kujenga mazingira mazuri ya kilimo cha biashara na Uratibu wa masoko. Kamati imebaini kuwa, katika nyakati tofauti Serikali imekuwa ikitoa maagizo na amri au zuio kuhusu biashara ya uuzaji mahindi nje ya nchi ambayo kwa kiasi fulani yamekua yakiathiri biashara ya mahindi na uzalishaji, hususan wanaofanya kilimo cha biashara. Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uratibu wa usimamizi kwa kutekeleza mikakati madhubuti ya kupata takwimu sahihi na kwa muda unaostahili kuhusu kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali zitakazosaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi kwa mwenendo wa biashara ya ndani na nje ya mipaka hususan kwa mazao ya nafaka bila ya kusababisha athari mbaya katika uzalishaji, biashara na wakulima. Aidha Kamati inaishauri Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kujenga na kukarabati maghala ili kuwa na uhakika na usalama wa hifadhi ya nafaka.

### 3.4 Mikakati ya kuimaririsha masoko ya mazao ya mahindi na mbaazi kwa wakulima nchini

Kamati inaitahadharisha Serikali juu ya uwezekano wa uzalishaji kwa msimu wa 2017/2018 kuwa pungufu kutokana na wakulima kutouza mahindi hivyo kukosa fedha za kununulia pembejeo kwa msimu huu. Aidha baadhi ya wakulima wa mahindi na mbaazi kutolima kabisa baada ya kukata tamaa ya kukosa soko la mazao yao. Kamati inalishauri Bunge, liitake Serikali kuharakisha kutafuta masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi ili wakulima waweze kuuza mazao yao na kufanya kilimo cha biashara. Kamati inaitahadharisha Serikali kutotegemea nchi moja ya India kwa ajili ya soko la mbaazi na kunde kwa ujumla. Aidha Serikali itoe fedha za ziada kwa NFRA na CPB kama hatua ya dharura ya kuziwezesha kununua mahindi na mbaazi ambazo bado hazijanunuliwa hadi sasa.

### 3.5 Uzalishaji na masoko ya mazao ya Biashara

**Mheshimiwa Spika,** kamati imebaini kuwa katika miaka ya hivi karibuni mazao ya biashara yakiwepo pamba, tumbaku na kahawa yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, matumizi duni ya teknolojia na pembejeo, masoko machache ya ndani na utegemezi wa soko la nje, kuendelea kupungua / na kukosekana kwa ruzuku ya Serikali pamoja na kukosekana kwa mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo. Hivyo kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kuchukua hatua madhubuti kusimamia na kuimarisha vyama vya ushirika, kuongeza matumizi ya teknolojia ya kisasa na pembejeo katika uzalishaji, kutafuta masoko ya uhakika ya mazao na muhimu zaidi kuchukua hatua za makusudi katika kuongeza mnyororo wa thamani kwa mazao hayo.

### 3.6 Uzalishaji na masoko ya mazao ya bustani

**Mheshimiwa Spika**, sekta ndogo ya mazao ya bustani ikihusisha mbogamboga na matunda imekuwa ikitoa ajira

kwa wananchi na hasa vijana na kinamama**.** Kuongezeka kwa mahitaji ya matunda na mboga kunatoa fursa ya ajira, kipato na uchumi wa wakulima na Taifa kwa ujumla. Ili kuwa na uzalishaji wenye tija, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira rafiki kwa kutunga sera, sheria, kanuni za kilimo hiki. Lakini pia kuongeza kasi kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ya uzalishaji, kuchakata na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa ili kuwa na uhakika wa kufikisha mazao hayo katika masoko bila ya kuharibika.

### 3.7 Kuongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika**, Ukosefu wa mikopo ya uhakika na yenye riba nafuu kwa wakulima walio wengi ni kikwazo kwa wakulima kutoweza kukopa na kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Benki ya Kilimo (TADB), hadi mwezi disemba, 2017 ilikua na mtaji wa kiasi cha shilingi **66,785,790,739.00.** Aidha kiasi cha mtaji kilichoombwa ni shilingi bilioni **800.**

Kamati inaishauri Serikali kuongeza mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ili ibebe jukumu hili la kutoa mikopo kwa wakulima wengi zaidi katika maeneo mbalimbai nchini. Aidha ili kufikia adhma hii Kamati inasisitiza kuwepo uwiano wa mtawanyiko wa huduma zitakazotolewa na benki hii katika maeneo ya uzalishaji vijijini ili kutoa elimu na kuhamasisha utoaji mikopo ya kilimo cha biashara badala ya ilivyo sasa ambapo inaendesha shughuli zake katika maeneo machache ya mjini, ambayo si wakulima wote wanaweza kuzifikia.

### 3.8 Suluhisho la migogoro ya matumizi ya ardhi

**Mheshimiwa Spika**, migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na kuathiri uzalishaji katika sekta mbalimbali za kilimo kutokana na hofu, uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mali na mazingira. Kamati inasisitiza kuwa, migogoro ya

matumizi ya ardhi ni mtambuka na hivyo suluhu yake inaweza kupatikana kupitia jitihada za pamoja miongoni mwa sekta husika. Kamati imeelezwa kuwa katika kulifanyia kazi suala hili, katika nyakati tofauti Serikali imeunda Tume na kuhusisha Wizara tano zinazohusika na migogoro hii ya ardhi. Kamati inahoji juu ya lini mapendekezo ya Tume hii yatatekelezwa kwa vitendo. Kamati imebaini kuwa taarifa za Mamlaka mbalimbali za Serikali zinaeleza kuwa suluhisho la migogoro iliyopo ni kutekeleza Mpango wa Matumizi bora ya ardhi nchini. Kamati inalishauri Bunge liazimie kuitaka Serikali kutekeleza kwa vitendo maoni na mapendekezo yaliyokwishatolewa na Tume iliyoundwa. Aidha Serikali iongeze kasi ya kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999, pamoja na kuhuisha sheria zingine zinazosimamia matumizi, umiliki, uhifadhi ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu ardhi.

### 3.9 Rasilimali za uvuvi na udhibiti uvuvi haramu nchini

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uvuvi haijalinufaisha Taifa kwa kiwango kinachostahili. Makisio ya rasilimali za uvuvi nchini ni tani **2,143,211** (maji ya bahari ya ukanda wa ndani wa Taifa, maziwa na mito, bila kuhusisha Bahari kuu) Makadirio ya kiasi cha samaki wanaoweza kuvuliwa ni tani za mita **730,000** kwa mwaka. Aidha kiasi kinachovuliwa kwa sasa ni tani za mita **350,000** kwa mwaka**.** Mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa ni asilimia **2%** (NBS, 2016. Uwezo wa mchango wa sekta ya uvuvi endapo kungekuwa na uwekezaji wa kutosha unaozingatia uwezo wa rasilimali za uvuvi zilizopo ni tani za mita **730,000** na ingeweza kuchangia asilimia **4.2** katika Pato la Taifa. (Bila kuhusisha Bahari kuu)

**Mheshimiwa Spika**, mipango ya kuongeza tija katika sekta ya uvuvi imeshindwa kutekelezeka kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa, kuidhinishwa na kutolewa. Kwa mfano katika Bajeti ya 2017/2018 miradi ya maendeleo katika sekta ilitengewa kiasi cha shilling **6,000,000,000**, hadi kufikia disemba 2017, hakuna fedha yoyote iliyotolewa. Kamati

inasikitishwa na mwenendo huu wa kutotolewa fedha zinazoidhinishwa katika sekta ya uvuvi. Aidha inaomba Bunge kupitisha Azimio la kuitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha na kuitoa kwa wakati stahili ili kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya uvuvi hususan kutekeleza Mpango wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika utendaji wake imebaini kuwepo malalamiko mengi yanayohusu namna kampeni ya kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Viktoria inavyoendeshwa na kwamba imesababisha hasara kubwa kwa wavuvi kwa kuchomewa kambi za wavuvi, mitumbwi, nyavu na nyenzo zingine. Kufuatia malalamiko yaliyopo, Kamati inatilia shaka njia zinazotumika katika udhibiti vitendo vya uvuvi haramu kama inaweza kuleta tija inayokusudiwa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, jitihada kubwa zilipaswa kuelekezwa katika kudhibiti utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi haramu, badala ya kuharibu nyenzo za uvuvi kama mitumbwi ambayo si nyenzo haramu na kuacha wananchi wavuvi wakiwa maskini na bila ya msaada wowote wa zana bora na mafunzo ya mbinu bora za uvuvi.

Aidha ikizingatiwa kuwa Ziwa viktoria linatumiwa pia na nchi ya Uganda na Kenya jitihada hizi zilipaswa kushirikisha nchi zote, ili kuwa na namna moja ya kudhibiti uvuvi haramu, kwani baadhi ya nyezo zinazokatazwa kutumika Tanzania, kwa nchi jirani za Kenya na Uganda zinatumika. Ipo hatari ya Watanzania kuhifadhi rasilima katika Ziwa Viktoria na wanufaikaji kuwa wavuvi wa nchi jirani. Kamati inashauri Serikali kutathmini hatua na njia zinazotumika kudhibiti uvuvi haramu ili ziwe shirikishi zaidi pamoja na msisitizo kuwa ni kuzuia utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi.

### 3.10 Uwekezaji katika Ranchi za Taifa

Ranchi za Taifa ni rasilimali muhimu na fursa kubwa katika kuchangia pato la Taifa na uchumi wa wafugaji. Tanzania ina jumla ya Ranchi **13** zenye ukubwa wa jumla ya hekta **627,856,** katika mikoa **10** chini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi, Kamati imeelezwa hali ya uwekezaji uliopo katika Ranchi za Taifa, changamoto na mafanikio na kujiridhisha kuwa fursa na rasilimali ya ranchi za Taifa haijatumika ipasavyo. Ili kuwa na uwekezaji wenye tija kwenye Ranchi za Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya uwekezaji wa kisasa katika Ranchi za Taifa ambao utasaidia wafugaji wengi kujifunza mbinu za ufugaji bora. Kamati inasisitiza ushauri iliokwishautoa mwaka jana wa kuitaka Serikali kufanya tathmini ya matumizi yaliyopo, kisha kuweka mikakati ya kuona namna ya kuruhusu wananchi waishio karibu na ranchi hizi, ili kupata huduma za malisho na maji kwa ajili ya mifugo kwa utaratibu utakaoonekana unafaa. Aidha, ni vyema Serikali ikaandaa na kutekeleza mkakati wa makusudi wa kuongeza thamani ya mazao ya mifugo kwa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo, ili kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

### 3.11 Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi

Kwa kutambua kuwa nchi yetu ina fursa na maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo takwimu zinaonesha Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa **hekta 29.4 milioni** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hadi sasa ni **hekta 461,326** sawa na **asilimia1.6** ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Ulinganisho wa uzalishaji *(productivity)* wa zao la mahindi kwa hekta kwa kufanya umwagiliaji ni tani **3.75** kwa hekta, wakati kulima kwa kutegemea mvua ni tani **2.7** kwa hekta. (Sakalilo Irrigation Scheme- Rukwa). Kwa zao la Mpunga ni tani **4.5-5.5** kwa hekta, wakati uzalishaji kwa kutegemea mvua ni tani **2.2-3.0** kwa hekta. (Mombo Irrigation Scheme-Tanga). Hii ni katika maeneo yanayofanana na matumizi ya pembejeo na teknolojia sawa.

Kwa tofauti hii ya uzalishaji, Kamati inashauri kuwa, katika kipindi hiki ambapo mabadiliko ya tabianchi yamepelekea mvua kutokuwa za uhakika na kuathiri

uzalishaji, umwagiliaji ni moja ya njia muhimu ya kuongeza na kuimarisha uzalishaji wenye tija, hivyo Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kuitengea Tume ya Taifa ya Umwagiliaji bajeti ya kutosha itakayowezesha Tume kuandaa miundombinu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na hivyo kupunguza utegemezi wa kilimo cha mvua ambacho kinazidi kutotabirika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuainisha maeneo machache ya kipaumbele yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha hizo katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

### 3.12 Kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya kimkakati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo miradi ya mabwawa nchini ambayo imechukua muda mrefu kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha. Kutokamilika kwa ujenzi wa mabwawa kwa muda uliopangwa kunaisababishia Serikali hasara kutokana na miundombinu ya miradi hiyo kuchakaa kabla ya kuanza kutumika, lakini pia kuongezeka kwa gharama za ujenzi tofauti na ilivyokadiriwa na hivyo kuwakosesha wananchi huduma iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kujenga na kukarabati miradi inayoendelea, ili kuepusha hasara inayoweza kutokea kutokana na miradi kuchukua muda mrefu, lakini pia kuweza kufikia malengo na makusudio ya miradi hiyo kwa wananchi kupata huduma.

### 3.13 Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa, hadi disemba 2017 hali ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa ni wastani wa asilimia **56 %** kwa vijijini na asilimi **69 %** kwa mijini. Aidha malengo ya upatikanaji maji safi na salama Kitaifa kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ( 2016/2017 hadi 2020/2021 ni asilimia **85%** kwa vijijini na asilimia **95%** kwa mijini ifikapo Mwaka 2021. Kamati

ina wasiwasi juu ya kufikiwa kwa malengo haya kwani, kumekuwa na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maji. Kwa mfano katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018, fedha za maendeleo zilizotengwa kwa fungu **49** ni asilimia **17.16%** tu zimetolewa hadi kufikia disemba, 2017 kiasi kikubwa asilimia **77%** zikiwa ni fedha za mfuko wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Aidha kutokana na kwamba fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maji vijijini ni kutokana na mfuko wa maji, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri iliyoutoa katika taarifa ya mwaka ya Kamati ya Mwaka 2016 kuwa, Bunge liazimie kuitaka Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria ya fedha ya mwaka 2018 kwa kuweka tozo ya shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli. Mapendekezo hayo yakizingatiwa yatawezesha miradi ya maji kutekelezwa kwa ufanisi nchi nzima. Aidha Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya uratibu wa mfuko wa maji mijini kwa ajili ya kupata fedha za uhakika kwa ajili ya miradi ya maji mijini, ambapo takwimu zinaonesha kuwa bado upatikanaji maji katika maeneo mengi mjini si wa uhakika.

Vilevile kutokana na dosari iliyobainika ya kuwepo na usimamizi usiokidhi wa uendeshaji wa miradi ya maji katika maeneo mengi vijijini, Kamati inalishauri Bunge liazimie kuitaka Serikali kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, ambao pamoja na mambo mengine utakuwa na jukumu la uratibu na usimamizi wa miradi ya maji vijijini. Aidha, Kamati inashauri Bunge liitake serikali kuongeza kasi ya utoaji fedha za bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya miradi ya maji kadri zilivyoidhinishwa na Bunge lako tukufu ili kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

### 3.14 **Kuweka mazingira bora ili kuchochea sekta binafsi kushiriki kuwekeza katika tasnia za kilimo, mifugo, uvuvi na maji**

**Mheshimiwa Spika,** utendaji wa Kamati katika nyakati tofauti na aeneo mbalimbali umebaini kuwepo malalamiko

kutoka kwa wadau wa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji ya kutokuwepo mazingira wezeshi ya kuwekeza katika sekta tajwa kwa tija. Kwa ujumla malalamiko yao yanajikita katika kuwepo changamoto ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuwepo mamlaka nyingi za Serikali za udhibiti unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa wawekezaji,

(i) Ushindani usio wa haki unaosababishwa na bidhaa kutoka nje na zisizo na ubora kusababisha kukosa masoko ya uhakika ya bidhaa za ndani,

(ii) Tozo nyingi kwa baadhi ya bidhaa, mfano ladha za maziwa na vifungashio,

(iii) Ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini unaopelekea ugumu wa wakulima kufikisha bidhaa katika masoko au viwanda kwa muda unaostahili, na

(iv) Ukosefu wa umeme wa uhakika kwa ajili ya viwanda.

Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi changamoto hizi, kwa kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora yasiyo na urasimu yatakayowezesha na kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwa faida katika sekta hizi.

3.15 **Kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe Kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on The Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi*)**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

a) Kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, na kwa kuwa mkataba huu unahusisha nchi za Tanzania na

Malawi ambazo zimekuwa na mgogoro wa mara kwa mara kuhusu mpaka wa Ziwa Nyasa, Kamati inaishauri Serikali kuchukua tahadhari na kuhakikisha utekelezaji wa mkataba huu hautaathiri faida ambazo nchi imekuwa ikipata kutoka Ziwa Nyasa na Mto Songwe.

b) Kwa kuwa nchi ya Tanzania na Malawi zimekuwa na mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa kwa muda mrefu, na kwa kuwa uhai wa Ziwa Nyasa ni Mto Songwe, pamoja na kwamba mkataba huu unahusu Mto Songwe, Kamati inaishauri Serikali kupitia fursa ya Mkataba huu kufanya utambuzi wa Mipaka ya Ziwa Nyasa hatua ambayo inaweza kumaliza kabisa tatizo la mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa.

c) Kwa kuwa Mkataba huu unahusisha nchi mbili ni vyema baada ya kuridhiwa na Bunge, Serikali iharakishe utungwaji wa Sheria na Kanuni zake ili wananchi wa Tanzania waanze kunufaika na faida zilizoainishwa kwenye mkataba huu.

d) Baada ya nchi wanachama kuridhia utekelezaji wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe, elimu ya kutosha itolewe hususan kwa wananchi waishio maeneo ya mpaka wa Tanzania na Malawi kuhusu utunzaji wa mazingira kwenye eneo la Mto Songwe pamoja na kutumia vizuri faida zitakazopatikana kutokana na mkataba huu pamoja na kutoa elimu kuhusu mipaka ya nchi husika.

### 3.16 Mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao ya pamba, viwavijeshi na panya

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepata taarifa ya namna Wizara ilivyoshughulikia mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao wakiwemo wadudu wa vijidudu viharibifu vya pamba, viwavi jeshi na panya. Kamati imefahamishwa kuwa, tayari Wizara imechukua hatua za makusudi kwa ajili ya kupata fedha ya kununulia viuatilifu ili kukabiliana na mlipuko huo. Kamati ilielezwa kwamba kufikia Januari 30,

2018 Wizara ilikuwa imepata fedha kiasi cha shilingi **bilioni 3** kwa ajili ya kununua viuadudu vya pamba na taratibu za kupeleka viuatilifu hivyo zimefanywa. Aidha, Wizara imefanya mazungumzo na Benki ya Kilimo Tanzania ili iweze kutoa mkopo wa **bilioni 3** ili kuongeza upatikanaji wa viuadudu vya pamba.

Vilevile, Wizara imewasilisha maombi ya fedha Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha maafa ili kupata msaada wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na dharura ya viwavijeshi. Wakati huo huo imefanya maombi ya fedha kiasi cha shilingi **bilioni 10** kutoka Hazina ili kuongeza kazi ya kukabiliana na viwavijeshi na panya.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na dharura ya mlipuko wa wadudu waharibifu wa mazao, Kamati imesikitishwa na kasi ndogo ya upatikanaji wa fedha inayohitajika. Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kutoa fedha zilizoombwa ili kukabiliana na wadudu waharibifu wa mazao, na kuepusha hasara ambayo inaweza kusababishwa kwa kushindwa kuwadhibiti kwa wakati.

### 3.17 Korosho kuchanganywa na mawe/kokoto

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata taarifa na malalamiko kuhusu shehena ya korosho iliyouzwa nchini Vietinam kiasi cha **tani 172** ambapo gunia **78** za shehena hiyo ililalamikiwa kuchanganywa na mawe/kokoto. Kamati ilielezwa pia kuwa kwa msimu wa 2016/2017 Jumla ya korosho yote iliyouzwa nje ya nchi inakadiriwa kuwa ni **tani 320,000** na kwamba hakuna malalamiko yoyeote yaliyopokelewa kuhusu korosho iliyouzwa katika nchi zingine. Kufuatia malalamiko hayo Kamati ilitaka maelezo ya kina kuhusu tuhuma tajwa, kwani ni fedheha kwa nchi na dosari kubwa katika biashara ya korosho.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ilieleza kamati hatua ilizochukua kushughulikia suala hili ikiwa ni pamoja na kuunda tume ya watu 9 ili kubaini ukweli dhidi ya tuhuma

tajwa na kushauri hatua madhubuti za kuchukua kukomesha vitendo vya aina hii visitokee tena. Tume imetakiwa kukamilisha taarifa yake ndani ya siku **14**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na tuhuma zinazotajwa ambazo zinachafua heshima ya Taifa letu na biashara ya korosho. Kamati inaliomba Bunge liishauri Serikali kufuatilia kwa karibu mazingira yanayozunguka biashara ya tasnia ya korosho, ili kubaini mianya yoyote inayoweza kusababisha hujuma na kuidhibiti. Vilevile kuchukua hatua za kinidhamu na Kisheria kwa wote watakaothibitika na tuhuma tajwa.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa pekee napenda kuishukuru Serikali kupitia Mawaziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hizi kwa ushirikiano wao wakati wote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Aidha, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta za Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao kwa namna moja au nyingine walishirikiana na Kamati wakati wa kuchambua Miswada, kutoa semina na mafunzo kwa wajumbe kwa lengo la kuongeza uelewa na hata wakati wa uchambuzi wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa, Mb | " |
| 5. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb | " |
| 6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | " |
| 7. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb | " |
| 8. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | " |
| 9. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | " |
| 10. Mhe. John John Mnyika, Mb | " |
| 11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb | " |
| 12. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb | " |
| 13. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb | " |
| 14. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb | " |
| 15. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb | " |
| 16. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | " |
| 17. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | " |
| 18. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mb | " |
| 19. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb | " |
| 20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb | " |
| 21. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | " |
| 22. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | " |
| 23. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | " |
| 24. Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani, Mb | ,, |
| 25. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | " |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Huduma za Jamii, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Martha Chassama kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

### 4.2. Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa

ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Mary M. Nagu, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

6 FEBRUARI, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru Wenyeviti wote, mmesoma vizuri sana, mmeonesha mnazitendea haki hizi Kamati zenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza mijadala na nimeambiwa hapa kutokana na muda mnachangia dakika saba. Tunaanza na Mheshimiwa Dokta Sware Semesi ajiandae Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nina mambo saba ambayo nataka nigusie na nitajielekeza katika taarifa iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi pamoja na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie kwanza suala la *NFRA.* Kumekuwa na sintofahamu mwaka wa fedha 2016/2017 kuhusu njaa, kukatokea *statements* mikanganyiko kuhusu kuna njaa au hakuna njaa nchini. Hii ilijitokeza kwa sababu baadhi ya mikoa ilizalisha vizuri na mikoa mingi zaidi nchini kwetu ilikuwa kwenye hali ya ukame na kutokuwa na chakula. Nchini kwetu tumejiwekea tu mfumo mzuri wa kuwa na *NFRA* ambayo *basically* inatakiwa i-*regulate* mifumuko ya bei ya vyakula kwa kuhifadhi na kutoa vyakula hivi masokoni ili ku-*balance* bei ya chakula na kuhakikisha kwamba kuna chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba *budget allocation* ambayo inatakiwa iende *specifically* kwa ajili ya *NFRA* ina utata, fedha hazitolewi kwa wakati na ni kidogo kwa hiyo mazao yanayonunuliwa ni machache na hayaendani sawasawa na msimu. Kwa hiyo, pesa zinapatikana nje ya msimu na kuathri mzungunguko mzima wa *stock* na mazao kwa ujumla wake. Naona tunaelekea kwenye dalili hizohizo kwa 2017/2018, kwa hiyo naomba Wizara iangalie tena hili kwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka niligusie ni kuhusu taasisi zetu za tafiti ambazo ziko chini ya Wizara ya Kilimo ambazo pia zipo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Huwezi kufanya mabadiliko yoyote au *decision* yoyote bila kuwa na *scientific back up* ya *information* au kuwa na *data* mahsusi. Cha kushangaza tunapopitisha bajeti humu ndani, hizi taasisi mahsusi za kufanya utafiti kwa ajili ya *fertilizers* au mbegu kadhaa au kwa ajili viuadudu kadhaa, haipangiwi hata senti tano. Inashangaza tunasema kwamba Tanzania inategemea kilimo, *majority* ya wananchi wetu ni wakulima, huu uti wa mgongo mbona hatuuwezeshi kwa kuziwezesha hizi taasisi zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu, tuna shida, nafikiri juzi tumeona Waheshimiwa Wabunge Ulanga imeingiliwa na panya, wanavamia mipunga, Serikali iliwahamasisha wakulima wa pamba wakalima sana wakaingiliwa na wadudu (viwavijeshi) na kadhalika. Kwanza hatuna hata bajeti ya kuweza ku-*handle,* mfano kwenye *issue* ya pamba Serikali imetoa bilioni tatu tu ili kuweza ku-*save* mazao hayo kati ya bilioni 39. Kuna Mfuko wa Waziri Mkuu hapa kuhusu maafa hakuna kitu, Wizara iliombwa iweze ku-*shuffle* kidogo bajeti yake, Hazina haijatoa hata senti tano kwa ajili ya ku-*deal* na hao wadudu wanaovamia mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* ina hela tata, *TPRI* kwa mfano au taasisi nyingine za shughuli za tafiti hakuna hela, yametokea majanga hakuna hela. Sasa tunaongelea matumbo yetu kuhusu chakula na pia tunaongelea mazao

ya biashara, hii nchi inasimamaje na wakati uti wa mgongo hatuuwezeshi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka niligusie kwa juu juuu pia ni bei elekezi na soko la bidhaa za mazao yetu. Tumeweza kulima mazao ya chakula, tumeweza kulima kidogo kwa kuchechemea mazao ya biashara. Serikali inaji-*commit* wakulima walime mazao fulani, mfano dhahiri ni mwaka jana na mwaka huu bado tuna-*suffer* na wakulima wetu wa mbaazi, soko halieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulihangaika huku kuhusu mazao ya mahindi, tukatokea na sintofahamu Kambi ya Upinzani ilishauri ruhusuni hata kutoa mazao hayo, *NFRA* inunue na kutoa mazao bei iwe elekezi ambayo ni nzuri kwa wahitaji, tuuze mazao yetu, mahindi yetu nje ya nchi. *Decision* imekuja kuongelewa hapa tukabezwa upande wa Upinzani lakini baadaye mlikuja kusema *go ahead,* lakini *it is too late.* Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuweka mikakati madhubuti ya mifumo ya masoko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie kuhusu uvuvi haramu na njia zinazotumiwa na Wizara husika kuudhibiti. Kwa mfano, mwezi huu uliopita, Wizara yangu hii ya Mifugo na Uvuvi ilijikita Mwanza ilikuwa Ukerewe, ikisema inadhibiti uvuvi haramu. Sasa unajiuliza ni kudhibiti au ni kumkandamiza huyu mvuvi? Ni ipi njia sahihi ya kumdhibiti huyu anayeitwa mvuvi haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye taarifa ya habari kwamba Katibu Mkuu wetu wa Uvuvi ameteketeza nyavu haramu za shilingi bilioni 2.6 Mwanza kwa ujumla wake. Unajiuliza hizi nyavu za gharama hii zimeingiaje nchini? Miaka nenda rudi tunasema tunachoma moto *tonnes and tonnes* za hizi nyavu lakini unajiuliza kwamba unadhibiti vya kwenye maji, vya kwenye ardhi je? Kwa sababu ukiangalia hata hiyo *mode* mnayoteketeza mnaharibu pia mazingira. Kwa hiyo, kwanza mnaharibu mifuko ya wale walionunua hizo nyavu, mnaharibu uchumi wa wale wavuvi wahusika kwa sababu hamwendi tu kuharibu nyavu bali hata zile

sehemu zao za kuvulia, *camps* zao mnachoma moto, vifaa vyao vya kuvulia kama maboti mnachoma moto, kulikoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, badala ya ku-*solve issue permanently* mnakuwa mnagusiagusia na kuweka gharama kubwa na kutia watu hasara na kuharibu mazingira mengine kwa kuchoma yale manailoni *in open space.* Kuna vikundi vya *BMU,* je, mmevihamasisha, mmeviwezesha kuweza kujikidhi kwa sababu vipo *specifically* kwa ajili ya ku-*regulate* uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ambalo naomba nigusie ni kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilomo *(TADB).* Benki hii ilianzishwa nafikiri 2015 na ikapewa mtaji wa *60 billion* na mpaka tunaongea sasa hivi benki hii haijawezeshwa, imeokoteza hapa na pale sasa hivi ina *only 66 billion* kama mtaji kati ya bilioni 800 ambayo inatakiwa iwe nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea maendeleo ya kilimo, yanatoka wapi? Hii benki iliwekwa mahususi kwa ajili ya kuendeleza kilimo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa, jiandae Mheshimiwa Dokta Ishengoma.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Naomba kuunga mkono taarifa za Kamati zote mbili, iliyosomwa na dada yangu, Mheshimiwa Kemilembe pamoja na mama Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kwenye ile Sehemu ya Tatu yenye maelezo ya ushauri, maoni na mapendekezo. Kabla ya hapo naomba nikuombe wewe kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kwa sababu Mwenyekiti wa

Kamati anapomaliza kutoa taarifa yake anasema naomba kutoa hoja na sisi hoja hiyo tunaiunga mkono lakini baada ya hapo tunachangia anakwenda anafanya *winding up* akishamaliza unatuuliza tunasema ndiyo. Kwa hiyo, unasimama unasema kwamba mapendekezo, maoni na ushauri tunaupeleka Serikalini na Serikali iuchukue. Sasa mimi swali langu, inapochukua ushauri, mapendekezo na maoni haya, hivi Bunge lako Tukufu kwa kila Kamati linapata *feedback* wapi na wakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu upo utaratibu baada ya kumaliza kwa mfano Kamati zote hizi kutoa taarifa zake, siku ya Ijumaa Ofisi ya Bunge inachukua mapendekezo, maoni na ushauri wa kila taarifa ya Kamati inatengeneza kitabu, hiyo ni Ofisi ya Spika, anakabidhiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu anatawanya yale mapendekezo kwa kila Wizara husika ili baadaye waje walete taarifa Bungeni, sasa sikumbuki mara ya mwisho ni lini ilifanyika hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sisi Wabunge tujitendee haki ni vizuri kwa yale mapendekezo tunayopendekeza ushauri na maoni yetu, tuwe tunapata *feedback.* Kama utakuwa ni utaratibu huu wa *business as usual,* tunatoa mapendekezo, ushauri, halafu hatupati mrejesho, hakuna kitu ambacho tutakuwa tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe tukianza kwa mfano na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwenye yale maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wangu wakati anasoma pale ambayo tuliyaridhia, lakini kwa yale maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mama Mary Nagu, hebu tujipe kwa mfano mwezi Machi, tuwe tunapewa taarifa na Wizara husika kwa yale ambayo tuliyopendekeza kwamba yametekelezwa kwa asilimia ngapi lakini kwa nini hatukuyatekeleza ili tuone namna nzuri zaidi ya kuishauri tena Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nakumbuka mwaka 2016 tulifanya hivihivi; mwaka 2017 tulifanya hivihivi; 2018 tunafanya hivihivi. Je, ule ushauri wetu,

sisi kama Bunge linalotoa mamlaka na sisi kazi zetu kama sikosei kupitia Ibara ya 65 ya Katiba, kazi yetu ni kuishauri Serikali, sasa tunapoishauri, je, tunapata mrejesho kutoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana uielekeze Serikali huu ushauri wetu ikiwezekana tutakaporudi kwenye Bunge la Machi kama siyo maoni, mapendekezo au ushauri wote angalau tupate ili tuweze kuisadia Serikali zaidi. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe sana Serikali kwa sababu kila taarifa iliyosomwa na Mwenyekiti wa Kamati humu ndani niliisikiliza. Taarifa nyingi au miradi mingi au utekelezaji wa shughuli nyingi umekwama kwa sababu ya upelekwaji au kutokupelekwa kwa pesa kwenye maeneo husika. Nimwombe sana ndugu yangu Waziri wa Fedha kwa sababu tunataka tutekeleze yale ambayo tunataka yatekelezwe lakini mengine yanashindwa kufanyika kwa sababu hakuna pesa, yale maeneo ambayo yanakulenga wewe moja kwa moja kuhusu upelekwaji wa pesa basi pesa hizo zipelekwe ili kusudi zikatekeleze haya maazimio au mapendekezo ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa sababu mimi ni *senior senator* si jambo jema kupigiwa kengele ya pili. Nakushukuru lakini kama nilivyoomba tafadhali mapendekezo haya Serikali iwe na utaratibu wa kutupa mrejesho ili tuweze kujua kwamba limetekelezwa kwa kiasi gani. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dokta Ishengoma, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kufuatana na takwimu ni asilimia 75 ya wananchi wanategemea kilimo na kilimo chetu kinachangia asilimia mia moja ya chakula. Mwaka 2016/2017, sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 1.7 na katika kipindi cha nusu mwaka yaani Desemba kilimo

kimekua kwa asilimia 3.1. Ukuaji huu wa kilimo hauridhishi, inabidi Wizara na Serikali ifanye jitihada za kuwezesha kilimo kukua na kuweza kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na kilimo chenye tija ni bora kutumia kanuni bora za kilimo na kanuni bora za kilimo ni pamoja na kutumia pembejeo za mbolea, mbegu na kadhalika. Imekuwepo tabia ya wakulima kutotumia mbolea ya kutosha na mojawapo ya sababu ni bei kuwa ghali. Kwa mfano, hapa Tanzania wakulima wengi wanatumia mbolea kilogramu 10 kwa hekta ambapo kilogramu zinavyoshauriwa ni 90 kwa hekta. Kwa hiyo, nashauri hili jambo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuja na huu mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja. Hata hivyo, naishauri Serikali iufuatilie mfumo huu kwa karibu kwa sababu umeanza kuwa na changamoto yake kwani viashiria vimeanza kuonekana. Kwa mfano, kuna maeneo katika Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi mbolea hii haikufika kwa wakati. *DIP* ni mbolea ya kupandia na *urea* ni mbolea ya kukuzia sasa unapeleka *DIP* wakati mazao yameshakuwa haiwezekani kwa sababu *DIP* ni mbolea ya kupandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali na Wizara kupeleka mbolea hii kwa wakati muafaka. Tulipopitisha kwenye Bunge lako hili Tukufu kuwa tuweze kununua mbolea kwa pamoja tulisema ni ili tuweze kupata mbolea kwa wingi na kila mdau aweze kupata mbolea ambayo anaitaka baada ya kufuta ile mfumo wa kutumia ruzuku ambapo ilikuwa inatoa mianya ya rushwa. Naomba Wizara ijitahidi ili kila mdau wa kilimo aweze kuipata kwa wakati na bei elekezi iweze kutumika kwa sababu mahali pengine mpaka sasa hivi hiyo bei elekezi haifuatwi bado bei iko juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee upande wa maji vijijini na mijini. Bado tuna tatizo kubwa kwenye maji mijini pamoja na vijijini, ni asilimia 56 vijijini na asilimia 69

mjini. Kwa hiyo, nashauri kwa upande wa maji Serikali yetu iweze kutilia mkazo kuona ni namna gani tunaweza kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana, lakini mpaka sasa hivi ni asilimia 1.6 tu ndiyo tunalima kwa umwagiliaji. Kwa namna hii hatuwezi kufika mbali kwa kilimo cha umwagiliaji na hatuwezi kusema kuwa tutakuwa na usalama wa chakula kama hatutatilia maanani kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasisitiza Serikali iweze kutoa hela za kutosha kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kuna mabwawa, kwa mfano, Bwawa la Kidunda, usanifu wake ulifanyika tangu 2004 lakini pia kuna mabwawa mengi ya umwagiliaji ambayo mpaka sasa hivi hayajakamilika. Nashauri Serikali pamoja na Wizara tuweze kuona jinsi ya kukamilisha mabwawa haya kusudi tuweze kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedheha ambayo imetokea kweli kwenye upande wa korosho. Naomba Wizara iweze kuangalia hiki kitu kichotokea cha korosho zetu kukutwa na mawe na kokoto huko Vietnam. Kwa hiyo, naomba nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye wadudu waharibifu wa mazao kwenye Mikoa yetu hata Morogoro tuna tatizo la viwavijeshi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha, mengine unaweza ukayaandika na ukampa Mwenyekiti wako.

Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma, ajiandae Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nitazungumzia kidogo suala la uvuvi. Wabunge wengi tuliomo humu kila mmoja ana neema ambayo Mwenyezi Mungu amempa na kila mtu ana kitu ambacho wananchi wake wanakitegemea. Jimbo la Geita Vijijini sisi dhahabu yetu kubwa ni uvuvi lakini toka nimezaliwa sijawahi kuona hizi sheria zinazotumiwa na Mheshimiwa Mpina. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wangu huu nimeshuhudia Mawaziri awamu zote, nafikiria sasa ndiyo tunaanza kutunga sheria au hii sheria ilikuwa imefichwa sasa ndiyo imeibuka. Nataka kutoa rai kwa Mawaziri kwamba Mawaziri wa dizaini kama hizi nawashauri sana mpunguze mihemuko kwa sababu hata sisi tunatamani kuendelea kuwa Wabunge humu ndani, lakini kwa dizaini mnazoenda mtuambie mmewapanga kina nani mnaotaka wakae Wabunge kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa Wabunge wanaotoka Kanda ya Ziwa; Mheshimiwa Lwakatale, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Tibaijuka, Mheshimiwa Kalemani, Mheshimiwa Lolesia, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Mabula wa Mjini, Mheshimiwa Mabula wa Ilemela, wa Magu, tunaenda kwa Mheshimiwa Bulaya, unaenda kwa Mheshimiwa Airo Musoma, sidhani kama sisi tutarudi humu Bungeni. Sijawahi kuona Waziri anasimama anasema mimi kwetu hakuna samaki natamani wote tusile samaki, Mungu ametupa neema tofauti. Sijawahi kuona unaenda unakamata mitego dakika 10 unaomba faini mtu hana unachoma, hujahakikisha ni ile feki unayoitafuta au *original*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Jimboni kwetu na huko kwenye Majimbo ya Kanda ya Ziwa debe la dagaa linauzwa Sh.50,000 yaani maana yake hata dagaa haturuhusiwi kula. Ukisikiliza madaktari wanatuambia tukila dagaa tunaongeza madini joto, akija Mpina anasema ni haramu, tufuate la nani? Namwomba Waziri Mpina atakapokuja hapa atuambie ni sheria zipi anazozitumia kama

siyo mihemuko. Kwa sababu hata Mheshimiwa Rais aliyepo sasa hivi Magufuli alikuwa Waziri aliunda *BMU* watu wakawa wanafundishwa na uvuvi haramu ukaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kwenye maeneo yetu hakuna samaki inayotakiwa kuliwa. Nina mfano halali, mimi nafanya biashara ya mabasi, basi yangu imesimamishwa na watu wa Maliasili wakaingia ndani kukagua wakakuta mtu ana samaki za kukaanga tatu naombwa kutoa Sh.10,000,000 na nimempigia simu Mpina anasema watu wangu wanasema sijui wamefanya nini, nikawaambia chukueni gari mkauze. Hivi inawezekana vipi watu wa mabasi anakaa *ruler* yake kupima samaki kwamba hii samaki inatafutwa na Mpina, kwa nini usiweke polisi stendi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mpina pamoja na apizo alilolifanya kwamba asipomaliza uvuvi haramu atajiuzuru, mimi nakwambia...

**TAARIFA**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Musukuma kwamba anachokifanya Waziri wa Mifugo na Uvuvi ni kutekeleza kauli ya Hapa Kazi Tu. (Kicheko)**[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hivi vitu vingine wala havihitaji kutoa taarifa na kupotosha Bunge, haya maneno nimeyafuta na wala hayatatokea katika *Hansard*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimimiwa Musukuma, endelea na mchango wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Anataka kukaa kwenye *Youtube* kwamba alimpa taarifa Musukuma. Tunajua Jimboni kwako unazomewa, kwa hiyo, unatafuta *kick* unatetea wanyonge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninachoomba Waziri Mpina pamoja na timu yake wajipange kuwafundisha wavuvi wetu kule siyo kuwafilisi. Nataka nitoe ushahidi mdogo tu kwamba Waziri Mpina wameenda kisiwa kimoja kule Izuma Cheli Jimboni kwangu wakakuta watu wameunda *SACCOs* wamekopa wanadaiwa shilingi bilioni 1.4, mitego ndiyo wameishusha usiku huohuo asubuhi imekamatwa hata kuombwa risiti wamenunua wapi ili wakapambane nao na siyo haramu imechomwa moto kwa kukosa rushwa ya shilingi milioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Waziri na wengine wanaosikiliza kwamba nashauri sana zoezi analoliendesha Waziri Mpina lazima liundiwe Tume iende ikachunguze na tuone hizo hela watu wetu walizotoa kama zimetolewa risiti za Serikali. Tuna ushahidi wa watu waliofanyiwa uhuni kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yanauma sana, unajua wengine humu ndani hawana hiyo bahati ya kuwa na ziwa, naamini hata Jimbo la Mheshimiwa Waziri wao wanakulaga panki zikikatwa kule kwetu wao wanapelekewa mapanki. Sasa asitake kutufananisha yaani sisi tufe njaa na ziwa liko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waje na shule maalum itakayotufundisha, hata sisi hatupendi uvuvi haramu lakini siyo kuzuia kila kitu. Kwa sababu kwanza kule ziwani hata ukizuia tusivue sisi Watanzania hakuna *barrier* samaki wataenda Kisumu, samaki wataenda Uganda na ndiyo kinachofanyika. Rais Magufuli anasema tufanye kazi, tukuze uchumi wetu, mwingine anaenda kusema choma kila kitu, wavuvi wote wa Kanda ya Ziwa wamehamia Uganda na Kenya sasa nani anapata faida? Nyie ziwa lenu mmekuwa

mnatunisha samaki wakikua wanatembea wanaenda Kisumu tunavua tunauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri sana Mheshimiwa Mpina utakapokuja kujibu hapa na hata ukichomoa hapa kwenye bajeti tutakutana lazima utueleze ili hii operesheni ya uonevu inayoendelea ikome. (*Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tuendelee na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa sababu ya muda itabidi niende haraka haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono taarifa ya Kamati zote mbili kwa asilimia mia moja. Pili, suala hili amelizungumza mwanangu Ndassa lakini kalizungumza kwa Kisukuma sikulielewa vizuri. Tunachokitaka maazimio tuyayoyapitisha katika Bunge hili yaundiwe Kamati ambayo itayasimamia. Kwa sababu hivi sasa tunapitisha tukiondoka hapa yamepita, tukirudi tena hakuna aliyenayo, hayasimamiwi, hatujui Serikali imetekeleza lipi na imeacha lipi. Kenya wana mfumo huu, kwa hiyo, iundwe Kamati ya Bunge ambayo itakuwa inasimamia maamuzi na maazimio yanayopitishwa na Bunge, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme tu mimi sijui tuna laana gani sisi Watanzania na miaka 60 ya Uhuru sasa tunayokwenda nayo bado tuna matatizo ambayo sisi wenyewe tunajitakia. Wizara ya Ardhi sasa hivi na hii Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Maji tutaendelea kuzilaumu kila siku kama hatuzipatii fedha zikafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anafanya kazi vizuri, lakini anakwama kwa sababu ya fedha. Sasa atalaumiwa kila siku, watu

watapigana, watauana kwa sababu anashindwa kupima ardhi kwa sababu ya fedha, apewe fedha afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara hii ya Kilimo ya Mpina kama hawajapewa fedha hawa za kutosha hatuwezi. Kama hatujapanga leo maana niseme sijui tuna laana gani Libya walikuwa wanachukua maji kutoka Mto Nile ambao umeanzia kwetu wanajitosheleza kwa chakula na matunda yote siye Tanzania tuna mito na maziwa mangapi hapa tunashindwa, tupange fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabia nchi yanayojitokeza katika nchi yetu, mwaka huu mahindi hayana bei, mbaazi hazina bei, tumbaku haina bei na vitu vingi tu. Mwakani hapa mabadiliko ya tabia nchi tutakuwa na dhiki ya chakula kama wangepewa fedha hawa wakanunua hivi vyakula wakaweka katika Hifadhi ya Taifa vingetufaa mwakani kukitokea tatizo, hakuna, fedha tunakusanya hatujui. Kwa hiyo, hebu tukaeni chini sasa kama Watanzania jamani tunataka nini, tujipange miaka 60 inatosha si watoto tena katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni misitu. Naomba Serikali misitu yote nchini isimamiwe na taasisi au mamlaka moja, halafu hiyo mingine iendelee tu, ile ya kijiji ibaki kuwa ya kijiji, ya Halmashauri ibaki kuwa ya Halmashauri lakini kuwe na msimamizi mmoja ili zile sheria zinazohusiana na masuala haya ya misitu zisimamiwe. Tanzania nadhani tunapoteza hekta laki tatu na nusu kila mwaka kwa matumizi tofauti lakini upandaji wetu sidhani kama tunafika hata hekta laki moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukichukulia hilo na hiyo miti ambayo ni *fast growing trees* ukiipanda inaweza ikachukua zaidi ya miaka sita ndiyo unaanza kuvuna, nchi yetu baada ya miaka 20 ijayo tutakuwa katika hali gani? Sasa kama sisi tunavimba kichwa kusema kwamba tuna asilimia 35, sijui 52 ya misitu katika nchi yetu lakini na matumizi ni makubwa, ongezeko kubwa la watu mahitaji ni makubwa.

Kwa hiyo, ni lazima matumizi yetu yaendane na upandaji wetu na tuone kwamba mti tukiupanda leo hatuvuni leo rahisi kabisa ni baada ya miezi sita, kwa hiyo, lazima tuwe makini katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala lingine, Mheshimiwa Musukuma kamzungumzia sana Waziri Mpina, mimi nampa tena ushauri Mheshimiwa Waziri wa Maliasili. Mheshimiwa Waziri nilikupa ushauri ndani ya Kamati, nakupa ushauri leo ndani ya Bunge. Nikwambie Wizara hii ya Maliasili na Utalii ni yai viza. Yai viza lina matumizi mazuri sana kwa wanaolitumia lakini yai viza ukilikosea linanuka vibaya sana. Nikushauri tu Mheshimiwa Waziri uwe mtulivu, hii Wizara haitaki amri, haitaki nguvu, haitaki ubabe na haitaki hasira, hii Wizara ni lazima utulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nawashauri humu ndani kwamba ndani ya Wizara hii lazima mkae mafiga matatu. *Community* iseme inataka nini, Serikali iseme inataka nini, mwekezaji aseme anataka nini, nyote watatu mkae mseme mnataka nini ili mwende kwa pamoja. Sasa ukichukulia nguvu ukasema leo kwamba kwa mfano tu, nafunga vitalu vya uwindaji, kesho unasema nawaachia mwaka mmoja, kesho kutwa nawaachia miaka miwili, hii biashara ni nyepesi sana kuharibika na ndiyo nikasema ni yai viza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima utulie vizuri sana na hizi *figure* tatu, hii *triangle* zikae kuweka mkakati wa tunakwenda vipi vinginevyo utakuwa ni Waziri ambaye umetumikia Wizara hii muda mfupi sana. Kwa sababu imebeba uchumi wa Taifa letu, ukikoroga kidogo tu katika sekta hii unakoroga *system* nzima ya utalii na ukikoroga *system* nzima ya utalii umekoroga uchumi wa nchi yetu ambao asilimia sasa hivi zaidi ya 20 inatokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikushauri ukae vizuri, uwe makini, tupo ambao tumeshafanya kazi katika sekta hii, tupo ambao tumesoma, tutakushauri vizuri kwa

nia safi kabisa ili twende mbele. Suala hili la kutumia nguvu ukaona labda ni sifa unapotumia nguvu si sifa unajiharibia na ukijiharibia wewe, unaliharibia Bunge, unaiharibia Serikali na unaiharibia nchi yote ya Tanzania. Kwa hiyo, nakushauri tu kwamba utulie vizuri sana sisi tutakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine la wawekezaji. Mtu ameshapewa vibali vyote vya kujenga lakini kuna tatizo la hii *Environmental Impact Assessment* inachelewa, mwekezaji anakaa miaka miwili, mitatu hajapewa hiyo, sasa atajenga lini huyu? Kwa hiyo, hili benchi la kutoa vibali vya ujenzi bora lote likae pamoja ili mwekezaji akipata kitu apewe kwa pamoja anaenda kuwekeza tujue kwamba mwekezaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sekunde mbili malizia.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji akishawekeza labda kwa miaka mitatu amejenga anahitaji tena miaka miwili kufanya *marketing* kupata wageni hapa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itulie vizuri, ijipange, muda unatosha, tuko tayari kuishauri vizuri Serikali kwa minajili ya faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Awamu yetu ya mchana inakwisha sasa hivi na jioni tutakuwa na Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Sebastian Kapufi, tutaporudi saa kumi na moja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na uchangiaji na tunaanza na Mheshimiwa Almas Maige, ajiandae Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya Kamati ya Kudumu za Bunge na hasa Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji. Maji limekuwa tatizo kubwa sana katika maeneo yetu hasa Majimbo ya vijijini kuliko mijini ambako maji hayapatikani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nianze kuishukuru Serikali kwa kubuni Mradi huu wa Ziwa Victoria ambao unakuja kuleta maji katika Jimbo langu la Uyui-Tabora Kaskazini na Tabora Mjini. Ukitoa mradi huu pekee, Jimbo langu la Tabora Kaskazini hakuna maji chini, yako katika maeneo machache tu na ningeomba Serikali itumie uonekanaji wa vyanzo hivi vya maji kuwagawia maji wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwa tatizo kubwa sana wakati Wizara ya Maji inazo fedha na Halmashauri kupitia Wizara ya TAMISEMI ndiyo nao wanatafuta wakandarasi au wazabuni wa kuchimba maji. Tunaye Wakala wa Maji kama alivyo Wakala wa *TBA* huyu ni *DDCA.* Hawa ni wataalam wazuri sana na wana bei chini kabisa lakini Halmashauri nyingi ikiwemo ya kwangu hawawatumii watu hawa, hawatumii wakala huu wa Serikali ambao wangeweza kuchimba maji kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mifano miwili. Hivi karibuni wananchi wa Kata ya Ikongolo ambayo ina vijiji vinne vya Majengo, Kanyenye, Ikongolo yenyewe na Kiwembe walitafuta eneo ambalo kiangazi chote wanateka maji pale kama chanzo kikubwa cha maji lakini kukawa na kutoelewana na Halmashauri kwamba watafute mzabuni apime maji pale ikashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge nalijitolea kutafuta hawa watalaam wa *DDCA* wakaenda wakathibitisha maji yako pale na vilevile wakatoa na ankara za uchimbaji wa visima vitatu. Bahati mbaya sana mwaka huu wa 2016 wakasema Halmashauri haina fedha, lakini baadaye ilipopatikana fedha kwa kutumia nafasi hiyo wakatangaza zabuni wakati mkandarasi *DDCA* ameshapeleka bei ya shilingi milioni 15 kwa kisima. Wakatangaza zabuni na wakachimba visima kwingine kabisa kwa bei ya milioni 27 karibu milioni 30 kwa kisima karibu mara mbili ya bei ambayo *DDCA* alisema, sasa mimi naona hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshamwona Mheshimiwa Waziri wa Maji, nimeshamwona Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na nafikiri kama walivyoniahidi watalifuatilia suala hili. Sioni kama ni halali tunaye Wakala wa Serikali na anaweza kuchimba maji kwa bei nafuu kama ambavyo Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli aliamua kuwapa kazi *TBA* ilitokana na matatizo ya wakandarasi wababaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waheshimiwa Mawaziri wote wawili watakapokuja kufanya majumuisho, waniambie tatizo hili la maji kwa nini hawakutumia *DDCA* wakatafuta wakandarasi wengine ambao watachimba kisima kimoja kwa bei ya visima viwili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika vijiji vyote vinne vile kisima kimoja hakitoshi. Kwa hiyo, bado tu wataendelea kuchimba kisima cha pili au cha tatu au vinne kwenye vijiji vyote vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kilimo. Kila mtu akisimama humu ndani anajua kwamba asilimia 75 mpaka 80 ya wananchi wanakaa vijijini na kilimo ndiyo msingi wa maisha kule na ndiyo wanaolima tunakula sisi tunaokaa mijini. Hata hivyo, kilimo hakipewi thamani kama vile ambavyo afya ikikosekana mahali tunapiga kelele wote, maji yakikosekana mahali tunapiga kelele wote, usafiri

ukikosekana mahali tunapiga kelele wote, hawa watu asilimia 75 hatupigi kelele sana na kuwasaidia wakulima wetu hawa ili Maafisa Ugani wafanye kazi sawasawa na Madaktari wanaotoka kwenye sekta ya afya au wanaofanya kazi kwenye sekta ya barabara yaani sekta hii ya kilimo haiangaliwi na matokeo yake haikui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kauli mbili leo asubuhi hapa, kuna kauli iliyosema sekta inakua kwa asilimia 1.2 nafikiri mwaka jana, mwaka huu sekta ya kilimo ambayo ndiyo sekta muhimu sana kinakua kwa asilimia tano, haisadiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kilimo kimekuwa cha kizamani. Siku za nyuma kulikuwa na vituo vya kufundishia mifugo kufanya kazi ya wanyamakazi, lakini vimetelekezwa. Pale kwangu Upuge kuna kituo kizuri sana alifungua Marehemu Mwalimu Nyerere kimetelekezwa na nimekuwa napiga kelele humu ndani kwa sababu mashine nyingine bado nzima zingeweza kusaidia kufufua utengenezaji wa mikokoteni au vifaa vya kilimo na ufundishaji wa maksai ili kilimo kiwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mazao ya biashara. Tumbaku imekuwa *issue* pale kwetu, sasa hivi kuna mpango wa korosho na sasa hivi korosho imetuaibisha huko nje, watu wasiojulikana wamepakia nusu ya gunia vitu vingine siyo korosho na nusu korosho. Mambo haya yametutia aibu kwenye soko ambalo tulilipata huko Vietnam lakini pia hapa waliopakia mizigo ile wamechukuliwa hatua gani? Serikali lazima ijisafishe iseme kwamba tatizo hilo ni watu wachache siyo Serikali nzima, siyo Tanzania yote tumefanya kosa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata soko ni kazi kweli kweli lakini siyo kazi kama kulitunza. Sasa kama kuna watu walifanya hivyo miaka iliyopita kwenye pamba, pamba ilituharibikia kweli kweli mikononi mwetu, soko la pamba lilipotea kabisa lakini baadaye limerudi na kwa vile limerudi kwa matatizo makubwa namna hii sasa litunzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani ni muhimu sana wasimamie pamba itoke safi, zamani sisi kule Usukumani na Unyamwezini pamba tuliita dhahabu nyeupe lakini baadaye ikawa takataka, ikatuangukia mikononi. Tunaomba sana sana Serikali itakapokuja hapa ituambie mikakati ya kutunza pamba itoke safi na mikakati ya kutunza korosho zitoke safi ili masoko tuliyoyapata tuweze kuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kupigiwa kengele mara mbili, naomba niseme hayo ndiyo nilitaka kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oran ajiandae Mheshimiwa Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kipekee nami niweze kuchangia hizi Kamati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuzipongeza Kamati zote mbili zimeleta ripoti zao nzuri na mapendekezo mazuri sana ambayo nina imani kama yakifanyiwa kazi na Serikali tunaweza kwenda kwenye hatua nyingine ambayo ni nzuri zaidi kimkakati kwenye mambo ya kilimo na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoeleza taarifa ya Kamati ya Kilimo nafikiri na jinsi walivyoongelea wenzangu, tuna changamoto kubwa sana kwenye sekta hii ya kilimo hasa ukizingatia kuwa kilimo ndiyo sehemu kubwa inayoajiri Watanzania zaidi ya asilimia 75, lakini kwa kiasi kikubwa hatuoni mikakati madhubuti kabisa inayochukuliwa ukilinganisha na umuhimu wa sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo kule kwangu katika Halmashari ya Mbeya tunalima pareto na zao hili lina umuhimu wa kipekee sana duniani. Halmashauri yetu tunaongoza kwa kilimo cha pareto Tanzania. Bahari nzuri kwa pareto ile inayolimwa kule vilevile inaongoza kwa

uzalishaji kwa Bara zima la Afrika. Pareto inayolimwa kwenye Halmashauri ya Mbeya na sisi ni namba mbili katika uzalishaji wa pareto duniani, lakini huwezi kuona mahali popote katika makaratasi ambapo limeupa umuhimu wa kipekee hili zao la pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri pamoja na Naibu Waziri wamechukua hatua ambazo kidogo zinaanza kuonesha mwanga wa kwamba labda hili zao nalo linaweza kuwaletea manufaa Watanzania. Kwa kipekee kabisa Naibu Waziri alitembelea Jimbo langu, akakutana na wakulima, akaona wakulima wanavyopata tabu ya soko la pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la pareto hii ni *monopoly.* Tuna mnunuzi mmoja tu anayenunua zao hili na kwa bahati mbaya mnunuzi huyu katika mnyororo wa zao la pareto yeye ana-*control* kutoka kwa mkulima, uzalishaji na mpaka soko la dunia kwa vile kwenye soko la dunia nako amelikamata yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida tunayoipata ni kwamba yeye sasa ndiyo atampangia mkulima bei na kwa bahati mbaya hana huruma na mkulima na Tanzania. Kwa bei ya mkulima ni Sh.2,300 kwa kilo lakini kwa bei ya pareto hiyo hiyo ni Sh.8,000 kwa kilo anayouzia yeye sasa angalia hiyo *spread*, angalia ni kiasi gani katika dunia ya leo mkulima ananyonywa kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo la langu, Kamati iongeze katika taarifa yake mapendekezo kuwa Serikali iweke mkakati wa kipekee kuangalia ni namna gani zao hili la pareto litakuwa na manufaa kwa wananchi. Vilevile huu uzalishaji wa pareto badala ya hii kampuni kupeleka *crude extract* na *powder* ya pareto waweze kutengeneza *finished product* ambazo zinaweza kuuzwa na zikapata jina ya kwamba hii pareto inatoka Tanzania. Tumenyonywa kwa kiasi kikubwa nafikiri hii itaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia Tanzania ya viwanda, nafikiri Serikali iweke mkakati namna gani tuwe na viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuchakata hayo mazao ikiwemo pareto. Kiwanda cha Pareto kinahitaji mtaji wa dola laki moja na nusu tu ambazo ni karibu milioni 300. Nafikiri hizi kwa kiasi kikubwa kama kweli tuna nia nzuri ya kukiendeleza kilimo, tunaweza tukaanzia kwenye pareto tukawa na viwanda vingi na tukawasaidia wakulima waweze kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachilia mbali pareto, kwa kiasi kikubwa mwaka huu tumepata matatizo sana kwenye mazao na hasa zao la mahindi. Serikali ilikuwa imepiga marufuku kupeleka mahindi nje ya nchi. Matokeo yake leo hii mahindi kwenye soko letu la Mbeya yameteremka bei kutoka Sh.12,000 mpaka Sh.5,000 kwa debe, leo hii linauzwa kwa Sh.3,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fikiria mkulima amepata hasara ya namna gani na hata hii Sh.3,800 huwezi kupata mnunuzi. Masoko ya huko nje tuliyozuia wenzetu wame-*take advantage* wamepeleka mahindi kutoka Zambia, Malawi na South Africa yamejaa kwenye yale masoko tuliyokuwa tunapaleka sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tujaribu kujitathmini na kuangalia kama hizi taarifa tunazozipata kwa wataalam wetu zinatusaidia katika ku-*make decision.* Nafikiri tunawaumiza wakulima na tukiumiza wakulima kwa kiasi kikubwa tunawaumiza Watanzania walio wengi ambao wanategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa pendekezo langu na kuiunga mkono taarifa ya Kamati ya Maji kuwa Serikali iweke mkazo tuanzishe Wakala wa Maji Vijijini kwa sababu kwenye Halmashauri zetu tuna tatizo kubwa, hatuna wataalam wa maji, tuna mainjinia na kadhalika lakini uwezo wao wa kusimamia miradi hii

mkubwa ya maji ni mdogo sana. Ni afadhali tuweke chombo cha wataalam kusaidia kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mbeya tuna maji mengi sana lakini toka 2013 hakuna mradi hata mmoja wa maji uliokamilika licha ya bajeti kubwa ya Serikali tuliyoletewa. Nina imani kuwa Wakala wa Maji atutasaidia kama tulivyoona kwenye *REA* na barabara. Kwa hiyo, naungana na Kamati wahakikishe kuwa hiki chombo kinaanzishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kapufi ajiandae Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nipongeze Kamati zote mbili lakini nitajikita kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na naomna nianze na suala la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuihuisha Sheria ile ya mwanzo ya mwaka 1959, *Ordinance* Na. 413 ya mwaka 1959, nasema imepitwa na wakati kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, tukumbuke kipindi kile cha mwanzo wenyeji katika eneo hilo walikuwa ni 8,000 lakini kwa sensa ya hivi karibuni wenyeji wamefikia 93,851. Kama haitoshi, kiwango cha kutojua kusoma ni zaidi ya asilimia 70 kwa maana ya takwimu za mwaka jana. Pale ndani kuna shule 21 za msingi na mbili za *high school,* hiki ni kigezo cha kuonyesha kwamba watu hawa wanakuwa masikini. Pamoja na kiwango hicho cha elimu kule ndani magonjwa yameongezeka na kuna ukame na kwa sababu hiyo naendelea kujenga hoja ya kwamba hii sheria imepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, naomba nije kwenye suala zima la utalii. Kumuunga mkono Rais wetu ni kwa maana ya kuunganisha mawazo ya kuiletea nchi mapato, napenda kusema kwamba eneo hili la utalii ni *sensitive,* nikimuongelea mtalii kwa ujumla wake maana yeye anaweza asije Tanzania akaenda sehemu nyingine yoyote. Ndiyo maana eneo hili la utalii kwa lugha ya kigeni wanaita ni *hospitality industry.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunatakiwa kuwa watu rahimu, tukicheza watalii hawa wanayo nafasi ya kwenda maeneo mengine, mbuga ziko maeneo mengine. Kwa hiyo, naomba sana na katika hili niendelee kumshauri Waziri husika tunatakiwa kuwa watulivu kwa maana hatuko peke yetu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo, niende kwenye eneo la matangazo kwa maana ya *TANAPA* na *TTB.* Ndiyo maana kwa mfano wenzetu wa *Coca Cola* sehemu nyingine kubwa wameingiza fedha kwa maana ya matangazo. Nami niombe, kazi nzuri ambayo imeendelea kufanywa kwa maana ya matangazo waiendeleze ndugu zetu wa *TANAPA* na *TTB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaunga mkono, najua mara ya mwisho kulikuwa na kitu kinaitwa *SITE (Swahili International Tourism Expo)* waliifanya mwaka jana na ilikuwa nzuri kwa sababu imeendelea kuwaita *tour operators* kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la matangazo naendelea kuisihi Serikali yangu, inatia huruma kuona kwa mfano, majirani wana-*take advantage* ya vyanzo tulivyonavyo. Mtu aseme njoo sehemu fulani utauona Mlima Kenya, kwa nini na sisi Watanzania tusiendelee kuchangamkia fursa hii, kama vyanzo ni vya kwetu kwa nini watu wengine watumie nafasi ya vyanzo vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo la wazawa waendelee kusaidiwa kwa maana ya biashara nzima ya utalii na uwindaji lakini naomba kuboresha najua ukanda wa Kaskazini tunaendelealea kuboresha maeneo hayo lakini watalii kwa ujumla wake kulikoni tukawapoteza tuendelee kuwafanya waje nchini kwa kuboresha na kanda nyingine kama Kanda ya Magharibi na Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo ukisema Kanda ya Magharibi, Mbuga kama ya Katavi tunayo nafasi ya kutoka Ruanga na Burundi wakipita Kigoma, wakaja kushangaa mbuga yetu nzuri ya pale Katavi. Kwa hiyo, naomba ukanda huo uendelee kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijikite tu kwa maana ya suala la mbuga hizi, tufungue vyanzo vingine kama fukwe, masuala ya utamaduni na mapango. Tulikwenda kuyaona mapango ya Amboni pale Tanga. Watanzania kwa ujumla wake tuna vyanzo vingi ni suala tu la kupanga tunaanza na nini tunamaliza na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Olduvai, naomba suala la maabara pamoja na maktaba ziendelee kufanywa za kisasa ili wanafunzi wetu waendelee kwenda pale kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa, eneo la Saadani. Hii Mbuga ya Saadani kwanza wanasema unakwenda katika eneo ambalo nyika zinakutana na fukwe. Kwa hiyo, ina sura ya pekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mgogoro wa kijiji kimoja kilichopo pale, naomba Serikali ifanyie kazi ili ile Mbuga ya Saadani iendelee kutoa mafao makubwa kwa maslahi mapana ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa maana ya Sera ya Taifa ya Misitu, naomba tuendelee kuiboresha hiyo kwa sababu pasipo kuwepo na misitu hata huu utalii wote tunaouzungumzia haupo. Vilevile pasipokuwa na misitu hata

masuala mengine mipango mingine tunayoikusudia kuifanya kama ya umwagiliaji na mambo mengine itakuwa ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mch. Msigwa na Mheshimiwa Sonia Juma Magogo wajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nawashukuru Wenyeviti wote wa Kamati waliowasilisha, lakini na mimi najikita zaidi kwenye Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi wengine tuliotoka Bunge liliopita na wakati ule Bunge la Tisa tulipokuwa tukiangalia kwenye *television,* Bunge kama hili lilikuwa Bunge lenye uhai, Bunge ambalo Serikali inasikiliza hoja ambazo baada ya Waheshimiwa Wabunge kutembea maeneo mbalimbali wanajaribu kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tofauti sana na Bunge hili ambalo kwa kweli limepooza, unakuta hata Kiongozi Mkuu wa Serikali hayupo hapa, Wabunge wanajaribu kutoa maoni yao na kuishauri Serikali, Mawaziri wanachelewa kama hivi Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ni hoja yake hapa, ndio anafika saa hizi. Kwa hiyo, hizi ni hoja ambazo tunakiwa tujitathmini kama kweli Bunge tunatimiza majukumu yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa

Mheshimiwa Msigwa kwamba Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Bunge siyo kwamba hayupo, anapokuwa hayupo taarifa rasmi inatolewa kwenye Bunge, lakini kwa mujibu wa utaratibu ambao Ofisi ya Kiongozi wa Serikali ndani ya Bunge alionao, akishakuwepo hapa *Chief Whip* na *AG* na Mawaziri, tayari Serikali iko ndani ya Bunge; na siyo laizma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siipokei. Labda ni Awamu ya Tano ndiyo utaratibu wake. Nimezungumza Bunge la nyakati za nyuma, Spika akiwa Marehemu Mheshimiwa Sitta au Mheshimiwa Anna Makinda, tulikuwa tunamwona Waziri Mkuu anakuwa hapa, tunampa taarifa jinsi tunavyofanya kazi huko. Utaratibu wa sasa hivi toka Bunge limeanza Waziri Mkuu hayupo, Mawaziri wenyewe wanakuwa hawapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa endelea na hoja iliyoko mbele yako.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ndiyo hiyo, Serikali haitilii maanani hoja ambazo sisi kama Wabunge tunataka kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisumbua ni jinsi ambavyo haya mambo tumekuwa tukitoa ushauri miaka nenda rudi, lakini tunarudia kila mwaka kuyazungumza yale yale. Kamati ya Maliasili katika kitabu chao ukurasa wa 33, wamesema, Kamati ilikutana na Mkutano wa Wadau na Uwindaji wa Kitalii nchini na kupokea malalamiko yao kuhusu hatua ya Waziri ya Maliasili na Utalii kufuta leseni zote za umilikaji vitalu kwa kipindi cha miaka 2018 na 2022. Sitaki niendelee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *industry* hii ya uwindaji kwa muda mrefu, kwa namna moja au nyingine ndiyo imekuwa inaibeba Wizara hii. Mheshimiwa Waziri anapotoa matamko ya mihemko ya haraka haraka anai-*disturb industry. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaposema anafuta hizi leseni, naomba nimshauri, kwa sababu kuna vitalu 61 ambavyo havina watu. Kama angetaka vifanyiwe minada anayoitaka, angeanza na hivyo vitalu ambavyo havina watu mpaka sasa huko maporini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia hii uwekezaji wake ni mkubwa sana. Anataka wakafanyie vitalu ambavyo wawekezaji wameweka pesa nyingi sana katika vile vitalu. Miaka mitatu ilioyopita, miaka mitano watu wamewekeza, wengine wamelea simba, halafu unasema wakafanye minada! Ni kuvuruga hii *industry.* Namshauri Mheshimiwa Waziri, hii tasnia inatakiwa achukue muda kui-*study. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimefanikiwa kwenda katika maeneo mengi ambayo nimeona wame-*invest* hao wawekezaji. Kwa hiyo, tukianza ku-*disturb* kwa mihemko haitatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri hawa Mawaziri vijana, fursa au *opportunity is attracted by talent skill performance and ability. Show your talent and ability, people will love you. Be humble!* Hao Mawaziri wa zamani kwa mfano, akina Lukuvi na Tizeba, tunawaona; wakijibu hoja, wanajibu hoja siyo za kimihemko. Unaridhika hata Mheshimiwa Waziri akikujibu, unapenda. Vijana wengi mnaonekana kama mnataka kufanya Serikali hii kiasi kwamba Serikali inayokuja mtakuwa hamna *use.* Kwa sababu mna mihemko sana. Onesheni *ability* na *performance* mnapofanya kazi zetu ili tuitunze Serikali...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Msigwa taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa rafiki yangu na ndugu yangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, wakati alipokuwa akichangia, natambua ana hasira, ana ghadhabu, lakini

akumbuke kwamba anapowatamka Mawaziri aidha kwa majina ama vyeo vyao, ni muhimu sana akakumbuka kuwaita Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Tizeba na watu wengine na huu ni utaratibu wa kawaida. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S.MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiilaumu Serikali kwamba inaonekana kila mtu anafanya kivyake, hamja-*synchronize.* Wakati natoa hotuba yangu ya mambo ya nchi za nje mwaka 2017 nilizungumza, naomba ninukuu mahali nilisemaje?

Nilisema diplomasia ya uchumi pamoja na mambo mengine inahusu kuvutia fursa za wawekezaji wa kigeni *(foreign investment),* utalii *(tourism)* na biashara huria *(free trade)* kwa kufanya ushawishi wenye kufungua masoko mapya ya kuuza bidhaa za Kitanzania kupunguza au kuondoa masharti ya kodi na kusaidia wafanyabiashara na wawekezaji wa Kitanzania kuzitumia kikamilifu fursa za kiuchumi zinazopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tasnia; utalii huu umejengwa kwa muda mrefu sana. Akitokea mtu mmoja anaamua kufanya tu kwa kutaka *cheap popularity* atauvuruga kwa muda mfupi sana. Utalii unaingiza *GDP* kwa asilimia 20 na *forex* kubwa inatokana na utalii. Kwa hiyo, hicho siyo kitu kimoja ambacho mtu anaweza akaamka leo akasema nimeharibu. Hii diplomasia ya kiuchumi inategemea sana na kutabirika. Wawekezaji wanataka waone kwamba kunatabirika, tukienda tutafanya biashara zetu. Haiwezekani huyu Waziri, huyu huyu Waziri anatoa amri mpaka na mapolisi wanamkataa, anashindwa hata kuwasiliana na Waziri wake wa Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu huyu Waziri anatoa amri, anapingana na Waziri wa Ardhi, huyo huyo mmoja! Huyu huyu Waziri anapingana na Waziri wa Uvuvi, huyu huyu Waziri mmoja. Hatuwezi kuwa na Mawaziri ambao wanafanya kazi kwa mizuka. Lazima wote kama

tunaliopenda Taifa letu tufanye kazi kwa kupendana na kuheshimiana katika mipaka. Ndiyo maana nimesema, kama Serikali hamja-*synchronize* kwamba vipaumbele vya nchi hii ni vipi? Kama vipaumbele hivi, tunataka tutekeleze diplomasia ya uchumi, maliasili ina-*fit* wapi? *Foreign* wako wapi? Uvuvi wako wapi? Tunataka tuuze wapi? Sasa kila mtu akiamka asubuhi ana mzuka wake, mara amebebe waandishi wa habari aondoke na makamera, akaseme anayoyataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema Waziri Mkuu anatakiwa awe hapa. Waziri wa Maliasili ndivyo tunavyomwona sisi kama Wabunge. Anai-*disturb industry. Full time* yuko kwenye *twitter,* kila wakati, utadhania Trump! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo nilisema ambayo nasema kama Serikali hamja-*synchronize,* nilisema Tanzania haina ajenda ya Taifa juu ya diplomasia ya uchumi wala mipango mikakati inayopimika *(strategic plans)* ambayo inabeba vipaumbele mahususi yaani *specific priority.* Tungekuwa na vipaumbele na mipango, maana yake tunge-*synchronize*. Waziri wa Maliasili anapoona mambo yake ya kiuchumi kuhusu wawekezaji lazima ashirikiane na Waziri wa Ardhi, atashirikiana na Waziri wa Kilimo, atashirikiana na Waziri wa Mifugo, lakini Waziri amekuwa na mihemko, anafanya mambo yake peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe ndugu zangu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dakika zako zimekwisha. Mheshimiwa Sonia.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza kabisa nianze kwa kuzipongeza Kamati zote kwa uwasilishaji mzuri. Pili, ningependa pia kuipongeza

Kamati ya Maliasili ambayo imeona umuhimu wa mapango ya Amboni na kuishauri Serikali kuyafanyia ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Tanga una vivutio vingi sana ambavyo vilikuwa vinausaidia mkoa wetu kuinuka zaidi kiuchumi, lakini kwa sasa vivutio hivyo vimekuwa kama vimetelekezwa. Hivyo, ninaishauri Serikali kupitia upya vivutio hivi na kuona inafanya nini ili kurudisha ile hadhi ya Mkoa wetu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine napenda kuchangia kuhusu migogoro ya ardhi. Hapa katika migogoro ya ardhi, ukiangalia sana chimbuko linakuwa ni Serikali ambazo ziko kule vijijini hasa viongozi wa Serikali za Vijiji. Viongozi hawa wamekuwa wakiuza ardhi za wananchi bila kuwashirikisha na kusababisha migogoro mikubwa sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakikosa ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji, hivyo kupeleka wenyewe kwa wenyewe kugombana na kusababisha uhasama mkubwa baina ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie na kudhibiti hivi vyanzo vya migogoro ya ardhi hasa kwa hawa Wenyeviti wa Serikali kwa kuwachukulia hatua ambazo zitasababisha waache hii tabia ya kuuza ardhi na kusababisha wananchi kushindwa kuendeleza kilimo chao ambacho ndiyo sehemu kubwa ya utegemezi ya kukuza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine na mimi naomba kuchangia kuhusu maji. Wewe mwenyewe umekuwa shahidi hapa, kila Mbunge anayesimama analia kuhusu maji katika eneo lake. Maji ni kama uti wa mgongo, hakuna shughuli yoyote inayoweza kuendelea bila uwepo wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia viwanda, lazima kuwe na maji, tukizungumzia afya, lazima kuwe na

maji na hata kilimo hakiwezi kuendelea bila uwepo wa maji. Mathalani mkoa wetu wa Tanga una vyanzo vya maji kama Ruvu na Pangani, lakini bado tatizo la maji limekuwa ni kubwa sana. Naishauri Serikali ingalie sehemu zile ambazo zina vyanzo vya maji iweze kuvitumia ili kupunguza haya matatizo ya maji kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna miradi mikubwa ambayo bado Serikali inaitekeleza, nilikuwa naishauri Serikali, wakati inatekeleza miradi hiyo, iangalie njia mbadala za kuwasaidia wananchi kama kuchimba mabwawa na visima ili waweze kujikimu wakati wanasubiri utatuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine niongelee kuhusu kilimo. Kipindi cha nyuma tulikuwa tunaona watu ambao wanajikita kwenye kilimo zaidi ni wazee, lakini kwa sasa tunaona asilimia kubwa ya vijana nao wameamua kuingia kwenye kilimo. Kwa hiyo, naishauri Serikali iwape motisha hawa vijana ili wasirudi nyuma kwa kuwapatia mitaji, kuwasaidia kupata masoko, kuangalia miundombinu, kuwapatia elimu ya nini walime na kwa wakati gani na kutokana na ardhi iliyoko katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile viwanda ni muhimu sana. Kwa mfano, Mkoa wetu wa Tanga, vijana wanalima matunda kwa wingi, lakini yale matunda yamekuwa yakiozea mashambani kwa sababu hakuna viwanda vya kuweza kusindika yale matunda. Iwapo watakuwa na miundombinu mizuri, watapatiwa viwanda vya kuwasaidia kusindika mazao yao, nina imani wale vijana hawatarudi nyuma na tutaondoa Taifa la wazembe na tutakuwa na Taifa la wachapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Serikali iangalie kuhusu suala la pembejeo. Wakulima wawezeshwe kuhusu pembejeo, pia zipatikane kwa wakati ili waweze kuendeleza shughuli zao za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zinapotokea ahadi, kwa mfano, kama kipindi walichoambiwa walime mbaazi na kwamba zitakwenda kuuzwa India na ikashindikana, Serikali ni lazima ije na mpango mbadala kuliko kuwaachia wananchi ule mzigo wa mazao kuwaaharibikia mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Nape ajiandae.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja za Kamati hizi mbili; Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Kamati ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono taarifa ya Kamati zote mbili. Taarifa imechambuliwa vizuri; na kwa kweli kama Serikali inaweza ikasimamia utekelezaji wa maazimio ya Kamati, tunaweza tukapiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

MheshimI Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo, naona kama Serikali imefika mahali inaenda tofauti na wakulima wa zao la mahindi, yaani wakulima wa zao la mahindi wakizalisha, wakianza kupata soko zuri, Serikali inazuia ili wapate hasara, na mimi sijajua ni kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi wangekuwa na fursa ya kuja hapa Dodoma, lugha ambazo wangezisema, Serikali sijui ingesema nini! Sisi tunatumia lugha ya kiuongozi, lakini Serikali ilivyo kwa wananchi ni mbaya mno, wananchi wamepata hasara kubwa mno. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kabisa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wananchi hawakuelewi kabisa! Ni kama Wizara hii haipo kabisa! Cha ajabu mwaka 2017 bei ya mazao ilianza kuwa nzuri, wananchi wakaanza kuuza shilingi 70,000 na shilingi 80,000 kwa gunia. Ghafla tu Serikali ikakata mrija, kwamba hamna kupeleka mazao nje. Sasa kilichotokea, wananchi sasa hivi debe moja la mahindi wanauza shilingi 3,500. Gunia shilingi 21,000. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Shilingi 18,000.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiuliza Serikali, hivi ina vyombo inavyotizama hali hii? Ina wataalam wanaochunguza hali hii? Hivi Serikali inapata taarifa sahihi za jambo hili? Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa mahindi wana hali mbaya kupita maelezo. Wamepata hasara kubwa sana. Sasa cha ajabu hata wale waliozalisha kwa sababu hawana maghala ya kuhifadhi mahindi, yamekaa yanaoza, yamepecha, hakuna kwa kupeleka. Sasa mnatarajia nini? Jambo hili linaumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali mwaka 2017 ilisema itapeleka mbolea mwezi Novemba, lakini mbolea ya kupandia inaenda palizi ya pili, halafu mbolea ya kukuzia inaenda wakati mazao yameshakua, ni kinyume kabisa na matamshi ya Serikali. Na mimi nashindwa kuelewa kama Wizara hii ina wataalamu sahihi kweli, lazima Serikali ifuatilie jambo hili, ni maumivu makubwa sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie maliasili. Kamati imeeleza vizuri sana juu ya mgogoro wa hifadhi na wananchi. Mimi nizungumzie juu ya mgogoro wa Hifadhi ya *Uwanda Game Reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Uwanda Game Reserve* ramani yake ya kwanza ilichorwa mwaka 1959 ikafanyiwa

marekebisho mwaka 1974 kuonesha kwamba *reserve* inaishia humu. Cha ajabu kuna mgogoro mkubwa sana. Na mimi niseme kwa ujumla kwamba *reserve* ile imebaki kama ni ya watumishi wa Maliasili, kwa sababu hata ukienda sasa hivi, wamechukua rushwa, mifugo imejaa mle ndani. Sasa hata *reserve* yenyewe iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimekueleza juzi kwamba ng'ombe wamejaa, lakini wafugaji wanalanguliwa, bila shilingi milioni mbili au tatu huingizi ng'ombe. Hata ukienda sasa hivi, utakuta mifugo imejaa, hakuna hata maana ya *reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu juzi wamemwendea mfugaji mmoja, tena yupo nje ya *reserve,* wakamwambia tupe hela, akawaambia siwapi hela. Wamefyeka mazao yake. Mimi nimekupa majina ya watumishi hao, lakini nashangaa kwa nini Serikali haichukui hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu umeanza toka Waziri wa Maliasili akiwa Mheshimiwa Maige. Ametoka Mheshimiwa Maige, akaja Mheshimiwa Kagasheki, ametoka Mheshimiwa Kagasheki, akaja Mheshimiwa Nyalandu, ametoka Mheshimiwa Nyalandu akaja Mheshimiwa Maghembe juzi ameenda kujionea, akakuta kweli wananchi wanaonewa. Akatoa suluhu kwamba atatuma wataalam wake kwenda kumaliza jambo hili, lakini mpaka sasa jambo hili bado linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ajue, akitaka aondoke hata sasa hivi, atakuta *reserve* hii imejaa mifugo, wala haieleweki. Kwa hiyo, vitu vingine hivi vinafanya wananchi wapate hasira kubwa sana. Ipo siku moja mtashuhudia mauaji ya ajabu, jambo ambalo siyo zuri kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Waziri wa Maliasili, kama atapata nafasi, aondoke hata kesho aende akajionee hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wanyama waharibifu. Juzi mamba amekamata mwananchi mmoja Mto Momba. Tumetoa taarifa Maliasili; Maliasili hawana habari, kwa sababu wanajua kwenda kumuua mamba hawapati rushwa, wamekaa tu wanaangalia. Mimi mwenyewe nimewajulisha, lakini hawana habari na mamba yule bado anavizia wananchi katika Kijiji cha Kipeta na Kinyamatundu. Kwa hiyo, naomba, kwa sababu Mheshimiwa Waziri umesikia, jaribu kuwapigia simu waende wakatatue tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa ni hayo tu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape, ajiandae Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kusema naunga mkono taarifa zote mbili na maazimio yake. Pia nawapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi kwa kazi nzuri waliyofanya pamoja na Wajumbe wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niende moja kwa moja. Nilitaka nichangie kwenye eneo moja la mahusiano yaliyopo kati ya wafugaji na hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu zilizopo, kwa nchi za Ukanda wa Kusini huku na Afrika Mashariki, Tanzania ni nchi inayoongoza kwa kuwa na mifugo mingi. Inasemekana tuna zaidi ya ng'ombe 28,000,000 na pointi zake, lakini pia kuna mbuzi, kondoo na mifugo mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu, sekta hii ya mifugo inasemekana inahudumia zaidi ya kaya 4,000,000 ambazo zinajumlisha zaidi ya watu 25,000,000 ambao ni karibia zaidi ya asilimia 50 ya *population* ya nchi yetu. Kwa takwimu hizo hizo, sekta hii ya mifugo inachangia zaidi ya

4% kwenye pato la Taifa ambalo inashindana karibu sawa na madini katika nchi yetu. Kwa hiyo, ni sekta kubwa na inagusa eneo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inayoendelea kwenye sekta hii ya mifugo ni mbaya sana. Bahati mbaya kwa miaka sasa hili jambo limekuwa linakuja, linazungumzwa hapa Bungeni, moto unawaka, halafu zinachukuliwa hatua za kuufunika ule moto, watu wananyamaza, halafu dhuluma na hujuma inaendelea pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2015 moja ya kazi nilizofanya ni pamoja na kupita kwa wafugaji nchi nzima, kuwasikiliza na kusikia manung'uniko yao. Nilitegema baada ya uchaguzi wa mwaka 2015 hali itabadilika. Bahati mbaya sana, juzi nikiwa Mjumbe wa Kamati hiiya Ardhi, Maliasili na Utalii, tumekutana na wafugaji walikuja hapa Dodoma, hali ni mbaya kuliko ilivyokuwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea na hatua hizi za kuzima moto kila unapowaka, maana yake ni moja, tunatoa kafara asilimia 50 ya *population* ya nchi yetu ambayo inahudumiwa na sekta ya mifugo na kuacha hali yao ikiwa mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyoongea na hapa nataka niijenge hii hoja tuuunge mkono pendekezo la Kamati la kuunda Kamati Teule ya Bunge kwenda kusaidia kumaliza tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa hatua za kawaida za Serikali, tukubali imeshindikana. Njia peke yake iliyobaki, tuunde Kamati Teule ya Bunge ikaisaidie Serikali kwa nia njema ya kuokoa zaidi ya asilimia 50 a *population* ya nchi yetu ambayo inahudumiwa na sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea mifugo ambayo imeshikiliwa kwenye hifadhi kwa takwimu hizi kama ni za kweli, basi hali mbaya sana. Meatu kuna ng'ombe 948; Kakonko ng'ombe 700; Bukombe ng'ombe 716; Bariadi 158;

Kasulu 90; Morogoro 401; Chemba 411; Mlele 640 na Kaliua ng'ombe 1,129; hawa wameshikiliwa kwenye hifadhi. Wapo wanaoendelea kufa kwa sababu hawana huduma za kutosha, wapo wanaouzwa kinyemela na wapo wanaouawa kwa risasi. Hali hii ikiendelea tunakokwenda ni kubaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu nilizonazo mwaka 2015 - 2018 ng'ombe ambao wameshauawa kwa kupigwa risasi na wengine kwa kunyimwa huduma, kwa sababu wako wengi ambao wamekamatwa, namna ya kuwahudumia ni ngumu, Katavi ng'ombe 6,503; Morogoro Vijijini ng'ombe 200; Bunda ng'ombe 150; Meatu ng'ombe 48; Chemba ng'ombe 196; hii ni mifano ya maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa…

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante Mheshimiwa Nape, tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gashaza na Mheshimiwa Mgumba ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa ya Kamati hizi mbili. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kupongeza kazi ambazo zimefanywa na Kamati hizi mbili kwa mapendekezo na ushauri ambao wameweza kuutoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji hasa katika upande wa mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona changamoto ambazo baadhi ya mazao ya biashara ambayo Watanzania ndio tumekuwa tukitegemea kama zao la kahawa, soko limekuwa ni changamoto kwa sababu pia bei imekuwa haipandi na hii ni kutokana na kodi nyingi ambazo zimekuwepo. Pamoja na kwamba Serikali imejitahidi kupunguza, lakini bado kwa kweli mazingira ya uzalishaji wa zao la kahawa na soko na bei bado haijawa nzuri, hususan kwa wakulima wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na zao hilo la kahawa, tumeona maboresho ambayo yamefanyika kwenye zao la korosho na tumeona jinsi ambavyo bei imekuwa ikipanda kwenye korosho. Pamoja na kwamba kumetokea changamoto hiyo ya baadhi ya watu kutokuwa waaminifu na kutaka kuvuruga soko letu, lakini naamini kwamba Serikali itaweza kufuatilia hususani katika uchambuzi huu ambao ulifanyika kwenye mzigo uliokuwa umeuzwa nje na kukuta kwamba kuna uchafu kama mchanga na mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa kujua kwamba kwa kadri tunavyoendelea, yapo mazao mengine ya biashara ambayo yamefanya vizuri duniani na kama ambavyo tunajaribu ku-*adapt* teknolojia mbalimbali kulingana na mabadiliko ya teknolojia, nafikiri ni wakati muafaka pia kuweza ku-*adapt* hata katika teknolojia ya kilimo ambayo inaweza ikatusaidia kuweza kuinua kipato cha wananchi walio wengi zaidi asilimia 75, lakini pia ambayo inaweza ikasaidia kuendana na kauli mbiu na sera ya Taifa ya kuwa na uchumi wa kati na uchumi wa viwanda kwa kuanzisha mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe wakati wa Bunge la Bajeti lililopita niliwahi kusema kwamba lipo zao linaitwa *stevia* ambalo linaonekana linafanya vizuri duniani, nikaomba tuanze kufanya utafiti wa zao hili kwa kushirikiana na *center* ya Utafiti ya Maruku, Mkoa wa Kagera. Naishukuru Wizara ya Kilimo ambao wamekuwa wakinipa ushirikiano kuhakikisha kwamba zoezi hili linafanikiwa, pamoja na kwamba changamoto bado yako kwenye bajeti, lakini

naiomba sasa kama ambavyo tulifanya wasilisho la utafiti wa zao hili Wizara ya Kilimo mapema mwaka 2017, basi waweze kupeleka fedha katika Kituo cha Maruku kwa ajili ya kuhakikisha kwamba utafiti huu unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mazao kadha wa kadha. Leo kuna zao kama *chia seeds,* wengine wanaita *super food,* ni zao ambalo linafanya vizuri duniani na ambalo katika hali ya kawaida linaweza likabadilisha uchumi wa wananchi wa kawaida, kwa sababu ni zao la muda mfupi, lakini ni zao ambalo linahitajika, pia ni *medicinal* kwa maana ya kwamba linaweza likaboresha afya ya Watanzania, lakini pia likaboresha uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Kilimo kwamba tayari wanaendelea kunipa ushirikiano na muda siyo mrefu tunaamini kwamba tutapata kibali kwa ajili ya kuingiza mbegu kwa ajili ya kufanya na utafiti wa zao hili ili kuinua uchumi wa wananchi wa Ngara, lakini na wananchi wa Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna tunavyoweza kufanya miujiza kubadilisha maisha ya wakulima wa kawaida tusipowekeza kwenye suala la kilimo na kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa sababu kumekuwepo na mabadiliko ya tabia nchi, mara kwa mara tunajikuta tunaenda tofauti na matarajio katika misimu yetu ya kilimo.

Kwa hiyo, naomba tuwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji. Hatujafanya vizuri, ukiangalia ni kwamba, ni asilimia 1.6 tu ambayo tumefanya kwenye sekta hii ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuwekeze katika miradi ambayo tayari imeanzishwa, kama mradi wa Bigombo kwenye Wilaya yetu ya Ngara ambayo takribani sasa miaka mitatu iliyopita ulitakiwa uwe umekamilika, lakini haujakamilika mpaka sasa hivi na

tumeshatumia fedha nyingi zaidi ya shilingi milioni 715 na miundombinu inaanza kuchakaa wakati haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tujikite katika kilimo cha umwagiliaji ili kuboresha maisha ya Watanzania, lakini pia kuandaa mazingira ya kupata malighafi kwa ajili ya kulisha viwanda vyetu ambavyo tunakazana navyo kwa ajili ya kuvianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii iko migogoro ambayo imekuwa ikiendelea katika sekta hii, migogoro ya ardhi ni pamoja na mipaka; mipaka kati ya wilaya na wilaya, kijiji na Kijiji, mipaka kati ya maeneo ya ufugaji na kilimo.

Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Mgumba halafu wajiandae Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kunipa nafasi kuchangia katika Taarifa za Kamati zetu zote mbili hizi. Kwanza nachukua nafasi hii kuzipongeza Kamati zote mbili kwa taarifa ambazo zinaakisi hali halisi iliyopo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nijielekeze moja kwa moja kwenye masuala ya mbaazi pamoja na mahindi, kwa sababu sisi watu wa vijijini na ukizingatia nchi hii, watu zaidi ya asilimia 70 wanategemea kilimo, siku zote lazima tuwasemee wakulima ambao ndio tumekuja kuwawakilisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbaazi limetikisa sana na limeathiri sana wakulima wetu Tanzania kwa ujumla. Tatizo kubwa kuna lugha inazungumzwa kwamba Serikali ilihamasisha sana. Mbaazi hatujawahi kuhamasishwa, tulikuwa tunalima siku zote kutokana na kuvutiwa na bei zilizopo sokoni, lakini kilichotokea mwaka 2017 tu alipokuja Waziri Mkuu wa India kuja kusema atanunua yeye mbaazi zote za Tanzania, ndiyo pale labda watu wengine tunachanganya kusema kwamba Serikali ilihamasisha tununue mbaazi hizi na leo hakuna mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea na kwa mbahati mbaya sana, kabla hatujafikia mwisho wa majadiliano na kusaini mikataba, baadaye India ikatokea kwamba wamezalisha mbaazi zaidi kuliko mahitaji yao. Kwa hiyo, wakawa hawahitaji tena kuingia mkataba na Tanzania wala na nchi nyingine kwa sababu walichozalisha wenyewe ni ambacho kilikuwa kinawatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri tu kwa Serikali kwamba ni vizuri tukafanya utafiti mkubwa na mahitaji ya soko husika kabla ya kubeba hiyo kauli kuipeleka kwa wananchi. Wanaweza kuichukua na kuongeza uzalishaji wakati hitaji hilo kwa wakati huo hakuna. Ni vizuri tukawekeza zaidi kwenye *research and development,* kufanya utafiti kwa maana ya masoko, nini kinahitajika kwa wakati gani, hata ambacho tukizalisha tunakuwa na uhakika muda gani kinahitajika na wapi tunakipeleka na kwa bei gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa pili, sasa hivi kuna taarifa nyingi tunaletewa kwamba sasa hivi China inahitaji sana mihogo. Kama viongozi tunaweza kuichukua kauli hiyo tunapeleka kwa wananchi wetu, tukawaambia kwamba mihogo inahitajika, lakini mpaka sasa hivi nina uhakika kwamba hata mikataba haijafanyika na hatujui ni bei gani? Kwa hiyo, tusije kuchukua kosa lile lile tulilofanya kwenye mbaazi kwenda kuwahamasisha watu wakaanza kulima kabla ya kuingia mikataba rasmi na kujua bei yake.

Matokeo yake wakulima watakuja kuilaumu Serikali pasipokuwa na sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu suala la mahindi, ni vizuri Serikali mkaliweka vizuri suala hili kwa sababu wananchi wengi wameaminishwa kwamba Serikali ndiye mnunuzi mkubwa wa mahindi kupitia *NFRA,* kitu ambacho siyo sahihi kabisa, kwa sababu labda sisi wenyewe Wabunge tunasahau. *NFRA* tumepitisha wenyewe hapa bajeti ni shilingi bilioni 100 tu. Shilingi bilioni 100 unanunua mahindi hata tani 100,000 hayazidi. Sasa kuwaaminisha watu kwamba Serikali itakuja kununua mahindi wakati pesa yenyewe tuliyotenga ni chache, *storage capacity* ni ndogo kwenye uzalishaji wa tani zaidi ya 4,000,000 za mahindi Tanzania ni *just a peanut. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza *NFRA* kama inavyofahamika yenyewe *National Food Reserve Agency.* Huyu ni wakala tu wa kuhifadhi chakula cha dharura cha msaada, kwa hiyo, sio mnunuzi wa mahindi yetu Tanzania. Katika hili naomba kuishauri Serikali, ni wakati muafaka sasa wa kuifufua na kuwekeza zaidi katika Shirika la Hifadhi la Chakula *(National Milling Corporation)* ili lichukue nafasi yake kama zamani ndiyo iwe kampuni mbadala ya kununua mahindi yetu na kuyahifadhi na kufanya biashara kwa niaba ya umma. Tuna uhakika tunatengeneza soko la mazao yetu ya nafaka badala ya kutegemea *NFRA* ambayo kazi yake ilikuwa ni kununua chakula cha hifadhi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, ni vizuri tukawatafuta wadau au Serikali yenyewe kulifufua shirika letu la usagishaji ili lifanye kazi yake kama ilivyokusudiwa kwa mujibu wa sheria na ndiyo itakuwa mkombozi wa mazao yetu ya kilimo. Kama mnavyojua, Serikali au Watanzania wengi tumejiajiri kwenye kilimo, kuwaacha nyuma wakulima ni kuliacha Taifa na watu wengi zaidi maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu labda ni uwekezaji katika mabwawa. Mimi natoka Morogoro na kama

mnavyojua sasa hivi mafuriko yako mengi sana, Kilosa, Morogoro Vijijini na sehemu nyingi tu ambapo yanatuathiri na kuturudisha nyuma kiuchumi. Sasa badala ya kutumia haya kama ni majanga, Serikali tuyageuze kama ni fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kuyaachia maji haya yaende baharini, ni vizuri sasa tukaanza kuwekeza na kuyavuna maji haya ya mvua kuanzia Manyara, Dodoma, Morogoro yote, kwa sababu maji haya yanayotuathiri Morogoro yanaanzia Manyara, yanapita Dodoma yanakuja huku, kote huko, tukijenga mabwawa halafu tukayatumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tutakuwa tumepiga ndege wawili kwa jiwe moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumeokoa maafa yanayosababishwa na mafariko, lakini pia tumetengeneza uchumi, maji haya tunaweza kuyatumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Tukiwekeza hivyo tutakuwa tumewaondoa wananchi wetu kwenye lindi la umasikini na kuondoka katika kilimo cha kujikimu cha kutegemea kilimo cha mvua. Sasa hivi tutakuwa na maji ya uhakika na hawa wananchi wanaweza kukopesheka hata na taasisi za fedha kwa sababu watakuwa na uhakika wa kuvuna, kwa sababu maji yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nizungumze Bwawa la Kidunda. Naipongeza sana Serikali kwa juhudi na mikakati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Maftah ajiandae.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu pale ambapo rafiki yangu na ndugu yangu Mheshimiwa Nape alipoishia. Alipoanza kutoa takwimu nyingi za kuhusu wafugaji kunyanyaswa nchi hii, labda kukumbusha

tu wiki mbili zilizopita Kamati hii ya Ardhi Maliasili na Utalii ilizuia Muswada ambao ulikuwa unakuja kwa ajili ya kuwaadhibu wafugaji tena ya kum-*charge* kila mfugaji, kwa mfugo mmoja kama ni ng'ombe au mbuzi shilingi 100,000 wanapoingia kwenye hifadhi ya wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi naipongeza sana Kamati hii kwa kufanya juhudi kubwa na kuzuia jaribio hilo baya kwa ajili ya wafugaji tena wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu nyingine, jana Mahakama ya Wilaya ya Same imetaifisha ng'ombe 36 wa wafugaji. Ni ongezeko la takwimu ambazo ametoa kaka yangu Mheshimiwa Nape na mimi naomba Bunge hili liangalie sasa kwa historia ya nchi hii wafugaji kunyanyaswa kwa muda mrefu. Hii imekuwa sasa ni *too much!* Naomba mtusaidie ili haya mambo yaishe, maana wakati Mheshimiwa Jaji Nyalali akihukumu ile kesi ya Mkomazi miaka fulani na hukumu yake naijua vizuri sana, mfugaji aliyehamishwa kwenye mbuga ile alilipwa shilingi 250,000; yaani haya ni manyanyaso ya miaka ya 1990 mpaka sasa hivi, wafugaji wanaendelea kutaabika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tu suala la Kamati, kwenye ukurasa wa 14 Kamati imeongelea suala la Ngorongoro na wanasema hivi: "Kuna uharibifu wa vyanzo vya maji, uoto wa asili unaosababishwa na ongezeko la binadamu Ngorongoro tangu mbuga ile iamuliwe kuwa mbuga mwaka 1956, maana wakati ule wakazi walikuwa 8,000 na sasa wako 93,000, kwa hiyo, kuna upungufu wa watalii kwenye Mbuga ya Ngorongoro."

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uongo mkubwa na mwendelezo wa Serikali hii kuwaumiza wafugaji. Kwa nini nasema hivyo? Mwaka 2014 takwimu sahihi zilizopo Ngorongoro ongezeko la mapato ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, imeongezeka shilingi bilioni 63 na mwaka 2017 ni shilingi bilioni 102. Hili hata Mheshimiwa Waziri Maghembe alikiri, Kamati inajua, imepewa mpaka taarifa na Chama

cha Wafugaji wa Ngorongoro, lakini Kamati hii haijataka kunukuu kwa makusudi ya kutaka kupotosha kwa sababu hawataki kuwasaidia wafugaji wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu barua waliyopewa ya tarehe 8 Machi, 2017. Serikali hii inaingia kwenye *record* tangu Uhuru wa nchi hii kuwanyanyasa wafugaji na wakulima kwa vitendo. Naomba *data* hizi ambazo zipo na Kamati imekabidhiwa, wafugaji wa Ngorongoro wameonewa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mwaka 2013 Hifadhi hii ya Ngorongoro, Mamlaka ya Ngorongoro iliibuka mshindi wa Umoja wa Mataifa baada ya maajabu ya saba ya asili inaitwa *One of the Natural Wonders of Africa,* kwa sababu wafugaji na wanyamapori wanaishi sehemu moja, lakini najua *target* ya Serikali ni kutaka kuwaondoa wafugaji wale. Tunaomba kwenye Bunge hili muwasikilize wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nape kwamba kwa mara ya kwanza tuunde tume itakayoshughulikia masuala ya wafugaji na uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la mipaka. Kama hoja ya Kamati inavyosema, kuna maeneo mengi ambayo yalitolewa kwa wanyang'anyi wa nchi hii, kuna ranchi nyingi nchi hii zilitolewa kwa wafanyabiashara. Kwa nini msiwarudishie wafugaji ili tuendelee na sisi kupata maeneo ya wafugaji? Kwa mfano, kama mmechukua Tarangire sehemu fulani, mtupe mbuga yoyote au eneo lolote, kama ni Kongwa au Kilimanjaro na sisi wafugaji tupewe na maeneo ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la maji. Inasikitisha sana, mamlaka inayodaiwa kuliko yote ni mamlaka za Serikali na ninyi mmeshindwa kuzilipisha. Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Maftaha, ajiandae Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hizi za Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja za Kamati lakini nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-Wataala* na kwa namna ya kipekee kabisa niweze kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa hii nafasi kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa ya kuweza kuchangia kwenye Kamati hizi zote mbili. Jambo la kwanza Mtume Muhammad *Swalallah-Alay-Wasallama* karne ya sita *(AD)* alisema *kullil-hakka laukana murra* kwamba sema ukweli japokuwa unauma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa mkweli sana katika maelezo yangu haya machache. La kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mpya wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kigwangalla kwa maamuzi yake magumu anayochukua usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa wakweli, sisi kama Wabunge ni mapema sana leo hii kuanza kum-*judge* Mheshimiwa Kigwangalla kwamba eti anaipotosha Wizara, Wizara haiendi sawa, atakaa kwa muda mfupi. Naomba nizungumze jambo moja tu ambalo kimsingi namuomba Mheshimiwa Waziri Kigwangalla achukue maamuzi magumu, kwa sababu nilishawahi kusema ndani ya Bunge hili kwamba kama nchi haichukui maamuzi magumu, tutarudi kule tulikotoka. Ni lazima tutoke tulipo, tuelekee mbele ili tuweze kuwa na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitia taarifa ya *AICC* mwaka 2017 tukiwa kwenye Kamati yetu pale Arusha, kwamba wale mkakati wao na *strategic plan* zao zote wamepewa tangu mwaka 1978 waendeleze utalii Tanzania na siyo kung'ang'ania pale Arusha kwenye yale majengo. Tukawa tumewaeleza, kwa nini mpaka leo hii Tanzania ina ardhi kubwa sana, hamjajitanua? Wakawa hawana majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukiwa tunapitia taarifa za *AICC* tuliweza kugundua ukarabati wa Jengo la Simba, ule ukumbi wa Simba hawa *AICC,* wamekarabati kwa shilingi bilioni 3.5. Tukiangalia nyumba walizojenga, wamejenga nyumba zaidi ya sita pale zenye ghorofa zaidi ya sita kila moja na zile nyumba zimegharimu shilingi bilioni 1.8. Kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha unaofanyika na Idara hizi za Utalii Tanzania na lazima Mheshimiwa Waziri asimame imara kufufua makaburi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine taarifa ya Kamati imezungumza suala la Olduvai Gorge kwamba ni sehemu ambayo binadamu wa mwanzo Tanzania kwa taarifa za kihistoria amegundulika Olduvai Gorge. Taarifa za mapato ya Serikali kuanzia mwaka 2012/2013 Olduvai Gorge kwa mwaka ilikuwa inaliingizia Taifa hili shilingi bilioni 1.7. Baadae akatokea kidudu mtu pale, Wizarani Idara ile ya Olduvai Gorge ikaondolewa kwenye Idara ya Mambo Kale na ikapelekwa kwenye Shirika la Umma la Ngorongoro na hivi sasa Olduvai Gorge kwa mwaka inakusanya shilingi milioni 700 pekee badala ya shilingi bilioni 1.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ufisadi watu wame-*under estimate* pale. Serikali lazima ifanye upembuzi yakinifu, ihakikishe ya kwamba Mheshimiwa Waziri anaunda Tume Maalum, anafukua makaburi ili tuweze kutoka hapa tulipo na nchi yetu iweze kupata mapato. Kwa hiyo, kusema kwamba eti Mheshimiwa Waziri anafanya maamuzi haraka haraka, hili siyo kweli na mimi siungi mkono hoja. Nampongeza na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu

aendelee kufufua makaburi ili sekta hii ya utalii iweze kuingiza pato kubwa kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mizungumzie kidogo, kuna pesa ambazo Serikali imekopa, pesa za *REGRO* ni pesa zilizokopwa Benki ya Dunia, dola milioni moja sawa sawa na shilingi 1,800,000,000 hivi za Kitanzania hivi sasa, ambazo zimepangwa kuendeleza utalii *Southern Circuit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukipitia taarifa za...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba utulivu ndani ya Bunge. Tafadhali sana, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia taarifa za *TTB,* zile pesa zimepangwa kuendeleza *Southern Circuit,* wanazungumzia Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza Kusini, tunazungumza Mtwara na Lindi, Morogoro siyo Kusini, Kusini ni Mtwara na Lindi. Kwa hiyo, naomba sana zile shilingi bilioni mbili kasoro ambazo zimepangwa kwa ajili ya kuendeleza utalii Kusini ziletwe Mtwara na Lindi watangaze vivutio vilivyopo Mikindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikindani kuna vivutio vingi sana, tuna soko la watumwa pale, tuna *custom* pale ya zamani, tuna majengo ya karne ya saba mpaka leo yapo Mikindani, kuna maeneo ambayo Vasco Da Gama alipita akaweka mahema na ndala pale Mikindani, lakini yameachwa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, Idara hii ya mambo ya kale ipewe pesa na hasa Mtwara Mikindani kule Kilwa Masoko, Kilwa Kisiwani, kuna mambo mengi ya kitalii ambayo Serikali hii inatakiwa iyaone na hasa kupitia idara hii ya mambo ya kale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Serikali imekuwa ikiangalia sana *Northen Circuit,* yaani

unavyozungumzia utalii, tunazungumzia sana Arusha, Ngorongoro na maeneo mengine kule, lakini huku Kusini kumesahaulika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naitaka Serikali kwamba bajeti inayokuja hizi shilingi bilioni mbili ambazo zimetengwa, basi ziletwe kule Kusini zitangaze vivutio hivi vya utalii kule Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atupele yeye ameomba udhuru. Kwa hiyo, nafasi zake amempa dakika tatu na nusu Mheshimiwa Bashe na dakika nyingine tatu na nusu Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mimi mkubwa kuliko Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi angalau dakika tatu hizi, ili niweze kuchangia. Naenda moja kwa moja kumgusa mkulima ambaye asilimia 90 ya Wanarukwa ni wakulima wa zao la mahindi. Nimekuwa nikilalamika sana hapa kuhusiana na zao hili la mahindi kwamba sisi wakulima wa Rukwa asilimia kubwa tunalotegemea ni zao letu la mahindi kama zao la biashara. Nasikitika sana leo hii Sumbawanga kama alivyosema Mheshimiwa Malocha, gunia la mahindi ni shilingi 21,000 kwa mara ya kwanza kwa miaka 15 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niliwahi kulisema na Mheshimiwa Waziri hapa akatoa kauli kwamba tumefuta,

sasa tunafungua milango ya kwenda kuuza mahindi kokote kule mkulima anapotaka. Kwa bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri akaweka kikwazo kingine cha kutaka kibali. Hivi kuna mkulima gani anaweza kutoka Sumbawanga kuja kufuata kibali Dodoma? Hapo tulikuwa tunakaribisha rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisikitisha sana, huwezi kuruhusu mazao yaende nje halafu tuweke kikwazo kingine. Mkulima hawezi kuhimili vikwazo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha sana mbolea leo Sumbawanga hakuna; na ikiwepo ni mbolea ya magendo na leo hii toka jana kuna foleni kubwa sana ya kununua mbolea. Mbolea *Urea* leo hii imefika shilingi 65,000 mpaka shilingi 70,000. Huyu mkulima tunamweka katika fungu gani? Kwanza kabisa anabanwa kwenye mbolea, pili anabanwa kwenye kuuza. Sasa afanye biashara gani? Halafu kubwa ninachosikitika mimi sijui Mawaziri wetu wanafikiria nini? Bahati mbaya tunapochangia, wao wanacheka, mimi hii kitu huwa naumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu kwa nini havichukuliwi kuwa *serious?* Leo hii Mkenya anatoka hapa anakwenda kununua mahindi Zambia, anayapitisha kwenye barabara yetu, kwa magari yetu, anakwenda kuuza kwao, anatuacha sisi Tanzania tunakosa soko la kuuza mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WFP* badala ya kununua mahindi Tanzania na baada ya kukosa kibali cha kusafirisha mahindi kwenda nje, wameenda kununua mahindi Zambia, wameleta hapa, yako hapa Dodoma, yanasubiri kwenda maeneo mengine, sisi tumeshindwa kuwauzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, ifike wakati sasa Serikali ikae chini iliangalie jambo hili. Sisi tunao wajibu wa kuwawakilisha wakulima wetu, tuna wajibu wa kuwawakilisha wananchi wetu, lakini zao kubwa ambalo sisi tunalotegemea ni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima huyu anahitaji akivuna mazao yake auze ili aweze kununua bati, auze ili aweze kumsomesha mwanafunzi. Tumesema kila siku hapa lakini Serikali haitusikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba leo Mheshimiwa Waziri, tunaanza kuvuna mazao mwezi wa tano na sita, lisije likatokea jambo lingine hapa ukatuambia unafunga tena mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hape kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nianze kusema kwamba naunga mkono taarifa za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 mpaka 2020, inasema: "Katika kipindi cha miaka mitano, Chama cha Mapinduzi kitaweka kipaumbele cha kuhakikisha kuwa kilimo nchini kinakuwa endelevu na chenye tija ili kuwezesha Taifa kujitosheleza kwa chakula, kuongeza mapato ya wakulima, kuwa chanzo cha kuaminika cha mapato." Hii ndiyo ahadi yetu kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wanapoapa mbele ya Mheshimiwa Rais, katika kiapo chao wanasema watamshauri Mheshimiwa Rais. Tunapochagua Rais na Wabunge na inapoundwa Serikali inaenda kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Humu ndani huwa Wabunge tunagawanyika, tunaotetea wafugaji, tunaotetea wakulima. Nataka niwaambie, hii ni *divide and rule.* Asilimia 70 ya wakulima wa nchi hii, asilimia 80 ya hii *docket* inafanya kazi ya kilimo na mifugo. Kwa hiyo, anapoathirika mfugaji ndivyo hivyo anavyoathirika mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe jambo hili dogo tu; Bajeti ya mwaka 2010/2011 asilimia 7.8 ndiyo ilikuwa bajeti ya kilimo; Bajeti ya 2012 asilimia 6.9 ndiyo ilikuwa bajeti ya kilimo; Bajeti ya 2016/2017 asilimia 4.9 ndiyo bajeti ya kilimo. Angalieni namna gani tunavyo-*lose focus. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mipango ya matumizi ya ardhi tumeweka maeneo kwa ajili ya misitu, maeneo kwa ajili ya *game reserves,* maeneo kwa ajili ya wanyama, lakini ukija kuna ardhi ya vijiji ambayo imepangiwa matumizi haizidi asilimia 30. Pia tunazo ardhi za miji. Nataka niulize leo, Mawaziri hapa watuambie, ni lini wamekaa chini kuja na *master plan* ya ku-*allocate* ardhi kwa ajili ya wafugaji na wakulima ili tuweze kujua namna gani tunawapanga watu wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tembo akila mahindi, akiua mtu, kuna kafidia na tembo anaheshimiwa kweli, lakini mwananchi akilima ndani ya *reserve* ya wanyamapori, ataadhibiwa kwa faini. Akivuna mazao yake, anaambiwa asiuze ili tuweze kudhibiti mfumuko wa bei. Tunatengeneza *artificial control mechanisms* za kuonyesha uchumi wetu uko vizuri, wakati tunawatia watu umaskini. *This is unfair. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nataka niseme kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, *we are not fair* kwa wakulima, kwa wafugaji, kwa wavuvi, na kwa wamachinga. *Who are we expecting* kesho kwenda kumwomba kura? Tusikubali kuingia kwenye *record* ya kukipeleka chama chetu kubovu kwa makosa ya Mawaziri Serikalini. *We should not allow* kuwatia umaskini Watanzania. Tusiruhusu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mahindi yanazalishwa tena...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mipata, halafu Mheshimiwa Maige.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Kamati hizi mbili. Wenzangu wamelisemea sana suala la kilimo ambapo na mimi nawakilisha wakulima, hivyo ni lazima niwasemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona, Wizara ni kama imewatoroka wakulima, wamebaki peke yao. Wakulima sasa hawana msaidizi na tumewatelekeza. Mwaka 2017 Mheshimiwa Waziri alitembelea Wilaya yetu na Mkoa wa Rukwa wakati wa masika, tukifikiri analeta suluhisho ama la mazao yetu yaliyokosa soko au pembejeo zilizochelewa. Yote mawili aliondoka bila suluhisho lolote na tukashuhudia uchelewaji mkubwa sana wa pembejeo. Mbaya zaidi mpaka sasa pembejeo hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilimsikia Mheshimiwa Rais akikemea kwamba maeneo ambayo yanafanya vizuri kwenye kilimo, yapelekeeni mbolea. Siku mbili, tatu watu wakamdanganya Mheshimiwa Rais wakaleta mbolea nyingi Rukwa, lakini hamna mbolea. Leo ninavyozungumza hakuna *Urea,* wafanyabiashara wanachokifanya, wanatafuta mbolea, wanaagiza malori na lori likisimama tu, mbolea yote inaisha. Hiyo ndiyo habari iliyoko Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu, kilimo sasa mnakiua, lakini mnawatia zaidi umasikini wananchi ambao wanategemea kilimo kwa kila kitu. Hii hatuwezi kukubali, lazima tuwasemee. Serikali msikwepe wajibu; chukueni wajibu wenu vizuri mhakikishe kwamba mnawasaidia wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la maliasili, mwaka 2017 Mheshimiwa Maghembe pia alitembelea Wilayani kwetu na akapata nafasi ya kutembelea kijiji kimoja ambacho kina mgogoro wa ardhi kutokana na uhifadhi. Ninavyosema hivi mpaka sasa migogoro iliyokuwepo wakati

ule haijasuluhishwa kabisa na tumeambiwa hapa kwamba kuna Kamati ya Wizara nyingi ambayo ilikuwa imeundwa kwa ajili ya kuangalia migogoro. Kamati hii haimalizi kazi? Ni lini matatizo ya wakulima na hifadhi yataisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vijiji vingi, kuna Vijiji vya Kasapa, King'ombe, Mlambo, vyote viko tunaambiwa viko kwenye hifadhi, wakati vimekuwepo tangu enzi. Yote hii ni kwa sababu Kamati hii haijakamilisha kazi yake. Ninaomba migogoro hii iangaliwe, lakini wapo wahifadhi wa *TFS,* ni wakatili sana kwa wakulima na kwa wananchi wetu. Mkaa hata debe moja akikamatwa nalo mtu anafanywa vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunavyojua, hakuna nishati nyingine mbadala zaidi ya mkaa, tunaweka nafasi gani ya kuwasaidia wakulima hawa wa ngazi ya chini? Mawaziri wetu waliangalie kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wakulima kutofikiwa na barabara za uhakika. Nina wakulima wangu wa Kata ya Kala hawafikiki kwa barabara na wala hawana mtandao wa simu. Maneno haya nimeyasema kwenye Bunge hili katika vipindi vyote viwili na leo nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri, Kata ya Kala haina mawasiliano ya simu, ni vipi watafikia masoko? Hawafikiki kwa barabara za uhakika, ni vipi mazao yao yataweza kuuzwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu, waone umuhimu wa kupeleka mawasiliano ya simu katika Kata ya Kala pamoja na kutengeneza barabara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaki na tutatizama, Mheshimiwa Chegeni kama atapata nafasi.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye hii mada iliyoko mezani. Kwanza naomba tu

niungane na Waheshimiwa Wabunge na hasa Wajumbe wa Kamati hizi mbili kwa taarifa walizotoa na kimsingi nakubaliana na mapendekezo yao kwa maana ya maazimio ambayo wameyaweka kwenye ripoti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, na mimi naomba ni-*register* masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo mambo yanakwenda kwenye sekta hii. Mwaka 2017 nilifanya ziara kwenye jimbo langu kujionea hali ya mazao kwa wakati ule, nilikumbana na tatizo kubwa la funza. Nilichukua kumbukumbu na niliwasiliana na Wizara kueleza kwamba kuna mdudu ambaye ametokea kipindi kile ambaye anaharibu sana mazao ya wakulima na tukaomba kwamba ni vizuri Serikali ikatoa mwongozo wa dawa gani itumike kukabiliana na mdudu huyu. Hatua hazikuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu 2018 mdudu yule amesambaa mikoa karibu 10 sasa nasikia taarifa, mpaka maeneo ya Kilimanjaro amefika, wakulima wa mahindi karibu wote ambao wamelima hii awamu ya pili, hizi mvua za pili zinazoendelea kwa mfano, katika Mkoa mzima wa Shinyanga, hawatapata mazao yao vizuri. Nilikuwa naomba sana, siyo vizuri kugombana hasa kwa watu mnaoheshimiana kama ambavyo sisi Wabunge tunavyoheshimiana na Mawaziri wetu na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi, aeleze ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kukabiliana na mdudu huyu. Pamoja na kwamba mwaka huu na mwaka 2017 tumeshapoteza mazao, lakini angalau tatizo lisiwe endelevu kutokea tena mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu tatizo la pembejeo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alipokuja na pendekezo hapa la kuanzisha *bulk procurement* ya mbolea, lilikuwa ni jambo ambalo Wabunge wengi tulilikubali, lakini maelezo aliyoyatoa wakati ule hayajatekelezwa kikamilifu katika *level* ya *implementation.* Mheshimiwa Waziri alituahidi kwamba atakuwepo mnunuzi mmoja wa mbolea

atakayepata kazi ile, atakayetoa bei ya chini kuliko washindani wote na atakuwa na mawakala kwenye maeneo yote na mawakala wale watatangazwa, watajulikana na bei elekezi zitatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie, Wakala wa Mbolea au wa Pembejeo kwa Wilaya ya Kahama ni nani, anauza mbolea kwa kiasi gani kwa kila mfuko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana ilikuwa ni *gear* kwa ajili ya hoja ile ikubalike, lakini utekelezaji wake umeachiwa njiani. Nilikuwa naomba sana maeneo haya Mheshimiwa Waziri aje atusaidie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono mapendekezo ya Kamati zote mbili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni dakika mbili na nusu na Mheshimiwa Mattar dakika mbili na nusu. Tunamaliza. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza, napongeza taarifa zote mbili za Kamati, lakini nina *concern* mbili za msingi sana; ya kwanza, upande wa migogoro ya wafugaji, wakulima na hifadhi zetu. Naomba Serikali hili iliangalie kwa mtazamo wa hali ya juu sana. Migogoro hii inasababisha maafa, inasababisha matatizo makubwa sana na kila malalamiko ya Wabunge, hapa tunalalamika kila wakati, sasa naomba Serikali itusikilize. Wananchi kule wana matatizo, lakini cha msingi ni kwamba tunaomba kuwe na ushirikishwaji wa wananchi katika kuainisha mipaka hii na wananchi wapewe nafasi ya kuweza kushiriki katika maamuzi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la mifugo kukamatwa hovyo hovyo, tunaomba Serikali iliangalie sana.

Tunawatia umasikini wananchi wetu. Tunaomba kama ni sheria, basi iweze kuangaliwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la uvuvi haramu. Hakuna ambaye anashabikia uvuvi haramu, lakini mtindo unaotumika siyo mzuri, unaumiza wananchi wetu. Leo tuna wananchi wanakuwa maskini; asubuhi tajiri, jioni maskini. Serikali ya CCM haisemi namna hiyo, wala Mheshimiwa Rais hasemi namna hiyo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii, hebu waonee huruma wananchi hawa, hawa ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alianzisha utaratibu mzuri sana wa *BMU.* Leo hii wananchi wanalia, wanaililia Serikali yao, Mheshimiwa Waziri upo, tusaidie! Tena unatoka sehemu ya Kanda ya Ziwa, kitu ambacho ni aibu. Sasa wananchi tusemeje? Wabunge tumesema, tunakueleza Mheshimiwa Waziri, hutusikii. Tunaomba utusikie kwa hili kupitia Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweke azimio, ni namna gani iliyo sahihi zaidi ya kuweza ku-*moderate* suala zima la uvuvi haramu? Hatupendi, samaki hawana mpaka. Sisi bila kushirikisha nchi ya Kenya na Uganda, tunafanya kazi bure. Zoezi hili lazima liwe shirikishi la wadau wote wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tena ukienda Mwibara kwa Mheshimiwa Kangi wanalia, ukienda Musoma wanalia, Busega wanalia, Magu wanalia, Geita wanalia, kila mahali wanalia, Kagera wanalia na sisi tulie humu Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri naomba uwe msikivu, acha kiburi, kuwa msikivu. Sikiliza maneno ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, unampa nani sasa?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Mheshimiwa Chegeni.

**MWENYEKITI:** Aah, *okay.*

**T A A R I F A**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Chegeni kwamba Bunge tumepewa mamlaka na Katiba ya kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, Wabunge tukichukua *route* ya kulalamika, hatuisaidii hii Serikali. Tufanye maamuzi ili tuweze kuisaidia Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL J. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nimeipokea kwa mikono yote, Bunge tufanye maamuzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze na suala la maji. Naiomba sana Serikali, Wizara ya Maji, Mamlaka za Maji, zinazidai taasisi za Serikali pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi, lazima Mheshimiwa Waziri wa Fedha atufahamu. Taasisi za Serikali zinadaiwa fedha nyingi sana kiasi kwamba Mamlaka zetu za Maji zinafika wakati zinashindwa kujiendesha. Naomba sana Serikali iweze kulipa madeni yale. Ikilipa madeni yale kuna hizi Mamlaka za Maji zitaweza kujiendesha zenyewe bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Kwa hili namuomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali iweze kusimamia tatizo hili kuhakikisha taasisi zetu za Serikali zinalipa madeni ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutamtua mama ndoo ya maji, sasa leo twende katika hali ile. Mheshimiwa Waziri...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MATTAR ALI SALUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna asilimia karibu...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** ...ya upatikanaji wa maji nchini.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe msemaji taarifa kuwa, kwenye Kikao cha Kamati ya Bajeti mwaka 2017 tulifanya maamuzi *unanimously* na wewe ukiwepo Mwenyekiti kwamba madeni yote yanayodaiwa Mamlaka za Maji za *class C* na *B* yachukuliwe yapelekwe Hazina na Wizara ya Fedha ifanye mpango wa kuyalipa madeni haya, jambo ambalo mpaka sasa halijatekelezwa na Watanzania wanazimiwa umeme kwa uzembe unaotokana na *central government* kutokupeleka fedha hizi kwenye mamlaka zinazohusika, ili kulipa madeni ya maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea Taarifa kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sisi kama Wabunge, ndio wananchi. Hawawezi kuja wananchi wote ndani ya Bunge hili kuja kuchangia ndani ya Bunge hili, halitoshi. Tumeishauri Serikali mara nyingi iongeze shilingi 50 ifike shilingi 100 kwenye petroli na dizeli ili tukaokoe matatizo ya maji vijijini na mijini. Nashangaa sana Serikali hii haitaki kutusikiliza sisi Wabunge. Sisi ndio tunaokaa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, naiomba Wizara iweze kutusikiliza sisi Wabunge. Sisi ndio wananchi wenyewe tunaokuja hapa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wewe sio peke yako. Naomba sana kwa hili Serikali iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la uvuvi. Suala la uvuvi namwomba sana Mheshimiwa Waziri, uvuvi tunao mkubwa sana katika bahari. Namwomba Mheshimiwa Waziri tena, uweze kuelekeza macho yako katika bahari. Tunaweza kukuza uchumi mkubwa katika nchi yetu. Mheshimiwa Waziri, kuna nchi nyingi sana zinategemea uvuvi wa bahari kuendeleza katika kipato cha nchi yao, lakini Mheshimiwa Waziri tunashangaa Serikali yetu, tatizo tumeshazungumza mara nyingi la kupatikana bandari ya uvuvi, hakuna; kupatikana meli za uvuvi hakuna… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante sana, mengine subiri bajeti. *(Makofi)*

## Michango kwa Maandishi

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa taarifa ya 2017 – 2018 Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwezesha sekta ya utalii, maliasili na ardhi iweze

kuwekeza kwa muda muafaka, hatimaye kuweza kuingizia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi wetu ili kuweza kutunza mazingira yetu ili yasiharibike na hususan ndani ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwekeze vya kutosha kutangaza vivutio tulivyonavyo nchini kwetu, si kwa mbuga za wanyama na Mlima Kilimanjaro tu bali hata vivutio vingine kama Mapango ya Amboni na kadhalika ili kuweza kuliletea pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge utaratibu wa kutatua migogoro ya ardhi kwa wakati ili kuweza kulimaliza tatizo hili na wananchi waendelee na shughuli za uchumi na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakiki mashamba (makubwa) yaliyotelekezwa ili kuyabaini na Serikali kutoa ardhi hiyo kwa wananchi waliokosa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi la Wanyamapori wawe na utaratibu wa kutoa fidia kwa wananchi ambao watajeruhiwa au kuuawa na wanyamapori.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapango ya Amboni ni moja ya vivutio vikuu vya utalii katika Jiji la Tanga. Ni mapango ambayo ni muhimu sana kwa mapato na mvuto kwa Jiji la Tanga , lakini kuna changamoto zifuatazo:-

(i) Miundo mbinu ya barabara kwenda mapangoni;

(ii) Mto unaopita pembezoni unamega kingo za mapango; na

(iii) Uchimbaji wa kokoto unaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Mpango mkakati na wa haraka na dharura ili kuboresha miundombinu yote muhimu ili kuongeza mapato; Eneo la mapango liainishwe ili liweze kutunzwa na kulindwa; Vivutio vingine kama Chemichemi ya Maji moto ya *Sulphur* Amboni, Mapango ya Tongoni na vivutio vingine ili kuvitangaza na kuviboresha zaidi; na Serikali ifuatilie na kuvitangaza vivutio ambavyo ni vya kipekee kama vile Msitu wa Asili wa Amani na Vipepeo adimu duniani ambavyo vinapatikana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka katika hifadhi; kumekuwa na migogoro mingi na ya muda mrefu kati ya wananchi wanaoishi karibu na hifadhi na Serikali au wahifadhi wa maeneo yaliyotengwa kwa hifadhi. Kumekuwa na mgogoro mkubwa kwa wananchi wanaoishi Kata ya Lunguza kwenye mbuga ya Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Serikali ikapime mipaka upya ili kuondoa migogoro; Katika kupima waweke *free zone* ili kupunguza migogoro na ukaribu wa makazi ya wananchi na hifadhi; Hifadhi zijitahidi na zisimamiwe ili zirejeshe kiasi cha mapato katika miradi ya kijamii ili kusaidia kuwajengea wananchi imani na nia njema ya kuwa na hifadhi ni kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza jitihada ya Serikali katika kutatua matatizo, migogoro na changamoto zinazokabili ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi kwa asilimia 80 wanatumia nishati ya kuni na mkaa na kuyumbisha uhifadhi wa misitu yetu hutupatia matatizo kadhaa kama vile ukosefu wa mvua, kutoweka kwa vyanzo vya maji pamoja na mito kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado umeme na gesi kuwa na gharama kubwa na kutokuwepo ama nishati hizo hazijasambaa nchi nzima na zikiwa ndiyo nishati mbadala kwa wananchi wetu. Hivyo, ni vyema Serikali ikaharakisha kuleta Muswada wa Sheria ya Mbegu za Miti kuwa na bei rafiki na wezeshi kwa wananchi ili kuwawezesha wananchi kupanda miti ya muda mfupi kwa wingi na kuwezesha kuitumia kwa nishati na kurejesha misitu yetu kwa miti ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mbegu za Miti wapewe Bajeti ya kutosheleza kuweza kufanya utafiti wa mbegu za miti na kubainisha upevu wa miti katika muda mfupi kwa kuharakisha kuondoa usumbufu utakaojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaenda sambamba na kuwa na maabara bora zenye vifaa vya kisasa viendavyo na wakati uliopo na kuharakisha matokeo ya ubunifu wa wataalam wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado upatikanaji wa nishati mbadala kwa wananchi, basi Serikali ni vema ikawa na udhibiti kwa watumishi wanaotoa usumbufu, kujenga kero na chuki kwa Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara/Serikali inajitahidi kushughulikia migogoro ya ardhi na hifadhi zetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujipanga kwa kuboresha majiji katika muonekano wake ni sawa, ila nashauri Serikali kwa hii miji inayokua au inayoanza nayo ni vyema ukawepo mpango kabambe wa kuipima na kuipanga kwa ajili ya mwonekano endelevu kuelekea mji au jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa hivi miji inakuwa changanyikeni na kutokuwa na miundombinu, kwa mfano Sumbawanga, Kigoma, Tabora, Mpanda na kadhalika, hivyo matumizi bora ya ardhi iwe ni zoezi kwa vitendo kila eneo la hapa nchini na kufanyiwa tathmini kwa

kipindi kifupi ili kuleta ufanisi na matokeo ya kuonekana na kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wananchi na hifadhi, wafugaji na hifadhi, wakulima na wafugaji sasa ni wakati wa kutokana nayo. Serikali ichukue hatua ya uthubutu kabisa wa kushughulikia tatizo hili la migogoro liweze kutoka ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara husika kwa namna moja au nyingine kukutana na wamekwishafanya hivyo ni vema wakatoa makubaliano yao ya utekelezaji mapema; kama ni kubadili sheria lifanyike; kama kuwekwa kanuni ziwekwe na kupitishwa; mpango wa matumizi bora ya ardhi kuwekwa kwenye sheria lifanyike na kama kufutwa kwa baadhi ya sheria zifutwe na kadhalika

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleweshwa kwa taarifa ya kikao cha pamoja cha Wizara husika kwa Bunge ili kufanyia kazi na kurejesha kwa jamii kwa utekelezaji ni hatari. Ni vyema sasa tukakamilisha zoezi hili la kufuta au kupunguza migogoro na kujenga imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuwasilisha vyema. Pia niishauri Serikali ichukuwe taarifa yote ya Kamati na kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wimbi kubwa sana la migogoro ya ardhi hapa nchini; na migogoro hii itaendelea kama tu Serikali haijachukua hatua za haraka juu ya suala zima la kupima ardhi katika maeneo yote ambayo ni mipaka ya ardhi ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi na wafugaji na watu binafsi wenye mashamba au viwanja kuvamia maeneo ya watu hasa wale ambao hawana uwezo. Kwa hiyo niishauri Serikali yangu Tukufu kuharakisha mchakato huu hasa kwa

kupeleka fedha za kutosha na kwa wakati ili maeneo yote yapimwe na kuanishwa ili makundi yote hayo yatambue mipaka yao hasa kwa kuweka mawe ya mipaka *(beacon).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha kwani kwa sasa Wizara ina watumishi wachache sana ambao hawakidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kupima miji na majiji kwa vile vifaa vya kisasa ambavyo vimetumia *Satellite*, hivi vifaa visambazwe kwa kasi vifike mpaka kwenye wilaya kuliko ilivyo sasa ambapo vipo tu kwenye baadhi ya majiji kwani hii itafanya wananchi wapate hati kwa haraka kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Misitu. Maeneo mengi hapa nchini hayana miti ya kutosha na kuna maeneo mengine hayajapandwa miti kabisa. Naomba niishauri Serikali iwape pesa za kutosha hasa Wakala wa Mbegu ambao ni *TTSA,TAFORI, DANIDA* pamoja na hawa Wakala wa Misitu Tanzania *TSF* na kuwasimamia na kuhakikisha wanazalisha miche ya kutosha na kupanda maeneo yote yenye ukame pamoja na yale ambayo misitu yake imeungua kama vile Misitu ya Lushoto takribani maeneo mengi ya Misitu ya Lushoto imeungua na kubaki vichaka tu. Kwa hiyo, niiombe Serikali maeneo hayo yapandwe miti haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kuwashirikisha watu binafsi wenye bustani za miti pia kuwapa *support* ili nao wawe wanachangia katika suala zima la kupanda miti. Pamoja na kusimamiwa Sheria Ndogo hasa hizi zinazotoka Halmashauri na kuwaelekeza mpaka Wenyeviti wa Vitongoji wasimamie zoezi hili. Serikali ikifanya hivyo, naamini nchi nzima hii itakuwa ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapango ya Amboni. Tulitembelea Mapango ya Amboni tumekuta Serikali inapoteza pesa nyingi sana kwani mapango yale ni ya asili ambayo huwezi kuyapata popote pale hapa duniani lakini mapango yale yanaendeshwa kikawaida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iyaboreshe maeneo yale ya Ambaoni kwani inapoteza fedha nyingi sana, patangazwe na kuwe na miundombinu ya barabara, waajiriwe watumishi wenye taaluma . Pia tutangaze mbuga zetu ndani na nje ya nchi kwani hii ndiyo secta inayoingiza pesa nyingi za kigeni. Pia nashauri kuundwe Tume hapa Bungeni itakayochunguza migogoro ya wafugaji na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwani hali si nzuri, kuna malalamiko ya wafugaji pamoja na wadau, yaani watu wanaomiliki vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie taarifa ya Kamati ya kwanza kwa kuwapongeza sana kwa kazi nzuri na kubwa wanayofanya. Naomba nishauri Bunge iangalie namna ya kuwa na mfumo wa Kamati za Kudumu kufanya kazi ya pamoja *coordination,* uratibu baina ya Kamati mbalimbali kwenye masuala mtambuka. Kwa sasa kila Kamati inajitegemea na sio rahisi kufanya kazi ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kushauri Kamati ichukulie kwa umuhimu suala la kulinda ardhi za kilimo, mifugo na pia maeneo ya uvuvi zisibadilishwe matumizi kiholela na pawe na sheria itakayowezesha Bunge kuridhia kubadilishwa matumizi ya ardhi hasa za kilimo, mifugo na uvuvi. Leo hii nyingi zenye rutuba za kilimo zimegeuzwa kuwa makazi, viwanda na matumizi mengine. Pia kuishauri Serikali kutatua mgogoro wa ardhi baina ya Hifadhi mbalimbali na wakulima, wafugaji na hata ushoroba mbalimbali zinapovamiwa ambazo ni muhimu kwa uendelevu wa hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeshauri tuangalie namna ya kuchangia kuboresha misitu na hifadhi zetu ili mchango wake uwe endelevu kwa Taifa letu. Ni vyema mapato yanayotokana na maliasili sehemu yake mfano asilimia 10% yarudishwe kuboresha mazingira. Kwenye kufanya

uratibu na Kamati zingine tuishauri Serikali kuangalia kilimo, hifadhi, kulinda vyanzo vya maji na pia kuzuia mmomonyoko wa udongo kwenda kwenye maziwa. Sheria zipo ila hamna ufuatiliaji na usimamizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Kamati ikubali kufanya utaratibu wa karibu na Kamati zingine na kupokea maoni ya Wabunge na wadau wengine ili kuboresha utalii. Tumejaliwa na Mwenyezi Mungu kupata vivutio vingi vya aina mbalimbali lakini hatujafikiria hata asilimia 10% kufaidi rasilimali tuliyonayo. Tunashauri tuangalie mfumo wa kuishauri Serikali namna ya kufuatilia na kusimamia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati pia iweze kushirikiana na taasisi ya Wabunge uliopo Bungeni ya *TAPAFE* ili kuendelea kupata tija. Ahsante.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro ya ardhi katika maeneo mengi kwa sababu hayajapimwa na wanapotokea Wawekezaji huyachukua maeneo makubwa na wananchi wanabaki hawana ardhi. Pia Wawekezaji wengi wanachukua maeneo makubwa lakini hawajayaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Kanisa la KKKT katika Halmashauri ya Njombe Mjini ambao wamemilikishwa eneo la hekta 120 wanashindwa kuliendeleza. Naiomba Serikali ichukue maeneo ambayo hayajaendelezwa na yarudishwe kwa wananchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA,* Shirika hili linawasumbua sana wananchi, mipaka iliyowekwa wameongeza na kuingia kwenye maeneo ya wananchi na kusababisha migongano kati ya wananchi na *TANAPA.* Niombe Serikali kuwaacha wananchi kwenye mipaka yao iliyowekwa zamani. Mfano, Wilaya ya Wanging'ombe, Kata ya Luduga kuna migogoro hiyo ya mipaka

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Ardhi ili kuweza kupima ardhi na kupanga matumizi yanayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuipongeza Kamati kwa kuandika kwa umakini na kuiwasilisha taarifa hii kwa ubora na kwa kufahamika vizuri na Wabunge wote. Katika kuchangia taarifa hii napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi; Serikali imezoea kupima na kuelekeza matumizi ya ardhi katika shughuli za ujenzi, mashamba na mipango miji, lakini kuna tatizo kubwa ambalo linasumbua na kuleta athari kubwa katika maeneo kadhaa ya nchi yetu; tatizo hilo ni tatizo la maeneo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika suala hili, Serikali ianze mpango maalum wa upimaji wa maeneo hayo na kuyaelekeza kwa jamii hizi mbili za wakulima na wafugaji. Hii itaondosha usumbufu mkubwa kwa watu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Matumizi ya Ardhi, Kamati katika taarifa yake ukurasa wa 23 imeshauri kuhusishwa kwa kampuni binafsi ya upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi. Mimi binafsi sikubaliani na ushauri huu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotumia kampuni binafsi katika kazi hii tunaongeza gharama za uendeshaji *(operation coast)* ambazo mwisho wake zinaenda kwa mtumiaji wa ardhi ambaye ni mwananchi wa nchi hii. Ushauri wangu katika suala hili ni Serikali kuwatumia vijana wetu

kwa kuwapa mafunzo ya kazi hii na mwisho wake kuwapatia ajira. Hii itakuwa ni moja ya vyanzo vya kuongeza ajira katika nchi *(source of job creation).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii haikuangazia utekelezaji wa Dhana ya Hifadhi za Jamii *(WMA).* Nilitegemea kupata taarifa kuhusu idadi ya *WMAs* zilizosajiliwa tangu dhana hii ianzishwe chini ya Sera ya Wanyamapori mwaka 2003 hadi sasa (miaka 15) na manufaa ya kiekolojia na uchumi yaliyopatikana. Jamii zenye *WMA* zimefaidikaje? Serikali imefaidikaje? Serikali ina mkakati gani kuendeleza dhana ya *WMAs* na *WMAs* ngapi zinatarajiwa kuanzishwa zaidi katika nchi yetu?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati kwa kuona umuhimu wa utalii zaidi ya wanyama pori na maeneo mengine yaliyozoeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu alipokuja Nyasa kwenye tamasha la utalii alielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuongeza kasi ya kuhamasisha na kuwezesha utalii wa fukwe. Hivyo aliagiza iundwe mamlaka ya utalii wa fukwe. Naomba, Kamati isaidie kufuatilia kufanikisha suala hilo. Nami napenda utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa ndio inayochangia kwa kiasi kikubwa sana katika pato la Taifa, lakini sasa imeanza kushuka. Ni vyema tukaanza kuimarisha miundombinu ili kuboresha utalii na vile vile ni vyema tukatengeneza utaratibu wa kuimarisha utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANAPA kuna hifadhi 16 ni tatu tu zinazo-*break ever point,* Wizara itengeneze utaratibu wa kuhakikisha kila hifadhi inajiendesha hakuna sababu za msingi ambazo zipo kwa hifadhi ambazo hazijiendeshi. Nchi ya Seychelles inajiendesha kwa utaliii tu *why not* Tanzania?

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Naomba kuchangia machache katika taarifa ya Mjumbe wa Kamati hii. Naomba kuongeza machache katika katika maoni yetu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi katika maeneo ya Hifadhi ni tatizo kubwa sana katika vijiji vinavyozunguka hifadhi zetu. Hivyo ni jukumu la Serikali kuhakikisha migogoro hiyo inamalizika na kuleta uelewano kati ya wananchi na watumishi wa Hifadhi (Askari) zetu. Kama Serikali haitachukua hatua za haraka, migogoro hii itasababisha vurugu na hata kusababisha majeraha hata vifo kwa wananchi wetu. Hivyo, ni muhimu sana wananchi kushirikishwa na Wizara husika kwenye zoezi hili ili kufikia muafaka kwenye suala hili la mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamekuwa na malalamiko mengi kuwa Askari wa Wanyamapori wamekuwa wakiwanyanyasa sana kwa kuswaga ng'ombe zao kwa nguvu na kuziingiza kwenye hifadhi na kulazimishwa kutoa rushwa na wakishindwa kutoa rushwa hiyo mifugo yao hupigwa mnada. Ziko taarifa kuwa Askari hao kutumia ndugu zao kununua ng'ombe hao. Kama Kamati tumeliomba Bunge liunde Kamati Maalum kuchunguza tuhuma hizo ili ukweli ujulikane na sheria ichukue mkondo wake kwa wale watakaokutwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvamizi wa mifugo katika hifadhi; katika ziara zetu tumeona jinsi vyanzo vya maji vikiharibiwa na mifugo na kukosekana kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mabwawa, malambo kwa ajili ya mifugo. Hivyo, tunaishauri Wizara husika kuweka malambo na mabwawa katika maeneo hayo ili kupungua au kumaliza kabisa suala hilo la uvamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuweka msisitizo kwenye ushauri wa Kamati yetu kuhusu uundaji wa Kamati kujua ni kwa nini mapato ya Sekta hiyo ya Uwindaji yameshuka? Siyo Mheshimiwa Waziri kukimbilia kufuta leseni za vitalu ambazo tayari wawekezaji wameshalipia na kupata *booking* za wageni; leo ukiwaambia unawapunguzia muda wa leseni zao, itakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zetu tumeona mapitio ya wanyama yamezibwa kwa shughuli za kibinadamu na hii imesababishwa na kutokuwepo kwa vibao vya kuonesha kuwa eneo hilo ni shoroba. Hivyo, tunashauri hifadhi zishirikiane na Halmashauri na Wizara zinazohusika kuweka mipaka na mabango kuonesha maeneo hayo ya shoroba ili kupunguza na kumaliza kabisa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo niliyochangia hapo juu na tukizingatia maoni yote ya Kamati, naamini migogoro inayoikabili sekta hii ya utalii itapungua na kwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha mchango wangu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Nianze na migogoro ya ardhi katika maeneo ya Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko mengi ya mipaka kati ya hifadhi na wananchi na wafugaji kuingiza mifugo kwenye hifadhi. Hii huchangia maambukizi ya magonjwa kwa wanyama na kusababisha wafugaji na walinzi wa wanyamapori na hifadhi kugombana na wafugaji, kuanza kuua wanyama kama samba na kadhalika. Ni vizuri kabisa katika bajeti ya mwaka huu zikatengwa fedha kwa ajili ya kuweka mipaka katika hifadhi zetu ili kumaliza migogoro iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la uwindaji wa kitalii. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alitangaza

kufuta leseni zote za uwindaji wa kitalii, jambo ambalo limeleta mtafaruku mkubwa katika sekta hii. Ijulikane kwamba katika utalii huu mwekezaji anatumia fedha nyingi sana kuandaa miundombinu ya uwindaji; na watalii wa uwindaji wanafanya *booking* zao hata miaka miwili kabla na wanalipa mapema *(advance payment).* Sasa leo hii ukikatisha ghafla siyo kuua kabisa utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengi wameshindwa kwenda kufanya maonesho/matangazo yaliyokuwa yafanyike mwakani, lakini mpaka sasa hivi hawana uhakika na biashara zao. Pengine Serikali ina nia njema ya kufanya mnada katika kuuza vitalu vya uwindaji, lakini lazima kufidia wale waliopo; wameshatumia kiasi gani kuendeleza vitalu? Tayari wana *booking* kiasi gani? Wamekata mingapi kwa miaka mingi? Bila kufanya hivyo, tutapoteza fedha nyingi sana ukizingatia sekta hii huchangia zaidi ya asilimia 17 ya pato la Taifa na huchangia kwa kiasi kikubwa kupata fedha za kigeni. Kwa sasa mapato yameshuka kutoka shilingi milioni 23.58 mwaka 2010 hadi shilingi milioni 11.28 mwaka 2015. Hii ni hatari kwa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaliwa vivutio vingi sana ambavyo vingine havipatikani sehemu nyingine. Mfano, mbuga ya Saadan, bado hazijafanyika juhudi za kutosha kuendeleza kivutio hiki ambacho wanyama wanaenda mpaka baharini. Miundombinu ya barabara siyo mizuri, bado hawajashirikisha sekta binafsi ili waweze kujenga hoteli za kitalii ili kuwavutia watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna haja ya kuiwezesha Bodi ya Utalii ili iweze kutangaza vivutio vyetu, siyo nje ya nchi tu, hata kwa utalii wa ndani bado mwamko ni mdogo kwa wazawa kutembelea mbuga zetu. Nashauri watangaze *program* ya kutembelea shule na kuwahimiza kutembelea mbuga zetu, yaweza ikawa njia moja ya kupata wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado *TANAPA* haijatangaza Hifadhi ya Mkomazi ipasavyo kwa sababu hii ingeweza kutumika kama *day trip* kwa watalii wanaokuja kupanda

Mlima Kilimanjaro. Wakiwa na siku moja ya ziada wanaweza kutembelea hifadhi hiyo na kuongeza pato la Taifa.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii na kwa kunimheshimiwa mwenyekitipa pumzi ya kusimama hapa kwenye Bunge lako Tukufu leo. Nianze kwa kupongeza Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii kwa kupata fursa ya kufanya ziara za kutembelea baadhi ya vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu ambayo kama mdau wa uhifadhi, ningependa kuyasisitiza ni Wizara hii kuwa na ubunifu. Kumekuwa na utalii wa aina moja miaka mingi, hivyo nashauri tuwe na aina nyingi za utalii ambazo zitafanya mtalii aache fedha zake, kuliko kutegemea fedha za lango kuu, wakati mgeni anaingia hifadhini. Mfano kivutio kilichopo Hifadhi ya Manyara ni mfano mzuri wa ubunifu. Nashauri maeneo mengine yafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la vitalu vya uwindaji. Kumekuwa na sintofahamu kutokana na kauli mbalimbali za kuzuia na kuruhusu uendeshaji wa vitalu vya uwindaji. Kutokuwa na msimamo wa matamko katika Wizara hii kunaathiri shughuli nzima ya uwekezaji kwenye vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, biashara hii inauzwa au inafanyiwa masoko kabla ya mteja kutumia bidhaa. Hivyo, tunaweza kupoteza mapato mengi na kuwafanya wafanyabiashara ya utalii wa uwindaji kukata tamaa ya kuwekeza nchini. Mfano, leo tuna vitalu 61 havina wawekezaji, lazima tujiulize tumekosea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mipaka. Kumekuwa na migogoro ya uhifadhi na wananchi wanaozunguka hifadhi zetu. Kama hatutaweza kuweka suluhisho la mipaka yetu ya hifadhi, tunakwenda kuwaumiza wananchi wetu kwa kuendelea kuwatoza faini kubwa na adhabu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kwamba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maliasili na Mifugo tuweze kukaa pamoja ili kuwa na mpango wa pamoja wa matumizi bora ya ardhi na kuweza kupunguza na kumaliza kabisa migogoro ya mipaka.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati kwa taarifa iliyosheheni maelekezo, mapendekezo na ufuatiliaji katika mambo mbalimbali yanayohusu ardhi, maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kuona Kamati imefanya ziara katika maeneo mbalimbali katika tasnia ya ardhi, maliasili na utalii na kujionea *physically* badala ya kukaa katika kumbi na kujadiliana bila kutembelea maeneo husika na mara nyingine hata Mahakama huhamia eneo la tukio. Ningeshangaa kama Kamati isingetembelea na kujionea hali halisi ya sekta ya ardhi, maliasili na utalii hali iliyopelekea kuishauri vema Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa mapori na mbuga nyingi za wanyama, lakini ni Watanzania wenyewe wanajihusisha na ujangili na uharibifu wa maliasili zetu. Ushauri wangu, ni vema Serikali ikatoa elimu ya ufahamu kwa wananchi. Wananchi wakipata elimu na uelewa kuwa hata nchi zilizoendelea zilikuwa na wanyamapori na maliasili nyingine lakini kutokana na matumizi mabaya (ujangili) leo nchi hizo wananchi wao wanalazimika kuja Afrika na Tanzania kujionea wanyamapori na vivutio vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo natoa wito kwa Serikali kuwapatia elimu ya ufahamu na waelewe pato linalotokana na utalii linachangia pato la Taifa. Mfano, ni vivutio vilivyopo katika Mkoa na Jiji la Tanga kama Hifadhi ya Amani, Hifadhi ya Taifa ya Saadani, Fukwe *(Beaches)* zilizopo Pangani, Magofu ya Tongoni na Amboni *Sulphur* pamoja na Amboni *Caves.* Niungane na mapendekezo ya Kamati lakini nashauri kwamba Amboni *Caves* iongezewe uwekezaji mkubwa pamoja na kupatiwa umeme na tochi zenye mwanga mkali na barabara pia iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendeleze mpango wa Kata Mti Panda Mti na iandae utaratibu wa kufanya mashindano ya kupanda miti mijini na vijijini kama inavyofanya nchi ya Malaysia. Nashauri maeneo ya mjini kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini zipatiwe miche ya miti ya matunda ambayo itatoa vivuli, itabadilisha mandhari za miji na itatoa matunda na itatoa kipato kitakachopatikana kutokana na zawadi zitakazotolewa kwa watunzaji wa miti hiyo pia itatoa matunda na wananchi watafaidika na matunda hayo kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi za Taifa kuvamiwa na wafugaji. Ni vema Serikali ikajipanga vizuri katika jambo hili kwani imekuwa ni tatizo la Kitaifa kwani wafugaji nao ni Watanzania wanafuga na wanauza mifugo hiyo ndani na nje ya nchi na kuingizia kodi Serikali. Wafugaji wanatoa kodi na tozo mbalimbali katika minada kwenye Halmashauri zenye wafugaji. Serikali itoe elimu kwa wakulima na wafugaji na kuwapangia maeneo ya kulishia mifugo na maeneo kwa ajili ya kilimo. Pia maeneo yenye Hifadhi na Mapori Tengefu, yawekewe alama maalum na zitambulishwe kwa wananchi wetu (wakulima na wafugaji). Tukumbuke ardhi haikui na watu wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi mijini/ vijijini. *If you fail to plan, you plan to fail.* Katika Halmashauri zetu nchini 98% kuna migogoro ya ardhi, mingine ni kwa wananchi kutokufahamu lakini mingine inasababishwa na wataalam wa ardhi katika Halmashauri kwa *interest* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kutoa shinikizo la kila Halmashauri kuwa na ukanda wa *EPZ (Exporting Processing Zone),* ardhi za wananchi zimetwaliwa na ama kulipwa fidia ndogo ama kucheleweshwa hadi leo fidia zao hawajalipwa. Mfano, ni katika Halmashauri ya Jiji la Tanga kuna Kata za Donge, Mabawa na Tangasisi na Masiwani Shamba, wananchi bado wanasumbuliwa katika fidia zao. Nashauri Serikali iwalipe wananchi fidia zao kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ujenzi wa uwanja ndege. Katika mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege Tanga kuna mgogoro wa nyumba kuvunjwa. Zipo nyumba 208 zilizofanyiwa *evaluation* mwaka 2008 hadi leo fidia haijalipwa. Pia zipo nyumba 802, nazo hazijalipwa fidia lakini zinatakiwa zivunjwe. Hivi ni kwa nini katika miradi lazima tuwatie wananchi hasara. Nashauri Serikali iwe na *vision* na *mission* na tulipe fidia.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono mapendekezo ya Kamati hii, naomba kusisitiza kwamba migogoro ya ardhi hasa vijijini imezidi kuongezeka siku hadi siku. Kutopimwa ardhi kumesababisha miingiliano na vurugu kubwa hasa ikizingatiwa kwamba maeneo mengi ya vijijini hayajapangiwa matumizi bora ya ardhi zao, kwa mfano, Jimboni kwangu Same Mashariki, wakulima na wafugaji na *TANAPA* (*Mkomazi National Park*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa wanyamapori kuingia kwenye mashamba na makazi ya wananchi umeongeza umaskini Jimboni kwangu. Mazao ya wakulima yamekuwa yakiharibiwa sana na wanyamapori. Wananchi wengine wameumizwa na wanyama hao. Badala ya kulipwa fidia, wananchi wamekuwa wakipewa kifuta jasho ambacho sio sawa na madhara waliyopata. Wanyamapori wamekuwa wakithaminiwa kuliko wananchi. Matokeo yake wananchi hawaoni faida ya kuwa na mbuga za wanyama katika maeneo yao. Nashauri Wizara hii ya Maliasili na Utalii ikishirikiana na Wizara ya Ardhi iweke utaratibu mzuri utakaoondoa matatizo haya ya wananchi.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uwasilishaji wa taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Napenda kuishauri Serikali kama ifutavyo:-

(i) Ipunguze mlolongo wa tozo kwenye utalii kwani umesababisha watalii wengi kushindwa kuja Tanzania hivyo kupunguza pato la Tanzania;

(ii) Iboreshe hoteli zetu za kitalii na huduma ziwe za kisasa na pia kutoa elimu kwa wahudumu wetu jinsi ya kuwahudumia watalii wetu. Vilevile iboreshe mitaala ya ufundishaji wahudumu wetu kwani wamekuwa hawakidhi kiwango cha kimataifa hivyo watalii wengi kutofurahia huduma zetu wawapo nchini.

(iii) Ishughulikie migogoro ya ardhi ambayo mingi inasababishwa na Maafisa Ardhi katika Halmashauri kwa kupima maeneo ya wananchi na kushindwa kulipa fidia na kuuza viwanja hivyo kama vyanzo vya mapato ya Halmashauri wananchi wakiachwa bila kipato chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri kuwa wanapogawa viwanja vilivyopimwa wazingatie kaya au nyumba husika ina vijana wangapi wenye uwezo wa kujiajiri ili kuondoa tatizo la vijana kukosa ardhi kwa ajili ya kujiajiri.

(iv) Iwakemee viongozi ambao ni Watendaji wa Kata na Vijiji wanaouza ardhi za vijiji bila kushirikisha wananchi.

(v) Itoe elimu kwa wananchi juu ya haki ya msingi ya ardhi na jinsi ya kumiliki ardhi. Niombe pia kuondoa urasimu wa upatikanaji hati miliki kwenye ofisi za ardhi.

(vi) Iharakishe urasimishaji wa ardhi ili wananchi waweze kutumia ardhi hiyo kwa ajili ya kujipatia mikopo ya kilimo.

(vii) Ishughulikie mgogoro uliopo kati ya Halmashauri ya Kibaha na wananchi wa Lumumba na Mwanangali ambao umepelekea wananchi kuwa maskini na kushindwa kuendeleza maeneo yao kwa miaka kumi.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa letu la Tanzania sekta ya kilimo inaajiri wananchi asilimia 70 lakini bado Serikali haiwekezi kiasi ambacho kitakuwa na uwiano na hitaji la sekta hiyo.

(i) Pembejeo haziji kwa wakati na za kutosha mahitaji.

(ii) Wataalam wa sekta hiyo wapo wa kutosha katika Halmashauri.

(iii) Bei ya mbolea si rafiki kwa wakulima hasa kwa mwaka 2017 - 2018, bei ya mahindi iko chini sana kuliko bei ya mbolea. Gunia la mahindi ni Sh.30,000 wakati mfuko mmoja wa mbolea ya *UREA* ni Sh.56,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo katika Taifa letu la Tanzania imekuwa tatizo kubwa kwa wafugaji kwa kukosa maeneo ya kufugia. Serikali iwe na mkakati wa makusudi kuhakikisha wakulima na wafugaji wametengewa maeneo kwa shughuli za kilimo na mifugo ili azma ya Tanzania ya viwanda iwezekane. Viwanda vinavyotakiwa kuwepo vinahitaji malighafi kutokana na kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi, matatizo ya Sheria ya Uvuvi itazamwe kwa macho ya faida ya wavuvi na Taifa, siyo kuchoma nyavu za wavuvi bila kuhakikisha vyavu hii ni zile zinazotakiwa au la hasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali bajeti inayopitishwa na Bunge ifike kwa wakati kwenye Wizara husika.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuchangia taarifa nzuri ya Kamati na kushauri kuboresha katika maeneo mbalimbali kwa kila sekta.

Kwanza, nishauri suala la mbolea, bado tozo ya *USD* 10,000 kwa mbolea mpya ingeondolewa na Serikali, hii imefanya aina nyingi za mbolea hasa za maji kwa ajili ya (*horticulture*) kilimo cha mbogamboga na matunda kukosekana sokoni. Pia Serikali iangalie jinsi ya makampuni za mbolea zitoe huduma za ugani *(soil testing)* kupima udongo badala ya kuiachia Serikali kama Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri tuwekeze kwenye utafiti, zaidi kwenye mbegu ambapo asilimia 75 za mbegu za mahindi zinatoka nje ya nchi, mbegu za mazao ya kahawa mafuta kama alizeti, soya na mbogamboga asilimia 95 zinatoka nje ya nchi. Tuna uwezo wa kuzalisha mbegu zetu nchini, pia hulinda viwanda vyetu vya mbolea na mbegu zinatozwa kodi, tozo, ushuru na ada mbalimbali tofauti zinazoingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali iweke bajeti ya kutosha kuboresha vituo vyetu 16 vya kilimo kwa kuongeza vifaa vya kazi na nyenzo mbalimbali. Makutupora wamalizie kuwekeza katika vifaa vya *tissue culture*, tuwekeze kusindika mazao yetu nchini badala ya kusafirisha mazao ghafi kama korosho, kahawa, pamba mbaazi mikunde na kadhalika. Serikali kupitia *ASA* na vituo vya utafiti, wapewe bajeti ya kuagiza miche ya matunda ambayo tunaweza kuzalisha nchini kama *(apple, peas, plums, citrus, grapes)* hata jamii ya michungwa, embe, nanasi, zabibu zikiletwa chache, tutazalisha nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iondoe au kupunguza kodi, tozo, ushuru na ada nyingine katika sekta ya kilimo ikiwemo kodi ya ardhi, malimbikizo makubwa mfano; ni *VAT*, *Income Tax, Withholding Tax, Land Rent*, *OSHA*, *Fire Rescue, TBS, TFDA, Weights and Measurements, WCF* na nyingine nyingi, uzalishaji nchini inakuwa gharama kuliko kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kuondoa kodi kwenye kuagiza *(Importation)* kwa mitambo ya kuchimba maji *(Borehole drilling equipment)* pamoja na mitambo ya kuchimba mabwawa ya kuvunia maji *(Excavators, Bulldozers, Shovels Rollers)* itasaidia kupunguza gharama za uchimbaji visima na mabwawa kama ushindani utakuwepo kutokana na mitambo kuwa mingi. Tutoze kodi kwenye kazi na siyo *Importation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nasisitiza iongezwa Sh.50 kwa maji vijijini na kuundwa kwa Wakala wa Maji Vijijini. Nashauri tuondoe kodi ya pampu za sola za maji *(Solar water*

*pump)* ili kuondoa adha ya akinamama kuchota maji mbali na makazi yao pamoja na kupunguza gharama za kusukuma maji kwa kutumia mafuta ya *diesel* na umeme kwa miradi midogo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugani wa madawa ya mimea na mifugo pia zitolewe na makampuni yanayouza hayo madawa. Serikali iondoe kodi kwenye madawa, chanjo vifaa tiba vya mifugo na chakula cha mifugo *(Supplements)* na kurudisha *VAT* kwenye chanzo cha mifugo ili waweze kupata unafuu wa kupata *taxes.*

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyotekeleza majukumu yake. Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mawaziri wote na Watendaji wote wa Serikali kwa kuwa na *sense of duty.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha chai; zao la chai ni zao ambalo lilikuwa linaingiza fedha nyingi za kigeni miaka ya 1970 na kabla ya miaka 1990. Mfano, chai ya Lupembe ipate soko kubwa na ikawa namba moja kwa ubora duniani. Katika miaka ya hivi karibuni baada ya kukaribisha wawekezaji uzalishaji ukapungua na kupelekea kupoteza soko lake. Hii ni kutokana na kutokuwa na usimamizi mzuri wa zao hili. Tunaomba Serikali ione umuhimu wa kusaidia kufufua zao hili kwani kwa Mikoa ya Njombe, Mbeya na Tanga zao hili huajiri watu wengi sana mashambani na viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Serikali kufuatilia uzalishaji wa zao hili toka shambani mpaka sokoni, mchakato mzima toka uhudumiaji wa shamba, uchumaji, namna biashara inavyofanyika toka kwa mkulima na wenye viwanda na uzalishaji wa majani mabichi, kwa majani makavu na hatimaye soko lake la nje. Ilivyo sasa wakulima wadogowadogo wanadhulumika sana kupitia mizani wanayopimia mashambani. Chai ikizalishwa zaidi ya mahitaji ya viwanda, wakulima wanaambiwa chai ni chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya chai. Bado bei elekezi ni ndogo sana, hivi karibuni bei iliyotangazwa ni ongezeko la Sh.35 hivyo kupanda toka Sh.230 mpaka Sh.250 na Sh.265 mpaka Sh.285 kwa majani mabichi. Bei hii haimnufaishi mkulima, gharama za uzalishaji ni kubwa kuliko gharama za kuzuia majani mabichi. Kwa sasa hivi, gharama za kuzalisha kilo moja ya majani mabichi takriban au wastani wa Sh.400 mpaka Sh.450 lakini bei ya kuuzia majani mabichi ni Sh.230 mpaka Sh.250. Bei hii ni bei nyonyaji kwa wakulima. Naomba Serikali hasa Wizara ya Kilimo kusimamia na kufuatilia bei ya zao hili la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya kuelekea kwenye maeneo ya uzalishaji chai. Barabara zinazoelekea kwenye mashamba ya chai ni mbovu sana, barabara hazipitiki wakati wa mvua. Hii pia inachangia kupoteza ubora wa chai. Zao hili la chai huzalishwa kwa wingi wakati wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu ili kupata ubora wa zao hili barabara zilitakiwa ziwe nzuri lakini mara nyingi zimekuwa hazitengenezwi. Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na mfuko rasmi wa barabara za maeneo ambako chai inazalishwa kama ilivyokuwa zamani, wakati wa Mamlaka ya Chai, barabara za mashamba ya chai zilitengenezwa na fedha kutoka *World Bank* na ndipo chai ilipopata ubora mzuri katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea. Bado kuna tatizo kubwa katika usambazaji wa mbolea. Mfano, katika Mkoa wa Njombe bei ya mbolea pamoja na kutangaza bei elekezi bado kumekuwa na ujanja ujanja wa mawakala wadogo wa mbolea. Kilichotokea mbolea hizi zilifika kwa wakati katika Miji ya Njombe na Makambako na zimekuwa zikiuzwa kwa bei elekezi yaani Sh.44,000 *(CAN)*, mpaka elfu Sh.52,900 *(UREA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mbolea hizi hazijawahi kupelekwa vijijini na kuuzwa kwa bei hizo, wafanyabiashara wanasema hawawezi kupeleka maeneo

ya Lupembe, Kichiwa na maeneo ya vijiji vilivyo nje ya barabara ya lami. Mbolea hizi zimekuwa zikiuzwa kwenye maeneo ya vijijini kwa bei zaidi ya ile bei elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi *UREA* ni Sh.61,000, wakulima wanatakiwa kununua mjini na kuisafirisha mpaka mashambani (vijijini) hivyo gharama kuongezeka mara dufu. Tunaiomba Serikali ipeleke mbolea hizi kwenye Makao Makuu ya Kata au Tarafa ili kuwarahisishia wakulima gharama kubwa za usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji. Tatizo la maji vijijini bado ni kubwa, mfano; katika Jimbo la Lupembe kuna zaidi ya vijiji 25 havina maji. Pamoja na Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuongoza Kitaifa kwenye usafi wa mazingira na vyoo bora lakini vijiji vyake havina maji safi. Njombe ni eneo ambalo limezungukwa na mito mingi na mito hii inamwaga maji yake katika Mto Rufiji, hivyo Njombe ni *catchment area* ya Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia eneo hili kutokana na kutokuwa na maji milimani ambako ndiko yaliko makazi yao hulima mabondeni, hivyo ili kulinda vyanzo vya maji katika Mkoa huu ni muhimu kuwapelekea maji wananchi hawa ili waanzishe bustani za mbogamboga milimani (kilimo cha umwagiliaji) tusipofanya hivyo mipango ya kuwa na miradi mikubwa hasa ule wa Rufiji utaathiriwa na kilimo cha mabondeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione umuhimu wa kuwapelekea maji safi ili iwe rahisi kuwashawishi wananchi kulima bustani zao milimani ambapo watatumia maji bomba kumwagilia bustani zao.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze taarifa ya Kamati, Mifugo na Maji. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ningeshauri Serikali kusaidia wananchi kupata soko au masoko ya mazao yao.

Ningependa kuishauri Serikali juu ya uwahishaji wa pembejeo kwa ajili ya kuendana na wakati wa uhitaji. Tunaposema tutaondoa umaskini pamoja na kuwapa uhuru wa kuzalisha na kuuza kwa faida ili kurudisha gharama zilizotumika wakati wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kupata matrekta badala ya kilimo cha mkono kisicho na tija kwa jamii kinachosababisha vijana wengi kukata tamaa na kukimbilia mijini kutafuta fursa na wanapozikosa hugeuka wahalifu. Ningeshauri Serikali kuangali upya juu ya Mto Ruvu kutumika kikamilifu katika umwagiliaji ili kuwakwamua wananchi hao kuondokana na lindi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali juu ya upigaji chapa mifugo kwani zoezi hili limeharibu soko la ngozi ambalo lilikuwa limeshamili sasa hivi limeporomoka ghafla badala ya ngozi za Tanzania kukosa ubora kutokana na chapa hizo. Nashauri Serikali kusaidia vijiji kuwa na majosho ya ng'ombe kama hapo awali miaka ya sabini ambapo uogeshaji ulifanyika kwenye majosho ya Serikali kwa kulipia ili kusaidia kupunguza vifo vya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali juu ya tatizo la maji ambalo ni lengo la Taifa kwani maeneo mengi ya Tanzania yana shida ya maji, hata yale ambayo vyanzo vyake viko bayana, ukiangalia utaona jinsi ambavyo wananchi wengi wanashirikiana na mifugo. Nashauri Serikali ifuatilie kwa karibu sana juu ya miradi ya maji ambayo inaendeshwa kwani inajengwa chini ya kiwango. Hivyo Serikali ifuatilie kwa karibu ili kuondoa pesa inayopotea. Nishauri kuwahisha fedha kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kutumika kwa wakati.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampeni ya kuchoma kambi, kuvunjwa mitumbwi na kuchoma nyasi, haiwezi kuandoa uvuvi haramu kwa sababu mwisho wa siku itatengeneza maskini wengi ambao maisha yao yote ni uvuvi na watavua kwa sumu au njia mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampeni ya kukata nyavu kutoka *double triple* kuwa *single*, haijafanyiwa utafiti, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika vina vyake haviko sawa. Ukiwafanya wavuvi wote kutega *single* watavua kwenye mazalia ya samaki na iwapo itakuwa hivyo zoezi lote hili ni kupoteza muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyavu ya *single;* iwapo itatumika maji marefu ile ya nchi 7", 8", 10" inaweza kukamata samaki wa robo kilo, kilo moja mpaka kilo 100. Utaratibu wa kupiga watu faini ovyo ni sawa na kuwaagiza wavuvi kutupa samaki kwenye maji kwa sababu samaki akinasa hufa pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu ya *single*; haiwezi kuvua maji marefu kwa sababu nyavu ina kina cha mita nne wakati ziwa lina kina cha mita 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu faini, zitumike sheria za uvuvi siyo sheria za mazingira kupambana na wavuvi.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba ya utekelezaji wa Kamati kama nilivyoainisha hapo juu. Tatizo la maji linazidi kuwa kubwa siku zinavyokwenda. Hii siyo kwa baadhi ya maeneo ya nchi bali kwa nchi nzima. Mfano katika Wilaya ya Arusha Mjini mahali ninapoishi tatizo hili limekuwa sugu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Njiro limekuwa na shida kubwa ya maji zinaweza zikapita hata wiki mbili au tatu bila kuona maji na wakati huo huo mvua zinakuwa zinanyesha. Nimeona kamati ilitembelea Mamlaka ya Maji *AUWSA* na kupewa taarifa kuhusiana na tatizo hili kama inavyoonekana katika ukurasa wa 45 -48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona niseme kuwa wahusika wa Mamlaka ya Maji Arusha Mjini hawakusema ukweli kwa Kamati kuwa tatizo kubwa la maji Arusha Mjini linasababishwa na tatizo la umeme. Hili alithibitisha Felix

Mrema mwaka 2015 wakati wananchi ilipobidi waandamane ili kuweza kujua nini hasa tatizo la maji katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya maji katika Jiji la Arusha kwa siku ni lita milioni mia moja, (1000,000,000) lakini kutokana na mgao wa umeme uzalishaji umeshuka hadi kufikia lita milioni arobani na tano tu (45,000,000) kwa siku ambapo katika eneo la Moshono (Kata) uzalishaji umeshuka hadi kufikia galoni 100 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana katika nchi kwa ujumla kwa upatikanaji wa maji, ikizingatiwa Mkoa wa Arusha kuna Mlima Meru sijui maeneo ambayo ni makavu kabisa ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu uvuvi haramu. Tunapata matatizo makubwa kama nchi kuhusu nyavu za kuvulia ambazo si rafiki kwa samaki zinazopelekea kuzaliwa uvuvi haramu. Niende mbele zaidi kwa kusema nyavu hizi ambazo si rafiki kwa samaki ni mara nyingi zinakamatwa na kuteketezwa lakini tatizo hili la nyavu haramu halijapata kamwe kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kwa kuwa wananchi wetu wanazipenda sana hizi nyavu na kupelekea wao kuingia hasara za mamilioni ya fedha kwani pindi wanapokamatwa zinateketezwa na kwa kuwa hawakomi wanaendelea kuzitumia kinyume na maelekezo ya Serikali. Basi sasa ni vyema Serikali yenyewe ichukue jukumu la kuingiza nchini nyavu za kuvulia na pia Serikali ichukue jukumu la kumiliki viwanda vya kutengeneza nyavu ili tuondokane na kuteketeza nyavu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu zinazoteketezwa ambazo ni haramu tunateketeza mabilioni ya fedha za wavuvi ambao ni Watanzania tunavuruga uchumi wa nchi.

Namalizia kwa kusema nyavu za kuvulia ziwe chini ya Serikali yenyewe, Serikali ihusike na utengenezaji na uagizwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili na utalii; naunga mkono taarifa zote mbili na mapendekezo yake yote. Migogoro ya hifadhi za akiba na wakulima itamalizika lini? Upo mgogoro mkubwa kati ya Hifadhi ya Uwanda na wananchi juu ya utata wa mipaka

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo ramani iliyokuwepo toka mwaka 1959 na ikafanyiwa marekebisho mwaka 1974. Cha ajabu ramani zote hizo zinapuuzwa na watumishi wa maliasili na kuingilia makazi ya wananchi. Naomba Wizara ifanye haraka kufanya makubaliano ya mipaka iliyowekwa Kisheria kwa kufuata ramani na siyo kukandamiza wananchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa wa Maliasili waliopo katika Hifadhi ya Akiba ya Uwanda hula rushwa na kuruhusu mifugo kukaa ndani ya hifadhi hiyo kwa kuwatoza wafugaji fedha kati ya milioni mbili na kuendelea bila kutoa risiti inakuwa ni fedha yao na haingii Serikalini. Majina ya Maafisa hao nilishayapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Maafisa wa Maliasili wamefyeka mazao ya mwananchi mmoja aitwae Langi Lusangija Nonga, kisa kukataa kutoa rushwa. Naomba Serikali ifuatilie suala hilo

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama wanaodhuru; tarehe 9 Januari, 2018 Mamba amekamata mwananchi aitwae Didas Chendelwa katika Mto Momba. Maafisa wa Maliasili wamejulishwa juu ya jambo hili hawajachukua hatua yoyote na mamba hao wanazidi kutishia maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; soko la mahindi linawatesa wakulima wa mahindi. Serikali imewatelekeza wakulima wa mahindi hawana kwa

kuuza mahindi yao. Leo hii Sumbawanga debe moja la mahindi ni Sh.3,500 hii siyo sawa kabisa. Serikali itueleze, je, hali hii itaendelea hadi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la pembejeo kuletwa kwa kuchelewa, uchache wa mbolea, bei kuwa kubwa ya pembejeo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima walipata ari ya kujihusisha katika kilimo hususan kilimo cha mahindi na alizeti katika Mkoa wa Iringa japo gharama za pembejeo ni ghali na wakafanikiwa kupata mazao hayo kwa wingi. Kitu cha kushangaza ni kutolewa kwa maagizo toka Serikalini ya zuio au uuzaji mazao yao hasa mahindi nje ya nchi na kuathiri wakulima hao kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweze kuruhusu wakulima hao kufanya biashara hiyo ya kutafuta namna ya kuwafanya wakulima hawa waweze kuendelea na kilimo kwani zuio hilo limeshusha bei ya mahindi hadi kufikia sh.6000 kwa debe moja gharama ambayo haitoshelezi hata ununuzi wa mfuko mmoja wa mbolea kwa gunia moja la mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa wanashughulika pia na kilimo cha nyanya na mbogamboga. Changamoto kubwa katika kilimo hiki ni ukosefu wa elimu hasa kwa wakulima kuhusu kilimo cha kisasa. Hii husababisha uzalishaji mdogo usio bora kwa zao hilo. Aidha, changamoto ya pembejeo na magonjwa ya nyanya, Serikali itoe elimu ya kilimo cha mazao haya na iyape kipaumbele. Itengwe bajeti ya kutosha kuwezesha shughuli za tafiti kwa ajili ya namna ya kutibu magonjwa ya nyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Wakulima walio wengi wanashindwa kukuza kilimo kwa kukosa mitaji. Benki ya Kilimo, *(TADB)* iliomba shilingi bilioni 800 lakini hadi Desemba, 2017 walikuwa na mtaji wa bilioni 66.7 tu. Hivi ukijiuliza watawafikia wananchi wangapi

kwa fedha hiyo tu? Naishauri Serikali iweke msisitizo katika upelekaji wa fedha katika benki hiyo kwani itawafikia wakulima walio wengi na kusaidia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Serikali iweze kutoa kipaumbele katika kilimo cha umwagiliaji kwani ndio utatuzi hasa pale ambapo kunakuwa na uhaba wa mvua. Ni asilimia ndogo sana inatumika kwa kilimo hiki, Serikali ikiweza kujenga mabwawa ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2017 mpaka Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu. Ili kutekeleza kwa vitendo Maoni na Mapendekezo ya Kamati, Serikali itoe bajeti ya kutosha ili itumike kwa muda sahihi kuweza kutekeleza mambo yote yanayojadiliwa na kupendekezwa katika Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge na iboreshe maghala ili kuweza kuhifadhi mazao ya nafaka sehemu salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze viwanda vya pembejeo za kilimo, madawa na mbolea nchini ili wakulima waweze kupata zana hizo kwa wakati na kuvitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutoharibu vifaa vya uvuvi mfano ngalawa ambazo si zana haramu katika uvuvi; hivyo visiharibiwe.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati kwa kazi nzuri ya kufuatilia kazi kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango. *T.F.C* ipelekwe Wizara ya Kilimo ili Wizara ya Kilimo iweze kuisimamia na kuifuatilia kwa karibu ili kuleta ufanisi wa kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo iweke utaratibu wa kukutana na wadau wote wa kilimo angalau mara mbili kwa mwaka ili kubaini matatizo na changamoto zinazokabili sekta ya kilimo. Pia, Benki ya Kilimo iongezewe mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji; kuwekwe utaratibu wa ufuatiliaji wa miradi ya maji kote nchini ili kuhakikisha vifaa na miundombinu ya maji vina ubora unaohitajika kwa mradi husika ili kubaini wakandarasi wasiofuata masharti na mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya mafuta iongezwe iwe Sh.100 ili kuongeza mtaji katika Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi; Serikali iharakishe ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli ya uvuvi.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais wetu ya kuwatua ndoo ya maji kichwani wanawake, ambayo Wizara imejipanga kuifanyia kazi lakini itachukua muda mrefu kufikia vijijini ambako wananchi wengi wazalishaji wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kukubali ushauri wa Sh.100 kwa lita ya dizeli na petroli, kwa ajili ya Mfuko wa Maji Vijijini. Kwa sasa na kuelekeza nguvu zaidi ya utekelezaji wa ukamilifu wa miradi ya maji kwani hata vyanzo vya maji vipo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ushauri huu wa Sh.100 utekelezwe ili kuharakisha kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais ya kuwatua ndoo wanawake. Ukimtatulia tatizo la maji mwanamke utakuwa umeitatulia jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Maji zinasisitiza umuhimu wa uwakilishi wa mwanamke ndani ya Kamati hiyo. Tunashauri kuanzishwa na kamati za kutunza vyanzo vya maji vijijini zenye ushirikishi wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwepo na ufuatiliaji na uthamini wa vyanzo hivyo na kuviweka katika madaraja ya ushindani ambako kutahamasisha utunzaji wa vyanzo na kuwa endelevu. Tutaepukana na ukosefu wa maji na wananchi watapata maji safi na salama kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndilo tegemeo letu hapa nchini kwa ajili ya upatikanaji wa bidhaa ndani ya viwanda vyetu vya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea kuchambua na kuona namna ya kuteremsha bei na kuboresha utaratibu rafiki zaidi kwa wakulima wetu katika upatikanaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuona umuhimu wa kuongeza Maafisa Ugani wa kukidhi mahitaji na kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri tunavyojipanga kuboresha kilimo na kuzalisha kwa ziada na kuingiza kwenye biashara na kukosa soko kutokana na nchi zinazotuzunguka nao kuanza kuzalisha hayo mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wataalam wa uwekezaji kuona utaratibu wa kukinzana na hali ya wakulima kuhangaika na mazao yao na kuona kilimo ni tatizo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati kwa kuwasilisha hoja nzuri na zenye tija na Serikali ichukue hoja hizo na izifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia uti wa mgongo wa Taifa hili ina maana umezungumzia kilimo. Naomba niishauri Serikali iwekeze kweli kweli kwenye kilimo kwani ukizingatia zaidi ya asilimia 75 ni wakulima. Kwa hiyo Serikali ipeleke pesa za kutosha katika sekta hii ya kilimo na ukizingatia sekta hii ikikaa vizuri hata vijana wengi hawatakimbilia mijini zaidi ya kubaki vijijini na kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inaweka miundombinu, hasa kujenga mabwawa ili wakulima walime kilimo cha umwagiliaji. Serikali iongeze Maafisa Ugani katika kila kata na kuwapa vitendea kazi pamoja na kuwashirikisha Maafisa Maendeleo ya Jamii ili waweze kuwapa elimu ya kilimo wananchi waliopo vijijini, ndiyo maana inafikia hatua wanauza ardhi ili wahamie mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukifanya hivyo hawatauza maeneo yao. Pia kuwapatia pembejeo wakulima kwa wakati hata wale wakulima wa mbogamboga na matunda, kwani hii tutakuwa tumeinua kilimo na wakulima hawa watalima kilimo chenye tija na kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maji; ukizungumzia maji katika nchi hii kila mtu atakuunga mkono kwa asilimia mia moja, lakini yote haya yanafanywa na watendaji wetu ambao si waaminifu katika sekta hii. Kwa hiyo niishauri Serikali kuwe na Mamlaka ya Maji Vijijini kama ilivyokuwa *TARURA.* Hii itasaidia sana hata wale watendaji wetu wasiokuwa na nia nzuri na nchi yetu hawatapata nafasi tena ya kuchakachua miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto kuna mito mingi sana inayotiririsha maji kutoka milimani na kuelekea baharini, lakini tukitumia kwa kujenga mabwawa hii itasaidia sana kwa wananchi wetu kupata maji safi na salama pamoja na kutunza vyanzo. Hata hivyo unakuta maeneo kama Lushoto kunakuwa na shida kubwa ya upatikanaji wa maji safi na

salama na yapo maeneo mengi tu yenye mito na vyanzo vya kutosha lakini mito hii haitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzipongeza Kamati zote kwa kazi nzuri ya kutoa taarifa ya utekelezaji kuhusu kilimo, mifugo na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa, nchi yetu ilishiriki katika Azimio la Abuja la tarehe 30 Novemba hadi tarehe Disemba Mosi, 2006. Katika Azimio la Abuja kulikuwa na makubaliano kuwa nchi zitenge angalau asilimia 15 ya bajeti za nchi zao katika kilimo. Sisi Tanzania bado tupo chini katika kufikia azimio hilo kuhusu kilimo. Kama ilivyobainisha Taarifa ya Utekelezaji ya Kamati, ukurasa wa sita na saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya nchi za Afrika zikiwemo nchi za Rwanda, Botswana, Nigeria, Malawi, Zambia na Burkina Faso wameweza kutenga bajeti zao za kilimo zaidi ya asilimia 15 ya bajeti zao. Wenzetu Rwanda wameenda mbali zaidi kwa kutenga asilimia 18.8 ya bajeti yake kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaingia katika uchumi wa viwanda na viwanda hivi vinahitaji malighafi itokane na mazao ya kilimo. Je, kwa bajeti ambayo haifiki asilimia 10 tutaweza kufikia huo uchumi wa kati wa viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda kuishawishi Serikali kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ili kuleta ufanisi katika kilimo na kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo cha umwagiliaji ni miongoni mwa nyenzo muhimu zinazoweza kuleta mapinduzi ya kijani. Suala la utegemezi wa mvua haliwezi kutuvusha kwa jinsi tunavyotaka mapinduzi ya kilimo kwa haraka. Tumeona jinsi mvua zilivyoleta maafa na

mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini. Iwapo ungekuwepo utaratibu wa kitaalam wa kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua yangeweza kutumika kwa umwagiliaji na hatimaye yangeleta tija. Naishauri Serikali yangu sikivu na Tukufu kuona unafanyika utaratibu wa kuhifadhi maji ya mvua ili yaweze kutumika kipindi cha baadaye na hata ikiwezekana katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utoaji miche ya mikorosho katika Mikoa ya Kanda ya Kati, Dodoma na Singida. Naipongeza Serikali kwa kutoa miche ya korosho. Nashauri ufanyike uhamasishaji wa kutosha kabla ya kipindi cha mvua, ili wananchi waweze kuandaa mashamba ya kupanda miche hiyo. Nashauri miche ya mikorosho itolewe mapema ili wananchi waweze kupata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa bei elekezi kwa wakulima wakati pembejeo zinauzwa kwa bei ya juu mfano, mbolea ya *DAP* Sh.60,000/= na Urea ni Sh.50,000/= siyo sahihi kabisa. Wananchi wamehamasishwa kulima mazao mbalimbali lakini bei za mazao hayo iko chini sana. Mahindi yanauzwa hadi Sh.3,000/= mpaka Sh.5,000/= kwa debe. Kwa kweli hii inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione ni namna gani itawatafutia soko la uhakika la mahindi na mbaazi na kushusha bei ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo na asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima, lakini Wizara hii haipewi bajeti ya kutosha itakayosaidia kuleta pembejeo za kutosha na kwa wakati. Naiomba sana Serikali itenge bajeti ya kutosha na kuitoa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, naiomba Serikali ione ni namna gani inatenga maeneo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ng'ombe wanazagaa ovyo ovyo kwenye maeneo ya wakulima, watu wamekuwa wakiuana. Naishauri Serikali ifanye haraka kutenga maeneo, mfano nimeshuhudia wakulima na wafugaji wanapigana pale Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo kulingana na changamoto hii, imekuwa ikiwaathiri wakulima wengi kulingana na changamoto ya bei ya pembejeo yenyewe, upatikanaji wake, kwani suala hili linawaathiri sana wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha umwagiliaji; pesa nyingi zimepotea katika mabwawa. Suala hili haliwezi kufanikiwa, kwa sababu bado ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti ni muhimu sana ili tuweze kuinua kilimo chetu kuwa chenye tija kwa kuwa utakuwa umefanyika utafiti kuwa wapi panafaa na panafaa kwa kilimo gani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la soko limekuwa changamoto kubwa kwa wakulima wengi nchini ikiwemo watu wa Mkoa wa Rukwa ambao wanalima mazao ya chakula, lakini Serikali ilitoa tamko au katazo juu ya wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi wakati huo Serikali imeshindwa kuwatafutia soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa bei elekezi kwa mbolea zinazopelekwa mikoani ikiwemo Mkoa wa Rukwa. Suala hili limeshindwa kutekelezeka kwani suala la barabara limekuwa linachangia bei elekezi, haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na uzoefu ambao tumekuwa nao, suala la wakulima wetu kusubiri msimu wa kilimo, ni vyema Serikali ikajenga mazingira rafiki kwa wakulima kuwa na kilimo cha umwagiliaji.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Waziri, viwanda vya mbolea vya Kilwa, Lindi, Mtwara na Kibaha ni lini vitaanza kujenga, kukamilika na kutoa mbolea. Namna hii tutapunguza tatizo la mbolea Tanzania.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa kuchangia Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati za Kudumu za Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wote kwa kuandika na kuichambua na kuiwasilisha kwa umakini mkubwa katika Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia taarifa hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni miongoni mwa vitu ambavyo ni tegemeo kubwa kwa wakulima hasa wakulima wa kipato cha chini. Hivyo naungana na ushauri wa Kamati juu ya Serikali kuipatia benki hii uwezo wa kila aina ili iweze kuwavusha wakulima katika azma zao za kilimo chenye faida. Aidha, kwa kuwa Serikali yetu inaelekea kwenye uchumi wa viwanda, lazima tujue kwamba msingi mkubwa wa kuendesha uchumi wa viwanda ni kilimo chenye manufaa. Hivyo, kuiwezesha Benki hii kutupeleka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi ni moja katika sekta muhimu katika nchi yetu na ulimwenguni kwa jumla. Sehemu kubwa ya wananchi wetu ni wavuvi, lakini bado wavuvi wa kipato cha chini hawajaweza kutimiziwa haja zao na Serikali kwa kuwapatia nyenzo za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika Sekta hii ya Uvuvi ni kwamba Serikali iwapatie zana za uvuvi kama vile mashine na mitego ya kisasa ili waweze nao kuepukana na kuvua kizamani. Aidha, Serikali iendelee kuwaelimisha wavuvi hawa namna bora ya uvuvi ili kuepuka kuvua kwa mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni vyema Serikali (Wizara ikawa inatoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge, kuliko ilivyo sasa, fedha kidogo inayotolewa na Serikali katika hizi Wizara ambazo zinatoa ajira kubwa kwa Watanzania. Pia nashauri Serikali iongeze bajeti katika Wizara hizi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa kawaida ya Serikali kutotekeleza ushauri na maagizo yanayotolewa na Bunge lako Tukufu kila mwaka, kwani mapendekezo yamekuwa yanajirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mbolea kutofika kwa wakati. Vile vile kutokuanza kwa uzalishaji wa mbolea katika viwanda vyetu viwili vya Kilwa na Mtwara pamoja na malighafi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo kuongezewa mtaji na kufungua matawi kwenye maeneo ya kilimo kuliko hivi sasa kwamba matawi mengi yako Mjini. Pia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo apewe nafasi kubwa katika kuendesha benki hii kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuongeza tozo kwenye Mfuko wa Maji hadi Sh.100/= kwa lita ya petroli na dizeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na mahusiano kati ya Wizara ndani ya Serikali ili kutekeleza dhana ya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uvuvi. Hapa pana ajira kubwa, Serikali inatakiwa kuacha tabia ya kuharibu zana za wananchi wanyonge badala yake ishughulike na viwanda.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu umuhimu wa Sekta ya Kilimo ambapo zaidi asilimia 57 ya wananchi wa Tanzania wanalima na kufuga na pia katika suala la ukuaji wa uchumi kwa mazao ya biashara na chakula, mfano zao la korosho ambalo leo Tanzania ni wanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wa kilimo katika Taifa hili kwa zaidi ya asilimia 28 katika pato la Taifa, lakini leo wakulima bado hawapati faida na mazao yao na hivyo wanufaika wakubwa wamekuwa wafanyabiashara wa mazao zaidi ya wakulima maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaweka mifumo mizuri ili wakulima nao wafaidike na mazao yao nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali kusambaza mbolea mikoani, lakini bado imeshindwa kwa asilimia kubwa kusambaza kwa wakati. Kwanza mbolea inasambazwa kwa kuchelewa na ikifika, wakulima wanapata mbolea wakati tayari kipindi cha kuweka mbolea kwenye mazao kimepita? Je, Serikali haioni kwamba kila mwaka inashindwa kusambaza mbolea? Nini mkakati wa kusaidia jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mbolea zinafika chache kwa wakulima. Tatu, bei ya mbolea ni kubwa sana, wananchi maskini ambao ni wakulima wa mikoani (vijijini) wanashindwa kununua mbolea hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, natumizi na elimu kuhusu mbolea hizi zinazotolewa, lakini ni lini wakulima watapatiwa elimu ya kutosha ili wapate mazao mengi na faida? Lingine ni mfumo wa ugawaji mbolea, pia una urasimu mkubwa; lini utakwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa iliyopakana na nchi jirani kuna hili tatizo la mbolea *fake.* Mfano Mikoa ya Mbeya, Katavi na Kigoma. Ni lini Serikali itasimamia mbolea *fake* inayopita mipakani ili kusaidia wakulima ambao wengi wao wananunua mbolea *fake* hizi ambazo ni bei rahisi? Nini Tamko la Serikali katika jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi Jimbo la Nsimbo, Mpanda Mjini na Tanganyika ni maeneo ambayo tumbaku inalimwa, lakini bei ya tumbaku kwa wakulima hawa ni ya dhuluma. Walanguzi wamekuwa wakipanga bei wao na kuacha wakulima maskini hawapati faida. Nini tamko la Serikali kuhusiana na wizi huu wa bei ya zao la tumbaku unaofanywa na walanguzi wasio waaminifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini; ni kwa nini Serikali inashindwa kutenga maeneo ya malisho nchini ili kupunguza kesi katika Mahakama kwa migogoro hii mikubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maoni ya ushauri wa Kamati, nashauri Serikali itenge maeneo ya malisho ili kuondoa malalamiko ya wafugaji; ng'ombe zao kupigwa risasi zikiingia kimakosa hifadhini, mfano, Kata ya Majimoto, Luhafwe na Ikuba. Je, ni kwa nini Askari wa Wanyamapori wanapiga risasi ng'ombe kwa maelekezo ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya? Ni lini Serikali itaacha uonevu huu kwa kushindwa kutatua matatizo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Tanganyika zoezi la kudhibiti uvuvi haramu katika ziwa hili, limesababisha uonevu mkubwa kwa wananchi. Ni kwa nini hamwoni haja ya Serikali kuwapatia nyavu zenye bei rahisi kwa mikopo

katika vikundi vyao na kuwasimamia ili kudhibiti uvuvi haramu na siyo kufanya zoezi la kudhibiti uvuvi haramu huku wavuvi hawajiwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hakiwezi kutegemea mvua tu. Naomba Serikali ipitie bajeti yake kwa upya na kuhakikisha inaharakisha kumaliza miradi ya maji kwa muda muafaka. Vile vile nashauri Serikali iendelee kutekeleza miradi hii kwani Serikali inapata hasara na wakulima hawapati faida.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze MVIWATA kwa kazi kubwa wanayoifanya kutoa ushauri, elimu kwa wakulima hapa nchini. Pamoja na hayo, niombe Halmashauri zetu kuunga mkono kazi wanayofanya kama vile kuunda vikundi vya umoja, kujenga masoko ya kuuzia mazao yao. Hivyo, nishauri Serikali kuunga mkono juhudi za MVIWATA kwa kutatua changamoto zilizopo hivi sasa kama ifuatavyo:-

(i) Kurejesha kwa wakati gawio la ushuru wa asilimia 35 wa kuendesha shughuli za masoko kwani Halmashauri nyingi hazirejeshi;

(ii) Kukarabati barabara za vijijini zinazokwenda kwenye masoko;

(iii) Kuzuia wakulima kuuza mazao yakiwa shambani;

(iv) Kuzuia mazao yanayozidi kilo 100 kama vile rumbesa;

(v) Kupunguza kodi ambazo ni utitiri kwenye vikundi vya *SACCOS* ambavyo vinaendesha masoko;

(vi) Kuweka ulinzi kwenye njia za panya wanazotorosha mazao bila kulipa ushuru.

(vii) Kupeleka mbolea kwa wakati;

(viii) Serikali itoe elimu kwa vikundi vya MVIWATA; na

(ix) Kujenga viwanda vya kuchakata mazao.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono taarifa hii ya Kamati, naomba kutoa yangu katika kusisitiza haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kilimo cha matuta. Bado Serikali haijasimamia vya kutosha kilimo cha matuta kwenye sehemu za miinuko ili kuzuia upoteaji wa maji na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni matumizi ya mito. Serikali haijafanya juhudi kubwa kuweka ramani ya mito yote tuliyonayo Tanzania na kuona jinsi inavyoweza kutumiwa kikamilifu. Kwa mfano, Jimbo la Same Mashariki tuna mito mikubwa minne, lakini mito yote inaenda baharini na wakati huo huo inapita porini bila kunufaisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimeuliza maswali Bungeni pamoja na kuandika barua Wizara ya Maji na Umwagiliaji nikiomba Jimboni kwangu mito hiyo itengenezewe miundombinu ya mabwawa ya kukusanya maji na ya umwagiliaji. Wizara imelifumbia macho jambo hili. Je, usalama wa chakula utapatikana wapi kama hatutilii maanani kilimo cha umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maji ya Jimboni kwangu kutoka mito hiyo tajwa hayajatumiwa kikamilifu kwa ajili ya kupelekwa katika Mbuga ya Wanyama ya Mkomazi. Maji hayo yangeweza kupelekwa kwa njia ya mtiririko *(gravity flow)*, badala yake wanachimba visima ambavyo baada ya muda mfupi mabwawa hayo hukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ufugaji wa kisasa. Ufugaji bado umeendelea kuwa wa kienyeji sana. Ningeshauri

Serikali ianzishe Mashamba Darasa sehemu za wafugaji ili kuonesha ufugaji bora unatakiwa uweje. Jimboni kwangu wafugaji walitenga maeneo ili wafundishwe jinsi ya ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kukubali kuwa wangeanzisha Shamba Darasa hilo ni takribani miaka miwili sasa bado Serikali haijaweza kusaidia wafugaji hao. Inasikitisha kila mara Serikali inawataka wafugaji wapunguze mifugo bila kuweka idadi ya juu sana inayokubalika kwamba mfugaji mmoja anatakiwa kuwa na mifugo mingapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ubovu wa barabara za vijijini. Kilimo hakiwezi kuwa na tija kama barabara za vijijini hazikuboreshwa kutokana na ubovu wa barabara hizo. Wakulima wengi huuzia mazao yao mashambani na hivyo kupata bei ndogo sana. Hivyo, naunga mkono hoja kwamba bila barabara nzuri, bila maji ya umwagiliaji na bila kuwa na mifugo iliyoboreshwa nchi yetu haitaondokana na umaskini kwani uchumi wetu unategemea sana hizo sekta tajwa hapo juu.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ikisemwa mara nyingi kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na 75% ya ajira inapatikana katika kilimo na 100% ya chakula Tanzania inatokana na kilimo lakini Serikali bado haijawekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa 80% ya wakulima wetu wanatumia jembe la mkono ambapo mazao yanayopatikana ni machache ukilinganisha na wakulima wanaotumia zana bora na za kisasa katika nchi za wenzetu. Hivyo inahitajika Serikali yetu iwekeze katika kilimo kwa kuwapatia wakulima zana bora za kisasa na pembejeo na kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ianzishe utaratibu wa kuwalipa fidia wakulima pale inapotokea majanga kama ukame, wadudu/wanyama waharibifu, mafuriko au mvua zinazoangamiza mimea mfano mvua za mawe na

bei inaposhuka. Kwa kufanya hivi itawasaidia wakulima kupunguza hasara wanayopata kutokana na majanga haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali iweke matawi ya benki katika kila wilaya ambazo zinajishughulisha na kilimo. Kwa mfano, katika Jiji la Tanga ziwekwe benki katika maeneo yenye wakulima na wafugaji kama Kata za Tongoni, Kirare, Mzizima, Mabokweni, Chongoleani na Kiomoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kilimo cha umwagiliaji. Katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji (*irrigation schemes*) imekuwa ikifanya kazi pale inaposimamiwa na wafadhili lakini wafadhili wakiondoka tu, miradi hii yote inakufa au kuwa na hali mbaya. Serikali iangalie kwa umakini miradi hii kwa kuitengea fedha za kutosha ili hata pale wanapoondoka wafadhili, miradi hii iendelee kuwa na tija na faida kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, maji ni uhai na ni nyenzo muhimu katika shughuli za maendeleo kama kilimo, lakini hata mashine nazo zinahitaji maji. Miradi ya maji vijiji 10 kila Halmashauri inakwenda kwa kusuasua, fedha za miradi zinacheleweshwa sana na ni kidogo. Wito wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ipeleke fedha kwa wakati;

(ii) Katika miradi ya maji ipite/itumie Mamlaka za Maji zilizopo kwa kuwa wanaweka mitambo ya maji kwa uzoefu waliokuwa nao na wanategemea mtandao wa maji kama chanzo chao cha mapato kila mwezi kwa kupitia bili za kila mwezi; na

(iii) Serikali ianzishe miradi ya visima virefu na vifupi katika maeneo yenye ukosefu wa maji hususani katika vijiji ambavyo havikubahatika kupitiwa na miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, uvuvi ni sekta ambayo imeajiri Watanzania wengi katika maeneo/mikoa yenye maziwa na bahari. Tanzania ina ukanda mrefu wa bahari

kilometa 1,425 kutoka Jasini, Wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga. Wavuvi hawaelimishwi juu ya uvuvi bora na wa kisasa bali mara kwa mara wavuvi wanasulubiwa kwa kisingizio cha uvuvi haramu, wananyang'anywa mashua na majahazi, nyavu na vifaa vingine vya uvuvi na vinatangaziwa kuharibiwa/kuangamizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa kama nyavu vinatengenezwa katika viwanda vya hapa nchini na pia vinaingizwa kupitia mipaka na bandari zetu na Serikali inakusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii nashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali itoe elimu kwa wavuvi juu ya nyavu zinazofaa na ipige marufuku nyavu zisizohitajika kuingizwa nchini;

(ii) Serikali isiangamize/kukamata wavuvi na mali zao na kufanya *replacement* ya vifaa haramu dhidi ya vifaa halali ili tusijenge uadui kati ya wavuvi dhidi ya Askari wa JWTZ na *Coastal Zone*;

(iii) Serikali ianzishe vipindi vya redio na televisheni kutoa elimu ya uvuvi na mazingira; na

(iv) Serikali ianzishe Benki ya Wavuvi kama ilivyo Benki za Wakulima.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu suala la makokora. Zoezi la uchomaji moto nyavu za asili zenye macho madogo madogo linaathiri uchumi wa wavuvi wa dagaa ambao hawana uwezo wa kununua nyavu maalum za macho madogo za kuvulia dagaa. Serikali iwatambue wavuvi wa dagaa na iwasaidie kuwapatia nyavu hizo ili waepuke kutumia makokora badala ya kutumia mabavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee suala la kuzuia usafirishaji wa viumbe hai. Sasa ni zaidi ya miaka miwili

toka Serikali izuie usafirishaji wa viumbe hai kama mijusi, panzi na kadhalika. Zoezi hili linawaumiza wajasiriamali wa shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa tunaanza upande wa Serikali kwa ajili ya majibu. Mheshimiwa Hasunga dakika tano na Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII :** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa Kamati zote mbili kwa kuleta hizi taarifa na hasa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameitoa. Kwa sababu ya muda nitakwenda haraka haraka, najaribu kuchangia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezungumzia juu ya utunzaji bora wa misitu yetu. Ni kweli kabisa kwamba tumekuwa na changamoto nyingi sana zinazoendana na misitu na kwa ujumla hatuna mamlaka ya kusimamia misitu yetu yote. Sasa hivi utakuta asilimia 35 inasimamiwa na Serikali Kuu, asilimia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge tumezungumza kwa muda zaidi ya saa tatu mpaka nne na hoja zenu za msingi kabisa. Serikali inajibu, *no one pays attention.* Sasa naomba kila mtu akae kimya msikilize Serikali inapojibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba asilimia 35 ya misitu yote inasimamiwa na Serikali Kuu; asilimia 45 inasimamiwa na Serikali za Vijiji; Serikali za Mitaa zinasimamia 7% na watu binafsi wanasimamia 7%, *general land* ni 5% na mengineyo ni 1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali ya namna hii na kwa kuwa misitu ni kitu muhimu sana, lazima kweli

tuje na mamlaka moja ambayo italeta usimamizi bora wa misitu yetu na ndiyo maana Serikali tunakusudia kwamba sasa hivi tumepitia Sera ya Misitu iliyokuwepo na sasa hivi tuko katika hatua ya mwisho ya kuja na sera mpya ambayo pamoja na mambo mengine tunafikiria kwamba lazima tuwe na mamlaka moja ya kusimamia hifadhi za misitu yetu, ili angalau kuleta manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nilitaka nitoe ufafanuzi kidogo, Kamati imezungumzia juu ya migogoro mbalimbali pamoja na Wajumbe mbalimbali pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia sana kuhusiana na migogoro. Ni kweli kabisa kuna migogoro mingi katika maeneo mengi na hasa katika hifadhi zetu. Migogoro hii imesababishwa na mambo machache yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni ongezeko la watu. Ongezeko la watu sasa hivi, tuko karibu milioni 52 na zaidi. Wakati tunapata Uhuru tulikuwa milioni tisa tu; ardhi ilikuwa hii hii haijaongezeka. Kwa hiyo, hii imekuwa ni changamotio kubwa na imekuwa *pressure* katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kwenye uwekaji wa mipaka yetu katika maeneo mengine mengi Waheshimiwa Wabunge wamedai kwamba kulikuwa hakuna ushirikishwaji. Inawezekana ni kweli, lakini nataka niseme, mambo yaliyogundulika katika hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumegundua kuna vijiji 366 vimepimwa kwenye hifadhi, vimo kwenye hifadhi. Katika Misitu yote iliyopo, vijiji vilivyopo ndani ya misitu viko 228, hifadhi zenye migogoro ziko 191, wakati huo huo hifadhi zetu kama *TANAPA* kuna migogoro kama 21, *TAWA* kuna 23, Mali Kale kuna mmoja na migogoro mingine mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana baada ya kuona kuna migogoro mingi, Serikali ikaamua kwamba tuwe na Kamati ya Kitaifa ambayo inajumuisha Wizara kadhaa

kwa ajili ya kuja na ufumbuzi wa migogoro hii yote ambayo imejitokeza katika eneo moja. Kwa sababu, hii migogoro ni mitambuka, haihusu Wizara ya Maliasili peke yake, ni maeneo mengi.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba hii Kamati itakapokamilisha hii taarifa sasa, itakuja na mapendekezo mazuri kabisa ambayo yatapunguza kwa kiwango kikubwa migogoro ambayo ipo katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka nizungumzie, linahusu masuala ya mapito ya wanyama. Katika mapito ya wanyama, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia sana. Ni kweli kabisa, hifadhi zetu sasa hivi kwenye maeneo ambayo yalikuwa ni mapito ya wanyama, shoroba, zimevamiwa na wananchi kwa sababu ya ongezeko la watu na shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake kutokana na uvamizi huo, labda niseme kuanzia Oktoba, 2016 mpaka 2017, ekari zaidi ya 42,562 ziliharibiwa na wanyamapori kwa sababu walikuwa wanataka kupita katika maeneo. Maeneo yamevamiwa, watu wanashughulika na kilimo, kuna mambo mengi yakiendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa matokeo yake ekari kadhaa zimeharibiwa. Watu waliopoteza maisha mwaka mmoja tu 484; mifugo iliyopotea 191, fedha ambazo Wizara tunatakiwa kulipa kama kifuta jasho, siyo kama fidia, kama kifuta jasho ni zaidi ya shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mengine atamalizia Waziri wako. Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe, atafuatiwa Mheshimiwa Dkt. Tizeba.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuishukuru Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Katika muda wote ambao wamekuwa na Wizara yangu wamesaidia sana kubaini changamoto, kuishauri Wizara katika utendaji, lakini pia wametoa ushauri mzuri sana kwa upande wa Serikali katika hatua ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ili tutakapofika mwaka 2020 tufikishe maji asilimia 85 vijijini na asilimia 90 hadi asilimia 95 mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebainisha kuhusu mtiririko wa fedha. Nikiri kwamba, mtiririko wa fedha, hasa upande wa mfuko wa maji ni mzuri sana kwa sababu hadi kufikia Desemba tulikuwa tumeshavuka asilimia 50 na leo hii tena Hazina imetoa bilioni 14 kwa ajili ya kulipia hati za madai za wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji vijijini na mijini. Lakini Kamati ilibainisha pia kuhusu asilimia ya maji iliyopo upande wa vijijini kwamba ni asilimia 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Sekta ya Maji nchini tulibainisha kutekeleza miradi 1,810 hadi desemba tulishatekeleza miradi 1,466. Katika miradi hiyo 1,466 vituo vya kuchotea maji tumefikisha 122,635 na iwapo kama vituo vyote hivyo vingetoa maji sasa hivi tungezungumzia asilimia 81.5 kwa hiyo, tulikuwa tunakaribia kwenda asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya maeneo kukauka maji pamoja na mambo mengine, matokeo yake ni kwamba vituo vinavyotoa maji ni vituo 83,575 ndiyo sawa na asilimia 56. Vituo ambavyo havitoi maji ni vituo 39,060 sawa na asilimia 44. Lakini kwa kutambua hilo katika bajeti ya mwaka huu wa fedha tulionao Serikali imetenga shilingi bilioni 53.6 na fedha hii imepelekwa kwenye Halmashauri zote kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vituo ambavyo havitoi maji basi fedha hiyo inatumika ili kuhakikisha kwamba vituo vinatoa maji. Kwa hiyo, kama Halmashauri zote zitafanyakazi vizuri tuna hakika mpaka tunafika mwezi wa sita tutakuwa tumeshapandisha hadi kwenda zaidi ya asilimia 76, 77 na tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana kwa kuendelea kusimamia Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji na ndiyo maana sasa hadi tunafika Ijumaa waheshimiwa wabunge inabidi sasa tutoe *table* ambayo tunasambaza kwa wabunge wote katika mikoa ili waweze kujua katika Halmashauri yako ni vituo vingapi ambavyo havitoi maji. Ili tuweze kusaidiana kuzisukuma Halmashauri kwa sababu fedha zipo watumie fedha ile waweze kurudisha huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kweli ni kilimo muhimu ili tuweze kuwa na uhakika wa chakula. Mwaka 1970 Serikali ya Japan ilitusaidia kufanya *study* na ikabainisha kwamba nchi yetu ina zaidi ya hekta milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na katika hizo tulitengeneza *scheme* za umwagiliaji hekta 461,326 sawa na asilimia 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tumekutana nayo kwamba *scheme* hizi zilitengenezwa bila kufikiria sasa vyanzo vya maji ambavyo vinaweza vikafanya kwamba kilimo ili kilimwe mara mbili, mara tatu kwa mwaka. Kutokana na changamoto hiyo sasa hivi kuna *master plan* ambayo pia tumepata msaada kutoka Serikali ya Japan ambayo ilianza mwaka 2016 na tunatarajia tarehe 1 Julai watakuwa wamekamilisha kufanya *study* ya hiyo *Master Plan*. Ili sasa kuweza kuainisha *scheme* za umwagiliaji pamoja na vyanzo vya maji ili tutakapokuwa tumezitengeneza wananchi waweze kulima muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia Wakala Maji Vijijini, Bunge lilituagiza tukaunda sekretarieti na tayari Sekretarieti imefanya kazi na kuwasilishwa kwa wadau wa Wizara ya Maji na TAMISEMI na sasa hivi mwezi huu wa pili mwishoni hiyo taarifa itafikishwa kwa Mawaziri wa TAMISEMI na Waziri wa Maji na Umwagiliaji tuweze kuipitia na baadaye tupeleke sasa kwenye hatua nyingine lengo itakapofika tarehe Julai, basi Wakala huu utakuwa umeanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ya kimkakati, miradi ya kimkakati tuna Bwawa la Farkwa, tuna Bwawa la Ndembela Lugoda lakini pia tumeweka Bwawa la Dongo. Bwawa hili litajengwa katika halmashauri ya Kiteto ambayo litasaidia sasa kuvuna maji ya mvua zinazonyesha maeneo ya Manyara kuleta mafuriko Mkoa wa Morogoro, tunaanza kujenga mabwawa ili sasa hayo maji tuweze kuyahifadhi maeneo na yaweze kutumika kwa matumizi ya majumbani ambayo tuna uhakika baada ya bwawa hili maji yatakwenda Gairo, yatakwenda Kibaigwa na vijiji vya Wilaya ya Kiteto pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa tayari tumeshatangaza *tender* na sasa hivi tuko kwenye uchambuzi ili tuweze kumpata muhandisi mshauri atakayefanyakazi kwa haraka sana na malengo yetu ni kwamba bajeti inayokuja tuweke fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Tizeba dakita 15. Mheshimiwa Mpina ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kutupa nafasi kutoa maelezo kuhusu hoja ambazo zimetolewa na Kamati na Wabunge ambao wamechangia taarifa za Kamati zilizowasilishwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru sana Kamati yetu kwamba tumefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana, wametushauri mambo mengi na katika ushauri wao yako ambayo tuliyaacha na tukachukua ushauri kuufanyia kazi. Kwa hiyo, katika mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kimsingi yote yanakubalika na tutaenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie mambo manne na kama muda utatosha nitazungumzia na lingine la tano, lakini nataka nizungumzie suala la masoko ya mazao,

lakini pia tunavyokabiliana na wadudu na visumbufu vya mimea, jambo la uagizaji wa mbolea kwa pamoja na tatizo la uchakachuaji wa korosho iliyosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na tatizo la masoko ya mazao. Nimewasikiliza kwa uzuri sana Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia ukosefu wa soko la mazao hasa mahindi na mbaazi. Lakini pia nimemsikia Mheshimiwa Maige akizungumzia suala la ukosefu wa soko la tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli haya mazao kama yalivyo mazao mengine ambayo pia hayakuzungumziwa hapa ndani. Masoko yake siyo mazuri sana. Na masoko haya siyo mazuri kwa mazao yanayozalishwa Tanzania tu, labda hili ndiyo naomba tuelewane vizuri. Ni hata wazalishaji walio nje ya Tanzania wanakabiliwa na tatizo hili hili la masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Tanzania mahindi yameshuka bei mpaka shilingi 5,000 kwa debe, jirani zetu Zambia debe la mahindi liko shilingi 2,600; Malawi debe liko shilingi 3,100. Mwaka juzi mahindi yalipanda bei sana kwa sababu nchi zote zilizotuzunguka hawakuwa na uzalishaji kwa hivyo soko likabaki chanzo cha mahindi kikabaki ni Tanzania peke yake.

Kwa hiyo, suala sasa hivi la uwezekano wa kupandisha bei ya mahindi wakati majirani zetu wote wanayo mahindi yanayowatosha halipo. Misimu inatofautiana, kwa hiyo wanavyozalisha na wao hawawi tena na sababu ya kuja kwetu ndivyo hivyo hivyo ilivyotokea kwa mbaazi.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *traditional* soko la mbaazi la Tanzania ilikuwa ni India na wazalishaji wameendelea kuzalisha na wakiuza huko India miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la Waziri Mkuu wa India alipokuja hapa akazungumza *yes* watu waliamasika wakazalisha zaidi na kwa sababu bei ya msimu iliyotangulia ilikuwa kubwa uzalishaji ukaongezeka watu wakaenda benki, wakachukua pesa ili wazalishe mbaazi kwa ahadi kwamba watapata soko la uhakika ambalo wamelizoea, India imezuia...

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hebu subirini kwanza. Wote Aeshi, nani, Frank kaeni chini.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

**MWENYEKITI:** Kaa chini nimesema. Endelea Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO.** Kwa hiyo, soko la mbaazi la India limesabaisha ku-*distort* soko la mbaazi la ndani ya Tanzania, na hapa namshukuru sana Mheshimiwa Mgumba amelieleza vizuri tatizo la *commodities* zile, lakini pia nimfahamishe kwamba nchi ya India walisaini mkataba na Mozambique wa kununua mbaazi sisi waka-*deal dull* kumbe wakichungulia uzalishaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wao ulipokuwa mzuri kuliko walivyotarajia wakaweka mguu chini hawakutaka kusaini mkataba wa makubaliano na kule Mozambique ambako waliingia mkataba wamenunua tani 135,000 ya mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo masoko ya mazao twende kwenye tumbaku, tumbaku inazalishwa kwa mkataba.

**TAARIFA**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hebu tumuache Waziri.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Anapotosha Bunge.

**WAZIRI WA KILIMO.** Tumbaku inazalishwa kwa mkataba, baada ya mabishano ya bei kwenye *Tobacco Council...*

**T A A R I F A**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Anachangia, naomba nimpe taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya Gekul sema ulichotaka kusema.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Naomba Waziri atuambie nampa taarifa tu hayo maelezo tumechoka nayo, tuambie *strategy* kama wewe Waziri wa Kilimo kuhusu soko la mbaazi usituambie habari za India wala za maeneo mengine kama nchi kama Waziri uliaminiwa una mpango gani na soko la Mbaazi hatuitaji hizo *story,* zimetuchosha. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Sasa si ngoja apokee taarifa ya kwanza wewe atakujibu nini sasa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimwia Gekul sijui niikatae kwa sababu bila maelezo ya kilichotokea tutazungumza nini hapa. Sidhani kama hata ni utaratibu mzuri, lakini *anyway* ndiyo Bunge lenyewe lilivyo. Kwa hiyo, masoko haya...

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwakajoka, taarifa nilitangulia.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa tu taarifa Mheshimiwa Waziri na Bunge kwa ujumla kwamba Mheshimiwa Waziri analipotosha Bunge.

Suala la mahindi mwaka jana wakati tumeanza kuvuna mahidi yalikuwa shilingi 60,000 mpaka 65,000; 70,000 mahindi yamekuja kushuka bei baada ya Mheshimiwa Waziri kufunga mipaka. Amekuja kufungua tayari nchi nyingine jirani zimeanza kuvuna mazao kwa hiyo, asitake kulipotosha bunge kwa kusema uwongo kwamba mahindi yalikuwa bei iko juu. Mahindi yamekuja kushuka bei baada ya yeye kufunga mipaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala tu la uelewa kwa sababu ukielewa kwamba tuna misimu tofauti na kwa hiyo sisi uzalishaji wetu unatangulia na wengine unafuata huwezi ukaacha mahali ambako soko la ndani haliko *regulated* kwa sababu ya nanilii... Historia ya mwaka jana nadhani iko bado *live* kabisa kwenye vichwa vya Wabunge. Tulienda tukakubaliana kwamba tuache mahindi yaende nje baada ya miezi miwili Bunge hili hili ndiyo likaanza kusema kwamba...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri kuna taarifa nyingine.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri haya anayoyazungumza afike mahali kwamba ajue kwamba yeye ni Waziri wa Kilimo na anatakiwa kuhakikisha kwamba wakulima wanalima kila siku vizuri na wanapata soko. Wakati anazuia mipaka soko lilikuwa zuri sana. Ni kwa nini Serikali haifanyi utafiti kwanza kabla ya kuzuia masoko yetu ya ndani ili wakulima hawa wasiingine hasara na wasishindwe kulima kama ambavyo wameshindwa mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mwakajoka kwamba utafiti tunafanya na utafiti tuliokwishaufanya hatua tutakazochukua mwaka huu zitakuwa tofauti sana na hatua ambazo tumekuwa tumechukua miaka ya nyuma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA KILIMO** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, utafiti tulioufanya tutachukua hatua tofauti na hizi ambazo zinatufikisha kuvutana na Serikali na Wabunge. Soko la kahawa la Tanzania limeendelea kuwa duni kwa sababu ya mazingira ya kodi ambayo tunayo Tanzania ukilinganisha na nchi zinazozalisha kahawa...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kuhusu utaratibu kanuni ya 68 ikisomwa na kanuni ya 64(a).

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi 68 ngapi?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kanuni ya 68(1) ikisomwa na 64(a) Kanuni inasema bila ya kuadhiri masharti ya Ibara ya 100 inaendelea pale inasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anapotosha watu na anacheza na maslahi ya wananchi waliotuleta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tunaishi mipakani mpaka wa Kenya, Wakenya walikuwa wananunua mahindi, mahindi yanatoka mpaka Usukumani huku yanaletwa pale yamekamatwa yanaozea pale malori yamekuwa *ceased* na watu wamepata hasara halafu yeye

anasema mahindi Tanzania na nchi jirani yalikuwa yamelingana bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anawadanyanga Wabunge na acheza na maisha ya watu. Leo tunazungumza hivi tumbaku watu wamelima tumbaku, Tanzania hawanunui tumbaku watu wanataka kwenda kuuza Tumbaku wanazuiliwa tumbaku inaoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri kama hana taarifa asitoe taarifa za uongo na kucheza na maisha ya watu ambao ni asilimia 70 wa nchi hii ambao ni wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika tu kwamba Mheshimiwa Heche anasema nimepotosha Bunge, ninachokisema ni ukweli na ukweli huu kama haumpendezeshi masikio bahati mbaya. Mazao haya yana sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa hiyo, hatuwezi tukaicha sheria tukaenda na mambo ambayo hayana utaratibu. Kupeleka tumbaku Kenya kuna hitaji utaratibu wa sheria, utoroshaji wa tumbaku ni uvunjaji wa sheria...

**T A A R I F A**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwneyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mna mpango kutaka kumchanganya Waziri, acheni hayo mambo. Na kuhusu utaratibu vilevile, Mheshimiwa Heche kwa mujibu wa kanuni zetu ulikuwa wewe ndiyo useme ukweli ni upi. Siyo yeye, kwa hiyo sasa mwacheni Waziri ajibu. Muda wake umebaki muda mdogo sana, akishajibu kiti kitafanya nini, endelea.

**WAZIRI WA KILIMO**. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nazungumzia habari ya masoko ya mazao,

*commodity markets* ziko *volatile* dunia nzima na siyo Tanzania peke yake kwa hiyo ikitokea hizi *fluctuation za* bei *fluctuation* za nini siyo kwa sababu nchi hii ni Tanzania, hili ni jambo ambalo sasa hivi lina *affect* dunia nzima uliza nchi yoyote bei za mazao zimeporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tunavyokabiliana na wadudu. Ni kweli suala la *worms* lilijitokeza mwaka jana na sisi tulitoa taarifa kwa umma namna ya kuwatambua na namna ya kudhibiti wadudu hawa. Bahati mbaya sana wadudu hawa wamekuwa wanafanana na wale viwavijeshi tuliowazoea, kwa hiyo, watu wakadhani kwamba wataporomwosha tu na mvua ikinyesha, hawakuchukua hatua. Serikali ilichukua hatua ya kupita mikoa yote ambayo ilikwishaonekana wadudu hawa wapo, kutoa mafunzo na kuelekeza wananchi namna ya kukabiliana na *...worms,* lakini wameendelea kuzaana hivi hivi. Sasa hivi kuanzia wiki wiki hii tutapeleka dawa kwenye Halmashauri ambazo Mikoa yote imekuwa-*affected* na hawa wadudu ili halmashauri zigawe hizi dawa kwa Wananchi wapulize kwenye mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo liko kwenye pamba kuna wadudu, funza na utitiri, wamekuwa wanashambulia pamba lakini tuseme tuu kwamba dawa imekwishapatikana fedha tuliyokuwa tunahitaji tumepata dawa imenunuliwa inaendelea kusambazwa na Bodi ya Pamba, nilikuwa huko mwenyewe jana, kwa hiyo, tatizo hili nalo tutakabiliana nalo kwa wakati.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu naona hujaulinda?

**MWENYEKITI:** Muda wako?

**WAZIRI WA KILIMO:** Walikuwa wanaingilia muda.

**MWENYEKITI:** Wewe endelea tu Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Nihurumie Mwenyekiti.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo wale kwelea kwelea wanaoharibu mazao Shinyanga na Simiyu, upuliziaji kwa ndege utaanza lakini pia dawa kwa ajili ya panya walioko kwenye maeneo ya Handeni, Morogoro, Ifakara, Mlimba na Chalinze na kwenyewe dawa imepatikana tutapeleka kule, ili Halmashauri zikasimamie uteketezaji wa hawa panya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja. Huu mfumo una tatizo la msingi la kwamba unanyang'anya faida kwa baadhi ya wafanyabiashara waliozoea kupata faida kubwa. Kwa hiyo, lazima yatengenezwe mazingira ya kuonesha kwamba mfumo huu haufanyi kazi vizuri na sisi tunachokifanya ni kukabiliana na hayo ambayo yanajitokeza, wakati tunatekeleza mfumo wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekti, Kamati imesema kwamba lengo halikufikiwa; jibu ni ndiyo na hapana kwa sababu yako maeneo ambayo bei ilikuwa kubwa sana mbolea tuliyoiagiza kwa ile awamu ya kwanza ilikuwa ya bei ya chini kulinganisha na bei iliyokuwapo kwenye maeneo hayo. Sasa hivi bei ya Urea imepanda katika soko la dunia hatuzalishi wenyewe Urea hapa kwa hivyo awamu ya pili ilipoagizwa imekutana na bei iliyopanda. Hata hivyo, *control* tunazoziweka ndio zinatuhakikishia kwamba mkulima hatauziwa kwa bei ya kinyang'anyi, tunaweka *mechanisim* ambayo itamhakikishia mkulima ananunua kwa bei himilivu, tukiacha hivi hivi ndio mfuko unakwenda mpaka shilingi 80,000; 90,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo suala la *BPS* limekutana na changamoto ya ufikishaji wa mbolea kwenye maeneo ya vijijini ambako miundombinu ya barabara iliharibika usafirishaji ukapanda bei. Kwa hiyo, wafanyabiashara wakawa wanashindwa kusafirisha na

kuuza kwa bei elekezi na sisi tulichukua hatua mara moja tukawaambia kuwa mikoa wafanye tathmini ya gharama halisi ili waweze ku-*adjust* gharama za kutoka kwenye Wilaya kwenda huko vijijini na jambo hilo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni habari ya korosho na uchakachuaji uliotokea. Taarifa tulizonazo, tatizo katika korosho halikuanza mwaka huu, limeanza mwaka jana kwa wafanyabiashara wa kutoka Vietnam. Uchakachuaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpina kwa dakika 10. Ajiandae Mheshimiwa Kigangwalla.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwa nafasi ambayo umenipatia, na nianze kwa kuwapongeza sana Kamati yangu hii Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo ambayo inaendeshwa na akina mama, nawapongeza sana kwa uendeshaji wa Kamati hiyo vizuri sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Dkt. Mary Nagu pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma ambaye ni Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa weledi wao mkubwa sana katika kutusimamia na kutuongoza kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, najua zipo changamoto nyingi sana ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na kwa dakika 10 haitatosha sana kuzijibu, lakini nijaribu kusema kwa kifupi kwamba Kamati hii yangu ambayo imewasilisha taarifa hapa chini ya Mwenyekiti wake, imezungumizia juu ya kushughulikia changamoto ambayo zinahusu viwanda vyetu vya maziwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu changamoto ya maziwa hapa nchini tunafahamu tatizo la uingizaji maziwa ambao leo imefikia zaidi ya kilogramu milioni 88 ya uingizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi na kusababisha

ushindani usio sawa katika Taifa. Tunafanya tathmini na tutapata majawabu. Lakini vilevile wamezungumza suala la Ranchi za Taifa *(NARCO)* kwamba tufanye tathmini tujue uwekezaji uliopo, tujue changamoto zilizopo ili tuweze kuja na mapendekezo sahihi ya namna bora ya kuwekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda Kamati hiyo tayari chini ya maagizo hayo hayo ya Kamati hii ilivyotuelekeza tukaunde Kamati na kamati hii imeshamaliza kufanya tathmini, kesho napokea ripoti ikiongozwa na Mheshimiwa Archad Mutalemwa *DG* Mstaafu wa *DAWASA* na kesho napokea taarifa hiyo na tutakapoipokea hiyo taarifa tutaenda mbele ya Kamati yetu kushauriana nayo au kama kuna *input* zingine ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu, nishukuru sana Kamati yetu imetupa msukumo mkubwa katika ukurasa wa 32 ya kwamba tuongeze bidii katika kupambana na uvuvi haramu, lakini tuongeze bidii katika kuhakikisha kwamba wale wanaotorosha samaki wetu mazao ya samaki, tunawadhibiti ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niihakikishe Kamati kwamba na Wizara yangu, tutahikisha hili tunalisimamia kwa nguvu zote, hizi ni rasilimali za Taifa, na rasilimali hizi haziwezi kuwa *shared* kwa ukanda. Rasilimali hizi zinakuwa *shared* kwa nchi nzima kwa hiyo kama Wizara, inayosimamia sheria ambayo zimepitishwa na Bunge hili, tutahakikisha kwamba hakuna kabisa uvuvi haramu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tutahakikisha hakuna mfanyabiashara atakayejihusisha na kuuza wala kusambaza zana haramu, hakuna kiwanda kitakachochakata samaki wasioruhusiwa, hakuna mtu yeyote atakayevua kwa kutumia nyavu haramu, lazima mali zetu tuzilinde kwa nguvu zote, na bila kumumunya maneno labda nitoe takwimu zilizopo kwa sasa hivi, tuko wapi katika rasilimali hizi za uvuvi, ukizungumzia Ziwa Victoria…

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Waziri asichenge maswali yaliyoulizwa na Wabunge, hakuna Mbunge anayetetea uvuvi haramu, *concern* yetu sisi hapa ni kwamba kwa nini unachoma nyavu zilizo halali na nina ushahidi wa kutosha kwamba sasa huruhusu kabisa hata dagaa kuvuliwa, utuambie nyavu zilizo halali ziko wapi, tununue tukavue?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi natoa majibu hapa kwa maelekezo yake yeye au natoa majibu kwa mpangilio ambao ulioko hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndio naanza kujibu tu sijafika hata mbali, anisubiri asikilize vizuri ninavyozungumza hili ni Bunge, mimi ni Mbunge na yeye mwenzangu huyu ni Mbunge, anisikilize vizuri. Sasa sijamaliza hata kuzungumza sijamaliza hata sentesi.

Mhesimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kusema kwamba takwimu kwa sasa hivi katika Ziwa Victoria, linasema hivi, samaki ambao wanaruhusiwa kuvuliwa, sangara, ambao ni sentimita 50 mpaka sentimita 85 wamebakia asilimia tatu tu, kwa hiyo hata uvuvi huo tunaouzungumza hauwezi kuwepo kama uvuvi haramu huu tutauruhusu. Samaki wazazi katika Ziwa Victoria wamebaki asilimia 0.4 huna wazazi, huna ziwa, huwezi kuvua samaki ambao leo sasa ambao ni wachanga na ndio wanaovuliwa, wachanga wasioruhusiwa, chini ya sentimita 50, ni asilimia 96.6.

Kwa hiyo, kwa mantiki hiyo hatuna samaki wanaofaa kuvuliwa katika Ziwa Victoria, Kamati imezungumza juu ya

viwanda kufungwa tulikuwa na viwanda 13 hapa viwanda 13 vilikuwa na uwezo wa kuzalisha tani 1,065 leo tumebakiza viwanda nane na viwanda nane hivyo vina uwezo wa kuzalisha tani 171 tu. Sababu ya kukosekana kwa rasilimali hizi za uvuvi, samaki hawapo wamekwisha kutoweka kwa sababu ya uvuvi haramu, watu wanavua mpaka mayai, watu wanavua mpaka wachanga wale, utapata wapi samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zilikuwa 4000 na kitu leo ni 2000 tu katika ziwa letu hilo la Victoria, lakini nataka niseme hii *operation* ambayo inayoendelea na kama Waziri niliyeapishwa kusimamia rasilimali hizi kwanza niweke kabisa wazi msimamo wa Serikali kuwa wananchi wanaojishughulisha na wafanyabiashara wanaojishughulisha na uvuvi haramu waache, kwa sababu wakiendelea kufanya hivyo, rasilimali hizi zitatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpina hapa ni mlinzi tu, kibarua sitaenda kuvua Ziwa Victoria wataenda kuvua wananchi wa Geita, wataenda kuvua wananchi wa Chato, wataenda kuvua wananchi wa Mara, wataenda kuvua wananchi wa Mwanza, mimi sitabeba nyavu, nazuia wale samaki na Wizara yangu kazi yetu ni kuhakikisha rasilimali zile zinakuwepo wananchi wetu wafanye biashara vizuri, wavue vizuri, wale samaki wazuri, ndio kazi ya Serikali. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri, mkakati wake na *operation* yake ya kukata nyavu, kubakiza *single* itawasukuma wavuvi kwenda kuvua kwenye mazalia ya samaki, sababu ni mbili.

La kwanza, nyavu ya *single* ya mita tatu haiwezi kuvuliwa kwenye mita 80 ambako sasa wanavua, lakini ya pili, *operation* yake ya kumkutaka mtu na samaki wawili wa kilo mbili kwenye tani tano akampiga faini milioni 20 wakati nyavu ya nchi 15 ambayo ni halali ina uwezo wa kukamata samaki wa kilo 200 na samaki wa kilo mbili sio sahihi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utunze muda tu muda wangu ili usiingie ndani ya miongozo ambayo inaulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika *operation* hii, niliyoiunda ya *operation* katika Ziwa Victoria, *operation sangara* mwaka 2008, *operation* hii ina wataalam hafanyi maamuzi mtu mmoja, timu hii ina wavuvi, ina *NEMC,* ina *TISS* toka Ofisi ya Rais, ina TAMISEMI na ina Polisi.

Kwa hiyo, watu hawa wanafanya *assessment* mambo ya vipimo vya ngazi mbili, ngazi tatu hayo ni kwa mujibu wa wataalam wetu, wataalam wetu wapo wanaofanya maamuzi na kutushauri kama Serikali, sisi tunasimamia maamuzi hayo. Katika *operation* hii tuliyoyaona yanatisha, ziko gari za Waheshimiwa Wabunge tumezikamata na samaki haramu, wapo Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri, wapo wenyeviti wa vijiji tumefukuza watu tumesimamisha kazi watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa katika kufanya *opetation* hiyo, tulipokagua viwanda vyote, hakuna kiwanda hata kimoja tulichokikuta kinachakata samaki ambao wanaruhusiwa, vyote vilikuwa vinachakata samaki ambao wasioruhusiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Tumekamata viwanda, tumekamata viwanda vya nyavu, viwanda vya nyavu hapa...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Mpina wakati akiota maelezo yake hapo, ametaja baadhi ya Wabunge na Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri wamekamatwa na nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ilikuwa ni vyema kwa sababu nyakati na wakati mwingi wa Bunge na watumishi wengi wa Serikali sisi hutuhumiwa kuwa tunashiriki moja kwa moja, aidha, kuhujumu mipango ya Serikali ama kukwamisha mipango ya Serikali. Kwa hiyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri aainishe na kutaja baadhi ama Wabunge wote na Wenyeviti ambao wamekamatwa na vyavu hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri taarifa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya awamu ya kwanza ya *operation sangara* mwaka 2018 inayoendelea iko karibuni mbioni hatua ya kwanza kumalizika na mimi mbele ya Kamati yangu, nilishaiahidi kwamba baada ya taarifa hii kutoka nita-*share* na Kamati na niki-*share* na Kamati itaaingia kwenye Bunge lako, hilo wala halina tatizo. Ninachotaka niseme sasa ni haya yafuatayo; katika *operation* tuliyoifanya...

**T A A R I F A**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa mwenyekiti, Waziri amesema katika shughuli hii ya kutokomeza uvuvi haramu kuna magari ya Waheshimiwa Wabunge yamekamatwa na samaki ambao wamevuliwa kiharamu, kuna Wenyeviti wa Halmashauri ambao magari yao yamekatwa na samaki waliovuliwa kiharamu, hawa watu ni wabaya wanaangamiza Taifa letu nakuomba Mheshimiwa Waziri uwataje Wabunge hawa ili tuwalaani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niruidie kusema katika *operation* hii tumesimamisha watendaji wa Serikali waliokuwa wanajihusisha na uvuvi haramu, tumekamata baadhi ya magari ya Waheshimiwa Wabunge ambao wako humu humu Bungeni, tumekamata baadhi ya Wenyeviti wa Halmashauri, tumekamata na hata kuwaweka ndani baadhi ya Madiwani, na nasema hivyo sasa kwa mantiki hiyo, kama nilivyosema kwamba tunakamilisha taarifa, *operation* hii inafanyika katika mikoa mitano. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wote kaani chini, nasema kaa chini wewe! Kaa chini, Waziri ameeleza vizuri, tuhuma za watu amezitaja, taarifa inaandaliwa, itawasilishwa kwenye muda muafaka, *End of the story*. Sasa ninyi mnakataa nini, ninyi mnakataa nini? Hatuchezi mpira, hatupiki daku hapa, sasa kuanzia sasa hakuna taarifa yoyote, ndio ukweli huo. Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekamata zaidi ya kilo 133,000 zikitoroshwa kwenda nje ya nchi, za samaki aina ya kayabo na dagaa, 133,000 zikitoroshwa kwenda Rwanda, zikitoroshwa kwenda Burundi, zikitorosha kwenda Kongo na Sirari, zaidi ya tani

133,000. Tumekamata samaki wachanga zaidi ya kilo 73,000 rasilimali hizi zote zinachezewa kwa kiwango hicho. Tumekamata mpaka wageni walikuwa wanaingia mpaka kwenye visiwa vyetu wanashiriki uvuvi, wanunua samaki mpaka kwenye visiwa ambayo ni kinyume cha sheria wageni kutoka Rwanda, wageni kutoka kutoka kutoka Kenya, wageni kutoka kutoka Burudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekamata viwanda, vilikuwepo hapa viwanda vya mabondo 22 vinafanya biashara ya mabondo lakini vilivyokuwa na leseni halali vilikuwa viwili tu. Kwa hiyo, tukisema tunapambana na uvuvi haramu, tunapambana nao kweli kweli na hii *operation* yangu hii haina mwisho hadi uvuvi haramu utakapomalizika hapa nchini mwetu na kwamba uvuvi wa wa bahari kuu na kwenyewe tumeshapata ya kufanya doria katika uvuvi wa bahari kuu walikuwa wamezoea wanavua wanaondoka Taifa letu linaachwa halina chochote. Tunashindwa kukusanya chochote na ndio maana mara ya kwanza tu nimeenda kukamata meli ile ambayo tumeikamata na tumepiga faini shilingi milioni 770.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Bunge hili litapongeza jitihada hizi kubwa za Wizara ambazo zinalinda rasimiali hizi, leo hii mkakati wa kulinda uvuvi wa bahari kuu tutazikagua meli zikiwa zinaendelea kuvua huko huko, hakuna mtu atakayeondoka kwenye maji ya Tanzania akiwa amebeba rasilimali ya Watanzania na tutaongeza meli zingine mbili za doria, tunahikisha kwamba uvuvi wa baharini kuu pamoja na bahari nzima, *coastal* nzima yetu inalindwa kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba rasilimali hizi nchini mwetu, Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zote rasilimali hizi zinanufaisha Watanzania, hatarusiwa mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeki, niseme nasema kabisa hapa kama mtu atajishirikisha na uvuvi haramu hata mimi Mpina hata Mzee Mpina mwenyewe ninyi doria mkamateni kama anajishughulisha na uvuvi haramu wa Taifa hili. Hatuwezi kuongelea kwa maneno mapesi katika rasilimali za Taifa, sisi

kama Serikali ni walinzi tu, makolokoloni, kolokoloni ukikuta mlango wa tajiri umevunjwa una shida kubwa, mimi ni kibarua wenu, kazi yangu ni kuhakikisha katika wizara mliyonipa rasilimali zinalindwa kwa nguvu zote na kazi hiyo na wizara yangu tutaifanya usiku na mchana. Lakini nasema kama kuna hoja ya msingi Wabunge wasituhumu kwa jumla, yawezekana kuna mtendaji akakosea katika kuchukua hatua unasema katika eneo fulani, katika kijiji fulani, kuna jambo hili na hili limefanyika Mpina - Waziri lishughulikie hata sasa hivi ukiniletea nitafanyia kazi na kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali hizi za Taifa zimetoroshwa kiasi cha kutosha na ninyi hapa Bunge hili muda wote limekuwa likilia makusanyo ambayo tunakusanya Halmashauri na Wizara kuhusu uvuvi ukijumlisha sisi sote ni takribani shilingi bilioni 20 ukiwaondoa wenzetu labda wa *TRA*. Kwa hiyo, makusanyo ni hafifu licha ya bahari kubwa tuliyonayo, licha ya maziwa tuliyonayo, licha mito tuliyonayo kwa hiyo ni wakati sasa wa Bunge hili kuisaidia hii Wizara, vijana hawa wanaofanya doria wanafanya kazi ya kujitolea sana, wangekuwa wepesi wasingeweza kufanya hatua kubwa hizi ambazo wanazozichukua sasa hivi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla dakika 10, ajiandae Mheshimiwa Lukuvi

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe mchango wangu kwenye hoja ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kuunga mkono hoja yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kabla sijaenda mbali. Lakini pili, kumpongeze Makamu Mwenyekiti ambaye kwa sasa anakaimu Mwenyekiti dada yangu Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuendelea kutushauri na kutuunga mkono

katika kutekeleza majukumu yetu tuliyopewa katika Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nitapenda kuanza kuchangia kwanza kwa kulitambulisha Bunge lako tukufu kwamba sekta ya maliasili na utalii ni katika sekta nyeti sana katika Taifa letu. Na unyeti wake unaanza pale ambapo Tanzania inatambulika kimataifa katika tafiti iliyofanyika mwaka 2012 kama nchi ya nne kati ya nchi 140 duniani zenye vivutio vya asili. Kwa hiyo, nchi yetu ina utajiri vikubwa sana wa vivutio vya utalii. Lakini pili, sekta ya maliasili na utalii inachangia pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 17.6 ya *GDP* yaani pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sekta hii inachangia kwa kiasi kikubwa na niseme tu ni sekta namba moja kwa kuingiza fedha za kigeni nchini mwetu. Katika mwaka wa fedha uliopita sekta hii ilichangia jumla ya shilingi bilioni 2.1 za Kimarekani, lakini pia sekta hii ina changamoto nyingi mbalimbali na changamoto zake zinatokana na uasili wenyewe wa sekta hii. Sisi kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii tunasimamia rasilimali ambayo inatumika lakini pia inajirudia, kwa maana kwamba wanyamapori wanazaliana; misitu inaweza ikaota ikakua. Kwa hiyo, ni sekta ambayo ina *rejuvenate* kadri ambavyo tunaendelea kui-*manage* kwa uendelevu.

Lakini pia sekta yetu inachangia kwa kiasi kikubwa sana kutoa ajira hapa nchini, inachangia takribani asilimia 12 ya ajira zote zinazotolewa katika Taifa letu na kwa msingi huo sekta hii ni nyeti sana na mimi katika hatua hii nikubaliane na Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliosema kwamba sekta hii kwa hakika inahitaji umakini wa namna ya kipekee katika kuiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoteuliwa kwenye nafasi hizi nina hakika mamlaka ya uteuzi ilizingatia umuhimu huo kuweka watu wanaoweza kuiongoza sekta hii kwa weledi lakini pia kwa uzalendo na uadilifu wa hali ya juu na ndiyo

maana tunatekeleza majukumu yetu bila kumwangusha Mheshimiwa Rais lakini pia bila kuliangusha Taifa letu.

Pamoja na fursa zote zilizopo lakini sekta hii ina changamoto kubwa sana ya maeneo yake kuvamiwa na watu mbalimbali, ina changamoto ya mipaka kutokuwa wazi, kutokueleweka vizuri baina ya wahifadhi na wananchi, ina changamoto kwamba sekta ya utalii imekuwa ikichangia kidogo sana kwenye kuondoa umaskini wa watu wetu japokuwa inaonekana ni sekta nyeti. Lakini pia ina changamoto kwamba sekta hii imejikita katika ukanda mmoja tu wa nchi yetu na kwa kiasi kikubwa kwa zaidi ya asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivyo sasa changamoto hizi tumeziwekea mikakati mbalimbali ya kuzitatua. Mojawapo ya mikakati tuliyoweka kwenye ya awamu ya tano ni utekelezaji wa mradi mkubwa wa kufanya *diversification* ya kijiografia kwa maana ya kutambua na kuwekeza nguvu zetu kwenye maeneo mengine zaidi ya kitalii. Lakini pia kufanya *diversification* ya mazao ya utalii yaani *toursim product* katika maeneo mengine mbalimbali na katika hili napenda kutambua *diversification* ya kijiografia ambayo tumeanza kuifanya na tutaifanya kwa mafanikio makubwa ya kuelekea kuifungua *circuit* ya utalii ya kusini ambapo tunaanza kuelekea kutekeleza mradi mkubwa unajulikana kama RIGRO ambao una dola za Kimarekani milioni 150 zaidi kidogo ya shilingi bilioni 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi huo tutafanya mambo mengi ikiwemo kujenga uwanja wa ndege wa Nduli na kuufanya uwe wenye kiwango cha kutua ndege kubwa. Lakini pia kujenga barabara ya kutoka Iringa mpaka geti la kuingia *Ruaha National Park* pale Msembe, lakini pia kujenga viwanja vidogo vidogo vya ndege 15 katika mbuga nne ambazo zinapatikana kwenye *circuit* ya kusini. Na hapa nazungumzia Udzungwa, *Ruaha National Park*, nazungumzia *Selous Game Reserve* lakini pia nazungumzia *Mikumi National Park*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo ambayo tunakusudia kuyafanya kwenye mradi wa *RIGRO* tunakusudia kuwekeza kwenye uhifadhi wa bonde la Usangu ambalo kwa kiasi kikubwa limeingiliwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu na hivyo kusababisha maji kwenye Mto wa Ruaha Mkuu kupungua kwa siku zaidi ya 60 katika kipindi cha miezi 12 ya mwaka hali ambayo inaweza kuhatarisha *bionuai* inayopatika kwenye hifadhi ya Ruaha na maeneo mengine yanayolindwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni *diversification* ya kijiografia kwamba kanda ya *circuit* ya kaskazini imeelemewa sana, lakini pia inafanya vizuri sana sasa tunaifungua *circuit* ya kusini ili na kwenyewe kuweze kuwa na hadhi ya kiutalii kama ambavyo *circuit* ya Kaskazini ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu pia unakuja na kufanya maboresho kwenye kituo cha treni cha Matambwe kilichoko pembezoni mwa Pori la Akiba la Selous lakini pia kujenga *air strips* zenye *hard surface* nne kwenye maeneo yote hayo niliyoyataja na mambo mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kufanya *diversification* ya kijiografia, tumejikita pia kufanya *diversification* kwenye mazao ya utalii yaani *tourist product* ambapo hatuangalii utalii wa wanyama pori peke yake tunaanza kufikiria kutanua wigo wa vivutio kwa kuwekeza kwenye kufanya maboresho ya utalii wa fukwe, utalii wa mikutano lakini pia...

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest* kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati. Tunategemea kwamba mchangiaji angejibu kama Waziri yale ambayo ni hoja iliyoko mbele yetu, ajibu hoja za Wanakamati na michango Wabunge ametokea *angle* nyingine kabisa hata huo mradi hatujawahi kuujadili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi wa *RIGRO* hatujawahi kuujadili kwenye Kamati yetu yaani Wajumbe tumejadili vitu vingine tumejadili sijui kichwa cha ng'ombe shilingi 100,000 sheria inatekelezwa bila Bunge kupitisha, Waziri kapita *angle* nyingine arudi kwenye mstari ajibu hoja zetu na hoja za Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu hoja umebakiwa na dakika moja hata hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na hii ni hoja ya Kamati kama Mbunge ninachangia hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo tunafanya jitihada nyingi mbalimbali ikiwepo jitihada kuongeza mazao ya utalii kama nilivyosema na hapa tunazungumzia mbali na hizo talii za fukwe, utalii wa kuvutia mikutano na matukio mbalimbali ya michezo ya kimataifa tunawekeza nguvu zetu kwenye kuandaa mwezi maalum wa urithi wa Mtanzania, ambapo tumekusudia mwezi wa tisa kuandaa...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia na kuashiri kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**T A A R I F A**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla muda wako umekwisha, Mheshimiwa Lukuvi. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo ndio Mnyamwezi Kingwangalla huyo. *(Makofi)*

Naomba niipongeze sana Kamati yangu chini ya Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango, lakini pia kwa maelekezo yao ya kila mara ambayo yamesaidia sana katika utendaji wa Wizara yangu. Lakini nawashukuru pia Wabunge wengine wote wa Bunge hili kwa ushirikiano wao mkubwa ambao unatusaidia kama Wizara ya Ardhi katika kutatua na kufanya kazi mbalimbali za kusimamia sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawapongeza vilevile Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wa sekta zilizotangulia ambazo ni watumiaji wa ardhi wote waliotanguliwa wa Mifugo, wa Kilimo, wa Maliasili wote ni watumiaji wa ardhi nawapongeza sana kwa mikakati yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikua tu niwakumbushe kwamba tunajua kwamba tuna migogoro mingi sana na kwa upande wa ardhi tuna migogoro ndani ya vijiji na ndani ya miji na tunajua kila Mbunge hapa alishawahi kuorodhesha migogoro yake kutoka kwenye Jimbo lake na hata tungeorodhesha yote tusingeweza tukaimaliza hata tungepata kipindi cha Bunge la mwaka mzima. Nataka muamini tu kwamba migogoro yote mliyoorodhesha kuanzia kwenye Kamati Teule ya Sendeka na ndiyo maana hata mdogo wangu Mheshimiwa Nape hapa mimi naona hakuna sababu ya kuunda Kamati Teule nyingine kwa sababu ile Kamati ya mwisho ya mwaka 2015 ndiyo tunafanyia kazi kama Serikali hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha yenu ya migogoro ndio tunafanyia kazi ndiyo iliyosababisha tuunde Kamati ya Mawaziri watano, nataka kuwaambia tunaendelea vizuri isipokuwa kama mnavyojua baadhi ya Mawaziri wameingia

karibuni tumepeana muda ili kila mtu akaangalie sekta yake, halafu tutakutana tena nafikiri wakati wa Bunge la Bajeti kila Wizara itakuwa na maeneo mapya ya kusemea kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, Kamati yetu inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe tu kwa sheria ya mipango miji na za vijiji za ardhi zote za mwaka 1999 masuala yote yanayohusu ardhi yanasimamiwa na Halmashauri zetu za Wilaya. Halmashauri za Wilaya ndio zinazohusika na mipango mijini lakini ndizo zinazohusika na mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji.

Kwa hiyo, kila tunachosema tujue mamlaka ya mwisho ya kuandaa mipango ya matumizi bora mjini au mipango ya matumizi bora vijijini ili kuepusha mapigano ya wakulima na wafugaji na wavamizi wengine ni sisi Halmashauri ndio tumepewa dhamana hiyo kwa mujibu wa sheria zote hakuna mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kila mara tuwe tunashiriki vizuri katika kusimamia ardhi yetu kwa kushiriki katika upangaji mijini lakini vijijini. Nawapongeza sana Halmashauri ambazo hivi sasa mijini wameshaandaa *master plan* ziko Halmashauri 23 za miji, lakini ziko Halmashauri nyingine 24 na miji midogo ambayo wameandaa mipango ya kati na ziko Wilaya karibu asilimia 20 ambao wameshaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Kwa hiyo, nawahimiza tu Waheshimiwa Wabunge angalau kila Wilaya kwenye bajeti ingeweka angalau kila mwaka kufanya matumizi bora ya ardhi vijiji vitano vile vyenye migogoro mikubwa ambavyo vinashirikisha jamii nyingi pengine tungepiga hatua. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tujue kwamba jukumu la mipango ya matumizi bora ya ardhi ni la kwetu sisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi dakika moja samahani kidogo. Kwa mamlaka niliyokuwa nayo naongeza nusu saa mpaka saa mbili na robo, endelea Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara kwa kutambua hilo na ninyi wote Waheshimiwa Wabunge mnajua sehemu kubwa ya nchi hii haijapangwa, mijini na vijijini hakujapangwa yaani utambuzi na upangaji wa matumizi mbalimbali mijini na vijijini haujafanyika kwa zaidi ya asilimia 75.

Kwa hiyo, Wizara yangu na Serikali kwa sasa tunaandaa mpango wa kitaifa wa kupanga na kupima kila kipande cha ardhi cha nchi hii. Kwa sababu hiyo tutakuja na mapendekezo kwenye *budget speech* yetu pengine kuanzisha *fund* maalum ambayo itasababisha zoezi hili la upangaji wa vijiji na upimaji na mijini liweze kutekelezeka. Kwa hiyo, tunakusudia angalau kila eneo na kila kipande cha ardhi kiweze kupangwa ili ulinzi wa ardhi uwe madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na zoezi hilo tumeliona linawezekana kwa sababu hivi sasa tuanza katika Wilaya ya Kilombero, Malinyi na Mahenge. Tumeanza kupanga kila kipande cha ardhi na katika mwaka ujao tutakuwa tunakamilisha mpango wa Wilaya hizo tatu tutakuwa tuna uwezo wa kutoa hati za Kimila zaidi ya laki nne katika Wilaya hizo tatu. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba kila mwananchi akiwa na hati katika eneo analomiliki ikiwa kijijini hati ya kimila na mjini *title deed* itamwezesha kutumia rasilimali ardhi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na zoezi hilo kwa sababu hii nchi hii haijapangwa kwa muda mrefu mijini hata vijiji kwa mijini tumekuja na programu ya urasimishaji wananchi wote ambao walijikuta wamejenga katika maeneo ambayo hayakupangwa na kupimwa kwa matatizo mbalimbali pengine kwa Serikali kuchelewa kupanga maeneo hayo. Tumeanzisha programu ya urasimishaji katika maeneo hayo ili wananchi hao waweze kupata huduma za msingi katika maeneo hayo kama vile barabara maeneo ya upitishaji miundombinu ya umeme na maji, lakini pia tuwawezeshe kuwa *title deed* waweze kumiliki ardhi kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe mjue jambo hili linahimizwa na Serikali kama una *squatter,* kama una wananchi katika Jimbo lako wanaishi katika makazi holela, jitahidi sana kuhakikisha mnashirikisha wananchi katika mitaa ile wanafanya urasimishaji ili watoke kwenye makazi holela wakae kwenye makazi yaliyo rasmi. Tunafanya zoezi hilo ni rasmi, najua wote mnaokaa mjini mna maeneo ambayo yanamakazi holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fursa imetolewa na Serikali ya Awamu ya Tano kurasimishwa maeneo hayo na mpaka sasa mikoa ambayo inaongoza kwa urasimishaji ni Mkoa wa Mwanza ambao kwa sasa Wilaya mbili tu za Ilemela na Nyamagana wanakaribia kutoa hati 30,000 kuwawezesha wao…

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nilikuwa napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri wangu Lukuvi kwamba na Waziri wa Uvuvi ajifunze kwa Waziri Lukuvi kwamba wakazi waliojenga kwenye makazi holela umewarasimisha, sio yeye anayewanyonga kabisa bila kuwaelekeza waende wapi. *(Vicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Wizara inasimamiwa na sheria zake. Sheria yangu inaniruhusu kurasimisha makazi holela, lakini halitakuwa jambo la kudumu, ndiyo maana tunahimiza *master plan* na tunakuja na mpango wa

kupanga na kupima kipande cha ardhi. Tukiweza kupanga na kupima kila kipande cha ardhi, kwa vyovyote vile urasimishaji utakoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwapongeze sana viongozi na wananchi wa Wilaya za Ilemela na Nyamagana peke yao wamewezesha wananchi wao ambao walikuwa wamejenga majengo ya fahari na hayana hati, leo wanamiliki wakiwa na hati katika makazi holela. *(Makofi)*

Pia Mkoa wa pili ni Dar es Salaam, Dar es Salaam kuna maeneo mazuri wanafanya vizuri Kimara, Makongo kule kwa maprofesa wanafanya kazi nzuri wamechanga wenyewe. Lakini na mikoa mingi wanaendelea kufanya zoezi hilo, kwa hiyo, nawapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati kwamba kuanzia sasa hatutatumia makampuni ya nje kufanya *master plan*. Tumefanya *master plan* kwa kutumia Kampuni ya Singapore kama walivyosema watu wa Kamati, Wajumbe wangu wa Kamati kwa gharama kubwa. Tumefanya Mwanza na Arusha ni kweli, lakini nimesema nimekubaliana na mapendekezo ya Kamati yangu ya Ardhi kuanzia sasa haitawezekana kabisa kuajiri makampuni ya nje kwa ajili ya kufanya *master plan*, kwa sababu vyuo vyetu vya ndani vimetoa wataalam wengi, na hizi *master plan...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na majibu sahihi, ahsante sana, hongera kwa majibu sahihi, ahsante. Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa

nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yetu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa kuweza kutusikiliza na nina imani Wabunge wote mmeunga mkono hoja zetu za Kamati, na pia niwashukuru sana Wabunge wote waliochangia, kwa sababu ya muda sitataja Wabunge wote, ila nitataja tu idadi. Wachangiaji waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 17 na wachangiaji waliochangia kwa kuzungumza Bungeni ni Wabunge 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea suala la Wizara ya Ardhi, nadhani Mheshimiwa Waziri ameongelea na amejibu hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo pia ya Kamati ameyaafiki, kitu ambacho pia sisi tunaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunasisitiza kama Kamati ni Serikali itenge fedha za kutosha ili mambo yote, na mipango yote mizuri ambayo Wizara ya Ardhi inayo ya upimaji na urasimishaji wa ardhi nchini kote ufanyike ili kuweza kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi ambayo inaendelea sehemu tofauti tofauti katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri, amejibu lakini hajajibu hoja za Kamati kama tulivyopendekeza. Lakini tushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi anazoendelea kufanya. *(Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Upo juu, endelea, endelea.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo kadhaa kwenye Kamati tuliyaona na ni vema nikayasemea hapa pia. Sheria Namba 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009 imeainisha baada ya Sheria hiyo kuanza kutumika mwaka 2009, ilikuwa

ndani ya miezi 12 itangaze upya mapori tengefu, maeneo oevu na hifadhi zote za Taifa, hii ilikuwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko kwa Kamati kwa sababu mpaka hivi leo tunaongea mwaka 2018, hii kazi haijafanyika na kufanyika kwa kazi hii kungeweza kusaidia mambo mengi sana ambayo yanaendelea hivi sasa. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anachangia amekiri kuwepo vijiji ndani ya Hifadhi, hili suala lipo na kwa kweli tungeiomba Serikali itenge fedha ili hili suala liweze kumalizika na jinsi inavyoendelea kuliacha ndivyo linavyoendelea kuwa kubwa. Hii kazi ingefanyika mwaka 2009 ingekuwa tofauti sana na kama itakapokufa kufanyika mwaka 2018/2019 au 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Wajumbe wengi wamechangia suala la migogoro ya mifadhi na wafugaji. Hili suala ni kubwa na karibia kila Mjumbe aliyezungumza na aliyeandika kwa maandishi wote wameliongelea hili suala, sasa tunaiomba Serikali hili suala likamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa Yussuf ameongelea suala la ushirikishwaji, sisi kama Kamati pia tuliliona ni vyema Serikali inapotaka kufanya jambo ishirikishe wananchi, ishirikishe wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Serikali ikitaka kufanya jambo lake bila kushirikisha wananchi na wawekezaji linaweza likakwamba. Vilevile mwekezaji akitaka kufanya jambo lake bila kushirikisha wananchi na Serikali ni dhahiri litakwama. Kwa hiyo, ni vema huu mtiririko huu ukafatwa na ukawa unafanyika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limeongelewa la uharibifu wa misitu, sisi kama Kamati pia tumeliona. Uharibifu wa misitu ni mkubwa sana unaoendelea nchini kwetu na hii yote inasababishwa na kazi na shughuli za kibinadamu, kuna ukataji miti hovyo ambayo miti tunayokata na tunayopanda ni vitu viwili tofauti kabisa.

Kwa hiyo, kama Kamati tunaishauri Serikali, kwanza kabisa ni kuelimisha hawa wananchi umuhimu wa kupanda miti na vilevile kuna suala la kuchoma mkaa, hili suala ni kubwa. Watanzania zaidi ya 80% wanatumia mkaa majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kulisaidia hili suala na kuokoa miti yetu, ni vema Serikali ikaja na mkakati na mpango mzuri wa nishati mbadala na kupunguza gharama ili wananchi waweze ku-*afford*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongelea pia suala la kuweka alama kwenye hifadhi, ili pia ni suala ambalo linatakiwa kufanyika mapema. Tumeona kuna matatizo kwenye shoroba, lakini kwa sababu hakuna mipaka na wala hakuna Sheria ya maeneo haya. Kwa hiyo, ni vema Serikali ikajipanga na kuja na huo mkakati na ukafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeongelea suala la Utalii ambao Mheshimiwa Waziri naye amelijibu, ni dhahiri kwamba Serikali yetu inapata mapato ya Taifa takribani 17.5% na vilevile fedha za kigeni kwa 12%. Kama Kamati tunataka tukushauri na kusema Wizara hii ni zaidi ya kidiplomasia, mahusiano ya nchi na nchi yanatakiwa. Tumeona *forex* hii inakuja kutokana na wageni wanaotoka nje. Kwa hiyo, kama Kamati tunaomba na tunaitaka Serikali kama inawezekana iweze kuwa na mahusiano mazuri na watalii vilevile na wawekezaji nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuunda Kamati Ndogo kama Kamati pia tulilipendekeza na napenda kulisisitizia. Mheshimiwa Lukuvi amejibu, amesema Kamati Ndogo ilifanyika na kina Lembeli na ndiyo inafanyiwa kazi mpaka leo, lakini sisi kama Kamati hatujawahi kuona majibu hayo. Kwa hiyo, kwa sababu hatujawahi kuyaona tumeona kama Kamati yetu sisi ni vema pia ikaifanya hii kazi upya na tukaja na mapendekezo hapa Bungeni na tukaona tunaanzia wapi kutokea hapo. *(Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Umemaliza.

**MHE. KEMILEMBE JULIUS LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mwaka 2017 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na *amendment* ya Mheshimiwa Richard Mbogo lakini ameitoa, ame-*withdraw* na kiti kimekubali. Kwa hiyo, sasa ni kipindi cha kuwahoji kwa sasa Bunge likubali taarifa na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa taarifa hii ni rasmi na Bunge imeipokea, na Bunge imeipitisha, na Serikali sasa ni kazi yenu kutekeleza mapendekezo ya Kamati kama ilivyoainishwa. Lakini nichukua nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti, umeonesha ukomavu mkubwa sana wewe na Kamati yako kwa ujumla *you have done a good job*, hongereni sana. *(Makofi)*

Nipongeze Wizara, nimpongeze Waziri wa Utalii, Naibu Waziri kwa ushirikiano mzuri mnaoutoa kwenye Kamati, mmefanya kazi nzuri sana, pokeeni ushauri wa Kamati, mwende pamoja, *open pages together* na nchi ita-*progress.* Hongereni sana. *(Makofi)*

Sasa namuita Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo na Mifugo na Maji.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mwenyekiti hoja ya kuunda Kamati Teule ya Bunge. *(Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Imesomwa.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa majumuisho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape subiri, ameshasimama Mwenyekiti muache amalize, halafu tutakusikiliza hoja yako, Mwenyekiti endelea.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri naanza ili dakika zangu zisipotee.

Naomba nichukue nafasi hii ya awali kabisa kukushukuru wewe kwa kuendesha majadiliano hapa Bungeni kwa umahiri mkubwa. Nawashukuru sana Wabunge kwa kujadili na kushauri na kuonesha maeneo ambayo yalikuwa na sababu ya kuyaonesha ili Serikali iweze kuyachukulia hatua na kutekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Wabunge wa Kamati yetu kwa ajili ya kufanya kazi nzuri na ninyi wote mmeshuhudia kwamba hakuna jambo jipya ila mlisisitiza zaidi yale yote yaliyokuwa kwenye taarifa ya Kamati yetu, ninawashukuru na kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge waunge mkono mambo mengi ambayo tumeyaongelea kwa sababu kwa kweli ni muhimu sana, na Wabunge wengi wamejadili kwa kuongea na maandishi, jumla yao imefika 51 katika muda mfupi huu, ninawapongeza sana na kuwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru vilevile Mawaziri wanaoongoza sekta hii kwa kujitahidi sana kutoa na wao majibu au kuelezea mambo ambayo wameyatekeleza ninaomba wazingatie yale yote ambayo yametiliwa mkazo na Waheshimiwa Wabunge wote. Ninawashukuru kwa kuchangia hoja na kusisitiza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana kuona matatizo yaliyoonekana *Lake Victoria* au Ziwa Victoria katika kuona kwamba Waziri kuhangaika na wenzake kuona kwamba wanajaribu kudhibiti uvuvi haramu, lakini ninaomba wachukue jitihada ambazo zitaondoa uvuvi haramu bila kukandamiza wavuvi. Vilevile jitihada zinazochukuliwa ziondoe uvuvi haramu ili tusiendelee na hayo mambo ambayo yanaumiza watu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo sikuweza kuliongelea pale kwenye taarifa lakini ipo ni kwamba Ziwa Victoria siyo la Tanzania tu ingawa sehemu kubwa ipo kwetu ni ziwa ambalo kuna nchi tatu ambazo zinazunguka, tusichukue hatua ya kunufaisha nchi zingine na kuinyima manufaa Tanzania. Vilevile nafikiri kwa sababu kuna malalamiko mengi kama walivyoomba Waheshimiwa Wabunge tuunde tume ili tuondoe malalamiko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni migogoro ya watumiaji wa ardhi. Mheshimiwa Lukuvi alisema kwamba tume iliundwa ya Mheshimwa Sendeka, ilikuwa zaidi kati ya wafugaji na wakulima. Lakini malalamiko ya safari hii ni zaidi ya wafugaji na Hfadhi za Taifa, ninaomba kama tulivyoomba awali kwamba tuunde Tume ili migogoro hii vilevile iweze kuondoka na malalamiko yaondoke. Ninaomba Bunge

liweze kuunga mkono hayo ili migogoro hii isiendelee na malalamiko ya wananchi yawe yametumika kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la pembejeo, Waheshimiwa Wabunge bila pembejeo hakuna kilimo na hakuna tija, kwa hivyo Mheshimwa Waziri na Serikali tunaomba sana hatua mliochukua Wajumbe wa Kamati waliwaungeni mkono na Wabunge waliwaunga mkono, lakini mmeona changamoto zilizojitokeza, naomba mzitathmini, msimamie na mratibu ili kudhibiti usambazaji na upatikaji wa wakati wa pembejeo. Serikali isipofanya hivyo kilimo kitazidi kudidimia.

Lakini vilevile kuna *issue* ya wadudu waharibifu, tusipochukua hatua haraka mazao yatakuwa hayapo na umaskini utazidi kuingia Tanzania. Kwa hiyo, naomba sana hatua ya haraka kwa upande wa Serikali na wale wote wanaohusika kuona kwamba dawa zinapatikana au viatilifu vinapatikana ili kunusuru kuingia kwenye janga la Taifa la mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Kuhusu masoko ya mazao, soko la uhakika na bei ya mazao lenye faida ni kichocheo cha uzalishaji wa mazao ya kilimo. Serikali iwe na utashi wa kusimamia kwa makini, kuratibu na kufanya utafiti wa soko la mazao. Ukosefu wa soko la mazao ya kilimo ni moja ya sababu inayofifisha kilimo nchini. Hivyo, Serikali iangalie bei ya mazao hasa katika kilimo cha mkataba, lakini vilevile Wabunge walilalamikia sana bei ya mahindi na masoko ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lazima tuchukue hatua wakati unaotakiwa kuchukua. Kama ukiangalia Tanzania inazalisha mahindi kabla ya Zambia na Malawi, na kwa hivyo tusipotumia masoko ambayo yapo wakati tumevuna, tutakutwa na nchi za jirani na hivyo itakuwa ni sababu ya kukosa masoko kwa ajili ya mahindi yetu. Kwa hiyo. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana pamoja na Wizara yako muwe makini sana katika kutoa uamuzi ambao unaleta hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho kuhusu kilimo, ninaomba Serikali ione umuhimu wa kutoa kodi, tozo, ushuru na ada mbalimbali kwenye pembejeo na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na zana za sekta hiyo. Tukifanya hivyo tutahamasisha kilimo na kodi zitalipwa kwenye kununua bati, kwenye kununua *cement* na maeneo mengine yote na uchumi wa nchi utachanganya kwa urahisi zaidi kwa sababu kilimo ndiyo chimbuko la uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Kwa upande wa maji; maji ni uhai, maji ni uchumi, maji ni usafi na afya. Umuhimu wa maji hauna mjadala, tunaomba wakala uanzishwe mara moja na tunaomba sana ile shilingi 50 Waheshimiwa Wabunge tuazimie tena, tulishaazimia tumuombe Waziri wa Fedha aone umuhimu wa maji ndani ya nchi hii kwa sababu utaondoa gharama za sekta zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo, tunaomba Tume ya kuangalia malalamiko kama nilivyosema, lakini mifugo ni rasilimali ya Taifa na ni mali ya wafugaji mmoja mmoja, naomba tuone kwamba wafugaji wanapaswa kuhamasiswa, wafugaji wanapaswa kusaidiwa, wafugaji wanapaswa kuangaliwa ili mifugo iwe sehemu ya rasilimali ya Taifa, tusigombane na wafugaji, haitusaidii lolote na ninaomba sana mgogoro huu wa wafugaji na hifadhi uangaliwe kwa kuunda Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu uvuvi, naomba tuunde bandari ya uvuvi na tununue meli za uvuvi na ili tuwe na samaki wengi ambao ni rasilimali kubwa kuliko hata hayo madini tunayoyapigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunaomba tuongeze thamani, kwa hiyo suala la viwanda vya kuongeza thamani na kuongeza muda wa maisha ya mazao ni jambo muhimu ambalo litawahakikishia wakulima wanaozalisha mazao ya kilimo na yanayoongeza maisha ili mazao ya kilimo yasiharibike sana kwa sababu mazao ambayo hayajaongezewa thamani, hayajachakatwa yanaharibika upesi na viwanda vinapaswa kuwa masoko.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru sana kwa yeye mwenyewe kusema kwamba viwanda ndivyo vitakavyookoa uchumi wa nchi hii na kutufikisha kwenye uchumi wa kati na mapato ya kati na tukifanya hivyo tutatuwa tumeiokoa nchi hii na mambo yataenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nami niokoe muda niishie hapa niwaombe Waheshimiwa Wabunge waunge mkono Maazimio ambayo yako kwenye taarifa ya Wabunge ili tuweze kuimarisha sekta hizi ambazo ni muhimu na wala haina mjadala kwamba kilimo, ufugaji, uvuvi na maji ni eneo muhimu ambalo tukiliangalia vizuri nchi hii itaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kutoa hoja ili Bunge liweze kupokea na kuweza kuunga mkono masuala ya Kamati hii, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na naomba muunge mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana. Hongera sana Mwenyekiti na Kamati yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Sware una *amendment.*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi katika ukurasa wa 55; kipengele cha 3(2) ya ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji inatoa mapendekezo juu ya suala la uzalishaji wa mbolea nchini na Kamati imeeleza juu ya utekelezaji wa ununuzi na upatikanaji wa mbolea nchini pamoja na changamoto zake. Sasa Kamati imetoa mapendekezo matatu nami ningeomba niongeze yangu mawili kwenye kuweka msisistizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuongeza mambo mawili zaidi kwa vigezo vifuatavyo:-

KWA KUWA Sera ya Kilimo ya Taifa ya mwaka 2013 inaelezea umuhimu wa kuongeza matumizi ya pembejeo ya kisasa ikiwemo mbolea;

NA KWA KUWA matumizi ya mbolea nchini ni wastani wa kilo 10 kwa hekta moja badala ya kilo 119.9 kwa hekta na kwa kuwa Serikali imeanzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea wa pamoja yaani *fertilizer bulk procurement* ili kuwawezesha wakulima kupata mbolea bora na ya bei nafuu;

NA KWA KUWA mfumo huu wa ununuzi wa mbolea unaonyesha changamoto ya usambazaji wa mbolea kutoka wilayani kwenda vijijini unatokana na changamoto ya miundombinu ya barabara na hivyo kuongeza gharama za usafirishaji na bei ya mbolea hiyo ambayo inapelekea kupanda kwa mbolea husika katika maeneo husika. *(Makofi)*

KWA HIYO BASI napendekeza tuongeze mapendekezo mawili zaidi kwamba Kamati ipendekeze Serikalini iangalie upya mfumo wa usambazaji wa mbolea ili ifike kwa walengwa kwa wakati ikiwa na bei elekezi, nikiwa na maana kwamba kila eneo liwe na bei yake inayoeleweka kama vile tunavyofanya kwenye mafuta ya petroli au dizeli inajulikana Dar es Salaam ni shilingi ngapi mikoani mingine ni shilingi ngapi ili kutoa ukakasi wa bei kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la pili ni kwamba Serikali iweze kuwekeza katika kuanzisha viwanda vya mbolea nchini ili kukidhi mahitaji ya mbolea kama alivyofafanua hapo juu tulichonacho sasa hivi ni kidogo sana hata tunachokiagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kutoa hoja yangu kama sita pata maelekezo ya kutosheleza kutoka kwa Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Dkt. Sware ni hoja nzuri tu, ni kwamba ni kweli baada ya kuanzisha huu mfumo moja ya changamoto tuliyokutana nayo wakati wa ukokotoaji wa bei elekezi tulikuwa tume-*estimate* gharama za kutoka kwenye wilaya kwenda vijijini kwa kuzingatia hali ya barabara na kadhalika ilivyokuwa. Lakini baada ya mvua kunyesha maeneo mengine usafirishaji ulivurugika kabisa kwa hivyo bei za usafirishaji zikapanda sana na kwa...

**MHE.RICHARD M. NDASSA:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa hebu samahani kidogo, hebu kaa kwanza.

**MHE.RICHARD M. NDASSA :** Ina maana Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa samahani kaa kidogo. Mheshimiwa Tizeba.

**WAZIRI WA KILIMO:** *Yes,* na kwa hivyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tizeba kama hoja yake umeikubali, useme umeikubali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Nimeikubali.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati...

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ehee kuhusu utaratibu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana kwa sababu hoja iliyoko mbele yetu niya Mwenyekiti wa Kamati, siyo ya Waziri. *(Makofi)*

Waziri hata kujibu pale siyo sahihi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa kaa chini.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kwa hiyo, nitakuomba Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa kaa chini, mnataka kuwaisha mambo mnakaa mna ambizana hovyo hovyo hamelewi shughuli zinakwendaje humu ndani, anaanza Serikali anakuja Mwenyekiti hoja inarudi kwa mtoa hoja, *period,* Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi, Kamati iliongelea sana umuhimu wa tathmini ya Serikali kufanyia huu mfumo mpya wa *bulk purchases* au ununuzi wa pamoja. Ya pili, Mheshimiwa aliyeleta hoja hii au jedwali la mabadiliko ni moja ya Wajumbe wa Kamati yetu. Sasa sisi tuliisema kwa ujumla kwamba tufanye tathmini na wakifanya tathmini hiyo ikiunganisha hayo wanayoyasema itakuwa haina madhara yoyote. *(Makofi)*

Vilevile tulisema kwamba tuanzishe viwanda vya kuzalisha mbolea nchini na ilisisitizwa sana kwa hivyo mimi sijaona kwamba kuna sababu ya nyongeza hapa kwa sababu hilo tayari lilishaongelewa vizuri na tuliisisistiza vizuri lakini haina madhara kwa sababu inaunga mkono mambo ambayo yalishajadiliwa na kusemwa na Kamati yetu na yeye yuko kwenye Kamati.

Kwa hiyo, sioni ubaya lakini Mheshimiwa Mjumbe alipaswa kuyaleta kwetu kwenye Kamati badala ya kuyaleta hapa, huo ndio utaratibu wenyewe kwa sababu ange-*declare interest* kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati yetu. Lakini nyongeza yake wala haina madhara na jambo ambalo tuliliongelea kwenye Kamati mkiongeza kuboresha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI**: Wewe ndiyo Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Umeafiki hoja yake au hujaiafiki?

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Naiafiki kwa kuunga mkono hoja ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Basi kaa ahsante, kaa chini, Dkt. Sware funga hoja yako. Shukuru tu huna lingine la kusema.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ambaye japo kuwa ameikubali kwa...

**MWENYEKITI:** Ahsante, kaa chini. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Dkt. Sware kuunganishwa na hoja ya Kamati.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWNEYEKITI:** Hoja imekubaliwa na itaingia pamoja na mapendekezo ya Kamati, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali taarifa na mapendekezo pamoja na mapendekezo ya Dkt. Sware na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli za Kamati za mwaka 2017.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nawapongeza tena Mawaziri mlio husika kwa Mifugo, Kilimo, pia Kamati mmeonesha umahiri mkubwa sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili. Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nasimama kwa Kanuni ya 120 naomba nisiisome yote lakini nisome 2(a) inasema; "Baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya kanuni hii anaweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule." *(Makofi)*

Kwa kuwa Mwenyekiti, hoja imekubaliwa na imekuwa *adopted* na Bunge sasa kwa kanuni hii natoa taarifa ya mdomo kwamba nina kusudio la kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule sasa kwa kufuata utaratibu wa kikanuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape, kanuni iko sahihi 120 lakini kanuni ya (b) inasema; "Mbunge ambaye anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule atawasilisha taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unafaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli kama ilivyoainishwa chini ya kanuni 30(4)." Kwa hiyo, sasa nakukubalia uandike taarifa yako mwandikie Katibu na yeye ataipanga katika shughuli za kawaida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza sasa hivi ni saa mbili na dakika kumi, tumemaliza shughuli za kazi ya leo, niwapongeze Wabunge wote kwa kazi nzuri mlizofanya mnastahili pongezi sana. Lakini nipongeze upande wa Serikali kwa majibu sahihi, majibu mazuri, majibu yanayoleta matumaini makubwa kwa Taifa letu.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.14 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 7 Februari, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*